

KIGUU NA NJIA

Kiguu na Njia

Ben R. Mtobwa

Heko Publishers Ltd

S.L.P 70319

Dar es Salaam

Tanzania

Chapa ya kwanza: 2016

ISBN 9987 416 08

Hairuhusiwi kuiga, kutafsiri, kupiga chapa wala kukibadili kitabu
hiki kwa njia yoyote bila idhini ya HEKO Publishers Ltd.

Ni miaka sasa imepita toka ulipotutoka mwaka 2008, tunakukumbuka kwa ucheshi wako, mapenzi yako na urafiki wako. Kitabu hiki ni moja ya zawadi yako uliyotuachia, ingawa leo haupo pamoja nasi, kimwili tunaamini upo nasi na unafurahia kuona tunaenzi kazi zako. Tunaamini siku moja tutaungana tena mbinguni. Tunasema ahsante kwa yote mema uliyotufanyia na ahsante kwa mema yote uliyotuachia. Maneno hayatatosha kueleza shukrani zetu kwako, kwa neema na rehema zake Mungu, tunasema

Ahsante baba,

AHSANTE BEN R. MTOBWA.

SHUKRANI.

Kitabu hiki kimetoka kwa michango ya watu mbalimbali ambao kwa namna moja ama nyingine, walikuwa msaada mkubwa katika kufanikisha kutoka kwa kitabu hiki. Wote waliochangia kufanikisha kutoka kwa kitabu hiki wanapaswa kutambua kuwa, tumethamini sana michango yao na tunashukuru kwa dhati.

Ni vigumu sana kuwataja wote ila haitakuwa vyema kutowataja baadhi yao ambao walijitoa kwa hali na mali ili kufanikisha kitabu hiki.

Kwanza kabisa tunapenda kumshukuru Mungu ambaye ametupa uhai mpaka siku hii ya leo kuweza kufanikisha kutoa kitabu hiki. Pia bila neema zake, leo hii tusingefika hapa tulipo.

Haitakuwa busara bila shukrani zetu kuzitoa kwa wazazi wetu; Magreth Johnson na Ben R. Mtobwa ambao bila ya wao leo hii tusingeweza kufika hapa tulipo. Roho zao zilazwe mahala pema peponi. Amina.

Shukrani kwa Kaka Innocent Ndayanse, ambaye alikuwa mstari wa mbele katika uandaaji wa kitabu hiki.

Shukrani kwa Chris Sholla kwa kutumia muda wake mwingi katika kusaidia kuandaa wa kitabu hiki.

Shukrani zetu hazitaweza kukamilika bila kuwashukuru wapenzi wote wa Hayati Ben R. Mtobwa ambao upendo wao juu yake ndio uliotusukuma katika kutoa kitabu hiki



BEN R. MTOBWA ambaye ni mwandishi mashuhuri wa
riwaya za **Joram Kiango** na zingine nyingi kama **Pesa Zako**
Zinanuka na **Zawadi ya Ushindi**.

Alizaliwa tarehe 28/8/1958 na kufariki Tarehe 9/11/2008
katika hospitali ya Heart Institute.

Kazi zake mbalimbali zimekuwa mchango mkubwa kwa taifa
letu kwa kuelimisha, kuburudisha na hata kuwa chachu kwa
vijana wadogo wanaochipukia katika fani ya uandishi.

MUNGU AILAZE ROHO YA MAREHEMU MAHALA
PEMA PEPONI.

AMINA.

SURA YA KWANZA

Mwanzo wa Kisa na Mkasa

Ilikuwa mara yangu ya kwanza kumuona baba akitokwa na machozi. Kwa kweli, ilikuwa mara yangu ya kwanza kumuona mwanamume yeyote mwenye umri wa baba akilia, iwe sirini au hadharani. Kitendo cha mwanamume kutokwa na machozi, iwe kwasababu ya maumivu au majonzi, hakikupata kukubalika katika jamii yetu.

Nakumbuka nilipokuwa mtoto mdogo, wa miaka mitatu au minne hivi, nilipojikwaa na kuumia au kupigana na wenzangu nikalia. Baba alikuwa akinicharaza bakora huku akisema, “Mwanaume gani wewe unalia? Mwanaume halii!”

Babu yangu pia, mzee Karimanzila, aliwahi kunicheka sana kwa suala hilo la kulia. Siku hiyo mtego nilioutega mwituni ulikuwa umemnasa kanga mkubwa sana. Rafiki yangu mmoja tuliyekuwa naye porini aliniita kwa sauti kubwa kuniarifu juu ya kanga huyo. Lakini nilipofika kwenye mtego huo nilimkuta Katato, ambaye alituzidi sana kwa umri na umbile, akimfungua kanga huyo kwa madai kuwa ni mtego wake. Tulibishana naye sana. Kwa kunikomoa Katato alimwachia kanga wangu, ambaye aliruka na kutokomea zake mwituni. Nilijaribu kupigana naye lakini akanizidi nguvu na kunitia ngeu katika paji la uso. Nililia njia nzima hadi kijijini. Babu

aliposikia habari hizo aliniita na kunidhihaki kwa kusema, “Ukiona mwanaume analia ujue na roho ya kike. Angestahili kuvaa gauni badala ya kaptula.”

“Lakini yule alikuwa kanga wangu wa kwanza. Nimekwishanasa njiwa, hondohondo na kware. Leo nimebahatika kumnasa kanga. Ningefurahi sana kumchinja na kumla!” Nilimjibu babu.

Babu alitabasamu kidogo kisha akasema, “Kanga elfu moja utawala. Tatizo ni hayo machozi. Machozi ya mwanaume yanatakiwa kuwa adimu sana. Leo jioni uje nikusimulie kisa cha mwanaume aliyepokonywa mke kwa ajili ya machozi.”

Nilizipenda sana hadithi na simulizi za babu. Kwa ujumla, kijiji kizima na hata vile vya jirani vilipendelea sana kuja kwetu kumsikiliza babu akisimulia matukio mbalimbali yaliyomkuta katika maisha yake. Hadithi zake zilijaa miujiza na maajabu kiasi kwamba baadhi ya watu walidiriki kumwita ‘mwongo’ au ‘anatia chumvi’. Lakini yeye aliwacheka watu wa aina hiyo na kuwaambia, “Hamjaiona dunia. Dunia yenu ni kijiji hiki pekee. Mimi nimeizunguka. Nimefika upande wa pili wa dunia!”

Hiyo ilikuwa kauli yake ya mara kwa mara, kauli ambayo iliongeza utamu wa simulizi zake. Hakika babu mwenyewe alikuwa hadithi, tena hadithi ya kulisimua kuliko zile simulizi zake. Inadaiwa kuwa, utotoni, akiwa na umri wangu, alitoweka kijijini hapo kama mzuka. Alitafutwa kwa siku kadhaa bila mafanikio. Watu walidhani kuwa ameliwa na simba au mamba. Lakini alipoibuka miaka kadhaa, baadaye, akiwa na simulizi tele za ‘kuizunguka dunia,’ watu walibadilika na kuamini kuwa alichukuliwa na mashetani ya chini ya bahari.

Pamoja na kuzipenda hadithi zake, pamoja na kiu ya kusikia kisa hicho cha ‘machozi ya mwanamume’ bado hasira dhidi ya kanga wangu aliyepeperushwa kwa makusudi na maumivu toka kwenye ngeu ya paji la uso kwa mara ya kwanza vilinifanya nikatae kwenda kumsikiliza.

Hivyo, kumwona baba akilia lilikuwa jambo jipya kabisa katika maisha yangu. Alikuwa kaketi juu ya gogo, mikono yake yote miwili ikiwa imekishika kichwa chake huku macho yake yakitazama mbele yake, ingawa ilikuwa dhairi kuwa haoni kitu chochote kutokana na wingi wa machozi. Nilijikaza na kumsogelea kwa nia ya kumuuliza kulikoni. Lakini mara nilipomfikia ushujaa ulinitoka. Nikajikuta nikiambulua kukaa ubavuni mwake, juu ya gogo lilelile. Kwa mshangao wangu, baba alifanya kitu ambacho hakupata kukifanya huko nyuma. Alinikumbatia kwa mkono wake mmoja huku mkono wake wa pili ukifuta machozi ambayo yalimiminika kwa wingi zaidi.

“Mwanangu!” nilimsikia akiniita kwa sauti ndogo yenye kigugumizi.

Sikumbuki kama niliitikia au la.

Wala yeye hakuzungumza neno jingine.

Nilipopata nafasi nilijichopoa toka katika mikono yake na kuingia ndani kwa dhamiri kuu mbili. Dhamiri ya kwanza ilikuwa kuficha machozi, ambayo mie pia yalianza kunilengalenga. Dhamiri ya pili ikiwa kumpata mama ili anifafanulie kisa na mkasa wa hali hiyo.

Mama hakuwepo. Wala hakuwepo mtu wa kumuuliza kwani mimi nilikuwa mtoto pekee katika familia hiyo. Na nilipatikana kwa shida baada ya mama na baba kuhangaika kwa waganga kwa zaidi ya miaka kumi. Hatimaye, walimpata mganga mmoja aliyebobea, ambaye alimtibu mama kwa kuchanganya mitishamba aina ya *Mhusu* na *Mnywanya* ambayo

mama alitakiwa kunywa kwa siku mbili. Siku chache baadaye alitangaza kuwa yu mjamzito. Hapo mganga alimbakilishia dawa na kumnywesha mti uliotajwa kuwa *Sagamba* mara kwa mara hadi nilipozaliwa.

Miaka mingine kumi tayari ilikuwa imepita bila dalili za kupatikana mdogo wangu. Mganga wake alishakufa na hakupata kumwonyesha mtu yeyote miti ile. Hivyo, mimi nilikuwa kama mboni ya jicho kwa baba na mama, ingawa hawakutaka kamwe nijisikie hivyo.

Wakati nikihangaika bila mafanikio kuwaza na kuwazua namna ya kumnyamazisha baba, mara nilimwona mama akirudi nyumbani, huku kafuatana na babu. Kumbe yeye pia alikuwa amehangaika sana kumtuliza baba na kumuuliza kulikoni bila mafanikio. Ndipo lilipomjia wazo la kutembea mwendo wa zaidi ya dakika ishirini hadi kwa babu ambaye kwa bahati alikuwa nyumbani.

Kama kawaida yake, tofauti na watu wengine wote kijijini hapo, babu alikuwa amevaa kaptula yake nyeupe, shati jeupe, soksi nyeupe na viatu vyeusi. Akiwa miongoni mwa watu wengi waliovaa lubega za kaniki, miguu yao ikikanyaga chini, siku zote babu alionekana mtu wa aina ya pekee.

“Kuna nini?” babu alimuuliza mwanawe akiwa ameketi pale nilipoketi mimi muda mfupi uliopita. “Kuna nini?” alirudia na kuongeza, “Nasikia tangu umetoka kuonana na Mwami umerudi unalia. Kuna nini?”

Baba hakujibu mara moja. Alimtazama baba yake kwa muda kabla hajainuka taratibu na kumshika babu mkono. “Ni mambo mazito yalionyipata leo. Twende faragha nikusimulie, ingawa nimekula kiapo cha kutotoa siri hii nje.”

Walikwenda pembeni, mahala ambapo masikio yangu na ya mama yasingeweza kusikia wanachozungumza. Hapo waliteta kwa muda mrefu, baba akizungumza babu akisikiliza. Baadaye, nilimwona babu akicheka na kuzungumza kwa muda kabla hawajarudi na kuketi tena kwenye gogo. Mama alipoona wametulia, aliingia ndani na kuwaletea kibuyu cha togwa ya mahindi. Waliinywa taratibu huku wakiwa kimya.

Nadhani togwa hii ilikuwa kali kwani baada ya muda mfupi nilimwona baba akichangamka huku babu akizungumza kwa sauti ya juu kidogo.

Sikubahatika kupata mtiririko wa maongezi yao. Lakini mawili matatu niliyoweza kudonoa katika matamshi yao yalinifanya nipate hisia kuwa nilihusika kwa njia moja au nyingine na majonzi yao. Imani hiyo ilijengeka zaidi pale nilipomsikia babu akisema kwa sauti ya juu kidogo, “Mjukuu wangu mie! Nadhani mwanangu hunifahamu hata kidogo. Haiwezekani!”

Baba: Lakini wamesema itakuwa siri. Huenda hata mimi mwenyewe hawatanishirikisha.

Babu: Nasema haiwezekani. Enzi za utukufu na uhuru wa kufanya chochote wanachotaka zimepita zamani. Wakithubutu nitahakikisha wananyongwa.

Baba: Watanyongwa kabla au baada?

Babu: Hawawezi kuthubutu!

Mmoja wao alinitupia jicho. Wakabaini kuwa nafuatilia maongezi yao. Wakapunguza zaidi sauti zao na kuendelea kunywa.

Usiku huo babu alinichukua nikalale kwake. “Twende zetu mjukuu wangu. Leo nina hadithi nyingi za kukusimulia, hadithi za kweli ambazo sijapata kumsimulia mtu yeyote.”

Nikiwa na hakika kuwa kwa kiasi fulani mwaliko huo ulitokana na kisa au mkasa nisioufahamu, wa hapo nyumbani, niliafiki kufuatana na babu hadi kwake.

Bibi alinipokea kwa furaha huku akiniita ‘mume’ wake. Akanipa kata kubwa iliyojaa togwa tamu, tofauti kabisa na ile waliyokunywa babu na baba. Baada ya hapo nilipewa ugali na pande kubwa la nyama ya nyati.

Babu alikuwa mwindaji, bibi akiwa mkulima. Nyumba yao katu haikupata kupungukiwa na chakula. Nilikula hadi nikavimbiwa, kabla sijatandikiwa mkeka na bibi kunipa moja ya kaniki zake nitumie kama shuka.

“Tutazungumza kesho, leo pumzika mapema.” Babu aliniambia alipoona dalili za usingizi katika macho yangu.

* * *

Hakuna mtu aliyeujua umri wa babu, ikiwa pamoja na yeye mwenyewe. Ilikadiriwa tu kuwa alizaliwa miaka ya 1850 au baadaye kidogo, kwani wakati huo zilikuwepo habari nyingi za nchi kuvamiwa na watu weupe wenye mianzi inayotoa moshi wenye uwezo wa kuua tembo hata akiwa mbali. Watu hao walidaiwa kutembea hovy katika misitu na kushangaa kwa kila walichokiona.

Miongoni mwa watu hao alitajwa sana mtu mmoja anayeitwa Hanning Speke na mwenzie Richard Burton. Hawa walitembea hadi maeneo yetu ya Buha na kupita na kushangazwa sana pale walipoliona ziwa kubwa la Tanganyika ambalo lilitenganishwa au kuunganisha nchi yetu na zile

za Kongo na Burundi. Inasemekana pia kuwa walitembea porini kwa miezi kadhaa hadi walipofika ziwa Lweru, ambalo walilibadili jina na kuliita Victoria huko katika nchi ya Wahaya na Wasukuma.

Wakati huohuo zilikuwepo habari za mtu mwingine aliyeitwa David Livingstone aliyeweka makazi yake Ujiji na akafia nchini Zambia. Wasaidizi wake maarufu, Susu na Chuma wanaelezewa kuwa waliibeba maiti yake hadi upande wa pili wa nchi, pwani ya Bahari ya Hindi ambako ilisafirishwa hadi kwao Ulaya.

Niliyajua yote hayo kutokana na simulizi za babu mwenyewe. Katika enzi hizo alikuwa tayari ana akili zake, nguvu za kutosha na uwezo wa kuanzisha mji wake mwenyewe, ingawa alikuwa hajaoa. Na ni wakati huo aliopatwa na ule mkasa wa aina yake, mkasa ulioacha gumzo hadi leo, na aliporudi, kimiujiza vilevile kama alivyoondoka, akiwa na simulizi za ajabuajabu, gumzo likaongezeka.

Moja ya maajabu aliyokuja nayo ni mavazi. Nguo zake zilikuwa sawa na zile zilizodaiwa kuvaliwa na watu weupe. Na siku zote alihakikisha kuwa ni safi.

Ajabu ya pili aliyoileta babu ni taarifa kuwa watu weupe kumbe siyo kabila moja bali ni watu wa makabila mbalimbali, wanaotoka nchi mbalimbali na kuzungumza lugha mbalimbali. Alizitaja nchi kama Uingereza, Ujerumani, Sweden, Ureno na nyinginezo kuwa ni nchi tofauti, zenye utawala tofauti na lugha tofauti kabisa.

Ajabu ya tatu, na pengine kubwa zaidi ni pale alipodai kuwa alikuwa na uwezo wa kuzungumza lugha mbalimbali za makabila hayo, kama Kiingereza, Kijerumani na Kisweden. Kwa hilo watu walielekea kutomwamini. Lakini pale Wabelgiji

walipovamia Buha, na kuzunga wakitokea Kongo, miaka ya 1916, babu alidhihirisha uwezo wake wa lugha kwa kuzungumza na mmoja wa makamanda wao waliopotea njia na kujikuta wamefika kijijini kwetu. Wageni hao walishangaa sana kumkuta mtu anayezungumza Kiingereza ambayo ni lugha ya jirani zao katikati ya pori kama hilo. Walijaribu kumshawishi babu afuatane nao ili awe mkalimani wao lakini alikataa katakata kwa kusema, “Nimekaa kwao na kukataa kuwa mtumwa wao, vipi nikubali kuwa mtumwa wao katika nchi yangu mwenyewe?”

Umaarufu wa babu kwa lugha uliongezeka maradufu miaka mitano baadaye, pale Uingereza ilipochukua madaraka ya utawala wa Tanganyika toka kwa Mjerumani ambaye alikuwa pia ameupokonya toka kwa Wabelgiji katika eneo hilo la Buha. Mwaka 1931 chifu, ambaye tulimwita *Mwami* wa Heru juu alifariki. Amri toka kwa Gavana G. S. Symes ilimtaka DC kuteua '*Mwami*' mpya. DC akaamua kupata mawazo ya wananchi kabla ya uteuzi wake. Ujumbe wake ulipofika kijijini kwetu na kumkuta mzee mmoja aliyevaa kama wao, akizungumza lugha ya Kiingereza kwa ufasaha kabisa mara moja babu alipendekezwa kuwa *Mwami*. Lakini kwa mshangao wa wengi babu alikataa cheo hicho katakata. Kwa maelezo yake alidai cheo hicho ni kidogo sana kwa upeo wake na kwamba thamani yake ni sawa na kilemba cha ukoka.

Hicho kilikuwa kitendawili kingine cha babu kwa jamii yetu na kwa Waingereza wenyewe. Kwa kuwa walimhitaji sana, walao kuwa karibu na uongozi ndipo walipomwomba babu amruhusu walao baba akawe *babariki*, yaani mmoja wa wasaidizi wa *Mwami*. Babu alimruhusu.

Uamuzi wa babu kukataa cheo hicho ulipelekea DC

kuteua machifu wengine wa Heru Juu, Kalinzi, Bushingo na Buhambwe kutoka katika makabila ya mbali kama Mmanyema aliyetoka Tabora na mwalimu Mfipa aliyetoka Sumbawanga kuwa machifu wa eneo letu kwa nyakati tofauti.

Simulizi, visa na mikasa ya babu haikuwa na mwisho. Kila siku alikuwa na kitu kipya cha kusimulia, ambacho ama kilishangaza ama hakikuaminika miongoni mwa wasikilizaji wake.

Kwa mfano, alizungumza juu ya vitu kama nyumba ndogo ambazo watu huko Ulaya huzitumia kwa kusafiri umbali mrefu bila kutuma miguu yao wala kuchoka. Pia, alisema kulikuwa na kijumba ambacho alikitaja kuwa kinaitwa gari.

“Uchawi?” mtu mmoja alipata kumuuliza.

“Hapana,” babu alimjibu. “Hayo ni maendeleo tu ya Sayansi na Teknolojia.”

“Sayansi na Teknolojia ndio nini?”

“Ni aina fulani ya elimu na ujuzi.”

Hadithi nyingine ya babu inayofanana na hiyo ni ile ya madai yake kuwa kuna vyombo vingine vikubwa zaidi ya gari ambavyo huruka angani, toka mji hadi mji, au nchi hadi nchi, kwa muda mfupi zaidi, vikiwa vimebeba abiria. Alivitaja vitu hivyo kuwa ni sawa na ndege mkubwa aliyeumbwa na binadamu.

“Huo sasa ndio uchawi wenyewe!” mzee mmoja aliyekuwa akimsikiliza alipata kumwambia. “Nikiwa mdogo mie pia nilipata kuchukuliwa katika ungo na babu yangu hadi pwani ya Tanga. Lakini safari hizo tulizifanya usiku tu, tukiwa tumejifunika sehemu za siri pekee. Kwa bahati mbaya, mpaka nakufa babu hakupata kuniambia siri ya uwezo ule.”

Babu alicheka sana kabla ya kumjibu mzee mwenzake

huyo akisema, “Nafasi ya uchawi inazidi kuwa ndogo katika dunia ya leo ya Sayansi na Teknolojia. Nani atakubali kusafiri usiku tu, tena bila nguo; wala kuiona mashine ya ndege hiyo?”

Utamu wa aina mbalimbali za vyakula, urahisi wa maisha, barabara za juu na chini ya ardhi, magari, ndege na meli kubwa, matibabu ya kisasa na mambo mengine tele ni miongoni mwa simulizi nyingi ambazo wasikilizaji wake walizifurahia sana.

* * *

Naam, huyo ndiye babu yangu, mzee Kionambali Mtukwao, kama alivyofahamika katika eneo lote hilo la wilaya ya Kasulu na vitongoji vyake. Ni babu huyu ambaye siku hiyo niliamka nikiwa nimelala chini, kando ya kitanda chake cha kamba, kilichotandikwa ngozi ya ng’ombe na blanketi nzito iliyoanza kuchakaa, ndani ya nyumba yake ya *tembe*. Niliamka alfajiri, lakini tayari babu alikwishaamka kitambo na kukoka moto nje ya nyumba. Bibi pia alikwishaamka na kuelekea mtoni kuchota maji.

Nikatoka nje na kumsalimu babu. Aliitikia kwa furaha kisha aliniamuru kumkamata jogoo mmoja mweupe na kumchinja ili awe kifungua kinywa cha siku hiyo. Ilikuwa kazi rahisi niliyoipenda sana. Kwa kuwarushia punje mbili tatu za mahindi, huku nikipiga mluzi, kuku wote ambao walishaanza kutawanyika huko na huko vichakani walirejea. Nikaendelea kurusha mahindi kwa karibu zaidi. Dakika mbili baadaye jogoo niliyemtaka alikuwa miguuni mwangu. Nikamdaka mara moja na kisha kumchinja. Bibi aliporudi alianza kumshughulikia mara moja.

Nikaenda mtoni ambako nilioga maji baridi yaliyouchangamsha mwili wangu. Nikasafisha meno yangu kwa mti wa *mdaa* ambao pia ni dawa ya kinywa na meno. Niliporudi bibi alikuwa akimalizia kutenga ugali wa muhogo kwa kitoweo cha kuku wa kuchomwa. Mimi na babu tuliketi mkao wa kula na kuanza kumshambulia jogoo yule ambaye muda mfupi alikuwa akiwika kama mfalme wa mji huo.

Pamoja na utamu wa kuku, pamoja na simulizi nyingi za babu, shahuku yangu kubwa ilikuwa kufahamu kile ambacho kilimfanya baba atokwe na machozi hadharani. Nikijua kuwa ni jambo hilo lililomfanya babu anichukue jana na pengine hata jogoo huyu amechinjwa kuhusiana na kisa au mkasa huo nilistahimili kwa muda nikimsubiri babu azungumze. Lakini babu alikuwa kimya. Chakula kilipokwisha nilitoa vyungu na kuvipeleka ndani. Niliporejea nilimsogelea babu na kumwambia taratibu, “Nadhani ulikuwa na jambo la kuniambia babu.”

Babu alitabasamu na kuruhusu meno yake yote kuonekana, tofauti na wazee wengi wa umri wake ambao walibakiwa na magego machache tu vinywani mwao. “Mbona una haraka mjukuu wangu? Tuna mengi sana ya kuzungumza. Tusubiri kidogo bibi yako aende shamba. Nataka tuzungumze kama wanaume wawili, si mtu na mjukuu wake.”

Kauli ambayo iliniongezea shahuku.

Mara bibi alipochukua jembe lake na kuelekea shambani babu alianza simulizi zake. Ajabu ni kwamba alianza kwa kunirushia maswali badala ya mimi kumrushia yeye.

Babu: Unajua wenzetu walioendelea zaidi huko Ulaya maisha yao ni bora zaidi yetu?

Mimi: Najua, umesema hivyo mara nyingi.

Babu: Umepata kujiuliza nilifikaje huko na kutembea nchi zote hizo?

Mimi: Niliwahi kukuuliza. Unasema ulienda Ulaya kwa ajali.

Babu: ni kwlei. Nilienda kwa ajali.

Babu: mtu kwao mjukuu wangu. Maisha yangu yote ya ugenini sikupata kujisikia.

Babu alisitia kidogo akitafakari jambo. Nikatumia mwanja huo kutumbukiza swali langu badala ya kuwa mtu wa kuulizwa, “Kwa hiyo babu, pamoja na raha zote hizo kwa nini ulirudi? Au kurudi kwako pia ilikwua ajali nyingine?”

Babu: Hapana nilirudi kwa hiari.

Mimi: Kwa nini?

Babu: Mtukwao mjukuu wangu. Maisha yangu yote ya ugenini sikupata kujisikia nyumbani. Baadhi ya mila na desturi zao haziendani kabisa na zetu. Mvulana mkubwa kabisa anamkumbatia mama yake na kumbusu mdomoni! Msichana wa makamo anamvalia baba yake nguo fupi na pengine kumkalia mapajani!

Alisita kabla hajaendelea, “Halafu waliniudhi kwa jambo moja kubwa.

Mimi: lipi hilo?

Babu: La kudharau utamaduni na mila zetu na kuamini zao ndio sahihi. Kwa mfano makabila mengi ya Kiafrika yalimkataza mwanamke mwenye mimba kula mayai au maini kwa visingizo mbalimbali. Lakini walikuwa na sababu kubwa za msingi kabisa.

Mimi: Zipi hizo kama sio uchoyo na uroho?

Babu: (Akicheka) Uchoyo? Kwa kweli ulikuwa ukarimu wa hali ya juu sana. Unajua mwanamke mwenye mimba akila mayai mengi wakati wa ujauzito wake atanenepa yeye na mtoto aliye tumboni pia?

Mimi: Hilo najua.

Babu: Basi kwa hekima za wazee wetu walibuni hila ya kuwatishia hivyo. Ukweli ni kwamba walihofia mtoto akinenepa sana tumboni asingezaliwa. Hatukuwa na vifaa vya upasuaji kama wao. Na hatukutaka kuhatarisha maisha ya mama na mtoto; wazee wetu walikua na hekima sana.

Mimi: kweli uzee ni dawa...!

Babu alisita tena, kama mtu aliyejisikia kichefuchefu kwa mambo yale. Halafu akaendelea, “Si hayo tu. Hata nchi na mazingira yao hayafikii kabisa ya kwetu. Ndiyo, wana barabara kubwa na magari. Ndiyo, wana majengo mapana na bustani za kuvutia. Lakini hawana ardhi nzuri, misitu ya asili, mbuga za kuvutia, wanyama na ndege wa kususimua kama sisi. Wengi wao hawana mito wala maziwa wenye samaki wengi kama yetu. Hata hali ya hewa kwao ni taabu tupu. Zipo nchi zenye baridi kwa mwaka mzima. Ziko zile zenye vipindi vya baridi kali na joto la kutisha katika mwaka mmoja. Sisi tumejaliwa sana.”

Nilimwona babu akitabasamu kidogo na kisha kuangua kicheko. Nikamwuliza kulikoni. “Nitakuambia jambo moja,” alisema akiendelea kutabasamu. “Lakini naomba iwe siri kati yetu. Moja ya mambo yaliyonifanya nitamani sana kurejea nyumbani ni uhuru wa kujisaidia porini. Miaka yote niliyokuwa huko vyoo viko ndani ya nyumba. Ukipanda meli choo, ukipanda treni choo, ukipanda ndege choo. Hata mara moja hupati fursa walao kujisaidia haja ndogo porini, uone faraja ya maji yaliyochujwa na mwili wako yakipokelewa na nyasi za kijani na baadaye kumezwa na ardhi yenye kitovu chako.” Sikuweza kujizuia. Nikaangua kicheko kirefu.

“Hapa tunazungumza kama mtu na rafiki yake. Nitakuambia sababu ya pili iliyonifanya niamue kurejea nyumbani.” Babu aliendelea.

“Lakini babu,” nilidakia, “Shida yangu kubwa ni kujua baba alikuwa analia nini jana. Hayo mengine tutayazungumza baadaye.”

“Tunaelekea hukohuko,” babu alisema. “Ungependa kujua sababu nyingine iliyonirejesha huku?” aliongeza swali.

“Nadhani ningependa kujua.”

“Nina tatizo kubwa. Sijui kusoma wala kuandika.” Babu alitamka ghafla.

Tamko ambalo lilinipiga kwa mshangao kama radi. Babu hajui kusoma wala kuandika! Pamoja na kujua lugha mbalimbali za dunia! Pamoja na kutembea huko na huko. Nilihisi huo ulikuwa utani mwingine wa babu na mjukuu wake.

“Naona huniamini. Sikubahatika kwenda shule. Baba yako vilevile hajui kusoma wala kuandika. Ninachotaka kufanya ni kuhakikisha wewe unapata kile ambacho wazazi wako hatukubahatika kupata. Tunataka upate elimu. Dunia inatawaliwa na kuongozwa na wenye elimu. Siri zote za dunia zimefichwa na kuhifadhiwa katika vitabu.” Aliongeza.

Wakati nikiitafakari taarifa hiyo ya kushangaza nikapambazukiwa na jambo moja. Ili kuhakikisha nikamuuliza babu, “Niambie ukweli babu. Ulikataa cheo cha uchifu kwa ajili ya kutojua kusoma na kuandika?”

“Mjukuu, naona una akili nyingi,” Babu alisema. “Ni kweli kabisa. Chifu gani ambaye atalazimika kupeleka barua kwa mtu mwingine ili asomewe? Ninge kubali, ningeumbuka.”

“Hizo lugha ulizijuaje bila kusoma?”

“Uzoefu. Huwezi kuishi na mtu miaka kumi bila kujua lugha yake. Labda uwe na kichwa cha boga.”

“Na kwa nini hukujifunza kusoma na kuandika?”

“Umri.”

“Umri?”

“Umri ulishapita. Ningeweza wapi mzee mzima kuketi na vitoto vya miaka sita kufundishwa **a e i o u**. Tena wanaokufundisha wakiwa watoto au wajukuu wako?”

Kwa kiasi fulani, nilimhurumia babu. Si kwa kukosa elimu ya vitabuni, bali kwa jitihada alizofanya za kujiweka wazi kiasi hicho mbele yangu hata akatoa siri ambayo naamini hakupata kumwambia mtu mwingine.

“Hawakukulazimisha?” nilimuuliza.

“Nini? Wanilazimishe kusoma? Baadhi yao pia walikuwepo wachache wasiojua kusoma wala kuandika. Wawili watatu walijaribu kunilazimisha kwa kuwatuma watoto wao wanifundishe. Lakini nilijifanya naumwa macho, kwa hila nikajitia vitunguu machoni na kutokwa na machozi kila kitabu au daftari lilipofunguliwa mbele yangu. Wakaniacha nilivyo.”

“Ni hilo la kutojua kusoma hasa lililokurejesha nyumbani?” niliuliza.

“Hilo ni moja wapo. Nisingerudi ningefia hukohuko nikiwa mpishi au mfagizi wao milele. Lakini kuna sababu nyingine”

“Ipi hiyo?”

Babu alikohoa kidogo kabla hajasema, “Ujinga ni mzigo mjukuu wangu. Wale watu waliojifanya wafadhili wangu, kumbe mimi ndiye niliyekuwa mfadhili wao. Walinitegemea mimi ili kupata mkate wao wa kila siku.

“Kwa vipi?”

Kwa sauti ya huzuni kiasi babu alieleza, “Wale jamaa kumbe walikuwa wakinifanyia maonyesho na kupokea fedha lukuki kwa jina langu. Unajua watu wa nchi nyingi Ulaya bado hawajapata kumwona mtu mweusi? Wengine ni wajinga kama wengi wetu tulivyo wajinga kwa kutopata kumwona mtu mweupe.”

“Kwahiyo walinigeuza biashara. Zile safari nyingi za hapa na pale, toka nchi hadi nchi, kumbe zilikuwa za kunifanyia maonyesho. Watu walitoa pesa nyingi ili wamwone *‘nyani mweusi’* anayekula kwa uma na kuzungumza Kiingereza. Kuna wakati niliombwa kuimba, au kualikwa kucheza muziki na wasichana wa Kizungu. Picha nyingi zilipigwa na kuuzwa kwenye vyombo vya habari.”

“Nikiwa nchini Sweden, katika mji mmoja uitwao Jonkoping niliajiriwa na familia moja ya watu ambao walikuwa wakiendesha shamba la wanyama. Wengi kati ya wanyama hao walikuwa wa porini ambao walikamatwa wangali wadogo na kufundishwa ama kuishi na binadamu. Wale wakali kama simba, chui na vifaru walifungiwa katika maeneo maalumu.”

“Ajira yangu kama nilivyoambiwa awali ilikuwa kusaidia kuwatunza wanyama hao. Niliingizwa katika mikataba ambayo sikuielewa na kushawishiwa kuweka dole gumba kwenye karatasi zao kama sahihi. Niliiona kazi rahisi na kuziona mia tatu kila wiki nilizokuwa nikilipwa kama za bure. Lakini nilishangaa pale nilipoanza kuvalishwa mavazi yaliyoandaliwa kitaalamu na kuonekana kama nyani dume. Hayo yalianza pale nyani aliyekuwa shambani humo alipofariki kwa uzee, wamiliki wakaifanya habari hiyo siri kwa hofu ya kupoteza wateja wao waliokuwa wakimiminika kila siku kumtazama nyani huyo anavyoruka toka tawi hadi tawi la miti iliyootesywa shambani humo.”

“Nikaelekezwa kujifanya nyani yule. Kwa kuwa nilikuwa hodari sana wa kupanda miti, kuachia tawi moja na kudaka jingine halikuwa jambo geni kwangu. Niliwafurahisha sana watazamaji, hasa watoto. Nadhani niliwafurahisha zaidi kwa kuwa nilikuwa binadamu nikisoma hisia zao na hivyo kufanya

mengi ambayo hawakuyatarajia.”

“Wajiri wangu walifurahi sana. Muda wote walikuwa na kamera za video ambazo walizitumia kunukuu kila kitendo changu. Baadaye wateja walipoondoka waliendelea kunipiga picha hata wakati navua mavazi yale ya kinyani na kuvaa ya kibinadamu. Mara kwa mara walinihoji vilevile, kwa lugha zote nilizoweza kuzungumza na kunukuu maongezi yangu kwa vinasauiti.”

“Ikaja siku ya balaa. Wakati nikiruka toka tawi hadi tawi la mti uliokuwa juu ya zizi la simba dume ilitokea bahati mbaya nikateleza na kudondokea ndani ya zizi hilo kando kidogo ya simba yule. Nadhani nilipiga ukelele wa hofu, kwani nilijua nimefika mwisho wa maisha yangu. Nilitetemeka zaidi pale simba huyo alipoanza kuninyatia taratibu akinguruma. Wakati nikijiandaa kwa vita ya kuipigania roho yangu nilishangaa kuona simba huyo akiweka kinywa chake kando ya sikio langu na kuninong’oneza, “Usiogope, mimi ni binadamu kama wewe!”

“Kweli? Wewe mtu wa wapi?” nilinong’ona vilevile.

“Mimi ni Mmarekani. Nipo hapa mwaka wa tatu.” Alisema.

“Nilipigwa na butwaa. Lakini walioduwaa zaidi ni watazamaji ambao kwao kitendo cha simba kuteta na nyani kilikuwa muujiza wa pekee. Walitegemea kuona nikiliwa hadharani, badala yake nanong’ona na simba!”

“Toka siku hiyo shamba hilo likawa linafurika wateja. Walitoka miji ya mbali na hata nchi za jirani kuja kushuhudia maajabu ya ‘nyani’ na ‘simba’ waliojenga urafiki.”

Lakini kwangu hiyo ilikuwa siku ambayo niliamua kuacha kazi hiyo. Pamoja na kulipwa fedha nyingi, nilikichukulia kitendo hicho kama udhalilishaji mkubwa.

Hivyo, mara tu nilipopata mshahara wangu wa mwezi huo, ambao uliongezwa mara dufu, nilitoweka.”

Nilicheka sana. Kwangu ilikuwa habari ya kulisimua sana. Ilinisisimua zaidi kumsiki babu, kwamarayakwanza, akisimulia tukio lililomuhusu kwa kirefu kiasi hicho. Mara nyingi yeye alikuwa mtu wa simulizi na kujibu maswali kwa mkatomkato.

Nilikuwa na kila sababu ya kumhurumia babu. Kwa upande mwingine, maelezo yake yalizidi kunithibitishia jambo moja kubwa; umuhimu wa elimu. Lakini mara nikakumbuka kuwa babu alikuwa hajafikia au kugusia kiini cha maelezo hayo. Sababu ya kulala kwangu kwake na kuchinjwa kwa jogoo wake bora kuliko wote; kwa kila hali kulihusiana na majonzi aliyokuwa nayo babu.

Nikamkumbusha hilo.

“Nakumbuka vizuri sana,” Babu aliniambia. “Lakini,” aliongeza. “Kama nilivyosema awali unahitaji kuwa na kifua. Taarifa nitakayokupa huenda ikakutisha au kukuogofya. Lakini unatakiwa kupokea kama mwanamume na kuichukulia kwa upande wa pili kama msukumo wa ufunguo mpya wa maisha yako.”

Niliona kama babu anazidi kunichanganya. Nikamtumbulia macho ya mshangao na kumtegea sikio kwa makini.

“Inabidi uondoke kijijini hapa mara moja,” babu aliniambia ghafla.

Kati ya yote niliyotarajia, hilo la kuondoka halikuwemo katika mawazo yangu, “Nani? Mimi!”

Babu akakubali.

“Kwa nini?”

“Wanataka kukuua.”

Sikuyaamini masikio yangu, “Wanataka kuniua mimi, watu gani hao?”

“Wanakijiji. Wakazi wa eneo hili.”

Bado sikumwelewa babu. Nilihisi huo ulikuwa utani wake mwingine, pengine kwa nia ya kupima ujabari wangu. Ili kumthibitishia hivyo niliangua kicheko na kumwambia taratibu, “Babu acha utani huo. Unanichulia kifo.”

Lakini macho ya babu yalikuwa hayana utani wala mzaha wa aina yoyote alipoongeza, “Wanataka kukutoa kafara. Lazima uondoke haraka iwezekanavyo.”

* * *

Kwa takribani miaka mitatu iliyopita eneo letu lilikumbwa na ukame. Mazao yaliyopatikana yalikuwa machache sana. Mimea mingi ilinyauka, hata baadhi ya vyanzo vya maji vilianza kukauka. Mbaya zaidi ni pale ilipoonekana wazi kuwa mwaka huo pia hakukuwa na dalili ya mvua.

Zaidi ya tatizo hilo la ukame lilikuwepo tatizo jingine kubwa zaidi, tatizo la ugonjwa wa malale. Eneo kubwa la mapori na misitu iliyovizunguka vijiji vyetu ilikuwa na mbung’o wengi sana ambao walidaiwa kusababisha malale. Mbung’o hao walianza hata kuvamia mifugo iliyokuwemo zizini na hivyo kusababisha maradhi ya usingizi na hatimaye vifo vya ng’ombe wengi. Wala haikuwa mifugo pekee. Zaidi ya watu wanane kijijini hapo walikuwa wamekwishakufa kwa malale huku wengine wasiopungua ishirini, wakiugua ugonjwa huo ambao haukusikia dawa.

Kwa mujibu wa babu, *Mwami*, wasaidizi wake na wazee wenye busara kijijini hapo waliketi vikao vingi kujadili namna ya kupambana na matatizo hayo bila mafanikio. Hali

hiyo ilisababisha wachukue uamuzi wa kuomba msaada wa bingwa wa ramli katika eneo hilo. Kwa mujibu wa mtaalamu huyo miungu ilikuwa imekasirika kwa kusahauliwa kwa muda mrefu. Hivyo, ilidai kafara ya damu ya mtu ili iwafukuze mbung'o na kuamuru mvua inyeshe kama kawaida.

Kwa maelezo ya mtaalamu huyo, kafara huyo alitakiwa azikwe hai, usiku wa manane; katikati ya msitu mnene wenye mbung'o wengi. Aidha, mtu huyo alitakiwa awe msichana au mvulana anayetoka kwa baba na mama mwenye mtoto mmoja.

Ni hapo nilipoingia mimi. Katika eneo lote hilo wazazi wangu walikuwa watu pekee wenye mtoto mmoja. Kwa bahati, baba alikuwa mmoja kati ya *babarike* walioteuliwa kufanya mawasiliano na mtabiri yule. Vinginevyo, zoezi hilo lingefanywa kwa siri. *Mwami* na viongozi wengine walimweka kitako na kumtaka apige moyo konde na kumtoa mwanae wa pekee ili kuiokoa nchi na maafa zaidi.

Ni hilo lililomfanya baba arudi nyumbani huku akibubujikwa na machozi. Alikuwa katika mtihani mkubwa wa kuchagua kati ya mwanae wa pekee na ukombozi wa nchi yake ili iondokane na maafa.

* * *

“Nadhani sasa umeona umuhimu wa kuondoka kwako hapa haraka,” babu aliniambia mara baada ya maelezo yake. “Ni sawa na kuua ndege wawili kwa jiwe moja. Utakuwa ukikimbia kifo, wakati huohuo ukiifuata elimu.” Alifafanua.

Nilimsikiliza babu kwa makini. Hata hivyo, moyo wangu ulikuwa mzito sana kwa ukubwa wa suala zito lililokuwa kichwani mwangu. Kwamba watu walikuwa wamekaa vikao na kufikia hatua ya kuamua kunizika nikiwa hai ili wapate mvua!

Haikuniingia kabisa akilini. Ndiyo, siku za nyuma nimewahi kusikia hadithi za aina hiyo. Hadithi za watu, hasa watoto, kutolewa kafara. Lakini sikupata hata mara moja kumfahamu mtu yeyote au mtoto wa mtu yeyote aliyepata kutolewa kafara. Pengine kafara hizo zilitolewa kwa siri? Pengine hilo ndio jibu la hadithi za kutolewa kwa baadhi ya watu kijijini hapo miaka ya nyuma?

Tishio la maisha yangu lilikuwa kubwa. Tishio la kulazimika kuondoka kwangu lilikuwa kubwa zaidi. Mimi, ambaye sijapata kutoka nje ya vijiji viwili vitatu vinavyotuzunguka katika eneo hilo, nitakwenda wapi? *Na nitarudi kweli?* Nilihisi chozi likinitoka na kuteleza hadi kidevuni kwangu. Nikalifuta harakaharaka kuchelea babu asilione. Aliliona. Lakini, kwa mara ya kwanza, hakunishutumu kwa kitendo hicho cha *Mwananume kulia*.

“Najua hiki ni kipindi kigumu sana kwako, mjukuu wangu. Lakini wewe ni mwanamume. Ulitarajia nini katika maisha yako? Uzaliwe hapa, ukulie hapa, ufie hapa? Bahati ya mwanamume iko miguuni mwake. Lazima utoke. Lazima ukatafute elimu ili ubadili maisha yako. Chukulia tishio la maisha yako kama changamoto inayokupa msukumo wa kuondoka hapa haraka zaidi, si vinginevyo.” Babu alinihubiria.

Aliongeza kuwa siku zote alikuwa na nia ya kuhakikisha naondoka hapo kijijini kwenda nchi za mbali kutafuta elimu ya maisha mapya. Lakini wakati ulikuwa haujajiri. “Wakati huo sasa umefika. Huna budi kuacha kijiji na kuikabili dunia.”

“Nitakwenda wapi?” niliuliza ghafla. Hisia fulani rohoni mwangu zikinishangaza. Nilihisi kama ambaye nilikuwa tayari nimeridhika na maelezo yake na kuanza kujenga shahuku ya kuifanya safari hiyo mara moja.

“Swali zuri sana,” babu alinijibu. “Ni swali ambalo nilikwishalifikiria kwa muda mrefu na kulipatia ufumbuzi. Utaelekea kaskazini, katika nchi ya Wahaya. Huko Wazungu wanaotangaza dini yao, tayari wamejenga shule na wanapokea watoto na kuwafundisha kusoma na kuandika.”

Nitafikia kwa nani? Nitakula nini? Nikiugua atanisaidia nani? Ni miongoni mwa maswali lukuki ambayo yalijaa katika kichwa changu. Nilitamani kumuuliza hayo babu, lakini nilisita kwa kujua kuwa angeyapuuza mara moja. Si alikwishaniambia kuwa bahati ya mwanamume iko miguuni mwake? Nikapiga moyo konde na kufikia uamuzi. *Lazima niondoke.*

Babu aliusoma uamuzi wangu katika macho yangu. Akatabasamu. Kisha akasema, “Wewe ni mwanamume. Siku zote nilijua kuwa mwanangu amezaa dume la simba. Kazi iliyobaki sasa ni maandalizi ya safari yako. Si unafahamu kuwa tunataka iwe siri?”

* * *

Kuagana na wazazi wangu lilikuwa jukumu zito kuliko nilivyodhania, hasa ukizingatia kuwa zoezi hilo lilikuwa la ghafla sana na lilifanyika kwa siri sana. Mara tu baada ya maafikiano yangu na babu tulirejea nyumbani ambako babu alimweleza mwanae uamuzi wangu. Baba hakuwa na hiari ingawa aliipokea habari hiyo kwa majonzi makubwa.

Tatizo kubwa lilikuwa kwa mama. Kwanza, hakuamini masikio yake. Kulikuwa na mpango wa mtoto wake wa pekee kutolewa kafara kwa siri. Hilo la kuondoka kwangu pia kwake lilikuwa pigo jingine. Mama alichukulia safari yangu sawa na kifo changu. Aliangua kilio cha kwikwi, huku akisema, “Sikubali mwanangu aondoke. Sikubali kabisa.”

Babu na baba walimsihi aache kulia na kisha kumfahamisha umuhimu wa kuondoka kwangu. “Ataokoa maisha yake na atapata elimu.” Walimwambia.

“Nani atampikia chakula? Akiugua nani anajua dawa zake? Akifa huko tutajuaje?” Mama aliendelea kulalamika. “Sikubali! Labda niondoke na mwanangu!”

Ilichukua muda mrefu kumshawishi mama. Aliporidhika alinitemea mate kwenye paji la uso kuniombea baraka, “Mwanangu, Mtukwao, nenda salama, urudi salama. Kumbuka wazazi wako tupo na tunakupenda sana. Usitusahau asilani.” Alisema huku akiwa ameweka mkono wake wa kushoto kifuani mwangu.

Nilishindwa kujizuia. Machozi yalinitoka.

Hakuna aliyenishutumu.

SURA YA PILI

Porini... Ana Kwa Ana Na Simba.

Safari ilianza alfajiri sana, yapata saa tisa au kumi hivi. Nyasi na majani yalijaa umande mwingi ambao ulifanya tulowe chapachapa, dakika chache tu baada ya safari. Kiza pia kilikuwa kimetanda huko na huko kuongeza ugumu wa safari. Kwa kweli, mimi sikujua kama tunaelekea upande upi; mashariki au magharibi, kaskazini au kusini. Nilichofanya ni kumfuata babu ambaye alikuwa mbele yangu, akitembea kwa ule mwendo wake mkali, wa hatua ndefundefu ambao mara nyingine ulifanya nitembee huku nikikimbia ili niwe naye sambamba.

Babu alikuwa amejitolea kunisindikiza hadi atakaponiacha katika mikono salama. Uamuzi wake, kwa kuzingatia umri wake na urefu wa safari, ulipingwa sana na baba. Lakini haikuwepo njia nyingine. Babu alionya kuwa umri wangu haukuniruhusu kusafiri maporini peke yangu. Hali kadhalika, alichelea kuwa kama baba angetoweka kijijini hapo pamoja na mimi ingekuwa dhahiri kuwa amenitorosha, jambo ambalo lingemlelea matatizo makubwa na wanakijiji wenzake. Zaidi, kwa kuwa babu alijua lugha mbalimbali za kigeni aliamini kuwa wamisheni wenye shule wangemsikiliza kwa makini zaidi na kunipokea, kwani shule nyingi alisema zimejengwa kwa ajili ya watoto wa Machifu.

“Lakini kuna sababu nyingine. Kwa umri wangu huu huenda mjukuu wangu atakaporudi hatanikuta nikiwa hai, wakati bado nina mengi ya kumfundisha. Hivyo, katika safari yetu ndefu nitapata wasaa wa kumrithisha hiki na kile ambacho kitamfaa katika maisha yake.” Babu aliongeza hoja ambayo si baba wala mama aliyeipinga.

Usiku huo wa kuamkia safari sikupata usingizi. Kichwa changu kilijaa maswali mengi pasi ya jibu hata moja. Kiwingu cha hofu kilitanda katika fikra zangu kiasi kwamba hata nilipopata lepe dogo la usingizi, ulikuwa wa mang’amung’amu; ukiambatana na ndoto za kutisha. Hali hii ilisababisha nikurupuke mara kwa mara na kukodolea macho kiza kilichotanda chumbani humo.

Kitu kingine kilichonikosesha raha ni mlilo wa bundi. Katikati ya usiku bundi mmoja alitua juu ya paa la nyumba yetu na kuanzisha kile kilio chake chenye sauti mbaya ya kutisha. Hakuna mtu ambaye hakujua kuwa bundi kukesha katika mji wako akilia ni dalili mbaya. Mara nyingi huashiria msiba au nuksi itakayoipata familia hiyo. Hivyo, wakati babu aliponiamsha na kuninong’oneza ‘tuondoke’ hata kabla jogoo hajawika nilianza safari nikiwa na moyo mzito sana.

‘Kwa heri Buha.... Kwa heri Kasulu... Kwa heri Heru...’ nilihisi moyo wangu ukinong’ona wakati nikichukua furushi langu dogo, lenye ngozi, kipande cha kaniki na akiba ya chakula njiani. Nje ya nyumba babu alikata fimbo mbili toka kwenye matawi ya miti na kunipa moja. Sikuhitaji kuambiwa kazi ya fimbo hizo. Zilitumiwa kupiga majani ya mbele yako kwa ajili ya kupunguza umande. Fimbo hizo hazikufua dafu kutokana na ukubwa wa pori ambalo katika sehemu fulanifulani nyasi zilitumeza kabisa.

Tulimsikia jogoo wa kwanza akiwika toka mbali baada ya mwendo wa dakika zipatazo arobaini hivi. Muda mfupi baadaye jogoo wengine walianza kuwika toka huko na huko wakiashiria mapambazuko. Hawa walifuatiwa na milio ya ndege wa alfajiri toka katika matawi ya miti mbalimbali. Muda mfupi baadaye dalili ya mapambazuko zilijidhihirisha zaidi. Hali ya hewa ilibadilika kwa namna fulani na kiza kuonekana kama kimetamalaki zaidi. Kisha, mashariki ilianza kubadilika na miale yenye rangi ya dhahabu kuanza kuchomoza toka nyuma ya vilima na mti toka mbali.

“Kumekucha,” babu alisema taratibu.

Nadhani hakutarajia jibu. Hivyo, sikumjibu chochote. Nilichofanya ni kuongeza hatua zangu ili kuwa naye karibu zaidi.

Jua lilichomoza kwa maringo, hatua baada ya hatua. Tahamaki miale yake murua yenye rangi ya dhahabu ilianza kupenya na kuifikia miili yetu ambayo ilikuwa taabani kwa baridi. Taratibu joto la miale hiyo lilikausha umande katika miili yetu na kuifariji. Nilijihisi nikichangamka si mwilini tu, bali pamoja na moyoni pia.

Nadhani babu alichangamka pia kwani nilimwona akitabasamu na baadaye kusema taratibu, “Jua ni Mfalme, unajua kuwa nchi nyingine huko Ulaya waliabudu jua na kulichukulia kama Mfalme wao?”

Sikumwelewa. Wakati bado natafakari kauli yake hiyo aliongeza nyingine, “Unajua huko Ulaya kuna nchi ambazo huwa hawalioni jua kwa karibu mwaka mzima?”

Babu alinichanganya zaidi.

“Sasa wanaishije bila jua?” nilimuuliza.

“Wanaishi kwa kuvaa makoti makubwa na

kujifunika mablanketi mazito. Mchana na usiku wanakoka moto majumbani mwao kutafuta joto.” Alieleza. Kwajinsinilivyomfahamubabunilijua baadaya kuchangamshwa na jua hilo amepata nguvu na kuanza hadithi zake zisizo na mwisho. Nilikuwa nimechoka. Nilikuwa tayari najisikia njaa. Nilichelea kumjibu kungemfanya aongeze hadithi nyingine. Nikakaa kimya nikifikiria namna ya kumwomba tupumzike kidogo.

Kana kwamba alikuwa akiyasoma mawazo yangu babu mwenyewe alishauri tupumzike. Nilishukuru kimoyomoyo.

Nikamwonyesha babu mbuyu mkubwa wenye kivuli mwanana na kumtaka tukapumzike pale. Babu alitikisa kichwa kukataa. “Mbuyu sio mti mzuri sana wa kukaa chini yake. Unajua mbuyu unaishi maisha marefu pengine kuliko miti yote duniani? Mara nyingi mizimu na mashetani pia hufanya mibuyu makazi yao. Jitahidi kuiepuka.” Babu alinielesha na kunishauri.

Haikuwa hadithi mpya kwangu. Mara kwa mara tulikuwa tukionywa kucheza chini ya mibuyu na hasa kuingia katika mapango makubwa ambayo huchimbika katika mashina ya mibuyu mikongwe zaidi. Tunaambiwa humo wanaishi majini au mashetani katika sura mbalimbali. Pia tunaambiwa kwamba baadhi ya viumbe hai huonekana katika sura ya nyoka, ndege au wanyama wengine.

Tulitembea zaidi ya dakika tano nyingine kabla hatujafikia eneo lililozagaa mivule mingi na kufanya kuwe na kivuli kikubwa. Tuliketi juu ya magogo ya miti iliyokufa na kuifungua akiba yetu ya chakula. Tulikuwa na mihogo ya kuchemsha, ndizi, nyama kavu ya nyati na ugali wa lowe. Tulikula kimyakimya, ndege wadogo wakitumbuiza kwa

nyimbo zao tamu toka kwenye matawi ya miti hiyo. Baadhi ya ndege hao, tetere na kitororo, waliruka juu yetu mara kwa mara kama wanaotushangaa kwa kuwepo kwetu pale. Muda mfupi baadaye kundi kubwa la tumbiri lilivamia miti hiyo na kuanza kuruka toka tawi hadi tawi juu ya vichwa vyetu kwa namna ya kutudhihaki

“Dalili njema.” Babu alisema. “Safari yetu itakuwa nzuri,” aliongeza.

Nikaona huo ulikuwa wasaa muafaka wa kutoa dukuduku langu. “Lakini babu,” nilimwambia. “Mbona usiku wa leo bundi amekesha akilia juu ya paa la nyumba yetu? Si wanasema bundi kulia juu ya nyumba usiku ni ishara ya balaa?”

Babu alitafakari hilo kwa makini. Baadaye alisema, “Bundi ni ndege wa usiku. Haoni mchana ndio maana kutwa nzima hushinda amelala. Usiku hutoka na kuanza mawindo yake. Anapenda kula panya na ndege wengine wadogowadogo. Kuna imani nyingi juu ya bundi katika makabila na mataifa mbalimbali. Kwa mfano, wakati huku kwetu wengi tunamchukulia bundi kama nuksi, nchi nyingine huko Ulaya bundi akikesha analia kwenye nyumba yao wenyeji hufurahi sana na hata kufanya sherehe. Wao wanakichukulia kitendo hicho kama dalili ya neema.”

Ilikuwa habari mpya kwangu, “Umejuaje yote hayo babu?” nilimuuliza.

“Kutembea mjukuu wangu, wanasema, *‘kutembea ni shule.’* Halafu kuna wale waliosema. *‘kuishi kwingi ni kuona mengi.* Mimi nimetembea sana, halafu nimekula chumvi nyingi.”

Kwa muda tuliendelea kula kimyakimya. Tulipotosheka tulifunga vibuyu vyetu ambavyo bibi alituandalia maziwa ya ng'ombe kwa ajili yangu na togwa kwa ajili ya babu. Tukanywa taratibu huku tukiwa tayari tumewapuuza ndege waliokuwa wakicheza juu ya vichwa vyetu. Nadhani baadaye nao pia walitupuuza kwani walishika hamsini zao na kuendelea na shughuli zao kana kwamba hatupo.

Babu alishauri tupumzike kidogo chini ya mti huo, uamuzi ambao niliupokea kwa mikono miwili. Nikajinyoosha chali, juu ya majani makavu na kuyafumba macho yangu kwa matarajio ya kupumzika kidogo. Kwa mshangao usingizi mtamu ukanipitia. Ama babu pia alilala, ama aliamua kuniacha nilale kwani nilipofumbua macho tena ilikuwa jioni, jua likielekea kuzama. Babu alikuwa kaketi palepale akinitazama.

“Umepumzika vya kutosha,” Babu aliniambia. “Tuendelea na safari. Leo ningependa tulale karibu na Makere, kesho jioni tuamkie Mto Malagharasi na kulala Nyakisogo ili ikiwezekana keshokutwa tufike Kibondo.”

* * *

Laiti babu angejua ratiba aliyopanga ingetibuliwa mara moja, bila shaka asingefuata njia hiyo tuliyokuwa tukiifuata.

Ratibayake iliharibika keshoyake tu, wakati tukiukaribia Mto Malagharasi. Tulikuwa tumejipumzisha chini ya mti, baada ya kula na kunywa maji safi toka katika kimojawapo cha vijito vingi vilivyokuwa vimetapakaa katika eneo hilo, vijito ambavyo kwa ajili ya ukame vingi vilianza kuonyesha dalili ya kukauka.

Mara tulisikia mlio wa bunduki, ukifuatiwa na vilio na kelele za watu wanaolia au kukimbia kwa hofu. Babu

aliniamuru kupanda mti mara moja kwa nia ya kujificha. Yeye pia akapanda mti huo. Tulienda hadi kwenye matawi ya juu na kutulia huku tukiangalia purukushani toka mbali. Tuliwaona watu wapatao kumi wakiwa wamefungwa mikono wawiliwawili, wakiongozwa na watu waliovaa kaptula za kaki na viatu vizito. Hawa walishika marungu. Nyuma yao kulikuwa na watu weupe wawili waliobeba bunduki.

Watu hao walipofika chini ya mti na kuona mizigo yetu hawakuangaika kututafuta. Walitupa macho yao juu na kutuona tulivyoning'inia kwenye matawi kama nyani.

“Shuka chini.” Mmoja wao aliamuru kwa sauti kubwa.

Nilimtazama babu kwa hofu. Nikamwona akianza kushuka taratibu. Nikamfuata. Tulipofika chini tuliamriwa kukaa chini pamoja na wale mateka wengine, amri ambayo babu alikataa.

“Nyie nani?” aliwauliza watu hao ambao walikuwa bado wameduwaa kwa kitendo chake cha kugomea amri yao.

“Huoni kama sisi ni askari?” wale askari weusi walijibu. Mmoja wao aliongeza, “Wale pale ni maafisa wa kodi.” Alielekeza kidole chake kwa Wazungu waliokuwa wakitazama zoezi hilo kana kwamba haliwahusu.

“Enhe! Mkiwa askari kwangu mnataka nini?” babu aliwahoji tena.

“Tunakamata watu wote wanaoishi juu ya miti kama tumbili,” mwingine alijibu.

Babu: Kwa nini?

Askari: kwasababu watu wanaoishi juu ya miti ni wale ambao hawajalipa kodi.

Tuonyeshe kipande chako cha kodi.

Hadi hapo nilijua mambo yameharibika. Babu alikuwa

mbishi sana katika suala la kodi. Kama nakumbuka vizuri hakupata kulipa kodi hata mara moja. Kila ulipofika msimu wa kodi yeye alibadilika na kuwa mkali kama pilipili. Ilifikia hatua askari wa kodi walimkwepa na kumkimbia kwa ukali na ubishi mwingi aliokuwa akiutoa kiasi cha wao kujiona wapumbavu mbele yake.

Nilimwona babu akitabasamu. Kisha aliuliza, “Kodi hiyo nimlipe nani?”

Askari: Unailipa serikali ya Uingereza. Ni amri halali ya Malkia. Wale pale ni wawakilishi wa Gavana.

Babu alicheka tena. “Majuzi,” alisema “Walipita Waarabu wakikamata watumwa na kuwauza kwa kisingizio cha kodi. Baadaye walikuja Wabelgiji na kuanza kudai kodi. Siku chache baadaye tukawaona Wajerumani. Wao pia walitudai kodi kwa jeuri na ukatili mkubwa. Leo tunaambiwa ni zamu ya Waingereza. Na nyie weusi kama mimi, ndio mko mbele kunidai kodi! Vichwa vyenu vinafanya kazi kweli nyie?”

Askari hao waliduwaa. Mmoja alikasirika na kuinua rungu lake tayari kumtwanga nalo babu kichwani. Mmoja wa askari wa Kizungu, aliyelekea kuvutiwa na mdahalo huo alimzuia askari huyo na kisha yeye mwenyewe kumkabili babu, “Weye iko nani?” alihoji kwa Kiswahili chake kibovu.

Askari huyo alipigwa na butwaa pale babu alipomjibu kwa Kiingereza fasaha, “Mimi ni raia wa nchi hii. Nimekaa kwenu nikawalipa kodi. Nimerudi kwetu mnataka niwalipe kodi! Tena mnadai kwa mtutu wa bunduki kama majambazi! Sijawahi na wala haitanitokea kamwe kumlipa kodi mgeni!”

Wazungu wale walipigwa na butwaa, kitendo ambacho yule askari mweusi, mwenye jazba, alikitafsiri kitendo hicho

kuwa ni kashfa kwa maafisa hao. Bila subira wala simile aliinua rungu ili ampige nalo babu kichwani. Lilikuwa kosa ambalo askari huyo atalijutia milele kwani babu alimkwepa na hapohapo kumpiga ngumi tatu za usoni ambazo zilimfanya askari huyo ateme mate yenye damu na jino lake moja. Pua yake pia ilitokwa na damu nzito. Askari wa pili alipotaka kuingilia kati Wazungu wale walimzuia. Badala yake walimkodolea babu macho ya mshangao mkubwa zaidi. Kwa umri wake, hawakuamini kuwa babu angeweza kuwa mwepesi na mwenye nguvu kiasi kile.

“Wewe ni nani?” walimuuliza tena taratibu.

“Naitwa Kionambali, Mtukwao.”

“Unatoka wapi, unakwenda wapi?”

“Natoka Buha. Nakwenda nchi ya Wahaya.”

“Unajua kutolipa kodi ni kosa kubwa? Unajua kumshambulia mtumishi wa Malkia ni kosa kubwa zaidi?”

Babu hakujibu.

“Unajua adhabu ya makosa yako? Kwa umri wako huo unajua kuwa tukikupeleka jela utafia huko na kupigwa viboko vitano kila siku ya uhai wako gerehani?”

Babu hakujibu vilevile.

“Mfungeni mikono,” mzungu huyo alitoa amri. Babu alipotaka kuanzisha vurumai jingine mzungu huyo aliinua bunduki na kufyatua risasi moja hewani. “Risasi ya pili hapana kwenda hewani. Takwenda moja kwa moja katika kifua yako.” Alionya.

Babu alinywea na kuruhusu mikono yake yote miwili ifungwe kwa pamoja.

“Twende,” Mzungu huyo alimsukuma babu kwa tako la bunduki yake.

Babu aligeuka kunitazama. Kisha alimgeukia Mzungu yule na kumuuliza “Mjukuu wangu nitamwacha na nani?”

“Hapana kazi yetu,” Mzungu alimjibu kikatili. “Taishi kwenye miti kama nyama. Takula matunda ya porini kama ndege. Kama nachoka tarudi nyumbani yenu.”

Babu alipojaribu kubisha tena yule askari aliyeumizwa aliitumia fursa hiyo. Alimpiga babu kichwani kwa rungu lake kwa nguvu zake zote. Babu aliopesuka na kuanguka chini. Damu nyingi zilimtoka kisogoni.

Sikuweza kuvumilia. Nilikurupuka na kumvamia yule askari kwa nia ya kumpiga tumboni. Aliniwahi. Akanipiga makofi makali na kunisukuma. Nilipesuka na kumfuata tena. Safari hii alinipokea kwa rungu la kichwa ambalo lilinifanya nipoteze fahamu na kudondoka chini kama mzoga

* * *

Sikumbuki nilipoteza fahamu kwa muda gani. Nadhani ilikuwa zaidi ya saa sita. Ninachokumbuka ni pale nilipokurupuka baada ya kupatwa na hisia za hatari. Kitu kama kishindo au mlio fulani ndio ulionizindua ghafla. Kweli. Mara nilipoinuka niliona kitu au mnyama fulani mkubwa akiruka na kukimbia. Tukio hilo lilifuatiwa na kicheko au kilio cha kuogofaya.

Fisi!

Wala hakuwa fisi mmoja. Milio yao iliashiria kuwepo kwa fisi wengi katika eneo hilo. Bila shaka walikuwa wakininyemelea kwa matumaini kuwa ningekata roho ili waule mzoga wangu!

Nilipatwa na hofu kubwa. Fisi ni mnyama mwoga lakini mwenye nguvu nyingi. Taya na meno yake pia yana nguvu sana kwani mifupa uliomshinda yeye hakuna mnyama mwingine

anayeuweza. Fisi huenda kushambulia wanyama wadogo au wagonjwa, ingawa mara nyingi uwa yuko nyuma ya simba akisubiri aue mnyama, amle ili yeye aambulie mabaki. Fisi ni mnyama mvumilivu pia. Anaweza kumfuatilia, mnyama au binadamu mgonjwa hata kwa siku tatu atakapoishiwa nguvu ili amle.

Sikuwa tayari kufanya mzaha na fisi. Mara moja nilitafuta mti uliokuwa karibu na kuuparamia. Pamoja na kiza totoro kutanda huko na huko niliufahamu mtu huo kuwa ni uleule ambao muda mfupi mimi na babu tuliutumia kujificha. Nikapanda hadi mahala penye tawi zuri ambapo niliweza kulala chali, nikajipumzisha. Ni hapo nilipopata wasaa wa kusikiliza maumivu makali niliyokuwa nayo toka kichwani, pale rungu la askari yule liliponipiga barabara.

Aidha, ni wakati huo nilipoweza kutafakari kwa kina masaibu yaliyonipata. Sikujua babu amepolekwa wapi. Sikujua kama alikuwa hai au tayari ameuawa. Sikuwa na hakika kama nitamwona tena mzee yule mwenye mengi ambayo nilitegemea hadi mwisho wa safari yetu awe amenichotea kiasi fulani, mzee niliyemchukulia kama fimbo au kitendawili ambacho kimetoweka kabla ya kuteguliwa.

Machozi yalinitoka.

Nikajifikiria mimi mwenyewe jana tu niliishi raha mustarehe kwa baba na mama leo nimekuwa yatima katikati ya msitu mkubwa wenye hatari zote. Sikujui ninapokwenda wala ninapotoka. Hata kama ningeweza kurudi nyumbani hatari ya kifo bado inanisubiri. Kuendelea na safari niliona ni kifo vilevile. Sikuwa mwerevu wa kutembea porini. Sikuwa na chakula. Zaidi ya yote sikujua njia. Sikujua kama nilipaswa kuelekea kushotoa au kulia, nyuma au mbele.

Machozi yalinitoka.

Sikuthubutu usingizi unipitie. Hofu ya kudondoka toka juu ya mti huo ni moja ya sababu zilizoinyima usingizi. Milio ya kuogofya ya ama wanyama wa porini ama ndege na wadudu wengine ni sababu ya pili. Lakini sababu kubwa zaidi iliyochangia kupaisha usingizi wangu ilikuwa mawazo tele yaliyojaa kichwani mwangu. Kwa kweli mawazo hayo yalinizidi kimo na hata umri. Iwapo ilinipasa kurudi au la iwapo ningeweza kuijua njia ya kurudi au la! Na kadhalika na kadhalika.

Hofu yangu iliongezeka maradufu, nusura nipige kelele pale nilipopata hisia za kitu kama mnyama au nyoka anayepanda taratibu juu ya mti huo. Huku nikitetemeka niliyakaza macho yangu kwa nguvu zote ili niweze kuona kitu hicho. Hofu yangu kubwa ilikuwa ya chui, mnyama ambaye anapenda sana kujificha juu ya mti wakati akiwinda. Aina fulani ya chatu pia wana tabia ya kuparamia miti na kujipumzisha juu ya matawi. Nilihisi maisha yangu yamefikia ukiongoni, kwani yeyote kati yao, angenishambulia ama kwa hofu ya kunikuta huku ama kwa njaa.

Kitu hicho kiliendelea kupanda juu, taratibu na kimyakimya kama kivuli. Nilianza kupapasa huku na huko kwa matarajio ya kupata tawi la mti lililokatika ili nilitumie kujitetea katika kupigania roho yangu. Sikupata. Akili fulani ikanishauri nijitetea kwa kukitisha kiumbe hicho kwa sauti. Nikakohoa kwa nguvu. Kwa mshango wangu kiumbe huyo alikohoa kwa sauti ya binadamu. Sikuyaamini masikio yangu. Nikakohoa tena.

Kitendo hicho kilifuatiwa na sauti ya binadamu iliyoita taratibu, “Mtukwao?”

Ilikuwa sauti niliyoifahamu fika, sauti ambayo

sikutarajia kuisikia tena katika maisha yangu!

“Babu,” niliita kwa sauti ya chini vilevile.

“Naam,” alinijibu.

Nilitamani kupiga ukelele wa furaha. “Umerudi? Wamekuachia?”

Nilimsikia babu akicheka kabla hajasema, “Wale ni watoto wadogo. Msitu huu ni wetu na ni mkubwa sana kwao. Umejaa miti na miti. Kwao kila mti ni mti. Kwangu mie kuna miti na mitishamba. Liko jani dogo tu, ambalo nimelichuma na kulitafuna, wakawa hawanioni wala hawanikumbuki tena. Nimewaacha wakihangaika ovyo, wasipoangalia hata njia ya kurudi walikotoka hawataiona.”

Zamani kidogo nilikuwa nikishangazwa na vitendo na simulizi za babu. Lakini baada ya kuishi nae kwa muda mrefu nilikoma kushangazwa naye. kila alilofanya, kila alilosema, nililichukulia kama lilivyo. Kwa mfano, sikuwa na uhakika iwapo ujio wake huo kweli ulitokana na ujuzi wake wa mitishamba au wa watekaji wake walikuwa wamwachie kutokana na ukubwa wa umri wake. Kwa kweli, sikujishughulisha kutafuta ukweli. Sikuwa na nafasi. Moyo wangu ulikuwa umefura kwa furaha ya kumwona tena. Matumaini ya kuendelea na safari yetu.

Nilitamani kushuka chini, ili nikutane naye na kumkumbatia. Lakini kana kwamba anayasoma mawazo yangu nilimsikia akisema, “Lala kama uko mahala pazuri. Kesho tutaanza safari mapema sana. Wale wajinga tayari wametuchelewesha sana.”

Sikuweza kulala.

* * *

Safari ilianza mapema kama ilivyokusudiwa. Tulishuka kwenye mti huo alfajiri sana, wakati kiza bado kimetanda. Tukakata miti ya kupunguzia umande na kujitoma tena katika vichochoro, katikati ya pori. Nilimfuata babu mgongoni mwake kiasi nikitetemeka kwa baridi kwa kweli sikujua tunaelekea upande gani wa dunia.

Aidha sikujua kama tunakwenda mbele au tunarudi nyuma.

Ilikuwa safari ngumu kuliko ilivyoanza. Akiba yetu ya chakula na maji ya kunywa ilikuwa imetoweka. Bila shaka vifurushi vile vikiwa vimeporwa na fisi au mbweha ambao walikesha chini ya mti ule tuliolala wakirandaranda huku na huko kwa matarajio waliyoyafahamu wao. Hata blanketi langu na nguo za babu za kubadili pia zilikuwa zimetoweka lakini kilichomsikitisha zaidi babu ni rupia zake kumi zilizokuwa ndani ya mzigo huo. Zilikuwa zimepotea pia.

Pamoja na kuficha hisia, zake niliweza kumsoma babu kuwa hana raha kabisa. Ile hamasa ya safari tuliyoanza nayo ilikuwa imetoweka tangu alipozita futa pesa zake bila mafanikio. Hata hivyo hakutamka neno lolote la kunung'unika zaidi ya kunihimiza niongeze mwendo kila alipogeuka na kubaini kuwa ameniacha hatua nyingi nyuma.

“Tutakula nini?” Nilimchokoza kwa nia ya kuanzisha maongezi.

“Msitu huu unawalisha ndege wasio na mikono na wanyama wasio na akili za kutosha. Itashindwa kutulisha mimi na wewe?” Alinijibu kwa swali jingine.

Wakati jua linachomoza tulikuwa tuko mbali sana. Jua lilileta neema kwa kutuzawadia nuru. Pia lilituondolea umande toka kwenye matawi ya miti yaliyotufunika. Lakini

neema hiyo haikudumu. Muda mfupi baadaye jua liligeuka kero. Lilisababisha joto kali kiasi cha kufanya miili yetu iliyokuwa ikitetemeka kwa baridi, muda mfupi baadaye ilianza kuloa kwa jasho. Nadhani jua pia lilileta njaa na uchovu. Nilitamani kumwambia babu tupumzike. Nikasita. Nilimwona kama mtu aliyekuwa mbali kimawazo ambaye hangefurahia kubughudhiwa kwa wakati huo.

Hata hivyo, tulipofika kwenye mti mmoja wenye matunda ya porini, ambayo sikubahatika kuufahamu jina babu alisimama. Akanyoosha mkono na kuangua tunda moja lililoiva akalila. Nilifuata mfano wake. Matunda ya karibu yalipopungua niliamua kuyafuata hukohuko juu ya mti.

Tulikula kefu yetu. Kisha tukaendelea na safari. Huku mbele tulipata kijito chenye maji murua ambayo tuliyatumia kwa kunywa na baadaye kuoga. Tulipumzika chini ya kivuli cha miti mingi iliyoneemeka kando ya kijito hicho kwa muda kabla ya kuendelea na safari yetu.

Sikumbuki tulitembea maporini humo kwa siku ngapi. Wala sikumbuki idadi kamili ya matukio tuliyopambana nayo na yepi yalikuwa ya kutisha, yepi ya kucheakesha na yepi ya kusionua. Nilichokumbuka ni kwamba ilikuwa safari ndefu, ngumu na ambayo iliambatana na kila aina ya visa na matukio. Baadhi ya matukio hayo yalikuwa ya kusionua yaliyoripa ari ya kuendelea na safari.

Kwa mfano, lilikuwepo tukio la kukutana ana kwa ana na simba dume. Siku hiyo babu aliapa kuwa lazima tule nyama badala ya matunda na mizizi kama ndege. Alitafuta vichochoro vya wanyama na kujificha kando ya kimojawapo huku mkononi akiwa na pande kubwa la gogo. Haikuchukua muda mrefu kabla hajapita nguruwe mwitu katika uchochoro huo. Babu

hakuwa amejitayarisha vizuri. Hivyo, aliporusha gogo lake kwa nia ya kupiga kichwa cha mnyama huyo, alikosea shaba. Gogo lilianguka kando ya kichwa hicho. Nguruwe alikurupuka na kutimua mbio kali. Nilishangaa kuona babu akiokota gogo lake na kujificha palepale akitazama kwa makini upande alikoelekea mnyama yule.

Babu aliusoma mshangao wangu. Akacheka kidogo kabla ya kusema, “Atarudi njia hiihii. Nguruwe ni mnyama wa ajabu. Nadhani ana ubongo mdogo kuliko wanyama wengine wote. Huko mbele atachoka. Atakapojipumzisha usingizi mzito utamchukua. Akiwa amelala ataota ndoto ya tukio hili la leo. Ataliona kama la miaka mingi sana. Ataona kwamba aliwahi kupita njia fulani. Akakurupushwa na kitu fulani. Atakuwa hakumbuki ni kitu gani. Hivyo, atakapoamka ataamua kurudi njia ileile ili akaone kitu gani kilichomkurupusha. Hivyo ndivyo ambavyo wawindaji huwapata nguruwe kwa urahisi. Wanachokihitaji ni subira tu.”

Nilitamani kucheka. Lakini kwa kuhofia sauti ya nguruwe ingefichua maficho yetu, nilikaa kimya nikiutafakari ubongo wa nguruwe.

Kweli! Haikupita muda mrefu tulimwona nguruwe yuleyule akirudi njia ileile kwa kasi ileile. Nilimwona babu akiwa ameshangaa. Bila shaka alitarajia nguruwe yule aje taratibu, alitazama huko na huko kutafuta kulichomkurupusha mwaka jana. Safari hii babu alikuwa amejiaandaa. Pigo la gongo lake lilitua barabaraba juu ya kichwa cha nguruwe. Nguruwe akapepesuka na kisha alianguka chali huku akirusha miguu yake huko na huko katika harakati za kuzuia uhai wake ulikuwa ukitoweka.

Mara jambo la ajabu likatokea. Hata kabla nguruwe huyo hajakata roho, mnyama mwingine mkubwa zaidi mwenye

shada la manyoya mabegani mwake alichupa na kutua juu ya nguruwe huyo!

“Simba!” babu alisema kwa nguvu. Mara moja mkono wake ukaelekea kiunoni mwake. Palipokuwa na kisu chake.

Inaelekea, kama babu, simba huyo hakuwa na ndoto ya kukutana na binadamu mahala hapo, muda huo. Ni wazi kuwa yeye ndiye aliyekuwa amemkurupusha nguruwe huko alikokimbilia kabla hajalala na kuota ndoto zake ambazo zingemfanya arudi njia hiyo. Simba alimkazia babu macho ya mshangao ambayo pia yalibeba dalili za hofu. Babu naye alimkazia simba macho yake. Akimtaazama jicho kwa jicho. Mara nilimwona simba akiepuka macho ya babu kwa kuinama chini, kisha alipiga hatua za taratibu, moja baada ya nyingine akiliacha windo lake na kutokomea porini.

Mara alipoondoka babu naye aliniashiria kuondoka mara moja. Anaweza kurudi na akirudi hatakuwa na simile tena.” Babu aliniambia wakati tukiondoka harakaharaka.

“Simba amekukimbia!” Nilimwuliza babu hali ya kutetemeka mwili ilipoanza kunitoka.

“Binadamu ni mfalme wa dunia hii.” Babu alinieleza. “Pamoja na ukweli kuwa sisi ni dhaifu kuliko viumbe wengi duniani, bado tunauwezo na utukufu fulani juu ya viumbe wengine. Wajuzi wa mambo wanasema kuwa, tuna uwezo wa kutawala hata majini na mashetani. Simba yule alishindwa kustahimili. Nuru yenye madaraka yaliyotoka katika macho yangu ilikuwa silaha tosha.”

Niliyatafakari maelezo yake kwa muda mrefu. Jambo hilo nahisi babu alilichukulia kuwa natilia mashaka maelezo yake. Hivyo, akanigeukia na kuniambia, “Zaidi ya utukufu huu tuliopewa na Muumba nina hii.” Toka kifuani mwake

alichomoa hirizi ndogo nyeusi iliyokuwa ikining'inia kifuani mwake siku zote.

“Hii ndio hasa inayotulinda,” alisema. “Niliirithi kwa babu yangu ambaye naye aliirithi kwa babu yake. Haijapata kutuangusha kamwe. Ilinipeleka Ughaibuni na ikanirudisha hapa salama.”

Tukio la pili ambalo pia sitalisahau ni lile la kujikuta tukiingia katika kundi la tembo wasipungua arobaini waliokuwa katika kitu kama tafrija au halaiki ya aina fulani.

Ilikuwa majira ya saa tisa au kumi za jioni. Mimi nilikuwa taabani kwa uchovu na njaa. Mayai mabichi ya kanga tuliyokula na matunda ya pori hayakukidhi haja yangu. Nilitamani sana kula ugali wa muhogo na kisamvu kisha nipooze koo kwa togwa tamu. Nadhani babu pia alikuwa amechoka. Alikuwa mkimya kuliko kawaida yake na alitembea taratibu kinyume na mazoea yake. Nilimwona akitazama huko na huko kama anayetafuta ama chakula ama mahala pa kupumzika. Wakati huo tulikuwa ndani kabisa ya msitu mnene wenye miti mingi mikubwa kwa midogo ambayo ilifanya nuru iwe hafifu na jua tulione kwa nadra sana. Mara tukasikia mlio wa *waaa... waaa... waaa...* uliosikika kwa sauti kubwa. Mlio huo ulifuatiwa na sauti kama hizo toka pande mbalimbali za msitu huo.

Tembo!

Wakati nikiwaza hilo niliona tembo watatu wakiwa wamesimama mbele yetu wakituangalia. Niligeuka kutaka kukimbia. Nyuma yetu walitokea tembo wengine huku mikonga yao ikielea huku na huku, pua zao zikichezacheza kama waliojaribu kuipata harufu yetu halisi. Mara tembo mkubwa zaidi alianza kusagasaga miguu yake ardhini huku akitumia

mkoa wake kukatakata matawi ya miti na kukanyagakanyaga kwa hasira.

Kamababuasingenivutamkonokwanguvunakuniashiria kukimbilia mti mkubwa uliokuwa karibu na kuupanda, pengine tembo huyo angenifuata na kunikanyagakanyaga huku nikiwa nimeduwaa kwa hofu na taharuki iliyonishika. Kwa jinsi nilivyokuwa nikitetemeka, miguu na mikono yangu ikawa imeishiwa nguvu kabisa. Sijui nilipata wapi uwezo wa kuparamia mti huo na kuupanda hadi juu, babu akinifuatia. Tulipofika mahala salama, ambapo tembo hao wasingeweza kutufikia, tuliketi na kuwatazama.

Wakati huo, zaidi ya tembo ishirini walikwishakusanyika chini ya mti huo wakipiga kelele kwa sauti zao mbaya, za kutisha. Yule tembo mkubwa alitufuata mbio na alipoufikia mti wetu alijaribu kuung'oa kwa mkonga wake lakini mti ulikuwa mkubwa mno. Mkonga wake haukuweza kuuzunguka ili aweza kuuongo'a. Alipokata tamaa, alianza kuupiga kwa pembe zake kubwa. Pia hazikufua dafu. Akaamua kumalizia hasira zake kwa kung'oa miti midogomidogo ya jirani na kuturushia. Haikufika.

Nilikuwa bado natetemeka mwili mzima hivyo nilimshangaa kumsikia babu akiangua kicheko ambacho kilifuatiwa na maneno ambayo katika mazingira tofauti na hayo, yangeweza kunichekesha pia. “Kweli ukubwa wa pua sio wingi wa kamasi.”

“Una maana gani?” Baadaye nilimuuliza kwa sauti ya mnong'ono.

“Si unaona tembo hawa,” alinijibu. “Ni mkubwa kuliko wanyama wote wa nchi kavu. Baadhi yao wana ukubwa wa

nyumba ndogo na uzito upatao hadi kilo mia nne au zaidi. Lakini ubongo wao ni mdogo tofauti na maumbile yao. Wameshindwa kung'oa mti huu. Sasa wanashambulia miti midogomidogo isiyo na hatia. Kama sio ufinyu wa akili ni nini?"

Sikumjibu babu. Hali haikuniruhusu.

Tembo walipochoka waliamua kukaa chini ya mtu huo kana kwamba wanatusubiri hapohapo. Tukalazimika kulala juu ya mti huohuo na njaa yetu na kiu zetu.

Mimi sikulala.

Tembo waliondoka alfajiri sana kuendelea na safari zao. Mie na babu pia tuliondoka na kushika hamsini zetu.

Ndiyo, ilikuwa safari ya kutisha iliyojaa visa na mikasa. Lakini kwa upande mwingine ilikuwa safari ya kulisimua ambayo kwangu ilitosha kuwa darasa mahususi ambalo si aghalabu sana kila mtu kukutana nalo. Ni safari ambayo ilinipa fursa na wasaha wa kuona mengi na kujifunza mengi.

Kwa mfano, tukiachana na tishio la simba na tembo, nilibahatika pia kukutana na burudani toka kwa ndege na wanyama wengine. Tuliweza kuingia na kutoka katika uwanda mpana uliojaa twiga na pundamilia kana kwamba wako zizini. Wakati pundamilia wanavutia kwa miramba yao iliyozunguka mwili mzima walitukimbia kidogokidogo kama mbuzi amkimbiavyo binadamu, twiga na mashingo yao marefu walitupuuza kana kwamba hatupo. Twiga walitumia shingo zao hizo kula majani na miche iliyochipukia juu kabisa ya matawi na miti. Miili yao mikubwa, miguu na shingo ndefu pamoja na rangi ya kuvutia yenye mabaka ya udongo kwa njano mpauko zaidi ule mwendo wao usio na haraka viliwafanya twiga waonekane kama wanaoringa na kujivunia umbile lao.

“Kama simba ni mfalme wa msituni basi twiga ni malkia wa mwituni.” Babu alisema baada ya kuona nilivyowakodolea macho yao kwa husuda kwa muda mrefu. “Nani kama twiga?”

Kabla ya twiga hao, nilikuwa nimevutiwa sana na ndege ambao tuliwakuta eneo moja lenye mabwawa mengi. Babu aliniambia kuwa eneo hilo linaitwa Moyowosi nje kidogo ya Kibondo.

Kando ya mkondo mmoja wa mto huo tuliwaona heroe, wenye miguu na shingo ndefu mfano wa twiga na mdomo ulipinda pia. Na ndege hao wekundu walipenda kuwinda ndani ya maji. Pia tuliwaona ndege waliofanana na jogoo ambao babu alinielegeza kuwa waliitwa jogoo mwitu Kwembe - Kisunzu ambao wanamkia mfupi na manyoya yaliyoota katikati ya paji la uso kwa mpangilio kama panga la jogoo. Hondohondo, kibeti, kisi, kiguudani kiparara na ndege wengine ainaaina pia tuliwaona katika safari hiyo. Kila mmoja alikuwa na rangi yake, mlio wake na tabia zake.

Jambo jingine lililonifuraisha katika safari hiyo ngumu ni jinsi babu alivyotumia kila fursa kunielimisha juu ya kile alichokiita, “mitishamba”. Alinionyesha majani haya na yale na kunieleza matumizi na manufaa kwa binadamu.

“Unaona mti hule? Unaitwa Mguluka. Ule ni mti muhimu sana. Jitahidi kuukariri. Unatibu magonjwa mengi sana hata yale sugu. Unatibu ngiri, degedege na magonjwa ya kina mama. Unachukua magamba au mizizi yake na kuichemsha kisha unainywa kwa siku saba, kwisha.”

Babu alinionyesha miti aliyoitaja kama mvumbasa, mshashu, muuka, mzungwa, ulenge, ungwia na mlonge kuwa ni matibabu muafaka kwa maradhi mbalimbali. “Si hiyo tu.”

Babu alinieleza, “Kabla hatujafika mwisho wa safari hii pia, nitakuonyesha pia mnyembe, uwe na mingineyo ambayo si tu kuw inatibu bali pia hurefusha maisha ya mtumiaji.”

Kuna wakati babu alinishtua ghafla, “Angalia! Usikanyage jani hilo. Ukilikanyaga kama uko porini peke yako, utapotea siku nzima bila kuona njia ya kurudi nyumbani! Litazame uzuri jani hilo na ulikariri!”

Wakati mwingine babu alisikiliza mlio wa ndege au mnyama fulani na kuniamulu kubadili mwelekeo kuwa huko mbele kuna hatari fulani, “Ama simba wanawinda au wameua wanyama ama sokwe mtu wametanda.” Alionya.

SURA YA TATU

Ile Palee, Nchi Ya Wahaya

Tulifika nchi ya Wahaya bila kutegemea. Mimi binafsi nilikuwa nimechoka kwa mwendo wa muda mrefu, kulala sehemu za ajabuajabu na kula chochote kilichoweza kulika, jioni hiyo nilikuwa nikitembea kwa kujivutavuta, kama mzigo. Tulikuwa tukishuka toka juu ya kilima tulichopanda mchana wa jua kali, niliposikia ukelele wa furaha toka kwa mmoja wa watu tuliokuwa nao. Kelele hizo zilipokelewa na watu wengine zikifuatiwa na vicheko vya furaha.

Nilipoinua uso wangu kutazama huko wanakotazama wengine nilipigwa na butwaa. Takriban dunia nzima mbele ya macho yetu iligeuka kuwa uwanda mkubwa, mweupe unaomeremeta hadi upeo wangu kuona. Sikuelewa ninachokitazama hadi pale babu aliponishika bega na kuniambia, “Tumefika!” huku akitabasamu.

Sikumwelewa, “Tumefika wapi? Na kile nini kinachomeremeta kiasi kile?” nilimuuliza.

“Yale ni maji. Lile ni ziwa Lweru, ambalo siku hizi nasikia linaitwa Victoria. Tumefika salama mwisho wa safari yetu. Ile pale nchi ya Wahaya.”

Ziwa! Ndio kwanza nikaelewa kile ambacho nimekuwa

nikikisikia juu ya maziwa na bahari. Katika safari yetu hiyo ndefu nilipata kuiona mito mingi, mikubwa, na kuivuka kwa mitumbwi. Kamwe sikupata kufikiria kuwa ziwa lingeweza kuwa kubwa na lenye maji mengi kiasi hiki! Niliduwaa kwa muda mrefu, nikiwa nimelitumbulia macho ziwa hilo kwa shahuku. Nilihisi uchovu ulikuwa umeniteka mwili mzima ukitoweka na nguvu mpya na ari mpya kuchukua nafasi yake katika nafasi yangu.

Msafara wetu huo ulioanza kwa upweke mkubwa kati yangu na babu, sasa ulikuwa wa kundi la watu wasiopungua kumi na wawili. Watu hao, Mwarabu mmoja mwenye ndevu nyingi nyeupe na upara kichwani, ambaye baadaye tuliambiwa kuwa anaitwa Sheikh Seif, alitajwa kama mfanyabiashara wa chumvi na pembe za ndovu. Mtu mmoja kati yao, mrefu sana, mweusi sana, tuliambiwa kuwa ni Mnubi toka Uganda na kwamba alikuwa msaidizi wake mkubwa kibiashara. Wengine, mmoja, akiwa Muha aliyelowea Kagera, wawili Wamanyema wa Kongo na waliobaki wakiwa Wanyamwezi wa Tabora walikuwa wapagazi wake, walioajiriwa kwa safari hiyo pekee.

Tulikutana na watu hao katika kijiji kidogo kilichoitwa Kakonko. Siku hiyo babu alishauri tutafute eneo lenye watu ili tuombe msaada wa chakula cha binadamu zaidi, baada ya kukinaishwa na matunda na nyama za kuchomwa ambazo tulizila bila ugali wala chumvi. Mzee mmoja kijijini hapo alitudokeza juu ya kuwepo kwa wageni wengine kama sisi, waliokuwa wakitokea kwenye biashara ya kubadilishana nguo na shanga kwa chumvi za magadi iliyokuwa ikipatikana katika mabwawa ya maji huko Uvinza, Kigoma.

Tulitambulishwa na watu hao na mara moja wale Wahaya wakaanza kumtania babu kwa kumwita 'mtani'.

“Msiwe na wasiwasi,” mmoja wao alisema. “Hawa Wamanyema hawawezi kuwala mbele yetu. Tutawafikisha kwetu salama na kuwapatia vibarua kwenye mashamba yetu.”

Babu naye hakuwa mgeni kwa matani, “Nyama yenu chungu hailiki,” aliwajibu. “Wakijaribu tu kuionja watavimbiwa na matumbo yao kufura kama ya tembo. Halafu, huko kwenu hatuendi kutafuta kibarua. Tunakwenda kutafuta vibarua, waje wafanye kazi ya kurina asali katika misitu yetu.”

Wamanyema wale walicheka sana, Wahaya walicheka pia. Hata Mwarabu, ambaye alicheka kwa nadra sana safari hiyo alitabasamu na kuruhusu pengo moja la meno ya juu kuonekana. Mmanyema mmoja, aliyeonekana kuvutiwa zaidi na mimi kuliko babu, alinivuta kando na kuninong’oneza, “Msimchekee sana yule Mwarabu. Mnajua alikuwa akifanya biashara gani zamani? Hata kabla sijamjibu aliongeza, “Biashara ya watumwa. Hapo ulipo bila shaka anakutamani sana. Kwa jinsi ulivyo kijana, mwenye afya nzuri na wajihi wa kupendeza, enzi zake angekuuza kwa faida kubwa sana kuliko babu yako. Tena kwa jinsi alivyokuwa katika enzi hizi, kama angekukamata wewe na babu yako angempiga babu yako rungu la kichwa na kumwacha aliwe na tai, wewe angekupeleka hadi Bagamoyo au Zanzibar ambako angekupeleka mnadani, huku ukiwa umefungwa mnyororo mikononi na miguuni.

Sikujua kama bwana huyo alitaka niichukulie vipi taarifa hiyo, nicheka au nilie? Nilimkodoea macho, jambo alilolitafsiri kuwa ni kuvutiwa na simulizi zake. Hivyo, akaongeza, “Siku hizi amekwisha. Tangu biashara ya utumwa ilipopigwa marufuku amekuwa mtu wa kuuza shanga na chumvi, sio binadamu.

Nilimtazama Mwarabu huyo. Kweli aikuwa akinitazama pia. Lakini macho yake hayakutoa tafsiri yoyote ya ama

kunitamani ama kunipangia bei. Alikuwa bado anatabasamu, tabasamu la kibinadamu!

Tulilala kijijini hapo siku mbili. Kwa kiwango fulani tulilala vizuri na kula vizuri. Hivyo, safari ilipoanza tena nilikuwa mchangamfu, tayari kwa safari.

Wenzetu hao walikuwa na mizigo mikubwa. Walikuwa na pembe nne, kubwa sana, za ndovu, ambazo walizibeba kwa kupokezana. Walikuwa pia na viroba vinne vya chumvi, makapu mawili ya chakula na gudulia la maji. Tuliambia kuwasaidia. Mimi nilikabidhiwa kapu moja la chakula, babu akabeba lile gudulia la maji.

Msafara ukiwa mkubwa kidogo, haukupungukiwa simulizi za uongo na kweli. Utani, michapo na pengine nyimbo za kikabila ziliibuka mara kwa mara kiasi cha kufanya niichukulie safari hiyo kama tukio la kuvinjari tu katika nchi yangu. Tulivuka mito na vijito, tulipenya msitu na misitu, tuliwaona ndege na wanyama wa kila aina. Ndiyo, kuna nyakati tulichoka na kukata tamaa kutokana na njaa, mbu, uchovu na kero nyingine za porini. Lakini, kwa namna moja au nyingine, kero hizi ziliondokea kuwa kama sehemu ya burudani, kwani hakuna raha isiyo na karaha. Hadi tunalionga ziwa likimeremeta mbele yetu, kana kwamba linatulaki kwa vicheko na tabasamu, nilipata hisia kuwa safari yetu ilikuwa ya kheri na mafanikio yalikuwa yakitusubiri.

Muda mfupi baadaye tulifika pwani ya ziwa, katika kijiji cha wavuvi kilichokuwa kando kidogo ya kijiji cha Kashozi. Ilionyesha kuwa Mwarabu huyo na msafara wake walikuwa wenyeji katika kijiji hicho, kwani tulipokelewa juu juu na kuandaliwa chakula murua, ndizi zilizopikwa vizuri kwa samaki wakubwa aina ya sato. Baadaye tulipewa *rubisi* ambayo mimi

nilionja kidogo tu, kabla ya kuonyeshwa sehemu ya kulala.

Usingizi ulinipokea juujuu, wengine wanaita usingizi wa kifo, kwani nililala zaidi ya masaa kumi na mawili, bila kushtuka, kuzinduka wala kuota ndoto yoyote ile. Nilipofumbua macho ilikuwa kesho yake, saa mbili au tatu za asubuhi. Wavuvi walikuwa wakitoka ziwani, mitumbwi yao ikiwa imejaa samaki aina ya sato na sangara.

Nilimwona babu akiwa kando ya ziwa, akizungumza na mmoja wa wenyeji wetu, mzee mpole, ambaye baadaye niliambiwa kuwa anaitwa Buberwa, rafiki wa karibu wa 'Mtume wa karagwe' mwalimu Ibrahimu Kazigu.

* * *

Ujio wa kigeni katika mkoa wa Kagera haukuwa lelemama. Kwanza kabisa, Wahaya walikuwa na mungu wao ambaye walimwamini na walamini kabisa kuwa aliwataatulia matatizo yao. Mungu huyu alijulikana katika majina mbalimbali kama *Ruhenga*; Mweza wa yote, *Mutonzi*; Muumba, *Nyakubao*; Aliyepo, *Nyakumerera*; Wa milele na kadhalika. Jina kubwa zaidi lililojumisha miungu hio likiwa lile la *Mugasha*; Mungu wa mvua, Mlinzi wa mito, ziwa, wavuvi na samaki.

Wahaya walikuwa hawatoi zaka wala sadaka. Hali kadhalika, walikuwa hawatoi kafara. Siku zote walamini kuwa mungu wao alikuwa na kila kitu, kamwe asingehitaji chochote kutoka kwa viumbe wake.

Dini za kigeni zinaweza kuelezewa kuwa ziliingia Kagera kwa kupitia mlango wa nyuma. Mnamo mwaka 1878 mapadri wa kwanza wa kikatoliki walifika Zanzibar wakitokea Algiers, Algeria. Mapadri hao walitawanyika hadi kufika Uganda kwa Kabaka Mutesa, aliyekuwa mfalme wa himaya ya Buganda,

kumwomba msaada. Mapadri hao walipata upinzani mkubwa sana toka kwa Waislamu ambao walikwishatangulia nchini humo na kumsilimisha Kabaka mwenyewe, pamoja na Wakristu wa madhehebu ya ki-prostetanti ambao pia walikuwa wametangulia. Hata hivyo, Mutesa aliridhia maombi yao na kuwapa mashua iliyowafikisha Bukoba April 1880.

Kumbe Mutesa alikuwa akiwala kisogo. Wakati akijitia kuwasaidia alikuwa pia akitangaza taarifa kwa watemi wa Kagera ambao wengi wao walikuwa wakiwajibika kwake, akiwaagiza kutowapa ushirikiano wamisionari hao. Iliwachukua wamisionari hao miaka kumi na miwili kuweza kuanzisha kazi yao ya kutawanya ‘neni la bwana,’ katika eneo hilo.

Katika eneo hilo la Karagwe watemi Kahigi na Kyobya walikuwa wameshiriki sana kugomea jitihada hizo za kuanzisha kanisa katoliki. Hali kadhalika, upinzani kati ya utawala wa Wadachi waliokuwa madarakani na Waingereza ambao waliwang’oa Wadachi madarakani ulichangia sana katika vita dhidi ya madhehebu ya kikristo. Itakumbukwa kuwa mtemi mmoja wa enzi hizo, aliyejulikana kwa jina la Ntare, alitolewa mhanga katika changamoto hiyo kwa kushtakiwa kwa Wadachi kuwa alikuwa akiwakaribisha Waingereza. Mtemi huyo alihukumiwa kifo na kunyongwa mwaka 1916.

Mwaka huohuo wakati Mwami Ntare ananyongwa mtu mmoja aliyekuwa itwa Ibrahimu Kazigu alibatizwa, akiwa na umri wa miaka kumi na mitano. Wana Karagwe wanamwelezea bwana huyu kuwa ni mfano wa mtume Paul, kwani alikubali kuacha kila alichokuwa nacho na kujitolea kulitumikia kanisa. Bwana huyu alitumikia kanisa kwa zaidi ya miaka thelathini na miwili akihubiri, kuanzisha makanisa, kuanzisha shule

na kubatiza. Mapadri walipokuja kuanzisha misheni eneo hilo, kule Bugere, mwaka 1934 walikuta tayari Karagwe ina waumini wapatao elfu mbili na wanafunzi, wake kwa waume takribani mia nane.

Ni mtu huyu, Kazigu ambaye babu alinikabidhi kwake kupitia kwa mwenyeji wetu Buberwa, ambaye aliondokea kuwa rafiki mkubwa kwa babu. Kitendo cha kuambiwa kuwa tumesafiri safari ndefu, toka nchi ya mbali, kwa ajili ya kuja kufuata ‘neni’ na elimu kilimfanya Ibrahimu Kazigu aliyekuwa hapo Kashozi wiki mbili baadaye kukutana na wamisionari, anipokee kwa mikono miwili. Akanitia mikono kichwani na kunibariki. Jumapili iliyofuata nilibatizwa na kupewa jina la Petro, badala ya langu la zamani la Mtukwao ambalo niliambiwa kuwa ni la kipagani. Kisha nikakabidhiwa katika shule maalumu ambazo zilikuwa zikipokea watoto yatima na wale waliokombolewa kutoka utumwani hasa wakitokea Kongo, Rwanda na Uganda.

Babu hakushiriki sherehe za ubatizo wangu. Alitoroka usiku wa kuamkia siku ya ubatizo kwani ‘mtume’ Ibrahimu Kazigu alikuwa amemtaka yeye pia kubatizwa kwa maelezo kuwa ‘ameona mwanga, hastahili tena kukaa gizani.’ Lakini babu hakuwa tayari. Alishindwa kumkatalia Ibrahimu kimachomacho kwa ajili ya kuchelea kuharibu jitihada alizofikia juu yangu. Ndipo akaamua kutoroka. Lakini haikuwa kabla ya kuchanjiana damu na rafiki yake Buberwa, hatua ambayo ilihitimisha urafiki wao na kuwafanya ‘ndugu wa damu.’

Tuliagana na babu kwa siri, katika uchochoro wenye kiza, hivyo sikuweza kuyaona macho yake kuona kama anachosema yalikuwa yakitoka mdomoni au moyoni. Alisema maneno machache yaliyojaa pongezi kwa uvumilivu wangu

wa kuweza kuikamilisha safari ile ngumu. Pia alishukuru kwa jinsi jitihada hizo zilivyoweza kuzaa matunda kwa urahisi kuliko alivyotegemea.

“Nakuacha mikononi mwa rafiki yangu wa damu na mtu wa Mungu. Sina shaka kuwa utaishi salama na utapata elimu itakayokupa nafasi katika dunia hii,” babu alisema na kuongeza, “Sina cha kukupa mjukuu wangu. Kitu pekee nitakachokuachia ni hiki.” Alivua hirizi iliyokuwa shingoni mwake na kunivisha. “Hii ni hirizi ya bahati. Ilinde nayo itakulinda maishani mwako. Kamwe usiiweke mbali nawe.”

Nilijikuta nikilengwalengwa na machozi. “Babu hii ni hirizi yako. Imekulinda maisha yako yote. Ukinipa mimi huoni kama maisha yako yatakuwa hatarini?” nilimwambia.

“Hapana mjukuu,” babu alinijibu. “Mie hirizi hii niliirithi kwa baba, ambaye aliirithi kwa baba yake. Ni hirizi ya familia. Wewe unaingia katika safari ndefu ya maisha. Unaihitaji kuliko mimi na baba yako tunavyoihitaji sasa.”

Nikaipokea na kuivaa.

“Halafu uifiche sana,” babu alionya. “Hawa watu wa kanisa kwao kila kitu chetu cha asili kwao ni dhambi. Wakiiona wataipokonya na kuichoma moto. Ifanye siri yako, siri ya moyo wako.”

Baada ya maneno hayo babu alinitemea mate katika paji la uso na kunitakia kheri. Kisha akageuka na kutoweka gizani.

Nilishindwa kujizuia. Machozi yalinitoka.

Laiti ningejua kuwa agano hilo lilikuwa la mwisho, kwamba nisingemwona tena babu yangu, nisingekubali kuachana naye kirahisi kiasi kile.

* * *

“A!”

“Ahaaaaaaaaaa!”

“E!”

“Eheeeeeeee!”

“I!”

“Ihiiiiiiii!”

“Oh!”

“Ohoooooooo!”

“U!”

“Uhuuuuuuuu!”

“a,” inaandikwa kama punje ya harage....’e’ iko kama ndizi iliyovimba juu.... ‘I’ ni kama msumari... ‘o’ ni kama yai.... ‘u’ ni kama shimo. Mnanielewa?”

“Ndiyoooo!”

Mtukwao, bin Karimanzira bin Kionambali nilikuwa nimeanza shule. Hapana! Sikuwa tena Mtukwao, wala Karimanzira. Nilikuwa na jina jipya, Petro Kionambali. Ndivyo nilivyoandikishwa. Ndivyo nilivyokuwa nikiitwa na walimu na wanafunzi wenzangu katika maisha na mazingira hayo mapya.

Tuliishi katika mabweni, tukiwa wavulana wapatao sitini au sabini hivi. Wengi wetu tulikuwa watu wa makabila tofauti, utamaduni tofauti na hata maumbile tofauti. Tulitofautiana pia katika umri. Wakati mimi nilijiona mdogo kwa umri wangu wa miaka kumi na mitatu, walikuwepo kaka zetu wenye umri wa miaka kumi na saba katika darasa hilohilo la kwanza. Wengine walikuwa wadogo kabisa kwa miaka yao kumi hadi minane.

Tulifundishwa kusoma na kuandika. Lakini mkazo mkubwa hata kabla hatujaanza kusoma na kuandika ulikuwa wa mafundisho ya dini. Tulifundishwa upendo, kusali pamoja

na kuimba nyimbo za kumsifu bwana. Tulifundishwa kila kitu juu ya mungu wa Izrael, aliyemtuma mwanawe wa pekee, ili azaliwe kama binadamu katika zizi la kondoo, ateswe, asulubiwe na kufufuka siku ya tatu baada ya kifo chake kwa ajili ya kutukomboza na dhambi zetu. Zaidi, tuliambiwa kuwa tayari siku zote, kwani haikujulikana siku wala saa ambayo angerudi tena duniani na kuwachukua ‘wateule’ wake na wale wasio wake kutupwa jehanamu ambako wangeungua kwa moto mkali wa milele.

Nikijua kuwa nilikuwa nimetembea safari ndefu na ngumu kuifuata fursa hiyo ya kupata elimu nilitilia maanani kila nilichofundishwa na kuzingatia kila fundisho la dini. Jambo hilo lilinifanya baada ya siku chache tu niwe mmoja wa wanafunzi hodari sana shuleni hapo. Walimu walinipenda, wanafunzi walinisikiliza. Hivyo, haikuwa ajabu pale, ulipofika mwisho wa mwaka huo nilipoteuliwa kuwa kiranja wa darasa langu.

Mafunzo ya dini pia niliyazingatia sana. Sikuwa na sababu wala wasaa wa kuiba, sikuwa na haja ya kumtukana mtu wala kumzulua uongo. Kama kuna dhambi pekee, ambayo siku zote ilinisuta moyoni basi ilikuwa ile ya kundelea kuthamini na kuivaa kwa siri hirizi yangu niliyoachiwa na babu. Sikuwa tayari kuitoa kwa shemasi au kasisi ili ichomwe moto. Nilichukulia ile kama kiungo pekee baina yangu na familia yangu, kiungo ambacho kukitoa ingekuwa sawa na kuukata mzizi wa mwisho; kati yangu na asili yangu.

Elimu niliyoipata katika nchi hiyo ya Wahaya haikuwa ile ya darasani wala ya dini pekee. Nilipata elimu ya mitaani ambayo kwa kweli ilinisaidia sana. Kwa mfano, wakati shule hazikufundisha lugha ya Kihaya, huko mitaani nilifundishwa.

Ndani ya mwaka mmoja tu nilikuwa tayari nikisikia na kuzungumza Kihaya kwa ufasaha kama Muhaya yeyote yule.

Shule hatukufundishwa kuogelea. Lakini mimi katika kipindi hichohicho cha mwaka mmoja tayari nilikuwa hodari wa kucheza na maji kama samaki. Niliweza kuelea juu ya maji kama boya au kupiga mbizi kama sangara. Hali kadhalika, nilijifunza kupiga makasia na kuvuta aina kwa aina za samaki. Kwa kushika maji au kuangalia mwenendo wa mawingu angani nilijua ni wakati gani ziwa lingechafuka kwa upepo mkali, wakati gani limepungua.

Kwa kiasi kikubwa ‘utundu’ wangu ziwani ulichangiwa na mapenzi makubwa niliyokuwa nayo kwa ziwa hilo toka pale nilipoliona kwa mara ya kwanza. Nililichukulia kama hazina ya pekee tuliyojaaliwa na Muumba kwa kuzingatia kuwa nchi nyingine badala ya maji hayo mengi wao wamejaliwa majangwa yaliyojaa mchanga na joto kali. Nililichukulia ziwa hilo kama hazina ndani ya hazina. Wingi wa samaki waliojaa katika ziwa hilo, aina waliokuwa wakiishi ndani au kando mwa ziwa hilo ulikuwa ushahidi tosha wa utajiri huo.

Mtu aliyechangia kunipa elimu na ujuzi mwingi juu ya ziwa hakuwa mwingine zaidi ya mzee Buberwa, baba yangu wa kufikia. Kila nilipopata likizo nilikuwa nikienda kwake ambako nilishirikishwa katika uvuvi na kuweza kujipatia si ujuzi tu bali pamoja na vijisenti vya matumizi kutokana na mchango wangu katika uvuvi. Mtoto wake mkubwa, Muleju, aliondokea kuwa rafiki yangu mkubwa na ndiye aliyenipa darasa la awali la kuogelea. Madarasa yaliyofuata nilijifunza mwenyewe kutokana na ujasiri na jitihada zangu.

Buberwa alikuwa mzee aliyependa sana utani. Hakuchoka kuniambia mara kwa mara, “Mwanangu

tumekupeleka shule kuchukua elimu. Hatukukupeleka pale kujifunza utawa na upadri. Chukua elimu yako, usichukue upadri wao. Nataka ukimaliza shule nikupe msichana mrembo wa Kihaya, umuoe na kurudi naye kwenu. Watu wa huko wajue Mungu alivyopendelea nchi ya Wahaya si kwa samaki na maji pekee, bali pamoja na wajihi murua wa wakazi wake.”

Kuoa! Nililichukulia kama jambo ambalo lingenitokea baada ya karne nyingine zijazo. Sikupata kumjibu kwa hilo. Naye nadhani hakutegemea jibu langu. Ilikuwa kama mtu anayenikumbusha jambo fulani, mara kwa mara, ili lisije likanitoka akilini.

Nimezungumza mengi juu ya raha za ziwani, raha za kula samaki watamu, raha za kuelea juu ya maji, raha ya kupata fedha kutokana na mauzo hayo. Pengine haitakuwa haki kama sitataja chochote pia juu ya karaha zake pia.

Wanasema, wavuvi wengi kwamba ukiwa ziwani ujue kuwa unatembea na ‘kifo mkononi.’ Madai ambayo niliyadhibitisha kwa vitendo kwa uhai wangu wa ziwani hapo.

Tukio la kwanza lilikuwa lile la kupotea ziwani. Siku hiyo tulikwenda kuvua samaki usiku. Ghafla, ulizuka upepo mkubwa ulioambatana na mvua nzito ambayo ilifanya karabai tulilokuwa tukilitumia kwa ajili ya mwanga lizimike. Upepo huo ulisababisha mawimbi makubwa yaliyofanya mara kwa mara maji yaingie ndani ya mtumbwi. Huku nikitetemeka nilipewa kazi ya kuondoa maji hayo yaliyoingia huku wenzangu wawili waliobakia wakijitahidi kupiga makasia kurudi ufukweni. Zilikuwa jitihada zisizo na matunda. Kwanza, kutokana na kiza kilichotanda hakuna aliyefahamu nyumbani ni upande upi. Pia, kasi ya maji kuingia katika mtumbwi ilikuwa kubwa kuliko ile ya kuyaondoa. Muda mfupi baadaye wenzangu walikata

tamaa ya kupiga makasia bila kujua kama wanakwenda mbele au wanarudi nyuma. Wakajiunga nami katika jukumu la kuondoa maji katika mtumbwi. Haikusaidia. Muda mfupi baadaye mtumbwi wetu ulizama na kupinduka. Tukaogelea na kupanda juu ya mgongo wake huku tukipiga kelele kuomba msaada.

Katika purukushani hizo mwenzetu mmoja alipotea. Nadhani alichoka kuendelea kuung'ang'ania mgongo wa mtumbwi ambao ulikuwa ukiyumba na kutupwa huku na kule kwa mawimbi hayo. Mimi na Muleju tuliendelea kung'ang'ania hadi alfajiri, upepo huo ulipopoa.

Tulishinda ziwani humo, juu ya mgongo wa mtumbwi huo tukiwa hatuna la kufanya. Makasia yetu yalikuwa yamechukuliwa na mawimbi na uwezo wa kuufunua mtumbwi huo hatukuwa nao.

Siku ya kwanza na usiku wake ukapita. Siku ya pili, jioni sana, tukiwa tayari taabani kwa njaa na uchovu, tuliona mtumbwi wa wavuvi ukitujia. Hawa walituzoa na kutupakia kwenye mtumbwi wao kisha wakajitahidi kuubinua mtumbwi wetu na kuondoa maji yaliyokuwemo. Wawili kati yao waliingia katika mtumbwi huo na kuupiga makasia kuelekea ufukoni. Ufukwe huo uliondokea kuwa kisiwa kidogo cha Bumbire, mbali sana kutoka Kashozi tulikoanzia safari.

Tulipumzika kisiwani humo kwa siku tatu zaidi, kabla ya kurejea nyumbani ambako walikwishakaa matanga wakiamini kuwa nilikwishakufa. Tuliopona tulifanyiwa sherehe ndogo, mwenzetu aliyepotea aliombolezwa kwa taratibu za kimila.

Nikiwa na hakika kuwa kilichoniokoa katika mkasa ule ilikuwa ile hirizi yangu niliyopewa na babu, ambayo muda wote ilikuwa kifuari mwangu, niliibusu na kuikumbatia kwa

furaha, “Nitakulinda daima, ili nawe unilinde,” niliinong’oneza.

Katika hali ya kawaida, tukio hilo lingetosha kabisa niliogope ziwa hilo kama simba mla watu. Lakini, kwa jinsi ziwa lilivyokwishiingia akilini niliichukulia tukio zima kama jambo la kawaida tu, katika pilikapilka za maisha. Nikaendelea na shughuli zangu bila hofu wala wasiwasi wowote.

Tukio lililofuata, ambalo pia sikulitegemea kiasi lilikuwa kama la kuchekesha. Nilikuwa nikiogelea kando ya ziwa, baada ya kazi ya kutwa nzima za mchana huo. Nadhani nilikuwa nimeogelea kwa muda mrefu kiasi, kwani nilijihisi uchovu mwingi. Mara nikaona kitu kama gogo likielea juu ya maji mbele yangu. Nikalifuata na kuparamia juu yake ili nipumzike kidogo. Nilishangaa kuona gogo hilo likizama ghafla na kisha likiibuka hatua chache mbele yangu na kufunua domo lake kubwa ama kupiga mwayo ama kunifokea.

Mamba!

Nilikuwa nimeparamia mgongo wa mamba. Kwa kujua kuwa mamba hana uwezo wa kumnasa mtu katika maji mengi niliogelea harakaharaka kupanda ziwani. Zilipogeuka nilimwona mamba yule akiogelea kurudi ufukoni. Ama alikuwa ameshiba sana, ama alishtuka mie kukimbia.

Hilo na lile la kukoswakoswa na kiboko mmoja aliyefanikiwa kupindua mtumbwi wetu ni miongoni mwa matukio mengi, ya kutisha yaliyoambatana na maisha yangu katika ziwa hilo.

Kwa kupona hatari baada ya hatari, huku nikiendelea kupata mafanikio kimaisha na kitaaluma niliamini kabisa kuwa hirizi yangu ilikuwa ikitimiza wajibu wake. Mara kwa mara niliibusu na kuinong’oneza, “Nitakulinda daima ili nawe unilinde.”

SURA YA NNE

Hirizi yazua jambo.

Hana mkasa iliyosababisha safari yangu kielimu ikome baada ya miaka mitano tu. Wakati huo nilikwishashuhudia watu wote waliovuka miaka kumi na minane akihesabiwa katika kile kilichoitwa sensa ya kwanza nchini Tanganyika. Tukio hilo lililofanyika Julai mosi, mwaka 1931. Mimi sikuhesabiwa kwa ajili ya umri na hata kama ningekuwa na umri nisingehesabiwa, kwani Makarani wa kazi hiyo walikuwa wakihesabu wakuu wa kaya pekee na kisha kwenda kutengeneza hesabu zao. Jambo hilo lilileta manung'uniko kuwa kazi hiyo haikufanyika kwa ufanisi.

Pia, wakati huo nilikuwa nikidonoadonoa maneno kadhaa yaliyoandikwa katika gazeti la Kiingereza lililoitwa *Tanganyika Standard*, ambalo lilikuwa limeanzishwa huko Dar es Salaam mwaka uleule wa hesabu ya watu.

Ni kupitia gazeti hilo nilipofahamu kuwa Gavana wa nchi wakati huo aliitwa H.A MacMichael akiwa amemrithi G.S Symes ambaye naye alimrithi D.C Cameron. Wote hao walikuwa wamemfuatia Gavana wa kwanza wa Uingereza nchini aliyetwa H.A Byatt, aliyepewa wadhifa huo mara baada ya Wajerumani kupokonywa nchi ya Tanganyika mwaka 1920.

Naikumbuka vizuri sana siku ya balaa. Ilikuwa tarehe 4 Novemba, 1934. Kule Dar es Salaam kulikuwa na kikao muhimu cha watawala kilichoitwa Kamati ya Ushauri wa Elimu kwa Mwafrika. Kamati hiyo ilipinga wazo la wanafunzi wa Kiafrika kuchangia mitaala na madarasa ya Wazungu au Waasia kwa madai kuwa uwezo wa watoto wa Kiafrika kuelewa wanachofundishwa ulikuwa duni sana ukilinganishwa na Wazungu na Wahindi. Hata hivyo, mjumbe mmoja, aliyeitwa Martin Kayamba, alipinga vikali madai hayo. Alisema, “Huwezo wa mtoto wa Kiafrika haukuwa na tofauti yoyote na ule wa Wazungu au Wahindi bali tatizo pekee lililosababisha hisia hizo zijitokeze ni watoto hao kutopewa nafasi sawa na wengine.”

Habari ambazo shuleni hapo, miongoni mwa walimu na wanafunzi, zilikuwa kubwa sana. Kayamba alisifiwa na kupongezwa sana kwa kitendo chake cha kuwapa wakoloni ukweli.

Kwa utoto wetu tuliadini kauli yake ingekuwa mwisho wa kutengwa na mwanzo wa kuruhusiwa kusoma pamoja na watoto wa Wazungu na Wahindi ambao walikuwa na shule bora mara kadhaa zaidi yetu. Tulikuwa katika vijikundi vidogovidogo tukijadiliana juu ya hilo baada ya masomo ya kutwa nzima tulipozinduliwa na kelele za baadhi yetu ambao walikuwa tayari wakikimbilia nyuma ya shule wakibeba mifuko na mabakuli.

“Senene!” mmoja wetu alitamka. Mara alikurupuka na kupiga mbio kuwafuata wengine.

Ulikuwa msimu wa senene. Mara nyingi msimu huo uliambatana na ule wa kumbikumbi ambao ni jamii ya mchwa ambao huota mbawa na kuruka kwa makundi makubwa angani kwa muda mfupi. Baadaye kuishiwa uwezo wa kuruka

na kudondoka ardhini huku mbawa zao zikinyofoka.

Wakishapoteza uwezo wa kuruka kumbikumbi huzagaa ardhini wakitafuta namna ya kurudi katika vichuguu vyao. Wengi huishia kuwa kitoweo cha binadamu na ndege. Kati ya wachache ambao hubaatika kunusurika mmoja wao hugeuka Malkia ambaye hutaga maelfu kwa maelfu ya mayai hivyo kuanzisha upya kizazi chao. Hao ni kumbikumbi.

Senene, ambao ni jamii ya panzi, ni maarufu zaidi kwa wakazi wa eneo hilo jirani. Wao wana tabia ya nziye, ingawa hawana madhara makubwa kama ndugu zao hao ambao wanaweza kugeuza pori kuwa jangwa kwa muda mfupi sana.

Senene, ni chakula maarufu zaidi, na kwangu mimi walivutia zaidi. Hivyo, kama wenzangu wote sikuweza kujizuia. Nilikimbia huko na huko na kuwakamata wengi tu ambao niliwajaza katika mfuko ili kesho niweze kuwaanika na kisha kuwahifadhi kwa matumizi ya baadaye.

Na baada ya pilikapilika hizo, wakati tukiwa katika sala ya mwisho kabla ya kulala nilipohisi upungufu fulani katika mwili wangu. *Nimepoteza nini?* Nilijiuliza huku nikijipapasa. Haikunichukua muda kubaini kuwa hirizi yangu, ambayo tunapokuwa darasani nilikuwa na tabia ya kuhifadhi mfukoni, ilikuwa imetoweka! Bila shaka ilidondoka katika zile purukushani za kunasa senene.

Hirizi yangu! Niliwaza kwa uchungu, nikihisi nguvu zote zikiniisha mwilini. Ibada iliyokuwa ikiendelea haikuniingia akilini. Nilitamani kutoka nikaitafute lakini tayari ulikuwa usiku mwingi, kwanza nisingeiona, pili nisingeruhusiwa kutoka.

Usiku huo usingizi ulinikata kabisa. Alfajiri sana, kabla ya mtu yeyote kuamka mimi tayari nilikuwa nje nikijaribu

kupita kila mahala nilipohisi kuwa ningeweza kuidondosha. Sikuipata.

“Unatafuta nini?” nilisikia sauti ya mtu ikizungumza nyuma yangu. Nilipogeuka nilimwona Byabato, mwanafunzi mfupi, mnene, ambaye kwa kweli hakupata kuwa rafiki yangu.

“Natafuta kalamu yangu,” nilidanganya.

“Kalamu! Utaiona kweli saa hizi? Kwa nini usingoje jua lichomoze?”

“Siyo kazi yako!” nilimwambia

Byabato alinitazama kwa mshangao. Mara nikamwona yeye pia anaanza kutafuta kitu huko na huko kama mimi. Ilikuwa zamu yangu kushangaa.

“Unatafuta nini?” nikamuuliza.

Naye akanipa jibu lilelile ambalo mimi nilimpa dakika mbili zilizopita, “Siyo kazi yako!”

Kihoro kilinipanda. Kwa jinsi nilivyomfahamu Byabato nilijua kuwa kama angeipata hirizi ile asingesita kubaini kuwa ndiyo nilikuwa naitafuta. Na kwa tabia yake asingekuwa mtu wa kuniwekea siri. Ingemchukua dakika chache sana kuitangazia shule na dunia nzima kuwa nilikuwa na hirizi. Sikuwa na namna ya kumzuia. Nilichofanya nilijaribu kumpoteza kwa kutafuta sehemu ambayo nilikuwa na hakika kuwa sikuifikia. Lakini, kwa mshangao wangu yeye alielekea upande wa pili, ambako ndiko hasa nilikopita katika nyendo zangu.

Nilishukuru pale kengele ya kujiandaa kuingia madarasani ilipolia kabla sijaipata wala kumwona Byabato akiokota. Nikaondoka kinyonge na kurejea bwenini kujiandaa.

Nilikuja kuiona tena hirizi hiyo saa nane za mchana. Kuiona, *siyo kuipata* rafiki yangu! Kwani ilikuwa mikononi mwa Padri Backhove aliyekuwa ametembelea eneo hilo ili

kukagua maendeleo ya shule na maendeleo ya wanafunzi na waumini wengine kiimani.

Ilikuwa baada ya mlo wa mchana, ambao mimi niliula kidogo sana, kengele ya dharura ilipigwa na wote tukakusanyika katika ukumbi wa ibada. Padri alianza kwa kutoa nasaha au somo refu juu ya raha inayotusubiri huko mbinguni na mateso makali ya moto wa milele unaowasubiri huko jehanamu wote ambao watakwenda kinyume na amri kumi za Mungu. “Mungu wetu ni mwenye wivu,” aliongeza Padri. “Moja ya amri zake kumi, alizozileta kwa mkono wa mtumishi wake Musa pale kwenye mlima Sinai inasema waziwazi, ‘Usiitumikie miungu mingine ila mimi’ Sawa?”

“Sawa,” wote tuliitikia.

“Mungu wetu ni msafi,” Padri Backhove aliendelea, “Anapenda wote tuwe wasafi wa miili na mioyo yetu. Sawa?”

“Sawa.”

“Kumfuata bwana maana yake ni kukana dhambi. Kukana mila na desturi zetu zote potofu na kuanza maisha mapya ndani ya Kristo. Maisha safi kimwili na kiroho. Mkristo wa kweli hatakiwi kuamini uchawi. Hatakiwi kuabudu sanamu... Hatakiwi kuvaa hirizi... sawa?”

Mara lilipotajwa neno ‘hirizi’ nilijua wapi mahubiri hayo yanaelekea. Nilihisi miguu yangu ikiishiwa nguvu na mwili wangu ukitetemeka. Sikuwa na uwezo wa kusikia tena chochote ambacho padri aliendelea kusema hadi pale nilipomwona akiwa ameishika hirizi yangu na kuining’iniza mbele yetu, huku akisema, “... Nauliza kwa mara ya pili nani kati yenu aliyeidondosha hii?”

Wote tulitazamana. Macho yangu yalikutana na yale ya Byabato ambayo yalinitazama kwa namna ya kunisuta

na kunidhihaki. Macho yaliyokuwa yakisema, “Unajua kuwa najua kuwa ni yako!”

“Nitaauliza kwa mara ya tatu,” Padri aliendelea. “Nani kati yenu aliyedondosha hirizi hii jana?”

Macho ya Byabato yalikuwa yameganda juu ya macho yangu, yakinicheka. Sikuweza kustahimili zaidi. Niliinua mkono wangu juu na kisha kusimama huku nikijibu taratibu, “Ni yangu, Padri.”

Si Padri wala wanafunzi wenzangu walioamini masikio yao. Kwa darasa langu, kwa shule nzima na hata jamii nzima ya eneo hilo mimi nilikuwa mfano bora zaidi kimasomo na kikanisa. Nilikuwa hata nikiwasaidia mashemasi katika huduma ndogo ndogo za kanisa.

“Ni yako?” Padri aliniuliza tena, kana kwamba alitaka nibadili kauli na kuikana hirizi yangu. Sikuwa tayari kwa hilo.

“Unajua kuwa mwili wako ni hekalu la Mungu? Aliniuliza Padri.

“Najua!”

“Kwa nini basi unavaa uchafu? Kwa nini unahifadhi dhambi na kuishi nayo? Hutaki kuingia katika ufalme wa Mungu?”

Sikumjibu.

“Sio neno,” Padri aliendelea. “Leo Bwana amefanya muujiza kwa ajili yako. Ameifichua hirizi hii chafu, ambayo umeivaa kwa muda mrefu, ili ujitakase upya. Tutawasha moto hapo nje, utaichoma hirizi hii kwa mkono wako mwenyewe. Kisha tutakuombea na kukubariki kwa kitendo hicho cha kuachana na upagani milele.”

Tulitolewa nje. Zikaletwa kuni, moto ukawashwa. Huku wenzangu wakiimba pambio mbalimbali, mimi na Padri

Backhove tulisimama mbele ya kadamnasi hiyo, mikononi mwake akiwa na Biblia na hirizi yangu.

“Wakati nikianza kusali, ichukue hirizi hii uitupe ndani ya moto ukitamka maneno yafuatayo ‘Shetani nakuteketeza sasa na milele, kwa jina la Yesu’ Umeelewa?”

Niliitikia kwa kichwa.

Nyimbo zilipamba moto. Sauti ya Padri akisoma sala ilisikika waziwazi. Lakini mkono wangu uliokuwa na hirizi uliishiwa nguvu huku nikitetemeka mwili mzima. Niliishikilia kwa zaidi ya dakika mbili, nikiining’iniza juu ya miale murua ya moto huo lakini vidole vyangu vilielekea kunigomea. Hisia zangu zilikwenda mbali sana toka hapo. Zilisafiri hadi usiku ule tulipoagana na babu uchochoroni. Masikio yangu yalisafiri pia. Yalikuwa pamoja nami huko uchochoroni, gizani, yakimsikia babu akisema; *Hii ni hirizi ya bahati. Ilinde nayo itakulinda maishani mwako*. Sauti hiyo ilikuwa wazi wazi kabisa masikioni mwangu.

“Ichome!” Padri alikatiza sala na kuniambia kwa ukali.

“Siwezi!” Nilimjibu.

“Huwezi nini?” aliniuliza kwa mshangao. “Tupa uchafu huo ndani ya moto!” nilishindwa kabisa kuviamini vidole vyangu kufanya hivyo. Mara nikageuka na kuanza kuondoka. Padri hakuyaamini macho yake. Akanifuata na kujaribu kunishika. Nikamsukuma.

Padri Backhove alikuwa mtu mnene na mzito sana. Lakini hakuwa na nguvu nyingi. Nilimsukuma kidogo tu, lakini akaanguka chali, kama gunia. Sehemu ya kanzu yake ndefu, iliyofika miguuni iliangukia ndani ya moto huo na kuanza kuungua.

“Nakufa!” Padri alipiga kelele akijiviringisha huku na

kule katika jitihada za kujizoa ainuke toka mavumbini hapo.

Nilishikwa na hofu kubwa. Wakati wenzangu wakihangaika kuzima moto katika mwili wa padri, wengine wakijaribu kuinua mwili wake wenye zaidi ya kilo mia na sitini mimi nilianza kukimbia kwa nguvu zangu zote huku nikihisi sauti za watu wanaonifuata wakizomea nyuma yangu. Sikugeuka wala kusimama hadi nilipofika vichakani, mbali sana, ambako niliamini mtu yeyote asiye na uwezo wa kukimbia kama mimi na ujuzi wa mambo ya porini kama mimi, asingeweza kunipata.

* * *

Nilijipumzisha kwa muda chini ya kivuli cha mti aina ya mvule, ulioonekana kupevuka sana. Nikaketi na kuegemea shina lake huku nikiitumia akili yangu kutafakari mustakabali wa maisha yangu baada ya tukio lile. Moyo wangu ulijaa kiza, hofu kubwa ikiwa imetanda katika nafsi yangu kwa kufikiria tu uzito wa mkasa ule.

Sikuwa na hakika kama padre Backhove alikuwa hai au la kwa moto na mweleka ule. Hata hivyo, hakika niliyokuwa nayo ni kwamba alikuwa ameathirika sana kimwili na kisaikolojia. Kwa vyovyote vile kama angenitia mkononi adhabu ambayo ningeipata isingekuwa kifani. Wazo ambalo lilinifanya nisahau kabisa ndoto ya kurudi shuleni pale na kuomba msamaha.

Zaidi ya hayo, hata kama ningerudi na kusamehewa ningeishi maisha gani shuleni pale bila kuwa kituko na kichekesho kwa kila mtu kwa miaka nenda miaka rudi? Sikuwa radhi kwa hilo.

Halafu, hata kama ungetokea muujiza nirejee shule na yote mengine yasahauliwe, jambo moja tu lisingeweza kusahauliwa kamwe. Hirizi. Kwa vyovyote vile msamaha wangu

na kutakasika kwangu kungeendana na kuiteketeza hirizi ile hadharani, hirizi ambayo ni urithi wangu pekee! Kiungo cha mwisho kati yangu na familia yangu!

Mara nikaikumbuka hirizi hiyo! Iko wapi? Nilijiuliza nikitia mkono wangu mfukoni kuitafuta. Haikuwemo. Nilikagua mifuko yangu yote na kujipapasa mwili mzima, wapi. Hirizi yangu ilikuwa imepotea, bila shaka katika zile purukushani za kukimbia!

Nilihisi nikiishiwa nguvu. Kwa muda nilipoteza mapigo kadhaa ya moyo, huku macho yakiingia kiza. Hirizi yangu ambayo ilikuwa kila kitu maishani mwangu. Hirizi ambayo ilisababisha nipoteze kila kitu maishani mwangu! *Imepotea!*

Wanasema binadamu katika uhai wake, anaweza kufa kidogo! Kama madai hayo ni ya kweli basi mimi Petro Kionambali, siku hiyo, chini ya mti ule wa mvule nilikufa kidogo.

Na hata pale uhai uliponirejea sikuwa mtu yuleyule tena. Sikuwa na pa kwenda. Nisingeweza kurudi Kashozi kwa mzee Buberwa na kumsimulia kuwa nimeshindwa shule wa ajili ya hirizi. Kadhalika, nisingeweza kurudi kwetu Buha na kumwambia babu na wazazi wangu kuwa nimeacha shule kwa ajili ya hirizi ambayo haipo tena. Shule nako kusingeendeka. Iko wapi hirizi tuichome? Ningeulizwa kabla ya mengine yote. Imepotea! Linge kuwa jibu langu. Nani ambaye angeniamini? Zaidi nani ambaye angenithamini? Haikuwepo namna.

Ghafla nikajiona yatima. Hapana, nilikuwa mwana mpotevu, asiye na mbele wala nyuma.

Nikainuka na kujitazama. Tayari nilikuwa kijana mrefu kuliko watu wote katika familia yangu. Nilikuwa mwembamba lakini mkakamavu. Mikono yangu ilikuwa na nguvu, miguu

yangu ikiwa na uwezo. Zaidi ya kaptula, shati na viatu nilivyovaa sikuwa na chochote mkononi wala mfukoni mwangu. Nilikuwa masikini. Lakini nilijiamini. Afya yangu, elimu yangu na ari yangu vilifanya niamue jambo moja; sirudi kwetu wala sirudi shule. Nitapiga mguu, kutafuta maisha upya. Hata kama nitaifika mwisho wa dunia!

* * *

Nilipiga mguu kuelekea Kanazi. Nilifika usiku sana. Kwa kuhofia kuwa habari zangu zilishafika hapo nililala porini, juu ya mti. Alfajiri nilianza tena safari. Kiguu na njia hadi Muhutwe. Hapo niliomba hifadhi kwa wavuvi waliokuwa wamejenga vibanda vyao pwani. Hawakuwa na hiyana, ingawa mavazi ya shule niliyoyavaa yalifanya wanishuku kuwa nimetoroka shule. Sikukosa uwongo wa kuwaambia hata mashaka juu yangu yakaisha.

Katika elimu yangu fupi shuleni nilikuwa nimepata ufahamu wa kutosha wa Jiografia. Baada ya kughairi kurudi kwetu au kwenda kwa mzee Buberwa niliamua kwenda nchi ya Wasukuma. Mengi yalikuwa yakizungumzwa juu ya nchi hiyo ambayo nilitamani kuyaona kwa macho.

Zilikuwepo hadithi za Msukuma aliyeitwa Ng'wanamalundi ambaye alisemekana kuwa mganga aliyewashinda wachawi wote kwa kutumia ngoma zake. Mtu huyo wa miujiza alisemekana pia kuwa alikuwa na macho yenye nguvu za ajabu, ambayo yaliweza kukausha miti na hata binadamu aliowakazia macho, jambo lililopelekea awe akitembea huku akiwa amejifunga kitambaa usoni kufunika macho yake. Mtu huyo alidaiwa kuwa katika moja ya hafla zake alipata kukausha msitu mkubwa na mamia ya watu waliokuwa mbele

yake. Jambo hilo liliifanya serikali ya mkoloni imkamate na kumhukumu kunyongwa. Lakini hakuna aliyethubutu, kwani kabla ya hukumu hiyo kutekelezwa alifungwa katika kimojawapo cha visiwa vidogovidogo vilivyo baharini katika pwani ya Bahari ya Hindi, huko Dar es Salaam. Hata hivyo, ilielezwa kuwa Ng'wanamalundi huyo kila jioni alionekana katika vilabu vya pombe Dar es Salaam akiwa amevuka bahari kwa kutembea juu ya maji. Wakoloni wikalazimika kumwachia.

Sifa nyingine ya nchi ya Wasukuma ni zile hadithi kuwa kulikuwa na milima ya mawe, ama majini ama nchi kavu. Baadhi ya milima hiyo ilielezwa kuwa ilikuwa katika maumbile ya binadamu, ikiwa imesimama miaka nenda rudi kama inayosubiri mwujiza fulani utokee, ili ipate uhai na kuanza kutembea kama binadamu wengine.

Nchi hiyo pia ilikuwa ikisifiwa sana kwa ukubwa wa ardhi na wingi wa rutuba yake. Kilimo cha mazao ya chakula na yale ya biashara kama pamba na katani kilielezwa kuwa hakikupata kumtupa mtu. Kwa bahati mbaya, mimi sikupata kuwa mkulima wa haja. Wala sikuona kama ningeweza kuwa na ustahimilivu wa kulima leo kusubiri mavuno miezi au miaka kadhaa baadaye. Mimi nilikuwa mtu wa maji. Mtu wa kutupa nyavu na kuzitupa huku tayari zimejaa samaki! Hivyo, sababu kubwa iliyonipa msukumo wa kutamani kufika huko hasa lilikuwa ziwa. Jiografia yangu ilionyesha kuwa Wahaya na Wasukuma walichangia ziwa hili. Wakati Wahaya wakiwa Magharibi wakilitumia kwa shughuli zilezile.

Kwa kuzingatia hali yangu ya kutokuwa na kazi wala ujuzi wowote wa kuweza kupata ajira nyingine nililichukulia ziwa hili kuwa mkombozi wangu pekee. Nilitegemea ziwa

liniajiri, linilee, kwani taaluma ya uvuvi niliyoipata katika likizo zangu ilitosha kabisa kunipatia ajira hiyo.

Ni kwa mtazamo huo ndipo nilipojikuta nikijiunga na vikundi mbalimbali vya uvuvi kwa lengo la kujipatia fedha. Siku zote za uvuvi wangu nilifuata ziwa kuelekea upande wa kushoto kwangu badala ya upande wa kulia. Kama ningeelekea kushoto, ningelazimika kufika Uganda na baadaye Kenya, kabla ya kuingia Tarime, Musoma, Bunda hadi kufika Mwanza. Ingekuwa safari ndefu isiyo na sababu yoyote.

Mimi nilielekea kulia. Nilivua katika pwani na visiwa mbalimbali kama Bambire, Iroba, Rubondo na Nyamiende. Ilikuwa safari ndefu na ngumu sana. Takribani mwaka mzima uliishia njiani. Ama nilikwamishwa na ukosefu wa majahazi yanayoelekea huko nilikokuwa nikielekea, ama upepo mkali wa siku kadhaa ziwani ulifunga kabisa njia. Msimu wa masika ulioambatana na mvua kubwa za radi na mingurumo ya kutisha ni miongoni mwa sababu nyingine iliyonichelewesha njiani. Nililazimika kusubiri kwa zaidi ya miezi minne katika kijiji fulani huko Biharamulo.

Urefu huo wa safari ulikuwa na faida moja. Kwanza, ulinipa fursa ya kupata ukomavu na uvumilivu mkubwa katika pilikapilika za ziwani na nchi kavu. Ningeweza kuvumilia mvua ya siku mbili au tatu ikinipiga mwilini, niliweza kustahimili jua kali linalochoma kama mkaa wa moto. Niliweza pia kuipuuza njaa kwa muda mrefu. Zaidi, mwili wangu ulijenga uwezo mkubwa wa kuyashinda maradhi madogomadogo kama homa au tumbo bila haja ya kutumia dawa za madukani au mitishamba tele niliyopata kuelekezwa na babu.

Faida nyingine kubwa niliyoipata kutokana na urefu wa safari hiyo ilikuwa udugu. Nilikutana na watu mbalimbali,

nikashirikiana nao kwa hili na lile na kujikuta nimepata ndugu na marafiki tele, ambao kila nilipoondoka kuendelea na safari yangu walisikitika sana, lakini haikuwa kabla ya kunitakia kheri na baraka za safari.

Nilikosa raha kiasi pale tulipofika kisiwa cha Kome tukikaribia kabisa Mwanza. Rafiki zangu hao walishauri tubadili mwelekeo na kwenda kwanza Ukerewe. Tulifika Nansio. Tukafanya shughuli zetu za uvuvi hapa na pale, katika kijiji hiki na kile hadi tukajikuta tumeingia katika kisiwa kingine kidogo kiitwacho Ukara.

Ulipata kuona au kusikia juu ya mawe yanayocheza muziki? Kama hujapata hata kusikia mwenzio niliyaona kwa macho yangu katika kisiwa hicho cha Ukara. Kisiwa hicho kina mawe yaliyokaa kiajabu ajabu. Mtu anaweza kufikiria kuwa yalipangwa na binadamu, kwani baadhi yako juu ya mengine, yakiwa yamegusana kwa sehemu ndogo sana lakini hayadondoki si kwa mawimbi wala dhoruba la ziwani. Nilikuwa nikiyakodolea macho mara kwa mara mawe yale hadi mwenzangu mmoja aliposema, “Unashangaa kuyaona yalivyokaa, jee ukiyaona yanacheza?”

Nilidhani ni mzaha. Tulipobishana jamaa hawa walinipeleka katika kijiji cha Kome, ambako tulipata mwenyeji aliyetupelekeka eneo la Kululibha yalipo mawe haya ya ajabu. Mwenyeji wetu alitoa amri kwa lugha yake ya Kikara. Mara mawe hayo yakaanza kucheza kama watoto mapacha moja juu ya jingine. Hadi leo sijui ni kitu gani kinachotokea hadi mawe hayo yamtii binadamu.

Lakini huo si muujiza pekee wa Ukara. Pale kijijini kuna kisu chenye makali pande mbili. Unapotokea uhalifu wa aina yoyote watuhumiwa hupelekwa kwa mtaalamu na kuamriwa

kukalia kisu hicho. Lakini si kwa mhalifu. Yeye hukatwa mara moja, hata awe amevaa nguo nzito kiasi gani. Kwa yale niliyoyaona, ya mawe kucheza, sikuwa na ubishi wowote kwa jambo hilo.

Maajabu mengine ambayo niliyaona kwa macho yangu, ni mti mmoja kijijini Chilabi huko Ukara. Mti huo ulipigwa na radi ukang'oka. Wenyeji wakaanza kujipanga ili waupasue mbao na kuni. Wakati kabla kazi hiyo haijaanza, mti huo ukiwa umesimama na kuota tena palepale ulipokuwa awali. Hata hivyo, haukuwa na majani. Mti huo upo hadi leo. Niliutazama, nikaupapasa. Unaonekana mkavu lakini unaishi.

Maajabu hayo yalifanya tulipoanza tena safari ya Mwanza niwe nimechangamka zaidi.

SURA YA TANO

Nawa Chifu Wa Wasukuma

Wakati huo nchi ya Wasukuma ilikuwa eneo kubwa kuliko yote nchini Tanganyika, lililojumuisha wilaya za Shinyanga, Maswa, Mwanza, Kwimba na Geita. Wilaya tatu za mwisho zikiwa zinapatikana na ziwa Vitoria.

Isipokuwa kwa tofauti ndogo za kimatamshi baina ya Wasukuma na Wanyamwezi ambao walienea zaidi maeneo ya Tabora, wakazi hawa walichukuliwa kama kabila moja ambalo liliongozwa kwa idadi ya watu. Eneo hili lililokadiriwa kuwa na ukubwa wa kilometa za mraba 20,000 miaka ya 1945 na 1950 lilikisiwa na kuwa na watu wapatao milioni moja hivi.

Kabla ya wahamiaji wengi walioingia eneo hili kwa sababu zile na hizi makabila mengine ya asili katika eneo hilo yalikuwa pamoja na jirani zao wa sasa Wanyamwezi, ndugu zao Wanyantunzu na Wasukuma wenyewe.

Zaidi ya mandhari ya kuvutia ya ziwa, eneo hili lilifurika utajiri wa asili. Licha ya ardhi ya kandokando mwa ziwa kuwa na rutuba tele iliyokubali mazao mbalimbali, mbuga kama zile za Serengeti, zaidi ya kuvutia macho zilijaa wanyama wa kila aina. Aidha, licha ya mibuyu mikubwa yenye umri wa miaka nenda rudi ilikuwepo misitu mikubwa iliyobeba miti ya asili

aina mbalimbali ambayo baadhi ilipanda juu kwa takriban mita mia moja.

Kama ilivyo kwa Wahaya, Wasukuma na Wanyamwezi waliunganishwa na watawala na kijadi, ambao wengi wao walikuwa na asili ya wa Hima waliotokea Uganda baada ya kuwashinda maarifa ya utawala wale wa kibantu waliokuwepo. Watawala hawa ambao waliitwa *Watemi*, wasaidizi wao waliitwa *Banagwa*, walikuwa na nguvu nyingi za kiuchumi kutokana na kodi walizokuwa wakitoza raia wao na maeneo makubwa ya ardhi walizomiliki. Kiutawala, pia walikuwa na mamlaka makubwa kiasi kwamba kutoa hukumu ya kifo na ikatekelezwa lilikuwa jambo la kawaida.

Hayo na mengine mengi niliyajua siku mbili tatu tu baada ya kufika Nyamagana ambako kwa namna ya ajabu nilipata hifadhi katika himaya ya Chifu Masanja mwana Kasanga.

Hadi leo sijui kama tukio hilo lilikuwa mwendelezo wa bahati iliyotokana na hirizi au la baada ya hirizi kupotea. Ilikuwa ndio kwanza tumemaliza safari yetu, ambayo ilituchukua muda mrefu. Tulikuwa wanne, mimi, mzee mmoja na vijana wawili walionizidi kidogo umri.

Nilikutana na wavuvi hao katika kisiwa cha Kome ambako walikuwa wakivua samaki aina ya sato na kuwakausha kwa moto. Nilikaa nao kwa zaidi ya wiki moja kabla hawajaamua kurudi Nyamagana ambako walinielekeza kuwa ndiko yalikuwa makazi yao.

Mara tulipofika nchi kavu na kuvuta mtumbwi ule, tulijikuta tumezungukwa na vijana wapatao kumi waliovaa nguo za aina moja na kufunga vitambaa vyekundu kichwani. kila mmoja alikuwa na mkuki mkono mmoja, rungu mkono

wa pili. Tuliamriwa kuketi chini, juu ya mchanga na kuanza kuulizwa maswali kwa lugha za Kiswahili na Kisukuma.

Mimi, nikiwa sijui Kisukuma, sura yangu ikiwa ngeni mbele ya watu hao ambao baadaye nilifaahamishwa walikuwa vijana wa Chifu, nilijikuta nikiwa mtuhumiwa namba moja mara hiyohiyo.

“Tuambie wewe ni nani... Unatoka wapi... Na unakwenda wapi...” aliamuru mmoja wao huku wenyeji wangu wakiruhusiwa kurejea makwao.

Waliniuliza kwa Kisukuma. Lafudhi yao haikutofautiana sana na Kiha au Kihaya. Niliwaelewa lakini sikuweza kuwajibu kwa lugha yao. Niliamua kuwajibu kwa Kiswahili “Mimi ni mimi. Sijui niendako wala nitokako.”

Walishindwa kuona mzaha katika jibu langu. Mmoja wao, mfupi, mnene mwenye tumbo kubwa zaidi ya umbile lake lilivyoruhusu alionyesha kukasirika sana. “Mnaona?” alisema “Huyu ni *mrugaruga*, mfungeni kamba twende naye.”

“Twende wapi?” nilihoji hofu ikianza kuniingia “Halafu nyie ni nani kwanza?”

“Unaona?” alifoka tena yule mnene ambaye alionekana kiongozi wao. “Anatuuliza sisi ni nani, mfungeni kamba.” Aliamuru tena.

Amri yake ilitekelezwa. Nilifungwa kamba za mkononi na kiunoni. Mmoja wao alishika ile ya kiunoni na kunivuta kama mbuzi. Ili kukwepa kuburuzwa nilikaza mwendo na kuwa nao sambamba.

Tulipita hapa na pale. Watu wengi waliwaona wakija, hasa vijana wa kiume, walitimka mbio na kutokomea maporini. Ajabu ni kwamba baada ya kunipata mimi hawakuonyesha nia ya kukamata mtu mwingine.

Katika maongezi yao, ingawa walipenda sana kuzungumza kisukuma, nilibaini kuwa mmoja wao alikuwa ‘akida’ ambaye ni mwakilishi wa serikali katika kaya mbili tatu za eneo hilo. Wale wengine walikuwa wasaidizi wa ‘Mwanangwa’ aliye msaidizi wa Chifu. Aidha, nilibaini kuwa jukumu walilopewa na chifu lilikuwa la kukamatwa kijana au vijana wenye umri wangu na kuwakabidhi kwake. Hakuna kati yao aliyefahamu Chifu alimhitaji kijana huyo kwa lipi, nilibaini kupitia maongezi yao.

Laiti wangepahamu hofu iliyonishika kwa taarifa hiyo, nina hakika kuwa watekaji wangu hao wangepahurumia na kuniacha niendeleo na hamsini zangu badala ya kunipeleka kwa mtemi huyo. Hawakujua kuwa nilitoroka nyumbani kuja Uhayani kwa ajili ya Watemi haohao ambao walitaka kunitoa kafara ili kuleta mvua! Hivyo, ni dhahiri kuwa hawakujua pia kujihusisha na mtu yeyote mwenye madaraka au mamlaka ya Utemi au Uchifu kwa namna yoyote ile, kwani lolote lingeweza kutukia.

Nilitetemeka! Machozi yalinilengalenga. Kwa bahati nilikuwa nyuma yao, hawakuiona hali yangu. Nikaamua kujikaza huku nikianza kubuni njia za kutoroka mara itakapotokea fursa yoyote ile.

Wakati huo kichwa changu kilikuwa kikijiuliza maswali mengi kuliko majibu. Inawezekana kuwa mganga mwingine ametabiri shida ya mvua na kupendekeza kafara ya binadamu ambaye ameondokea kuwa mimi tena? Au watu weupe huko kwao wamenzisha vita nyingine kubwa kama ile iliyoitwa vita kuu, ya mwaka 1914 hadi 1918 ambayo waliwakamata babu zetu kwenda kuwasaidia bila khiari yao? Au ameibuka Mtemi Milambo mpya, aliyewachachafya sana Waarabu na

kuwakomboa mateka wao hadi alipofariki 1884, ambaye Mwingereza ameona hana jinsi ya kumshinda bila vijana wenye asili yake? Au kazi ya ujenzi wa reli ya kati, uliokamilika mwaka 1914 imeibuka tena hivyo wanahitajika manamba wenye damu changa?

Nilijiuliza mengi. Hadi tunafika katika himaya ya Mtemi au Chifu Masanja mwana Kasanga, sikuwa na jibu lolote zaidi ya mzigo wa hofu, mshangao na mashaka tele kichwani.

Mapokezi niliyoyapata katika himaya hiyo yalikuwa muujiza mwingine. Nilipelekwa moja kwa moja katika nyumba ambayo baadaye nilifahamu kuwa ilikuwa ya mke mkubwa wa Chifu. Mmoja kati ya wake zake kumi, ambao kila mmoja alijengewa nyumba yake na kuishi na wasaidizi wake, wake kwa waume, jambo lililoufanya mji huo wa Chifu kuwa kama kijiji kidogo chenye watu wapatao mia mbili hivi. Ng'ombe mia saba, mbuzi elfu moja, kuku, bata na njiwa wasio na hesabu walifanya kijiji hicho kiwe kama mji mdogo ndani ya mji.

Mama Chifu, mtu mnene wa maungo, ambaye mvi zilianza kumeza sehemu kubwa ya nywele zake fupi, alinitazama kwa makini kwa dakika mbili au tatu. Akatikisa kichwa. “Mara akawageukia wale walionikamata na kuwauliza, “Kwa nini mmemfunga kamba?” hakusubiri jibu lao, “Mfungueni mara moja,” aliamuru, amri ambayo ilitekelezwa mara moja.

“Chifu amepumzika,” mama huyo aliongeza. “Hapendi kuamshwa katika usingizi wake wa mchana. Kijana huyu amefika. Mwache aoge, ale, alale. Kesho ataonana na Chifu.”

Watekaji wangu waliondoka zao. Wasaidizi wa mama huyo wakapokea jukumu hilo. Nilitayarishiwa maji ya moto, ambayo sikupata kuyaoga kwa muda mrefu. Nilipotoka kuoga nilipewa ugali mkubwa kwa kuku mzima. Niliula karibu wote.

Nikaushushia kwa kibuyu cha maziwa ambayo pia nilikuwa na hamu nayo. Baadaye nilionyeshwa chumba cha kulala ambacho kilikuwa na kitanda chenye godoro la sufi. *Kama haya ni maandalizi ya kunitoa kafara, kwa fadhila hii niko radhi!* Niliwaza wakati nikijibwaga kitandani na kuchukuliwa na usingizi mnono uliofanya nisahau shida za mkesho, uchovu na malazi mabaya ya muda mrefu katika safari yangu hiyo.

* * *

Sikuonana na Chifu hadi baada ya siku tatu. Zikiwa siku za kula vizuri, kulala vizuri na kupumzika, huku tayari nimepewa nguo na viatu vipya, nywele zangu zikiwa zimekatwa vizuri, nilimwona Chifu akinitazama kwa makini kabla ya kutikisa kichwa kama alivyofanya mkewe na kisha kutabasamu.

Nilikuwa nimepelekwa kukutana naye katika *'Ikulu'* yake, chumba kikubwa chenye viti vipatavyo mia moja vilivyoelekea kwenye kiti chake cha enzi, ambacho kilichongwa kwa mbao za mpingu na fundi anayejua kila aina ya nakshi. Sehemu kubwa ya kiti hicho kilimeremeta kwa aina fulani ya mawe ambayo baadaye nilikuja kufahamu kuwa ni almasi.

Chifu alikuwa amekikalia kiti hicho, mimi nikiwa nimesimama wima mbele yake. Tulikuwa wawili tu chumbani humo baada ya walinzi ambao huwa wako nyuma yake siku zote kuamriwa kuondoka.

“Karibu mwanangu!” Chifu alitamka baada ya kunitazama kwa muda mrefu. “Karibu katika himaya ya Masanja mwana Kasanga, Msukuma halisi aliyewashinda wavamizi na wahamiaji wote. Jisikie uko nyumbani.”

Nilitikisa kichwa kumkubalia ingawa nilikuwa sijamwelewa.

“Hata hivyo, ningependa kukufahamu vizuri, wewe ni nani, kabila gani, ulikuwa ukitokea wapi na kwenda wapi kabla vijana wangu hawajakuleta hapa?” Chifu aliniamuru. Sauti yake ilionyesha upole na upendo kama ya mkewe. Ikanitia moyo.

Nilieleza ukweli juu ya kwetu, Buha, ambako nilizaliwa na kukulia. Kwa hofu kuwa ule mweleka ulikuwa umemwua padri Backhove na kwamba habari za kifo chake zilikwishawafikia huku, nilidanganya juu ya maisha yangu ya elimu. Nilimwambia Chifu kuwa ingawa nilifuata elimu huko kwa Wahaya niliishia kuvua samaki katika ziwa kwa kukosa mtu wa kunisomesha.

Kwa mshangao wangu habari hiyo ilimfurahisha sana Chifu. Alipotabasamu, akacheka kabla hajakohoa kwa kupaliwa na kicheko chake. Baadaye alisema, “Mungu amekuleta nyumbani, upate elimu uliyokuwa ukiitafuta. Utasoma shule ya watoto wa Machifu. Kama ubongo wako unachemka barabara utafika hadi Ulaya. Utakuwa Cheyo lakini Cheyo ataendelea kuwa Cheyo.

Sikumwelewa. Nikamtumbulia macho ya mshangao na kutoamini, macho yaliyojaa maswali ambayo Chifu aliyaona na akaamua kuyajibu, “Nitakuibia siri moja. Nataka ibakie siri, kati yangu na wewe tu. Unaweza kutunza siri?”

Nilikubali.

“Pamoja na umri huu,” Chifu alisema. “Pamoja na kuwa na wake tele hadi leo nimejaliwa kupata mtoto mmoja tu, wa kiume. Anaitwa Cheyo. Tena ana umri kama wako.” Alisita kidogo kabla hajaongeza, “Himaya yangu iko mashakani. Nikifa himaya itapotea mali zangu zitaparanganyika. Hivyo, walipokuja wazungu kutaka kumchukua mwanangu huyu wa

pekee ili wampeleke nchi ya mbali akapate elimu, naona tukio hilo litaiweka mashakani zaidi himaya yangu. Nani atarithi Ufalme wangu?”

“Na hata kama akirudi, akiwa amepoteza maadili ya utawala na mila za kabila langu na kuambulia tamaduni za mila za wageni nitakuwa nimejiweka katika nafasi gani?” Chifu alihoji na kuishia kujijibu mwenyewe, “Hapana. Nimekataa. Cheyo ni mwanangu. Nitamlea na kumfundisha mwenyewe. Sitaki kuchekwa na Machifu wenzangu wenye watoto lukuki.”

Alisita kwa muda akiwa amejinamia. Alipoinuka alinikazia macho, “Mwanangu,” akasema “Ni hapo unapoingia katika familia. Kama kweli unataka elimu, kama kweli unaweza, nitakupeleka wewe badala yake. Utatumia jina langu na hadhi yangu. Utalelewa kwa upendo na amani maisha yako yote, kama mtoto wangu wa damu.”

Alinikazia tena macho, kwa muda mrefu kama anayejaribu kuusoma moyo wangu. Kisha akaniuliza taratibu, “Unasemaje?”

Niseme nini? Kwanza sikulitegemea swali hilo. Lakini sikutegemea kabisa kuwa matokeo ya kutekwa kwangu majuzi yangukuwa habari njema kama hiyo. *Shule!* Ni kitu nilichoondokea kukipenda kuliko chochote kile katika uhai wangu. Jambo lililofanya nishindwe kuamini iwapo nilichokuwa nimesikia ilikuwa ukweli au niko ndotoni. *Niseme nini?* Sikuwa na la kusema zaidi ya kuhisi machozi ya furaha yakinitoka na kuteleza juu ya mashavu yangu. Nilijaribu kuyafuta kwa mkono wangu ambao pia ulikuwa ukitetemeka.

Chifu hakuhitaji sauti yangu kupata jibu langu. Alielewa. Akainuka na kunikumbatia. “Hutajutia uamuzi wako. Naapa...” alininong’oneza.

Siku mbili tatu zilizofuata zilikuwa za maandalizi ya safari. Niliandaliwa vizuri sana kwa kufundishwa historia ya ukoo na majina ya mababu zao, ambao walikuwa wangu pia. Nilitakiwa kukariri majina hayo pamoja na mambo mengine tele ya kifamilia, kiukoo na kikabila. Haikuwa kazi rahisi.

Kiafya niliandaliwa pia. Ilikuwa nile mayai sita, kuku mmoja, ugali au ndizi za kutosha na kunywa kibuyu kimoja cha maziwa kila siku. “Ili ukifika pale ufanane na mtoto wa Chifu,” mzee Masanja alisisitiza. Amri hiyo iliambatana na kulala mapema, kuoga mara mbili kutwa, kuchana nywele zangu na kujipaka mafuta ya mgando mwili mzima. Hilo liliambatana na kununuliwa nguo za maana, viatu vya bei, mfuko wa safari na noti ya shilingi kumi ambayo Chifu alisema ni ya *‘kulinda mfuko.’*

Matokeo ya kazi hiyo yalimshangaza kila mtu, ikiwa pamoja na mimi mwenyewe. Liliibuka dume lililopanda juu, lenye maungo yenye nguvu na afya tele, dume ambalo ile sura ya hofu na mashaka ilitoweka, nafasi yake ikachukuliwa na sura ya ucheshi, iliyojaa matumaini. Sura ya Mtanganyika halisi, aliyependwa na kupendeza kwa kila aliyemtia machoni. Sura ya Mtukwao au Petro mwana wa Karimanzira, mjukuu wa Kionambali. Hapana, sasa nilikuwa Cheyo mwana Masanja mwana Kasanga!

Nilikuwa mimi yuleyule, lakini mpya! Msomi mtarajiwa!

Pamoja na maandalizi hayo ya kuisisimua, kitu kimoja kilikuwa kikisumbua sana akili yangu. Toka nilipokuja katika familia hiyo na kupewa nafasi ya kuwa mwana familia na fursa ya kupata elimu sikuwa nimebahatika kukutana ana kwa ana na mrithi halali wa familia, ambaye nafasi yake ya elimu nilielekea kuipokonya. Ningependa sana kumwona mtu huyu.

Nijue ni mtu wa aina gani kitabia na kimaumbile. Lakini zaidi ningependa kujua msimamo na fikra zake juu ya uamuzi wa baba yake wa kumnyima fursa ya elimu ili awe mrithi na Chifu wa baadaye wa eneo hili.

Nilipata kumuuliza Chifu juu ya hilo, iwapo mwanawe ameridhia maamuzi hayo au la, lakini, kwa mshangao nilimwona Chifu akionyesha dalili za kukasirika kabla hajanijibu kwa mkato, “Yule ni mwanangu. Atafuata matakwa yangu,” jibu ambalo lilinitia mashaka zaidi.

Nilipopata wasaa nilimuuliza bi mkubwa juu ya jambo hilo. “Ni kweli mwanao hataki shule. Ni kweli atafurahi akisikia kuwa nakwenda kule kutumia jina lake na nafasi yake kujipatia elimu? Halafu yuko wapi mbona hajaonekana?”

Mama Chifu alinifumbua macho kidogo. Alisema, “Cheyo alikuwa anapenda shule. Hiyo sio siri. Lakini anatupenda zaidi wazazi wake. Hawezi kututupa kwa ajili ya kujua kusoma na kuandika. Alikubaliana na baba yake na ameachana na ndoto zote za kwenda shule. Amejiandaa kuja kuchukua nafasi yake mara Mungu atakapomchukua baba yake.”

“Yuko wapi?” nilimuuliza.

Nilimwona mama akisita kidogo. Baadaye alisema, “Nitakuibia siri. Chifu amemficha, hadi suala hili litakapokwisha.”

“Amemficha wapi?” nilisisitiza.

“Amemsafirisha. Yuko Misungwi kwa wajomba zake. Watamrudisha hapa mara wewe utakapoondoka na kuingia shule ili Wazungu waache kutuma matarishi wa kumtaka Chifu apeleke mtoto wake shule.”

Kiasi nilifarijika, walao kwa kuelewa ukweli.

Hata hivyo, usiku wa kuamkia safari yangu mashaka

yangu yaliibuka pale mmoja wa wajomba hao wa Misungwi alipofika kwa Chifu akiwa na taarifa ambayo ilimchanganya Chifu mwenyewe na kila mtu katika familia hiyo. Kwamba Cheyo alikuwa ametoweka kwa wajomba zake na hajulikani aliko!

Chifu aliduwaa. Alimtolea shemeji huyo macho makali, yaliyojaa hasira. “Kwa nini hamkumwangalia?” alifoka. “Mtafuteni, arudi hapa!” aliamuru.

SURA YA SITA

Kwa treni hadi Tabora

Safari ya Mwanza hadi Tabora ilikuwa ya kuisisimua sana. Ilikuwa safari yangu ya kwanza maishani kusafiri bila kutumia nguvu za miguu au mikono yangu. Toka Kigoma hadi Kagera hadi Mwanza nilitumia mikono au miguu yangu. Toka Kigoma hadi Kagera hadi Mwanza nilitumia mikono yangu kupiga makasia hadi tulipowasili majuzi. Safari hii kazi yangu ilikuwa kukaa kitako, kando ya dirisha, huku macho yangu yakifaidi kilometa zote 453 za safari kwa kuburudishwa na mazingira aina aina.

Tulisafiri kwa aina mpya ya usafiri iliyotambulishwa nchini na utawala wa Mjerumani, gari moshi. Ujenzi wa reli, vyuma imara ambavyo vilitumiwa na gari moshi hiyo kuteleza juu yake, ambao ulianza huko Darisalama mwaka 1912 uliweza kufika Mwanza 1923, ikiwa moja ya matawi ya reli hiyo lililoanzia Tabora. Reli hiyo, maarufu kama reli ya kati inayokata nchi toka mashariki hadi magharibi na toka kaskazini hadi kusini inakadiriwa kuwa na urefu wa kilomita 2600. Ni moja kati ya kumbukumbu za utawala wa mjerumani, ambazo kamwe hazitafutika katika historia ya nchi hii.

Reli hii ni kiungo pekee muhimu kinachoiunganisha nchi toka bahari ya hindi kwa upande mmoja hadi ziwa

la Tanganyika kwa upande wa pili, jambo linaloifanya iwe tegemeo kubwa kwa usafirishaji wa watu na mizigo si kwa nchi yetu pekee bali pamoja na zile za Burundi, Kongo na Rwanda pia.

Licha ya sababu hizo za kiuchumi reli ilikuwa pia mshirika mkubwa katika masuala ya kiutamaduni na kijamii nchini. Kwanza iliwezesha makabila yapatayo mia na ishirini ya Tanganyika kufahamiana kwa urahisi. Mzaramo wa pwani angeweza kukutana na Mmanyema wa Kigoma, au Mchaga wa Kilimanjaro kufahamiana na Mfipa wa Mpanda kwa urahisi zaidi ya siku zile za akina Livingstone kutumia miaka maporini toka pwani ya Bahari ya Hindi hadi pwani ya ziwa Tanganyika.

Na hilo halikuwa kwa makabila ya ndani tu. Ujenzi wa reli hiyo ulimfanya mkoloni wa Kijerumani alete vibarua wengi wa kazi hiyo toka nchini India. Hawa ni chanzo cha msamiatai wa ‘*kuli*’ neno lililozaliwa kutokana na lile la kiingereza ‘*Coolie*’ wakatii huo likitumiwa kama kashfa kwa vibarua wasio na ujuzi wowote. ‘*Kuli*’ haikutofautiana sana na ‘*manamba*’ wa hapa nyumbani ambao walikamwatwa kwa visingizio mbalimbali kubwa ikiwa kushindwa kulipa kodi ya kichwa, na kupelekwa kufanya kazi za mikono katika mashamba ya mkonge kaskazini magharibi mwa nchi yetu.

‘*Kuli*’ wengi walitoka India, ama walinogewa, ama hawakuwa na uwezo wa kurudi kwao, ama yote mawili, wakaishia kuwa wakazi wa hapa. Leo hii jamii mpya ya akina Gulamali, Manji, Adamjee; na kadhalika inapatikana sehemu yoyote ya Tanganyika; hasa vijijini.

Jing-janga-jing-jang-jing-jang garimoshi lilihangaika kuvuta mabehewa sita wa abiria na manne ya mizigo yaliyofanya tuwe kama joka refu linaloteleza kwa kujikongoja.

Injini ya garimoshi hilo, ambayo sikuhitaji kuambiwa kuwa ilikuwa ikitumia kuni kutengenezea mvuke wa kuiendesha ilikuwa ikitoa moshi mwingi na mzito sana. Moshi ambao ulilala juu ya treni kama wingu jeusi lisilopendeza machoni. Nadhani hiyo ni sababu pekee iliyowafanya waswahili waamue kuita usafiri huo wa ‘*garimoshi*.’

Nikiwa nimeketi raha mustarehe dirishani pangu nililitazama kwa masikitiko ziwa nililolipenda la Nyanza likitokomea machoni mwangu taratibu. Ziwa hilo lilinilea, lilinihifadhi na kunifadhili kwa muda wa kutosha. Ndilo lililonifundisha kuogelea na kutafuta pesa. Ziwa lililonitoa Kagera na kunifikisha Mwanza. Hilo ndilo ziwa ambalo leo naliacha bila kuwa na uhakika wa kuliona tena. “*Nitarudi!*” nilinong’ona taratibu.

“Nini?” jirani yangu, mzee wa makamo ambaye tulichangia kiti, alinihoji akidhani nazungumza naye.

Sikumjibu.

Tukapinda na kupenya katikati ya majabali marefu mfano wa milima. Tuliacha jabali moja baada ya jingine, mbuyu mmoja baada ya mwingine huku tukivuka vijito na mito ya hapa na pale.

Mara tukazama katika mapori na misitu mikubwa, kwa mbali tukawaona wanyama mbalimbali kama ngedere waliokuwa wakirukaruka kwenye miti au mbuzimawe ambao walirandaranda juu ya majabali ya hapa na pale. Katika eneo moja lenye mabwawa tuliwaona ndege aina ya flamingo wenye miguu mirefu na midomo myekundu wakiwinda samaki au wadudu ndani ya maji hayo. Ndege wengine, aina mbalimbali pia walikuwa wakiruka huku na huko kama wanaotushangaa au kutushangilia hadi tulipotokomea.

“Mantare!” Yule jirani yangu aliropoka.

Ikawa zamu yangu kumshangaa, “Nini?” nilimuuliza.

“Tumefika stesheni ya Mantare,” alifafanua.

Kweli. Nililiona garimoshi likipunguza mwendo na hatimaye kusimama kando ya nyumba mbalimbali ambazo zilionekana kuwa za wafanyakazi wa reli hiyo.

Palikuwa na purukushani fulani, watu wakipanda wengine wakishuka. Miongoni mwa watu hao walikuwepo pia wafanyabiashara wenye bidhaa mbalimbali kama vyakula, mapambo na mifugo. Walionunua walinunua, wasionunua tulijifanya hatuoni.

Tulisimama hapo kwa dakika kumi tu. Mara garimoshi hilo lilianza tena safari yake kwa mwendo wake wenye maringo, taratibu kama halitaki na baada ya kuchochea huku likikohoa kwa uzito wa mabehewa.

“Kwimba!” mzee aliropoka tena. Nilikuwa nimeanza kusinzia. Nikafunga macho na kuona tukiingia katika stesheni nyingine. Nikatoa kichwa dirishani na kuwatazama wanaoshuka na kupanda.

Tukaondoka.

Jirani yangu huyo alikuwa amejipa kibarua. Kila tulipokaribiakituofulani nilimsikia akitamkakwanguvu, “Malya,” kisha “Seke.” Sikufumbua macho yangu hadi pale aliponitikisa kwa nguvu huku akiniambia, “Amka tumefika Shinyanga!” nilifumbua macho. Jina la Shinyanga lilikuwa na uzito wake katika kumbukumbu zangu. Hata hivyo, nilimwambia taratibu “Siendi Shinyanga. Nakwenda zangu Tabora.”

“Tabora! Kuna nini Tabora?”

Sikumwelewa, “Kuna nini Tabora?” nikamjibu kwa swali jingine. “Kwani Shinyanga kuna nini?”

Kumbe mzee alikuwa na hamu ya maongezi. Alianza kwa kutabasamu. Baadaye aliporomosha sifa za Shinyanga. Kuna kila kitu ambacho binadamu anahitaji. Ardhi bora yenye rutuba tele. Misitu imejaa wanyama kila aina. Ng'ombe wa hapa wamenenepa na wanatoa maziwa mengi kuliko popote pale. Hata Wazungu wengi siku hizi wanatembelea milima yetu mara kwa mara. Kuna fununu kuwa huko ardhini kuna mali nyingi ambazo huko kwao ni utajiri mkubwa.”

Nilitabasamu lakini sikumjibu. Sikuwa na jibu la haraka.

“Enhe na Tabora?” alihoji.

“Tabora nini?” nilimuuliza.

“Kuna nini Tabora?”

Niliamua kumnyamazisha kwa kumpa kile ambacho nilikipata vitabuni, ambacho nina hakika kuwa alikuwa hakijui. “Tukianza na reli hii tunayoitumia sasa. Roho yake iko Tabora.”

“Kwa vipi?” alihoji akicheka.

“Tabora ni kituo pekee muhimu sana. Pale Tabora ndipo ambapo reli hii inajigawa, moja ikienda Kigoma, ambako inafika hadi ziwa Tanganyika linalotuunganisha na nchi za Kongo, Burundi na Zambia. Pia, kuna reli inayokwenda hadi Mpanda, kusini mwa nchi yetu.”

Wakati akitafakari hilo nilimpa la pili.

“Unaijua *eroplenti*?” nilimuuliza.

“Ndege Ulaya!” alisema akicheka. “Sio najua, nimeipanda mara nyingi.”

“Kutoka wapi kwenda wapi?” nilimuuliza kwa mshangao.

“Burma,” alinijibu. “Kwenye vita kuu ya kwanza nilikuwa mmoja wa wapiganaji tuliorushwa kwa ndege kwenda kusaidia

wenzetu waliozingirwa na maadui,” alisita kidogo kabla ya kuniuliza, “Ndege ina uhusiano gani na Tabora?”

“Tarehe 22 Julai mwaka 1920 ndege ya kwanza kutua nchini Tanganyika ilitua katika uwanja wa ndege Tabora. Ndege hiyo ndogo ya Mwingereza iliruka toka Nairobi Kenya hadi hapa na kuweka historia ya pekee kwa nchi ya Tabora.

Mzee alicheka. “Hilo tu?” aliniuliza.

“Yako mengi, “ nilimjibu. “Yule kiboko wa Waarabu, Mtemi Milambo, aliishi katika ngome yake Iselemagazi iliyokuwa Tabora. Yule Mwingereza Davidi Livingstone aliyekataa kurudishwa kwao na akafia Zambia alipata kuishi Tabora kwa muda, kabla hajahamisha makazi yake Ujiji, Kigoma. Tabora ulikuwa mmoja kati ya miji michache nchini iliyokuwa na watu wengi, toka miaka ya 1700, mji mdogo huo?”

Mzee aliyatafakari maneno yangu. “kichwa chako kinafanya kazi vizuri sana, mjukuu wangu. Naweza kutabiri unakwenda Tabora kufanya nini.”

“Naenda kufanya nini?” nilimjaribu.

“Kusoma,” alinijibu. “Kweli au uongo?”

“Kweli tupu.”

Mzee akacheka kabla hajaongeza, “Naweza hata kukuambia jina la shule unayokwenda.”

“Shule gani?”

“Unakwenda Tabora *School*. Shule ya misheni inayopokea watoto wa machifu. Kweli au uongo?”

“Ni kweli,” nilimjibu kwa mashangao. “Umejuaaje mzee?”

“Uzee dawa. Uzee ni kuona mengi ni kuona mbali. Jinsi ulivyovaa, jinsi ulivyotulia, jinsi unavyoongea, ni wazi kuwa wewe ni mtoto wa Chifu. Na nina imani kuwa utafika mbali katika safari yako ya maisha.”

Nilitamani kucheka, nilitamani kulia. Sikujua nifanye lipi katika hayo. Kwa mara ya kwanza, baada ya muda mrefu nikamkumbuka babu yangu, mzee Kionambali.

Mtoto wa Chifu!

* * *

Tulifika Tabora siku mbili baadaye.

Stesheni ya Tabora ni sehemu moja yenye kila aina ya pilikapilika. Ilikuwa na watu wengi wenye purukushani hii na ile, huyu akihangaika kupanda behewa, huyu akishuka, yule akibadili behewa kuhamia lile, huyu akipiga kelele kuuza asali na bidhaa nyingine na kadhalika na kadhalika. Lakini purukushani kubwa zaidi ilikuwa ya magari moshi yenyewe. Vichwa vilikuwa vingi mno, vikienda hapa au pale, kuhamia reli hii au ile huku vikicheua moshi na honi za mara kwa mara, hali iliyofanya pawe mahala ambapo mtu asingependa kukaa kwa muda mrefu.

Nilishuka, nikachukua mzigo wangu na kutoka nje ya stesheni. Huko nje kitu cha kwanza kilichovuta macho yangu ni wingi wa maembe. Barabara nzima toka stesheni hadi mjini zilizingirwa na miembe mikubwa, kila upande kwa namna iliyofanya iwe na kivuli murua cha kulisimua. Nilipiga hatua moja kwenda nyingine kuifuata barabara hiyo ya aina yake. Kila hatua ilinifanya nione kuwa wingi huo wa miembe haukuwa wa kando ya barabara pekee. Mapori yote ya mji yalitawaliwa na miembe mingi, mikuwa, ambayo baadhi ilikuwa na maembe yaliyoiva, ambayo yalionyesha kuwa watoto wa mji huo walishachoka kuyala.

Mji wa Tabora ulikuwa mdogomdogo, wenye nyumba za kawaida, ambazo hazikutofautiana sana na zile za Mwanza. Tofauti pekee kubwa niliyoiona ni mavazi na lafudhi. Kimavazi

nilishangaa kuona watu wengi wakiwa wamevaa mavazi yenye asili ya Kiarabu, kanzu nyeupe na kiko mdomoni kwa wanaume na baibui jeusi lililofunika moja ya kumi ya mwili isipokuwa sehemu ndogo ya uso kwa wanawake. Katika mazungumzo yao nilibaini pia kuwa lafudhi ya wengi wao ilikuwa ya Pwani zaidi. Japo walizungumza kwa namna iliyofanya nihisi ama wanaibembeleza lugha ama inateleza kwenye ndimi zao.

‘Karibu Tabora mwanangu!’ nilijikaribisha.

Nikauliza njia ya kwenda shule ya Tabora School. Nikaelekezwa. Nikaifuata njia hiyo taratibu, mzigo mkononi, mluzi mdomoni, ndoto za mafanikio zikiwa tele moyoni.

Nilipokelewa na mlinzi nje ya geti la kuingilia shuleni. Nikajitambulisha kwake. Alinifungulia geti na kunielekeza iliko ofisi ya mkuu wa shule. Nilikwenda kwa mwendo wa kujiamini, huku nikiwa tayari nimetoa barua yangu ya utambulisho toka kwa *‘baba yangu,’*

Chifu Masanja mwana Kasanga. Wanafunzi wenzangu tayari walikuwa madarasani. Niliweza kuwasikia baadhi ya walimu wakifoka kwa sauti kubwa katika jitihada za kujaribu kuingiza kitu fulani katika vichwa vigumu vya wanafunzi.

Karani wa mkuu wa shule alinipokea, akaipokea barua yangu na kuiingiza chumbani kwa bosi wake. Muda mfupi baadaye niliitwa katika ofisi hiyo.

Mkuu wa shule alikuwa Mzungu. Mtu mnene miraba minne, ambaye angefaa zaidi kuwa mwalimu wa ngumi badala ya taaluma. Nilimkuta kasimama nyuma ya meza yake, barua yangu ikiwa mkononi mwake. Alinikazia macho makali kwa dakika moja au mbili kabla hajatamka neno moja tu “Keti.” Nikaketi kwenye kimoja wapo cha viti viwili vilivyomuelekea mwalimu mkuu, miguu yangu ikianza kupoteza nguvu, mikono

ikianza kutetemeka kwa sababu ambayo sikuifahamu.

“Barua yako hii?” alinihoji baadaye.

“Ndiyo.”

“Umeipata wapi?”

“Kwa nini? Nimepewa na Chifu... baba... nikuletee.”

“Chifu nani?”

“Masanja mwana Kasanga.”

Mkuu huyo wa shule alinitazama kabla hajaongeza swali jingine, “Unaitwa nani?”

Nusura nitaje jina langu halisi. “Cheyo,” nikatamka.

Nilimwona mkuu wa shule akizidi kushangaa. Mara akawa kama kakumbuka jambo. Akatoka na kumnong’oneza jambo karani wake. Kisha akarudi na kuketi. Muda mfupi baadaye mlango uligongwa, mwanafunzi mmoja akaingia na kuelekezwa kuketi kiti cha pili kilichokuwa wazi.

Mkuu wa shule akimkazia macho kama alivyofanya kwangu kabla ya kumuuliza, “Ulisema wewe ni nani, unatoka wapi na baba yako ni nani?”

“Naitwa Cheyo. Kwetu Mwanza. Mimi ni mtoto wa Chifu Masanja mwana Kasanga.”

Miguu yangu iliishiwa nguvu. Nilitamani ardhi ipasuke, inimeze yaishe. Ardhi haikufanya hivyo. Nikahisi nimeanza kutetemeka mwili mzima, jasho jembaba likinitoka.

Mkuu wa shule alikuwa akinitazama kwa makini.

“Nani anasema uongo, nani anasema ukweli kati yenu?” aliniuliza. “Juzi tu,” aliongeza. “Alikuwa huyu kijana, akatuambia kwamba anaitwa Cheyo na ni mtoto wa chifu Masanja. Kwa maelezo yake baba yake hataki aje shule, anataka akae nyumbani kusubiri kurithi Uchifu wake atakapokufa. Kwamba amekuja hapa shuleni kwa kutoroka baada ya

jitihada za kumsihi baba yake kumruhusu kushindikana. Na kwa jina na nafasi yake ilikuwa wazi bado tumempokea na kumruhusu kuendelea na masomo. Leo umekuja wewe. Unadai wewe ni Cheyo mtoto wa Chifu Masanja na una barua yake ya kuomba upokelewe hapa. Nataka kujua nani mkweli nani mwongo kati yenu,” aliniuliza akitutazama kwa zamu. Cheyo naye alishangaa. Akageuka kunitazama. Nilijitahidi kuinua uso wangu nimtazame pia, ilikuwa kazi ngumu kuliko zote nilizopata kufanya. Hicho kidogo nilichobahatika kuona katika uso wake kilionyesha wazi kuwa si kwamba hatufahamiani tu, bali pia tulikuwa hatufanani kwa namna yoyote ile. Pale ambapo mimi nilikuwa mng’avu yeye alikuwa mweusi tii, pale nilipokuwa mrefu yeye alikuwa mfupi na mwenye kiribatumbo.

“Mnafahamina?” mkuu wa shule aliuliza baada ya kutupa dakika za kutumbuliana macho.

Wote tulitikisa vichwa kukataa.

Mkuu wa shule akacheka, “Iweje watoto wa mtu mmoja, tena waotumia jina moja wawe hawafahamiani?”

Hatukumjibu.

Haikumchukua mkuu wa shule muda mrefu kubaini ukweli wa mambo hayo. Kutokana na udadisi wa Chifu Masanja juu ya kumpeleka mwanee shule, bila shaka kwa muda mrefu sasa, ndipo akabuni hila ya kuteua mtu mwingine ili aache kusumbuliwa, jambo ambalo limetibuka baada ya mwanawe kutoroka nyumbani na kuja shuleni bila ridhaa wala khiari yake.

Mkuu huyo alinikazia macho kama anayesubiri uthibitisho wa kile kinachopita katika fikra zake bila kutamka. Nilitamani asome jibu la ‘ndiyo’ katika nafsi yangu ili yaishe, niondokane na aibu hiyo. Nadhani alisoma hilo katika macho

yangu, kwani nilimsikia akisema taratibu, “Sipendi kucheze. Sipendi kudanganywa. Natoa dakika kumi tu, yule ambaye anafahamu kati yenu kuwa si mtoto halali wa Chifu masanja aondoke mbele yangu na ndani ya eneo la shule yangu. Vinginevyo, nitamchukulia hatua kali za kisheria.”

Sikungojea dakika hizo kumi. Moja tu ilinitosha. Niliinuka, nikachukua begi langu na kutoka taratibu. Nyuma yangu nilisikia kicheko, kicheko ambacho kiliashiria mwisho wa ndoto yangu ya kupata elimu zaidi ya ile ndogo niliyokuwa nayo.

* * *

Niliduwaa kwa muda nje ya eneo la shule. Nilihisi akili yangu ikiwa imedumaa kiasi kwa kuwa mvivu wa kufikiri, hali ambayo ilitokana na uchovu wa ubongo wangu kwa ajili ya tukio hilo zito. Nikatafuta kivuli na kukaa.

Kelele za wanafunzi ambao walikuwa wakitoka, ndizo zilionizindua hapo chini ya mwembe nilipoketi. Nikainuka nikachukua begi langu na kuitumia miguu yangu kuniondoa hapo. Sikujua naelekea wapi. Lakini sikushangaa pale miguu yangu iliponifikisha stesheni ya treni, mbele ya dirisha la mkata tiketi.

“Nipe tiketi,” nilimwamuru.

“Ngapi?”

“Moja.”

“Ya kwenda wapi?”

Niende wapi? Nilijiuliza. Sikuhitaji kujiuliza sana, “Tiketi yoyote ile. Kigoma, Dar es Salaam au Mpanda,” nilimjibu.

Mkata tiketi huyo alinitazama kwa macho ya mshangao wa muda, akinichungulia toka katika kijidirisha chake.

“Unaumwa?” baadaye alinihoji.

Sikutarajia swali hilo, “Kuumwa! Kuumwa nini?”

“Chochote kile. Kama akili hivi?”

Ikawa zamu yangu kumshangaa, “Kwa nini uniambie hivyo?” nikafoka.

“Mtu yeyote asiyejua anakokwenda ama ni mngonjwa wa akili, ama ameiba anataka kukimbia. Wewe uko katika kundi gani katika hilo?”

Lilikuwa swali la kifedhuli kuliko yote. Lakini nadhani alikuwa akinitendea haki. Mwenyewe pia nilianza kujishuku. Ninakwenda wapi? Ninakimbia nini? Nimechanganyikiwa kwa kupoteza nafasi yangu nyingine ya kupata elimu? Lakini mara ngapi nimesikia kuwa kukosa elimu ya darasa siyo mwisho wa elimu duniani? Wangapi duniani wamefanya maajabu na kuingia katika vitabu vya kihistoria kwa kiwango cha elimu kama yangu au ndogo zaidi.

Wazo hilo lilinifanya niangue kicheko. Nilicheka kwa muda wa dakika mbili nzima mpaka nikapaliwa. Nikaanza kukohoa.

Kicheko changu kilifanya mkata tiketi huyo aamini hisia zake, kuwa *naumwa*. Na siumwi kitu kingine zaidi ya akili. Nilimwona akichukua simu na kuzungusha namba kadhaa. Alizungumza kwa sauti ya kunong’ona huku akiwa amenikazia macho ya tahadhari. Baada ya hapo alifunga dirisha lake.

Huku nikicheka niliinua begi langu na kuanza kuondoka eneo hilo. Lakini sikuweza kupiga zaidi ya hatua kumi kabla sijajikuta nikivamiwa na watu wawili waliovaa sare za polisi, shati na kaptula za kaki, kofia zilizovaliwa upande, soksi na viatu vyeusi. Mkononi kila mmoja alikuwa na rungu.

“Polisi! Tulia kama unanywolewa!” mmoja aliniamuru.

Nikiwa nimeshikwa na mkanda wa suruali kwa nyuma, hali iliyofanya nining'inie juu juu na kutembelea ncha za vidole vyangu sikuwa na nguvu zozote za kujitetea. Niliburuzwa hadi katika chumba chao kidogo ambako nilisukumwa na kufungiwa kwa nje bila kuulizwa swali lolote.

“Nimefanya nini jamani?” niliwapigia kelele.

Hakuna aliyenijibu.

SURA YA SABA

Lyampa Iya Mfipa

Nilipohoojiwa na polisi kwa dakika kumi tu kabla hawajathibitisha kuwa nilikuwa na akili zangu timamu. Lakini ilikuwa baada ya kufungiwa chumbani humo kwa siku nzima.

Alikuwa mmoja kati ya wale walionikamata, akiwa amefuatana na mtu mwingine mfupi, mnene, ambaye alinukia dawa za hospitali. Sikuhitaji kuambiwa kuwa mtu huyo alikuwa daktari, pengine wa maradhi ya akili, toka hospitali ya Kitete. Walipoingia ndani yule daktari aliketi mbele yangu na kunikazia macho. Mie pia nikamkazia macho. Hata hivyo, nusu dakika baadaye niliyakwepa macho yake kwa kuinamisha uso wangu.

Akiwa bado amenikazia macho daktari yule alitabasamu, mimi sikutabasamu. Aliangua kicheko. Mimi sikufanya hivyo. Kisha alitikisa kichwa chake kwa kujiyumbisha huku na kule kama aliyekusudia nifuate mfano wake. Sikufanya hivyo. Nikamwona kama mtu aliyepatwa na mshangao.

“jina lako?”

Nikamjibu kwa kutaja lile nililopewa na chifu Masanja, “Cheyo.”

“Kabila lako?”

“Msukuma. Ingawa sikijui vizuri.”

“Kwa nini?”

“Nilizaliwa na kukulia Buha. Nafahamu Kiha kuliko kisukuma.”

“*Mwakeye!*” Akanijibu.

“Saa hizi sio *mwakeye*, ni *mwidiwe*,” nikamsahihisha.

Akatabasamu. Nadhani akiba yake ya Kiha ilikuwa inaishia pale, kwani alirudi kwenye Kiswahili. “Enhe, una tatizo gani?” alihoji.

“Nadhani hawa walionifungia hapa ndio wenye matatizo. Wamenikamata bila sababu na kunifungia humu bila maelezo,” nilisema kwa sauti yenye hasira.

Daktari huyo alinitazama kwa makini, toka kichwani hadi miguuni. Mavazi yangu yalikuwa safi, viatu vyangu viking’ara kwa kiwi. Hata mwili wangu pia ulikuwa safi, ukimeremeta kwa afya na mafuta niliyopaka kabla ya kwenda mbele ya mkuu wa shule ile iliyonikataa. Begi langu pia lilikuwa safi, jipya, lililofura mali ambazo mgonjwa wa akili hawezi kuwa nazo. Daktari huyo aliacha kunitazama mie akawa akimtazama yule askari. Nilihisi kuwa alikuwa katika wakati mgumu wa kuamua nani mgonjwa wa akili kati yangu na hao walionikamata. “Wamekuhangaisha bure,” alisema baadaye. “Ilikuwa tukukamate, upelekwe Dodoma kwenye hospitali ya wenye maradhi ya akili. Unaonekana huna tatizo loolote.”

Askari huyo hakuweza kunitazama usoni kwa aibu.

Mara niliporuhusiwa, nilichukua begi langu na kurudi katika dirisha lilelile la mkata tiketi. Nilimkuta karani yuleyule bado akiwa kazini. “Nataka tiketi,” nilimwamuru.

Aliponitazama alishtuka kama aliyeguswa na waya wa umeme. “Ya kwenda wapi?” alinihoji kwa sauti ambayo

haikuwa imara kama awali.

“Popote,” nilimjibu kama awali.

Alitazama huko na huko kama anayetaka kuomba msaada. Kisha akasema, “Leo kuna treni mbili. Moja inakwenda Kigoma, itapita usiku. Nyingine inakwenda Mpanda, itaondoka hapa baada ya nusu saa.”

Nipe ya Mpanda.” Nilisema bila ya kufikiri sana.

“Shilingi tano, njia moja.”

“Nipe,” nilimjibu nikimlipa. Nikapokea tiketi na chenji zangu na kuzitia mfukoni. Nikaenda mgahawa mmoja uliokuwa karibu ambapo nilinunua wali kwa maharage, nikayashushia kwa chai ya rangi. King’ora cha abiria wa treni ya Mpanda kilipolia nilikuwa mmoja wa abiria wa kwanza kuiparamia.

* * *

Sikuhitaji kufikiri sana kabla ya kukata tiketi hiyo kwa sababu nyingi. Kwanza, nilikuwa na hisia kuwa Tabora haukuwa mji wangu wa bahati. Kuumbuliwa na mkuu wa shule kwa kiwango kile kulinitia doa na dosari kubwa iliyofanya nijisikie aibu isiyo na kifani. Mimi sio yatima. Nina baba na mama. Nina babu mwerevu kuliko mamia ya mababu ninaowajua. Kiu ya elimu haikuwa sababu nzuri ya kunifanya nikubali wazo la kipuuzi la kufanywa mtoto wa kambo wa Chifu Masanja.

Ni wazo hilo lililofanya nitupilie mbali wazo la kurejea Usukumani. Ningemwambia nini Chifu?

‘Nimebainika. Mtoto wako halisi yuko shuleni, kwa hiyo nitafutie hifadhi mpya!’ Aibu iliyoje. Ningemwambia nini mkewe na watumishi wa himaya yake ambao bila shaka wengi waliijua kinachoendelea?

Ndipo nilipowaza juu ya kurudi nyumbani. Nipande garimoshi hadi Kigoma, huko nitafute njia ya kufika Kasulu. Huenda tayari kulikuwa na malori ambayo yalibeba watu na mizigo kama sehemu nyingine za nchi.

Hata hivyo, hilo pia sikulitekeleza kwa sababu tele. Moja ilikuwa aibu. Mwanamume akitoka ametoka. Akirudi ana kitu cha kuonyesha kijijini. Ama vyeti vya kuhitimu masomo yako ama fedha au mtaji au kujenga nyumba bora zaidi. Mimi ningerudi na aibu tupu. Sikuwa tayari kufanya hivyo.

Sababu nyingine iliyonizuia kwenda nyumbani ni babu yangu. Ni kweli alinipenda sana na angefurahi sana kuniona. Lakini sikupenda kujitokeza mbele yake kichwa kitupu, mikono mitupu. Alitegemea nirudi na elimu. Alitegemea nirudi na mali. Kamwe asingefurahi kuona nikirudi mnyonge, kama kindi la ndege, linalotegemea mama akutafutie, akutafunie, umeze.

Lakini kuna sababu nyingine, kubwa zaidi, iliyonifanya nisijisikie kumtazama babu machoni. Hirizi yake. Hirizi hiyo ya familia, ambayo kwa mujibu wa maelekezo yake ilivaliwa na babu yake, baba yake na kisha yeye mwenyewe. Hirizi ambayo ilimpeleka Ughaibuni na kumrejeshha salama. Naam, hirizi ambayo aliivua na kunivisha mimi, badala ya baba, ili nipate kile ambacho aliamini kingeinua ukoo na familia yetu.

Hirizi ambayo nilipoteza kwa uzembe!

Haikuwa kweli kuwa chanzo cha migogoro yangu hii mipya, ikiwa pamoja na kukataliwa nafasi ya kusoma, kwa namna moja au nyingine ilihusiana na kupotea kwa hirizi ile? Mara kwa mara niliwaza.

* * *

Gari moshi liendalo mpanda hulazimika kueleka magharibi kwa kilometa kadhaa kabla ya kuchepuka kuelekea kusini. Kwangu mimi ilikuwa sawa na kuelekea nyumbani, Kigoma. Tuliacha stesheni ya Tabora, tukatafuna reli hadi Usoke. Toka hapo tuliingia Urambo. Tuliacha Urambo na kufika Kaliua ambako tulianza safari ya kusini.

Kama ilivyokuwa safari ya kutoka Mwanza safari hii pia ilikuwa sawa na kusafiri katikati ya bustani ya *Eden*. Kila upande tulizungukwa na ama misitu minene iliyoashiria kila aina ya hazina, ama mapori ya kutisha yaliyoonya juu ya wingi wa mbolea katika ardhi yake.

Mara kwa mara tulipishana na wanyama ainaaina waliokuwa kando wakitushangaa, pamoja na ndege ainaaina walioruka hapa na pale juu ya miti, wakifaidi asali ya maua na wadudu wadogowadogo. Baadhi ya maeneo kulikuwa na mabwawa makubwa yaliyoshawishi kilimo cha mpunga au mito ambayo ilinikumbusha samaki wa ziwa Nyanza.

Toka Kaliua tuliingia Mfulu, baadaye Ugalla na hatimaye tukawasili Mpanda. Huo ulikuwa mwisho wa reli hii, lakini haikuwa mwisho wa safari yangu.

Pamoja na shahuku yangu kubwa ya kuondoka Tabora, ndoto yangu ya kuja Mpanda ilikuwa na malengo yake. Zilikuwepo fununu za hapa na pale kuwa maeneo mbalimbali ya huku yalikuwa dhahabu. Uchimbaji wa dhahabu hiyo sikuona kama kwa namna yoyote ile ungenishinda. Kuchimba udongo hadi ufikie mchanga maalumu kuchekecha mchanga huo hadi uone chembechembe za dhabahu na kuiokoteza, vipi kungenishinda?

Hilo lilikuwa wazo la kwanza. Wazo la pili, ambalo nilikuwa na hakika nalo zaidi ni uvuvi. Toka Mpanda hadi

Ikola au Kerema ambayo ni miji ya kandokando mwa ziwa Tanganyika haikuwa safari ndefu. Ningeweza kufika huko hata kwa miguu. Nilipanga, kama kazi ya kuchimba dhahabu ingeshindikana ningeelekea huko na kujiunga na uvuvi. Ndiyo, nasikia ziwa Tanganyika lina kina kirefu kuliko maziwa yote duniani. Kama kuna ukweli kwa hilo bila shaka samaki wake pia ni wengi zaidi na watamu zaidi. Ningekuwa mmoja kati ya walaji wake. Wala nisingeishia kula tu; samaki hao wangenipatia fedha za mtaji ili nirudipo kwetu nirudi kishujaa.

Hivyo ndiyo ilikuwa ndoto yangu. Kwa bahati, nzuri au mbaya, haikwenda kama nilivyotarajia. Hali hiyo ilitokana na kukutana kwangu ana kwa ana na mtu ambaye sikutarajia kamwe kumwona tena katika maisha yangu, mtu ambaye sikupata hata kulifahamu jina lake. Alikuwa mmoja kati ya wale Wamanyema wawili waliofuatana na Mwarabu katika safari yetu ya miguu toka Buha hadi kwa Wahaya, miaka zaidi ya mitano iliyopita.

Ni yeye aliyeniona kwanza, “We mtoto wewe! Kama nakufahamu vile?”

Nikageuka kumtazama. Mara moja nilimkumbuka, “Mmanyema! Unafanya nini huku?” niliuliza kwa mshangao.

“Wewe je? Umefikaje huku?”

Sikujua nimweleze nini.

“Babu yako hajambo?”

Sikuwa na jibu. Nikainamisha uso kwa aibu.

Nadhani Mmanyema alisoma kitu fulani katika uso wangu, kwani alinitazama kwa muda kabla hajanikaribisha chai kwa mihogo ambayo alikuwa akiila. Nikapokea kikombe cha chai ya maziwa na kipande cha muhogo. Njaa iliyoanza kuninyemelea ikakimbia mara moja.

Wakati tukinywa chai hiyo yapata saa kumi na moja za alfajiri. Gari moshi lilikuwa limechelewa sana njiani kutokana na mafuriko katika maeneo mbalimbali. Ilibidi gari hilo liendeshwe taratibu sana. Tulikuwa tumeketi nje ya stesheni, kwenye benchi la chuma ambalo bila shaka lilijengwa kwa ajili ya wasafiri.

Nilishangaa pale Mmanyema aliponiambia kuwa tulisafiri katika behewa moja toka Tabora hadi hapo. Kuwa aliniona lakini hakuwa na hakika na macho yake hadi aliposikia sauti yangu na kuniona nikimkumbuka.

Alikuwa mzungumzaji sana mzee huyu. Alinieleza jinsi alivyoacha kazi ya kumtumikia yule Mwarabu baada ya kufilisika. “Yaelekea Mwarabu yule hakuwa na ujuzi wowote zaidi ya biashara ya watumwa. Kila alichotaribu kushika kiliteleza. Hata mishahara yetu alishindwa kulipa. Tukaachana naye na kuanza shughuli zetu binafsi,” Alinieleza kwamba yeye sasa alikuwa akifanya biashara ya kununua dagaa toka kwa wavuvi wadogowadogo wa kandokando ya ziwa Tanganyika na kuwauza kwa walanguzi wakubwa ambao waliwapeleka Tabora, Dodoma na Dar es Salaam kwa matumizi ya binadamu na mifugo. Kwamba sasa hivi alikuwa na mtaji wa kutosha ambao utamwezesha kupeleka mwenyewe dagaa hao hadi Dar es Salaam ili apate faida kubwa zaidi. “Toka huku nitanunua nyavu na vifaa vingine vya uvuvi na kuwauzia watu Kigoma na Kongo. Nikijaliwa miaka miwili baadaye nitakuwa mmoja wa matajiri wakubwa wa nchi hii,” alisema kwa kujipamba.

“Sasa unakwenda wapi? Mbona huku hakuna dagaa?” nilimuuliza.

“Nakwenda Sumbawanga.”

“Kufanya nini?”

Alinitazama na kucheka kidogo kabla hajasema, “Unaonekana wewe ni mtoto mdogo sana kuliko umbile lako. Hujui watu huenda Sumbawanga kufanya nini?”

Mie: Sijui

Yeye: Pole sana. Kwa hiyo, hata maana ya jina Sumba - Wanga hujui?

Mie : Sijui

Alitikisa kichwa kwa namna ya kunisikitikia. Kisha alisema, “Sumba-Wanga maana yake ‘*Tupa Uchawi.*’ Kwa maana ya kuwa mji huo ni wa watu wazito, watu waliokomaa. Hivyo, ukiingia huko na vijiuchawiuchawi vyako utaumbuka. Ni huko ambako watu wazima huenda kugangwa, ili wasichezewechewe ovyo kishirikina. Huwezi kufanya biashara kama hujafundwa ukafundika.”

Ilikuwa habari mpya kwangu. Niliipokea kwa mshangao na kutoamini. “Lakini Biblia inasema...” nilijaribu kumwambia.

“Achana na Biblia. Mimi ni Mwislam. Tunatumia Msahafu wa Mwenyzi Mungu. Ulioshushwa toka peponi kwa mkono wa mtume Mohamed S.A.W.”

“Lakini hata Uislam unakataza ushirikina.”

“Kujikinga sio ushirikina. Hayo ni mambo ya wakoloni tu, walipoamua kututawala miili na mioyo yetu. Walitarajia kuwa mila na tamaduni zetu kupotea huku wao wakihifadhi za kwao. Kila binadamu ana nyota na anahitaji kuisafisha mara kwa mara. Kila binadamu ana wahenga ambao anahitaji kuwaenzi kwa sadaka na tambiko. Asiyefanya hivyo kamwe hawezi kufanikiwa.”

Lilikuwa somo jipya kwangu, somo ambalo sikuwa na ujuzi nalo. Nikaamua kunyamaza. Mmanyema alichukulia ukimya wangu kama dalili ya kumwelewa.

“Haya na wewe nieleze ukweli wa kile kilichokufanya ufike huku. Kama nakumbuka vizuri babu yako alikupeleka Uhayani ukasome. Nadhani ulipata shule kwani nilipoonana naye mwaka mmoja baadaye alinidokeza kuwa ulishaingia shuleni,” alisema.

Nusura niruke kwa shauku, “Ulionana na babu?”

“Ndiyo!”

“Wapi?”

“Nyumbani kwenu. Kasulu. Tulilala pale siku mbili na alituchinja beberu mkubwa sana. Babu yako ni mkarimu sana.”

Bila kutegemea nilijikuta nikitokwa na machozi. *Babu yuko hai! Babu alirudi salama!* Sikupata kupokea habari njema kama hiyo kwa miaka nenda rudi.

Sikuiona haja yoyote ya kumficha chochote Mmanyema huyu. Nilimwona kama baba yangu. Kama *malaika*, kwa kuweza kunipa walao fununu tu ya habari za nyumbani. Nikamweleza kila kilichonisibu, toka mwanzo wa mikasa yangu hadi nilipofikia.

Alinisikiliza kwa makini sana, mara kwa mara akitikisa kichwa kwa masikitiko. Mwisho wa maelezo yangu alinishika mkono na kuninong’oneza, “Pole sana mtani. Usijali. Hujafika mwisho wa safari yako kimaisha. Nitakusaidia.”

Nilimwamini. Sikujua kwa nini nilimwamini haraka kiasi hicho.

* * *

Safari ya Ikola au Karema ilikufa. Ndoto ya kuchimba dhahabu nayo ilikufa. Safari ya Sumbawanga ikazaliwa.

Tulikaa kwa siku mbili kabla ya kupata gari lililotufikisha

Sitalike. Hapo tulipumzika tena kwa siku tatu tukifaidi kula nyama pori ambazo zilikuwa tele toka katika mbuga za Katavi. Tukaondoka hadi Kisi, Chala, Nkundi na hatimaye Sumbawanga.

Wakati huo sumbawanga kilikuwa kimji kidogo tu, chenye wakazi wachache lakini kikiwa na mambo makubwa. Mandhari ya mji, ambayo yalipambwa na mlima Malonje wenye urefu wa mita 2418 toka usawa wa bahari, mito na misitu tele yalifanya nitamani kuishi hapo kwa muda mrefu zaidi.

Lakini Mmanyema ambaye baadaye alinitajia jina lake kuwa ni Baraka Khalfan alikuwa na ratiba tofauti na yangu. Alikuwa na majina ya vijiji mbalimbali na waganga mbalimbali ambao alipanga kuwaona. “Huku ni Ufipa, mdogo wangu. Lyampa Iya Mfipa, umepata kulisikia?”

Sikupata.

“Lyampa Iya Mfipa kwa tafsiri ya kawaida ni mlima mdogo tu, ambao unatambaa hadi kando ya ziwa Tanganyika na kupita chini hadi Kongo, katika eneo la Moba, nchi ya Watabwa. Lakini kwa wajuzi wa mambo Lyampa Iya Mfipa linabeba uzito wa pekee. Ni jiwe la tambiko ambalo ukikaangwa juu yake hakuna mtu yeyote atakayekuchoma. Na hayo hafanyiki mjini, isipokuwa vijijini kwa wazee, waliofundwa na babu zao,” alinieleza.

“Watu wengi wenye nafasi zao wamepitia huku. Watu toka sehemu mbalimbali za dunia huja huku kufanyiwa mambo. Watabwa wa Kongo nao huja huku, ingawa ni kweli pia kuwa wazee wa huku katika kuimarisha uwezo wao huvuka ziwa kwenda Kongo,” aliongeza.

Hivyo, zilianza safari za hapa na pale. Mara Chapota, mara Kasanga, mara Wampembe na kwingineko. Safari hizo

zilitufikisha Pwani ya ziwa Tanganyika na kuniwezesha kuona milima ya Kongo mbele yetu na ile ya Zambia kushoto kwetu. Ziwa hilo lilinikumbusha hamu ya kurudi nyumbani, kwani kwa kuambaa nalo tu, nikielekea kulia ningeweza kufika Kigoma. Kwa bahati mbaya, sikuwa tayari kwa safari hiyo.

Mmanyema alikuwa na pilikapilika nyingi. Mara kwa mara aliniacha peke yangu na kwenda hapa na pale na aliporudi alikuwa kachanjwa chale ama za kwenye paji la uso ama katika viwiko vya mikono na miguu. Wakati mwingine alinituma kumtafutia vifaa mbalimbali kama mayai viza, mizoga ya paka au njiwa weusi.

Siku moja aliondoka alfajiri na hakurudi. Nililala peke yangu katika chumba tulichofikia cha mwenyeji wetu mmoja. Kwa kuwa nilikuwa peke yangu nililala mapema sana, mara baada ya chakula cha usiku. Nilipofumbua macho tena ilikuwa alfajiri. Baridi kali iliyotokana na upepo ziwani nadhani ndiyo iliyoniamsha. Nilipotazama huko na huko sikuweza kuyaamini macho yangu. Nililala ndani, juu ya kitanda, lakini niliamka nikiwa nje, tena juu ya mbuyu mkubwa ulikuwa mbele ya nyumba hiyo. Isitoshe nilikuwa mtupu, bila nguo yoyote mwilini!

Nilishuka harakaharaka na kuingia ndani. Nguzo zangu zilikuwa zimetupwa ovyoovyo chumbani humo. Nikaziokota na kuvaa harakaharaka. Ni wakati nikivaa nilipobaini kuwa nilikuwa nimechanjwa chale mbili katika paji langu la uso na kupakwa vitu vyeusi kama masizi ya mkaa.

Nilikosa raha. Niliduwa katikati ya chumba hicho huku nikitetemeka kwa hasira.

Mara mlango uligongwa na kufunguka kabla sijaitikia. Mwenyeji wetu, mzee Imilio Kahigi aliingia ndani. Alikuwa akicheka huku anatikisa kichwa. “Mtoto, mbona unasafiri

ukiwa mwepesi hivyo?” aliniuliza.

Sikumwelewa, hivyo sikumjibu.

“Uko mtupu mno. Mwepesi kupita kiasi. Kwani hukuaga kwenu?” aliuliza tena.

“Niliaga!” nilimjibu.

Alicheka kabla ya kusema, “Hukuaga. Na kama uliaga wazazi wako ni watoto vilevile. Jana watoto wenzako wameamua kukupima baada ya kuona huelewekiheleweki. Wakakuta ni mwepesi mno. Ndiyo maana wakakuacha pale juu ya mti baada ya kukuchezea usiku kucha.”

Sikujua mzee huyo alitarajia jibu gani kwangu. Hivyo, niliendelea kukaa kimya wima, nikiwa nimemkodolea macho.

“Utafanyaje?” aliniuliza ghafla.

Nilijua nitakachofanya. “Nitaondoka, leo hii hii,” nilimjibu.

Alicheka tena kabla hajasema, “Unadhani utafika unakokwenda?”

“Nitafika. Kwa nini?”

“Wenzako wamekutia alama. Popote utakapokwenda wajuzi wa mambo watakubaini mara moja na kukugombea kama mpira wa kona, maana una alama, alama ya shari.”

Nilizidi kuduwaa. Nadhani hata mdomo wangu niliusahau ukiwa wazi wakati nikiwa nimemtumbulia macho.

“Huyu Mmanyema unamfahamu kwa kiwango gani?” Aliniuliza ghafla.

“Simfahamu vizuri. Tulikutana naye safarini miaka mingi iliyopita. Tumekutana naye tena majuzi na kufuatana naye. Basi.”

Mzee Kahigi alitikisa kichwa kwa namna ya kunihurumia sana. Kisha aliongeza swali jingine, “Alikuambia anatafuta

nini huku?”

“Waganga.”

“Wa?”

“Kujiganga. Anataka kinga.”

Mzee akachekeka tena. “Humjui vizuri,” alisema. “Humjui hata kidogo. Huyu bwana anatafuta kizimba, dawa ya mali. Ametakiwa kutoa kichwa cha mtu. Alitakiwa atoe mtoto wake wa kwanza, ageuzwe ndondocha, awekwe chini ya maji kumswagia dagaa. Hana mtoto wake wa kuzaa. Anachofanya sasa ni kukutoa wewe. Utageuzwa akili, utawekwa chini ya maji maisha yako yote, hadi kifo cha kweli kitakapokutokea.”

Sikuyaamini masikio yangu.

“Mmanyema!”

“Naam!”

“Mimi!”

“Naam... tena mipango yake inakwenda vizuri sana. Kesho au keshokutwa utakufa, tutakuzika. Lakini wajuzi wa mambo tutaona tunavyozika mgomba huku wewe ukiongozwa kikondoo kupelekwa ziwani.”

Baada ya taarifa yake hiyo ‘njema’ alinikazia macho kabla hajaniuliza tena, “Utafanya nini?”

Bado sikujua alitaka nimjibu nini, “Nitaondoka,” nilimjibu.

“Nimekwishakwambia umetiwa alama. Hutaifika mbali.”

“Nitaondoka nikafie mbali. Siyo hapa.”

Baada ya kuwaza sana alisema, “Nitakusadia. Utaondoka hapa salama ufike salama kokote uendako. Siwezi kukubali mtu wa kuja afanye ushenzi katika milki yangu. Kaa kama kawaida, kula kama kawaida, usiku ufunge vitu vyako vyote tayari kwa safari.”

Sikujua ilinipasa kumshukuru au la. Kwa ujumla, sikujua kama nilipaswa kumwamini au kutomwamini. Nilichojua ni kwamba maisha yangu yalikuwa katika mashaka makubwa. Unapopigania roho yako, bila kumjua nani adui nani rafiki, sio suala la mzaha.

Nilifanya kama nilivyoelekezwa. Sikumwambia mtu yeyote juu ya masaiibu yaliyonipata usiku huo. Nilioga, nilikula na baadaye kutembeatembea kijijini hapo kana kwamba hakuna lolote la ajabu lililonipata.

Mmanyema alirudi mida ya saa nne hivi. Alionekana mtu mwenye furaha na matumaini makubwa. Huku akitabasamu alinivuta chemba na kuninong'oneza, "Mdogo wangu mambo yamekwisha. Kama nilivyokuambia baada ya miaka miwili tutakuwa watu katika watu. Pesa halitakuwa tatizo tena. Wewe, kwa kuwa umesoma kuliko mimi utakuwa mhasibu. Utatunza hesabu ya fedha na mali zetu zote." Aliongeza kwa kunidokeza kuwa jioni hiyo angesafiri tena. Atakaporudi tutakuwa tayari kurudi Kigoma.

"Unakwenda wapi safari hii?" Nilimuuliza.

"Nakwenda Kipili hadi Mtakuja. Nitajitahidi kurudi keshokutwa. Nikirudi tu yamekwisha," alinijibu. Kisha alinitazama usoni na kuniuliza "Hapo umefanya nini?"

"Nilijikuna," nikamjibu.

Nilihisi hakuniamini. Alizikagua chale zile kwa muda mrefu kidogo.

"Sidhani," alisema. "Nikirudi tutaangalia suala lako vilevile. Isije kuwa washenzi wanakuchezea, maana umekaa mweupemweupe kama kinda la ndege."

Nilitamani sana kumwamini. Sikubahatika kuipata fursa hiyo.

Mara tu alipoondoka nilifunga vifaa vyangu katika begi langu. Baada ya mlo wa usiku nilijilaza mapema nikisubiri usingizi unichukue ili kesho ifike nione mzee Kahigi atanisaida vipi ili niweze kuondoka nchi hiyo ya Wafipa salama.

Sikujua usingizi ulitokea wapi. Nilihisi ghafla kama naota, mlango ukifunguka na mzee Imilio Kahigi akiingia chumbani humo. Alikuwa mtupu, isipokuwa kwa kipande kidogo cha kaniki alichofunga mbele ya kiuno chake. “Inuka,” aliniamuru. Niliinuka. “Chukua begi lako unifuata,” nilifanya kila alichoniamuru na kumfuata hadi nje ya nyumba.

Hapo kulikuwa na ungo mkubwa wenye vikorokoro mbalimbali ambavyo sikuweza kuvifahamu. “Ingia ukae hapo,” aliniamuru tena. Nikamtii.

Mara alianza kuimba kwa lugha ya Kifipa, maneno ambayo sikuweza kuyaelewa. Akaninyunyizia kitu fulani chenye harufu mbaya kwa usinga wake huku akiendelea kuimba. Ghafla nikaona ungo ukianza kupaa. Ulipaa, ukapaa, ukapaa hadi mawinguni. *Naota?* Nilijiuliza. Kama ilikuwa ndoto, basi ilikuwa ndoto ya aina yake ambayo ningependa nirudie kuiota mara kwa mara.

SURA YA NANE

Kwa Ungo Hadi Mbeya

Nilizinduka toka usingizini. Nadhani kilichonizindua ni baridi kali iliyoambatana na upepo wa kipupwe ambao ulinipiga mwili na kunifanya nijikute nikitetemeka, meno yangu yakigongana. Nilikuwa katika kituo cha mabasi, peke yangu. Jogoo waliokuwa wakiwika huko na huko waliniashiria kuwa ilikuwa alfajiri.

“Niko wapi?” nilijiluliza nikiinuka na kutazama huko na huko. Begi langu lilikuwa miguuni mwangu, kama nilivyolifunga jana. Kwa mbali nilianza kuona mtu mmojammoja wakipita hapa na pale, baadhi yao wakija kituoni kuwahi usafiri. Baadhi ya magari yalianza kuwashwa.

Niliinama na kuliinua begi langu, ambalo nililiinua kwa taabu sana. Vidole vyangu vilikuwa vimekufa ganzi. Hata pale nilipojaribu kutembea miguu yangu ilikuwa kama haipo kwa ajili ya baridi hiyo kali. Nikajikongoja hadi nilipomfikia *taniboi* mmoja ambaye alikuwa akimimina maji katika injini ya gari lake, tayari kwa safari.

“Samahani, hapa ni wapi?” Nilimuuliza.

“Huwa tunasalimiana kwanza,” alisema akinitazama kwa mshangao.

Sikumjibu. Si kwa ajili ya ujeuri bali kwa kuwa sikujua

alitaka salamu za aina na lugha gani, kwani lafudhi yake ilikuwa tofauti kabisa na ile ya watu wa Sumbawanga. Alipoona kimya aliniuliza kwa mshangao, “Kwani wewe umetoka wapi hata uulize hapa ni wapi?”

“Nimetokea Sumbawanga.”

“Umekuja na gari gani?”

Sikuwa na jibu, jambo ambalo lilimshangaza zaidi.

“Ulilewa?”

“Hapana.”

“Ulikuwa unaumwa?”

“Hapana.”

“Sasa umewezaje kutoka Sumbawanga hadi hapa Mbeya bila kujua unapokwenda?”

Sikuendelea kumsikiliza. *Mbeya!* Niliwaza kwa mshangao. Niliyakumbuka maongezi yangu na Mzee Imilio Kahigi na ahadi yake ya kunisaidia. Nikakumbuka tukio la usiku, aliponijia katika mavazi ya ajabuajabu na kuniamuru kuketi katika ungo, nikiwa nimepakata begi langu. Nilikumbuka kwa mbali nyimbo zake alizoimba akichezesha usinga wake hata nikaanza kupaa! *Mbeya! Nimekuja Mbeya kwa ungo!* Sikuamini.

Lakini sikuwa na sababu ya kutoamini. Baridi kali ambayo ilianza kunila mifupa ilikuwa ushahidi tosha kuwa niko katika eneo jingine, lililo juu zaidi ya usawa wa bahari zaidi ya Sumbawanga. Hata mavazi ya watu wengi waliokuwa wakiongezeka mitaani yaliashiria hali ya hewa nyingine kabisa. Makoti au majaketi makubwa, kofia au vitambaa kichwani na viatu vizito miguuni. Majina mengi yaliyokuwa yakitajwatajwa pia yalikuwa mapya masikioni mwangu; Mwakipesile, Mwangonda, Mwamasika, Mwanjelwa na kadhalika.

Nilipapasa mifuko yangu. Pesa nilizopewa na Chifu Masanja bado zilikuwemo. Nikajikongoja hadi nilipopata mgahawa mdogo na kujinunulia chai ya moto sana. Nilikunywa vikombe viwili *chapchap* na cha tatu taratibu kabla ya kubaini kuwa chai hiyo ilinichubua midomo na ulimi kwa kiwango kikubwa sana.

Toka hotelini hapo nilitafuta nyumba ya wageni ya bei nafuu ambamo nilionyeshwa mapipa ya maji ya moto na kuchota ndoo moja niliyoitumia kuoga. Baada ya hapo nilipanda kitandani na kujilaza, nikiwa nimejifunika mablanketi mazito mawili. Usingizi mzito ulinichukua na kwa muda ukawa umenisahaulisha masaibu yote yaliyonitukia katika muda mfupi wa maisha yangu. Hata hivyo ulikuwa usingizi wa mang'amung'amu kwani niliandamwa na ndoto za kutisha, mara nikiwa juu ya mbuyu, mara nikipaa angani, mara nikiwa nimezingirwa na wachawi wanaopanga kunila nyama na kadhalika.

Nililala mchana kutwa na usiku kucha. Nilipoamka kesho yake jambo la kwanza nililofanya ilikuwa kwenda madukani ambako nilinunua mavazi yanayoendana na hali ya hewa ya Mbeya; koti, sweta zito, kofia na soksi nzito.

Katika pitapita yangu mjini hapo niliingia duka la vitabu ambamo nilinunua ramani ya mji na vitongoji vya Mbeya. Nikaketi mahala na kuisoma. Jambo la kwanza lililovuta macho yangu ni urefu wa safari ambayo nilisafiri kwa miujiza toka Sumbawanga hadi Mbeya. Kama ningelazimika kusafiri kwa gari ningetumia zaidi ya siku mbili njiani kwa kupita katika miji na vijiji mbalimbali kama Mpui, Ndalambo, Tunduma, Ihanda, Iwanda na hatimaye Mbalizi.

Jambo jingine lililovuta macho yangu ni kubaini kuwa

mkoa wa Mbeya ulikuwa mpakani mwa Tanganyika na Zambia kwa upande mmoja, nchi ya Malawi kwa upande wa pili. Mji mkubwa zaidi wa mpakani kwa upande wa Zambia ukiwa Tunduma na kwa upande wa Malawi mji mkubwa zaidi ukiwa Kyela na Itundi. Mbeya ilikuwa na sifa nyingine. Ilibahatika kuwa na ziwa kama yale ya Nyanza na Tanganyika, ingawa kwa asilimia ndogo. Bahati hiyo iliwezesha si kuvua samaki tu, bali pamoja na kuwawezesha kuwa na bandari, Itungi, ambayo ilihudumia miji ya Karonga kwa upande wa Zambia na mikao kama Iringa kupitia wilaya ya Ludewa.

Ramani hiyo ilinionesha kuwa Mbeya haukuwa mji mdogo kama ulivyokuwa ukionekana. Ulikuwa na mengi ya kusesimua kiutamaduni, kiuchumi na kimazingira. Pamoja na ukweli kuwa kabila lililojulikana zaidi la mkoa huo lilikuwa la Wanyakyusa bado kuna makabila mengine tele kama Wandali, Wasafa na Wasangu ambao ni wenyeji asilia. Aidha, kuwepo kwa mkoa huo mpakani kulichangia kufanya uhamiaji wa kutokea nchi za Malawi na Zambia kuwa sehemu ya wakazi.

Sikuhitaji ramani hiyo kusoma ukweli kuwa wakazi wengi walikuwa wakulima. Mazao kama mahindi, mpunga, migomba, viazi na mimea mengine ilikubaliana sana na ardhi na hali ya hewa ya huko, jambo lililofanya katika pitapita zangu nipishane na wakulima waliobeba mazao ama kwenye baiskeli ama katika mikokoteni wakielekea sokoni.

Lakini Mbeya ilikuwa na kitu kingine cha ziada. Dahabu. Purukushani za kutafuta dhahabu, kwa mujibu wa maelezo toka kwa baadhi ya watu niliobahatika kuzungumza nao, zilianza tangu mwaka 1905 kufuatia fununu za kuwepo kwa madini hayo. Hata hivyo, miaka kumi na mitano baadaye ndipo ilipodhihirika rasmi kuwepo kwa madini hayo katika

mji wa Chunya. Hali hiyo iliyopelekea mji huo mdogo upanuke ghafla na kupokea watu wa aina mbalimbali, wa makabila na mataifa mbalimbali, kila mmoja akijaribu kuutumia mwujiza wa dhahabu kujipatia chochote. Walikuwemo wachimbaji, madalali, wanunuzi, wauzaji wa vifaa vya uchimbaji na vyakula na wengineo.

“Nafikiria kwenda huko kesho,” nilimwambia mmoja kati ya watu niliobahatika kuzungumza nao juu ya suala hilo. Alikuwa mtu wa makamo, ambaye muda mwingi nilimwona kakaa mbele ya hoteli niliyofikia. Sikupata kujua kazi yake ilikuwa ipi.

Mtu huyo alinitazama kwa mshangao, “Nani, wewe?” aliniuliza.

“Ndiyo,” nilimjibu.

“Unakwenda kufanya nini?”

“Kuchimba.”

Akacheka na kunitazama kwa dharau ya dhahiri. “Inahitaji mtu kichaa sana kwenda kuchimba madini,” alisema.

Ikawa zamu yangu kumshangaa. “Kwa vipi?” nilihoji.

“Kwanza hutarudi salama. Na ukirudi utakuwa masikini kuliko hapo ulipo.” Alinionya.

Sikumwelewa. “Mbona kuna watu huko na wanachimba?”

“Mdogo wangu, hao walioko huko huwa hawarudi. Kazi ile ni kama laana hivi. Unaweza kuchimba maisha yako yote bila kupata chochote cha maana. Unaweza kubahatika kupata mali ya maelfu lakini siku mbili tatu ukawa huna hata shilingi moja. Fedha za madini ni kama za mashetani. Hupotea kimiujiza kama zinavyopatikana.”

“Na hawa wanaotajirika?” nilihoji.

“Hao sio wachimbaji. Ni wanunuzi au wamiliki wa maeneo utakayochimbia. Wachimbaji wa kawaida wako huko, wanazeekea huko na kufa huko!” alisisitiza.

Laiti angejua taarifa yake ilinikata maini. Toka nilipofika mjini hapo kimiujiza nilikwishafanya uamuzi. Uamuzi wangu ulikuwa kwenda Chunya, kujiunga na wachimbaji madini ili nikibahatika nirudi kwetu sina elimu lakini nina mali. Taarifa za kwenda kuzeekaa huko na kufia huko ziliniacha hoi, taabani.

Mshauri wangu aliweza kusoma msugvano wa mawazo yangu, nilidhani, kana kwamba anapigilia msumari wa mwisho kichwani mwangu, aliongeza, “Kama umetoka kwenu kwa nia ya kwenda machimboni isahau kabisa ndoto hiyo. Utakufa siku si zako. Utaugua kifua kikuu kwa vumbi la machimboni, utazikwa hai kwa kubomokewa na kuta za shimo, utauawa na wachimbaji wenzako ukibahatika kupata mali nyingi. Kuna hatari elfu moja na moja.”

Ushauri wake wa bure ulianza kunichosha. “Kuna kazi gani duniani ambayo haina hatari kwa namna moja au nyingine?”

“Nyingi tu,” alijibu harakaharaka.

“Kama?”

“Udaktari kwa mfano,” alijibu harakaharaka.

Nikacheke. “Daktari lazima asome kwa miaka nenda rudi. Huwezi kuamua tu kwamba unataka kuwa Daktari.”

“Tunazungumzia kazi, sio kisomo.”

Nikabaini kuwa nazungumza na mtu mweye asili ya ubishi. Nikaamua kumuuliza yeye binafsi anafanya kazi gani.

“Wengine kazi zetu huwa hazitajwi hovy.” Alisema.

Nikaanza kuamini hisia zangu kuwa hana kazi. Hiyo ilikuwa siku yangu ya tatu toka nilipofika Mbeya na kila

siku namwona ameketi anazungumza na watu mbalimbali. Nikaamua kupuuza hata mawaidha yake juu ya hatari za uchimbaji madini. Watu hujiunga na jeshi, wakijua fika kuwa kazi yao ni kwenda vitani ambako kifo ni jambo la kutarajiwa. Watu hujifunza urubani, wakiwa wanajua vizuri sana kwamba ndege ikidondoka kupona ni nadra sana.

Nadhani sihitaji ushauri wako zaidi, nilitamani kuwambia hivyo. Hata hivyo, sikuthubutu. Nilimwona kama mtu ambaye asingekuwa mwepesi wa kusahau na kwa kila hali sikuhitaji maadui bila sababu za msingi.

* * *

Nilikaa Mbeya kwa wiki nzima zaidi. Bado nilikuwa na hamu kubwa ya kwenda Kiwira kujaribu bahati yangu machimboni. Tatizo lilikuwa usafiri. Hakukuwa na magari ya abiria ya mara kwa mara isipokuwa yale ya kuvizia tu. Na hayo ilikuwa lazima kuwe na mtu atakayekudokeza gari fulani, linakwenda siku fulani. Sikuwa nimebahatika kumpata mtu wa aina hiyo.

Hivyo, niliutumia muda wangu mwingi kutembea huku na huko katika mji na vitongoji vya Mbeya. Nilifurahia sana vijilima vingi vilivyotapakaa huku na huko na kufanya safari zangu ziwe za kupanda na kushuka toka kitongoji hadi kitongoji. Salamu za Kinyakyusa ‘*Ugonile*,’ ziliniandama kila nilipokwenda. Nami sikujivunga, nilijibu kwa kujiamini, ‘*Ndaga*,’ ingawa ilipofuata midahalo mirefu ya kilugha niliufyata ulimi wangu na hivyo kufanya nijulikane kuwa mimi ni ‘Wakuja.’

Kama fedha zingeniruhusu ningeweza kusafiri hadi maeneo mbalimbali maarufu kama Tukuyu, Mbarali, Ileje,

Kyela na Rungwe ambako nilisikia kuna mlima mrefu kwa mita 2961 juu ya usawa wa bahari.

Mto Kiwira pia ni kitu kingine kilichonivutia sana huko Mbeya. Ukiwa unapokea maji yake toka vijito vya Matogola, Sinini, Kipoke, Kilosi na Mulagala mto huo ulisafiri hadi Ziwa Nyanza ambamo ulimwaga maji yake siku hadi siku. Kama ilivyo kawaida ya bahari na maziwa, kamwe ziwa Nyasa halikupata kushiba wala kutapika kwa wingi wa maji hayo. Pengine ni kweli kuwa hiyo ndiyo kanuni ya maisha? Samaki mkubwa hummeza mdogo!

Ziwa hilo la Nyasa halikuwa pekee kwa Mbeya. Walibahatika kurithi sehemu nyingine ya ziwa jingine ambalo lilijikita katikati ya Mbeya na Rukwa. Hilo ni ziwa Rukwa. Wakati Rukwa walilifaidi kwa sehemu kubwa ya kusini, Mbeya walilitumia kikamilifu upande wa Kaskazini. Wakazi wa miji kama Manda na Ngomba walilitumia kwa masuala mbalimbali, ikiwa pamoja na uvuvi wa samaki.

Kitu kingine kilichonisumbua hapo Mbeya ni lile shamba la aina yake la maua na miti asilia. Shamba au pori hilo lililoko Kitulo lilikuwa kama moja ya mashamba ya wafalme wa kale, hata kabla ya kalenda ya sasa kuanza, jambo lililofanya liwe hazina ya pekee duniani. Kwa kweli shamba hilo lilinifanya nimkumbuke babu yangu. Alivyokuwa mpenzi wa miti na mitishamba kama angebahatika kufika shambani humo angekuwa mtu wa kushinda maporini akinukuu na kukariri hiki na kile.

Mfuko wangu ulianza kukaa vibaya. Akiba yangu ya pesa nilizopewa na Chifu ilianza kuyoyoma, hali iliyofanya nianze kufikiria umuhimu wa kupata ajira mapema zaidi. Nikiwa kijana, mwenye nguvu na afya tele sikuwa na wasiwasi kwa kazi yoyote ambayo ingenitokea mbele yangu. Hivyo, alipotokea

mzee Ayubu Mwalongo na kuniuliza kama ningependa kuwa mmoja wa wafanyakazi wake wa lori la abiria na mizigo kama kondakta sikusita kukubali.

Nilikutana na mzee huyo kwa namna ya ajabu kidogo. Kwa mara ya kwanza tulikuwa hotelini. Nilikuwa nikinywa uji wa ulezi. Nilipata hisia kuwa kuna mtu ananitazama sana. Nikainua uso na kukutana na mzee mmoja mwembamba na mfupi sana. Kwa kweli, ni mvi na ndevu zake ndizo zilionifanya nijue kuwa ni mzee. Vinginevyo umbo lake lilikuwa la mtoto mdogo. Hata mavazi yake nadhani alitoa vipimo vya mtoto. Tulipokutanisha macho alinitazama kwa muda kama mtu aliyepata kuniona mahala lakini hakumbuki ni wapi. Mimi binafsi, nikiwa na hakika kuwa sijapata kumwona mahala popote nilimpuuza na kuendelea kuufaidi uji wangu.

Kesho yake, nikipitapita zangu katika kituo cha magari kwa matarajio ya kusikia taarifa za gari liendalo Kiwira nilimwona tena. Na alikuwa akinitazama kwa jicho lilelile la aina fulani. Wakati nikiamua kuondoka alinifuata. “Samahani kijana,” aliniambia aliponifikia. “Hivi tulionana wapi?”

“Nina hakika hatujapata kuonana. Mimi ni mgeni huku na nimefika majuzi tu,” nilimweleza.

Hakuoneka kuamini, “Unaitwa Nani?” aliuliza tena.

“Kwa nini unahitaji jina langu?”

“Bado ninahisi nilipata kukuona mahala,” alijibu na kuongeza. “Ulipata kuishi Iringa?”

“Mimi! Hapana.”

“Tanga?”

“Hapana.”

“Morogoro?”

“Hapana.”

Akazidi kushangaa, “Unaitwa nani?” aliuliza tena.

“Jina la nini?” nami nikahoji.

“Siulizi kwa nia mbaya. Ninapata hisia kuwa nakufahamu. Kama sikufahamu wewe nitakuwa namfahamu baba yako. Kwani unakotoka hasa ni wapi?”

“Kigoma,” nilimjibu.

Akaonekana kuchanganyikiwa zaidi. Nadhani hakupata kufika huko.

“Unafanya kazi gani?”

“Sina kazi. Natafuta kazi.” Nikamwona akitafakari kabla ya kuuliza, “Unajua kusoma na kuandika?”

“Mie! Vizuri sana.”

“Unajua mahesabu?”

“Najua. Kwa kiwango cha kutosha tu,” Nilimjibu

Ndipo aliponielea kuwa yeye ni mfanyabiashara wa magari. Kwa jina alijitambulisha kuwa anaitwa Ayubu Mwalongo.

Alikuwa nayo magari manne ya mizigo yanayokwenda huku na huko. Moja likiwa jipya ambalo halijaanza safari. “Tayari nimepata dereva. Bado nilikuwa na shida ya kondakta. Kama wewe umesoma na unataka kazi umepata. Unasemaje?”

Nikatae? Tuliafikiana na kupangiana mshahara na majukumu. Nilitakiwa kuripoti kazini kesho yake.

Mtu mmoja aliniona wakati nikizungumza na yule mzee pale stendi. Mara tu tulipoachana aliniita kwa jina. Sikujua alijuaje jina langu. Ni yule aliyejitokeza kuwa mshauri wangu wa masuala ya madini wa pale nyumba ya wageni niliyofikia.

“Unamfahamu yule mzee uliyekuwa unazungumza naye?” alinihoji.

“Nani? Mzee Ayubu? Namfahamu.”

“Unamfahamu vizuri?”

“Kwa nini? Nimemfahamu leo tu. Najua ni

mfanyabiashara mkubwa wa magari na anayo mengi. Kesho naanza kazi katika moja ya magari yake,” nilimwambia.

“Nini?” alishtuka. “Unaanza lini?”

“Kesho”

“Kwenye magari...!”

“Yake,” nilimjibu. “Kwani kuna tatizo gani?”

Alinitazama huku akitikisa kichwa kwa namna ya kunihurumia. Mdogo wangu hujipendi. Naona mji umeingia kwa pupa. Acha tabia ya papara. Kaa na watu uliza, kabla hujakurupuka. Oh! Shauri yako!”

Hasira zikanipanda. “Kwani lini nilipata kukuteua wewe kuwa mshauri wangu? Shika hamsini zako, acha nishike zangu. Nitakapohitaji ushauri labda nitakuomba, siyo leo.” Nilisema nikiondoka zangu na kumwacha akiwa kanikodolea macho.

Kwa namna fulani nilihisi kuwa nimefanya makosa. Pengine isingenigharimu chochote kumsikiliza mshauri huyo wa bure, kumsikia tu, sio kumsikiliza, kwani nilikwishamchukulia kama mtu mwenye muda mwingi wa kuzungumza na tabia ya kujifanya anajua kuwa ningeishia kuwa kama yeye, kuketi toka asubuhi hadi adhuhuri akizungumza kwa hofu ya kufanya hili na lile.

Vilevile, sikutaka mtu yeyote anishawishi kuacha fursa ya kazi hiyo ya kusafiri. Tangu nilipoanza safari toka Buha hadi Uhayani na kisha Usukumani hadi Ufipa na sasa huku kwa Wanyakyusa nilijikuta nimeanza kupatwa na maradhi ya kupenda safari. Nilifurahia sana kuona sura mpya za nchi za watu, mazingira mapya na tamaduni mpya. Sikutaka mtu yeyote anishawishi vinginevyo kwa hilo.

SURA YA TISA

Nchi Ya Mkwawa, Kiboko Ya Wajerumani.

Kati ya wageni walioingia katika nchi yeti kwa mikiki, jeuri na ukatili mkubwa ni pamoja na Wajerumani. Baada ya kusikia sifa za uzuri na utajiri wa Tanganyika, toka kwa Waarabu na Wareno ambao walifika kwanza katika pwani ya nchi yetu wajerumani walishikwa na tamaa isiyo kifani.

Tamaa hiyo ilichochewa zaidi na bwana mmoja aliyelitwa John Rebman tarehe 11, mwezi wa tisa mwaka 1848 alipoondokewa kuwa mtu mweupe wa kwanza kuutia machoni mlima mrefu kuliko yote afrika, Kilimanjaro. Mlima huu, huko Kaskazini mwa nchi yetu, unakwenda angani kwa mita zipatazo 5895, ukiwa umepambwa kwa theluji nyingi inayong'ara kwa kumeremata kwa namna ya kufanya uwe kama shada la ufalme wa Afrika na dunia pia. Hali nzuri ya hewa iliyootesha vizuri aina mbalimbali za mimea na utulivu wa wakazi wake vilimtia Rebman wazimu. Aliporudi kwao nchi yake ikapata wazimu, wazimu wa mapenzi kwa Tanganyika.

Hivyo, mwaka 1884, Novemba 23, Mjerumani aliposimika bendera yake kule Bagamoyo na mwaka mmoja baadaye, February 27 kujitangaza wamiliki wa Tanganyika haikuwa muujiza kwa mtu yeyote. Uvamizi huo wa Wajerumani

kwa kiasi kikubwa ulifanikiwa kwa ajili ya hila zilizofanywa na mtu wao mmoja, aliyeitwa Karl Peters, ambaye alipita huko na huko akiwaingiza Machifu na watu wengine katika mikataba ya ujanja ujanja kuhalalisha utawala wao. Kwa upande mwingine, vitisho vilivyoambatana na mauaji, kwa kutumia silaha zao ambazo zilikuwa bora zaidi ya zetu kulifanikiwa azma yao ya kuimeza nchi yetu.

Mnamo mwaka 1991, Mjerumani mmoja, kwa jina Julius Von Sodden aliteuliwa kuwa gavana wa kwanza wa Ujerumani kwa Tanganyika. Ni yeye aliyeamua kuhamisha makao makuu ya serikali yao toka Bagamoyo hadi Dar es Salaam.

Kam Sodden na magava wenzake waliomfuatia, akina Von Echele, Von Wissman, Von Libert na wenzao wengine; Von Gotzen, Von Rechenberg na yule wa mwisho Von Schnee walidhani kuwa walikuwa wameipita Tanganyika kwa urahisi kiasi kile basi walikuwa wamejidanganya.

Huko Tabora aliibuka shujaa mmoja, Isike Mkasiwa, ambaye alipigana nao kwa muda mrefu hadi Januari 9, 1893 alipozidiwa na kuamua kujiua badala ya kuchukuliwa mateka.

Huyo hakuwa mhanga pekee. Huko Kilimanjaro mnamo Machi 2, 1900 Machifu tisa wa koo mbalimbali za makabila ya huko walinyongwa hadharani kufuatia upinzani wao mkali dhidi ya Wajerumani. Miongoni mwa Machifu mashuhuri kati ya walionyongwa alikuwemo *Mollelia wa Kibosho*, Ngalami pamoja na Meli wa Moshi. Madai ya watawala wa Kijerumani ni kuwa walikuwa wakichochea upinzani dhidi ya utawala wao.

Haikuwasaidia, kwani ndio kwanza Watanganyika walizidisha mapambano. Vita ya majimaji vilienea sehemu mbalimbali za kusini ikiwa pamoja na Songea, Mtawara, Lindi na kwingineko. Majimajii walishambulia misheni ya

Mikukuyumbu Nachingwea, wakateka makao ya Wajerumani ya Liwale, misheni ya Masasi na kuteketeza ile ya Nyangao, Lindi. Hali hiyo ilipelekea Septemba 1, 1905 Wajerumani waombe msaada zaidi wa kijeshi toka kwao, ambao uliwezesha kurejesha utawala wao.

Uamuzi waliouchukua baada ya kuona hata baada ya kumteka Kinjekitile Ngware mganga aliyekuwa akiwapa kinga wapiganaji ili wasidhurike na risasi za Mjerumani na kumnyonga hadharani katika kijiji cha Muhoro, Rufiji bado mapambano yalizidi kuwa makali.

Chifu mwingine, akitokea Iringa, kwa jina Singoyangili Mkwawa hatasahulika kwa kupambana na Wajerumani kwa nguvu zake zote. Chifu huyu alitokea katika kabila la Wahehe, makazi yake yakiwa kijijini Kalenga, aliwachachafya Wajerumani kwa kiwango ambacho hawatakaa wasahau.

Mara kadhaa majeshi ya Mkwawa yaliwateketeza Wajerumani na kuvunjilia mbali ngome zao. Hali hiyo iliwasababishia Wajerumani waamue kujenga ngome imara ambayo ilikuja kuwa chanzo cha mji na baadaye mkoa wa iringa. Mji huo ulijengwa karibu na ngome ya Mkwawa ya Kalenga. Ndiyo, Mkwawa pia alishindwa na kuamua kujinyonga badala ya kukamatwa akiwa hai, lakini mji wa Iringa ukawa kielelezo tosha cha nguvu na misimamo thabiti wa babu zetu dhidi ya utawala wa kigeni.

Niliyafikiria yote hayo nikiwa ndani ya gari karibuni kuingia katika mji huo wa kihistoria. Ilikuwa safari yangu ya kwanza kama kondakta. Nilikuwa na muda mwingi wa kufikiri na kutafakari yale ambayo nilibahatika kuyasoma shuleni na katika vitabu mbalimbali vilivyopata kunipitia mbele yangu. Mambo hayo yalikuja kama ndoto kutokana na macho yangu

yaliyokuwa yakitazama nje ya gari muda mwingi zaidi.

Tulisafiri kwa zaidi ya siku tatu, toka Mbeya hadi kuufikia mji wa Iringa. Tulishusha hapa na kupakia pale, mara abiria ama mizigo, mara mizigo na abiria. Mara kadhaa tulilala porini kwa ubovu wa magari, mara nyingine ilikuwa kusubiri mzigo ya michele au matunda yaliyokuwa yakivunwa.

Kinyume na nilivyoahidiwa kuwa ningetumia gari jipya, gari hili lilikuwa chakavu lililochakaa sana. Kama lingekuwa binadamu lingeweza kusema hivyo na kuacha lipumzike kwa amani, lakini kwa kuwa halikuwa na uwezo huo liliacha liburuzwe kama ng'ombe mzee huku mlio wake ukionyesha kuteseka sana kwa mashine yake hata kwa mtu asiye na ujuzi wa ufundi wa magari. Lilikuwa lori, aina ya *Bedford*. Kila baada ya kilomita kumi tulilazimika kusimama na kujaza maji katika *rejeta* ambayo ilikuwa ikiyakausha kwa kasi ya pekee.

Alichoniambia tajiri yangu juu ya kutumia gari hilo badala ya lile jipya nililoahidiwa sikupata kukielewa vizuri. Alitumia maneno kama '*Ngoja uzowee*' au '*Vibali vimechelewa.*' Kauli ambazo sikuona kama alitaka nizielewe vizuri. Kwa kuwa wahanga wanasema '*mchagua jembe si mkulima,*' nikapokea jukumu hilo bila maswali zaidi.

Lakini dereva wangu alinishangaa zaidi pale nilipomuuliza juu ya gari hilo. Alionekana kuwa mtu mwema, mchangamfu na mkimya. Nilimkadiria kuwa alinizidi umri kwa zaidi ya mara mbili. Kwa jina alijitambulisha kuwa ni Kalinga.

"Gari jipya?" alinihoji akicheka sana. "Alikuambia analo jipya? Basi litakuwa hili," aliongeza.

"Kwa vipi? Kwani hana gari jipya?" nilihoji.

"Huu kwangu mie ni mwaka wa tatu toka niandikishwe kazi kwake. Na nilijiunga kwa hadithi hiyohiyo ya gari jipya.

Sikupata kuliona hata kwa macho.”

Nilipatwa na mshangao wa mwaka. “Kwanini basi anasema uongo?” nilimuuliza.

“Hata mimi najiuliza hilo mara kwa mara,” Kalinga alinijibu. “Mtu mzima kwa nini useme uongo? Unajua madereva wawili kabla yangu na makondakta watatu wameshaacha kazi kwa jili ya ahadi hizo za gari jipya?”

Ghafla nikajiwa na wazo. “Kwa hiyo mimi nimeingia baada ya kondakta wa mwisho kuacha kazi?” nilihoji.

“Kawambwa! Yeye hakuacha,” alisema.

“Ila?”

“Alikufa.”

“Alikufaje? Ajali?” nilizidi kudadisi.

“Wala haikuwa ajali. Kifo chake kina utata mwingi. Nadhani tuachane na maongezi hayo. Hayakufai kwa sasa,” alishauri.

Nikamuuliza Kalinga juu ya magari mengine saba aliyonayo tajiri yetu. Hilo lilimfanya aangue kicheko.

“Mbona unacheke. Hana?”

Kalinga alikohoa kwa namna ya mtu aliyepaliwa kabla ya kusema taratibu, “Anayo.”

Nilimwona kama mtu aliyeacha neno alilotaka kulisema. “Anayo, lakini?” nilimshurutisha.

“Lakini ni mabovu kuliko hili. Yote yako katika magereji mbalimbali, taabani hata mafundi wameyakatia tamaa. Wanamwambia akayavute, mwenyewe anasema yatatoka yakitembea.”

Ilibidi nami niangue kicheko. Kilikuwa *kicheko cha uchungu*. Sikujua kama nilikuwa nikijicheka mie au kumcheka mwajiri wangu mpya, tajiri wa magari mabovu. Kwa namna

fulani nilihisi fahari. Niliona kama mimi na dereva Kalinga ndio tuliokuwa matajiri wenye ufunguo pekee za kumkwamua tajiri yetu ili anunue gari jipya na kufufua yale mengine yaliyoozea kwa mafundi. Fikra hizo zilinifanya nitupile mbali wazo ambalo lilianza kunijia la kuacha kazi hiyo mara moja na kutafuta nyingine.

Nikakumbuka yule mshauri wangu wa masuala ya madini na kubaini kuwa kweli alikuwa na jambo la kunishauri juu ya tajiri yangu, mzee Ayubu Mwalongo. Kwa mara ya kwanza nilijilaumu kwa kutomsikiliza.

* * *

Hali ya hewa ikiwa, kwa kiasi fulani, kama ile ya Mbeya, mji ukiwa juu ya vilima kwa takribani mita 1550 juu ya usawa wa bahari nilijikuta nikiridhika sana na maisha yangu ya hapa na pale katika mji, vitongoji na vijiji vya Iringa.

Tulikuwa watu wa safari kila siku. Tulikwenda Mafinga, ambako baridi ilizidi ile ya mjini kwa kiwango kikubwa. Tulikwenda Kilolo ambako niliweza kuupanda mlima Luhembelo na kuvutiwa na wanyama wa ainaaina katika pori moja lililoitwa Udzungwa. Wanyama ambao walikuwa tele kama wale tuliowaona pia kule Ruaha. Tulifika Makete, tulifika Njombe, tulifika pia Ludewa.

Kila nilipopata wasaa nilitembelea kijiji cha Kalenga ili kuona kumbukumbu za yule mzee shujaa, Mkwawa na ngome yake. Kaburi lake lilikuwa pale, nasikia alizikwa bila kichwa, kwani Wajerumani walikipokonya na kukipeleka kwao ili kuchunguza uwezo wa ajabu wa mtu huyu aliyewatoa jasho vigogo waliokaribia kuitawala dunia.

Nilipata pia kutembelea kijiji cha kumbukumbu cha

Isimila. Niliweza kuona michoro na vifaa vilivyochongwa kutokana na mawe ambavyo ni sehemu ya uthibitisho kuwa mtu wa kale, zaidi ya miaka 70,000 aliishi Tanganyika. uthibitisho huo umefanywa na wataalamu mbalimbali waliobobea katika taaluma za macho ya kale.

Uzoefu wangu mkoani humo ulinifanya nibaini kuwa hata jina la Iringa lilitokana na udhaifu wa matamshi ya wageni hao kwa lugha ya Kihehe, kwamba wenyewe walikuwa wakiuhita mji huo *Lilinga*, kwa maana ya ng ngome.

Biashara yetu ilikuwa ikienda vizuri, kama kila mmoja wetu alivyotegemea. Kwanza gari lilipunguza tabia ya kuharibikaharibika mara kwa mara. Jambo lililomfanya dereva Kalinga ambaye pia ni fundi anichekelee na kunisifu kuwa nina ‘nyota’ ya biashara, “Sio siri, gari hili lilianza kushindikana. Mimi mwenyewe nilishaamua kuifanya safari hii iwe ya mwisho,” alinitobolea siri yake.

Aliyefurahi zaidi , alikuwa tajiri yetu mzee Ayubu. Kila tuliporejea Mbeya tulikuwa na fedha nyingi za kumpa na taarifa chache tu za kuharibika kwa gari lake. Kwa mara ya kwanza nilimwona akitabasamu. Miezi miwili mitatu baadaye nilipomtazama nilihisi amenenepa na kurefuka kidogo.

Kwa bahati mbaya, mafanikio hayo yalianza kuambatana na ajali za mara kwa mara. Ajali hizo zilikuwa ngumu kuelezeka. Ya kwanza, ilitokea katika maeneo ya Ruaha. Nilikuwa nimeshuka nje ya gari nikimsaidia abiria mmoja mwenye mguu moja kushuka. Mara alipofika chini mbele yetu, lilisimama gari dogo, aina ya *Landrover*, lililokuwa na Wazungu wawili. Waliniita. Nikawaendea. Mara tu nilipowakaribia gunia la mahindi lililokuwa juu ya gari liliporomoka kwa kasi na kutua palepale nilipokuwa. Kasi ya gunia hilo lilimwangusha yule

abiria na kumfanya ateguke mguu wa pili. Ilibidi tumrudishe kwenye gari na kumpeleka hospitali moja ndogo huko Iringa.

Ajali ya pili ilikuwa mbaya zaidi! Ilikuwa katika milima ya Kitonga. Gari letu kongwe lilipanda kwa taabu sana milima hiyo kiasi kwamba abiria wengi walishuka na kutembea taratibu, wakiwa wamelitangulia gari. Tulibakiwa kwenye gari mimi na dereva pekee. Mara gari ikaanza kurudi nyuma kwa kasi. Kwa kila hali lilielekea kuporomokea katika yale mashimo makubwa ambayo hufanya abira wengine wafumbe macho kila wanapofika hapo, kwa uoga. “Ruka nje!” dereva aliniamuru.

“Na wewe?” nilimuuliza.

“Ruka.” Alifoka

Nikafungua mlango na kuchupa nje. Dakika hiyohiyo gari liliangukia upande nilioshukia na kunikosa kwa nusu nchi tu! Mimi pamoja na abiria wangu ambao walikuwa wakishuhudia purukushani hiyo tulilikimbilia gari kumwahi dereva. Tulimkuta akifungua mlango na kutoka nje akiwa safi bila hata vumbi kana kwamba alijilaza tu. Kila mtu alishangazwa na ajali hiyo.

Lakini ajali ya tatu ilishangaza zaidi. Ilitokea miezi miwili baada ya ile ya mwisho. Tena ilitokea katika kituo cha kazi, Mbeya. Tulikuwa tukilikagua gari kwa makini kabla ya kuanza safari yetu nyingine ndefu ya mijini na mashambani.

Baada ya dereva kuwasha gari na kubaini kasoro fulani katika mlio wake, alikagua maji, oili, mafuta ya breki na kila kilichohitajika. Kila kitu kilikuwa safi. Alipoiwasha bado ilitoa mlio usioeleweka. Akaniumuru niingie chini ya gari kuangalia kama kulikuwa na nati au sukurubu yoyote iliyolegea. Nilikuwa tayari nimevaa vizuri, shati jeupe, suruali nyeusi na tai shingoni. Nilijitazama, kisha nikakutazama huko chini

nilikotakiwa kuingia. Kulijaa vumbi na topetope la manyunyu ya ukungu wa baridi.

“Hakufai,” nilimwambia dereva.

Aliponitazama aliridhia kuwa sikustahili kuingia huko. Akaniamuru kuingia ndani ya gari, niwashe na kupiga resi wakati yeye akikagua huko chini. Haikuwa kazi kubwa kwangu kufanya hayo. Katika safari zetu nyingi nilikwishajua kuendesha gari vizuri, ingawa uzoefu mdogo ulifanya niwe na wasiwasi kidogo.

“Washa!” dereva aliita toka chini.

“Kanyaga resi!”

“Kanyaga breki!”

Ni wakati nikikanyaga breki hiyo lilipotokea jambo ambalo hakuna aliyeweza kuelewa. Nilisikia mlio wa ‘ka ka ka ka’ kana kwamba kuna kitu kinachokatika. Haikuwa uwongo kwani mara hiyohiyo niliona nyufa zikitokea kwenye bodi ya gari na baadaye sehemu iliyobeba injini ikaanza kudidimia.

“Kalinga! Toka haraka!” Nilipiga kelele nikifungua mlango na kuruka nje.

“Kanyaga bre....” Ilikuwa kauli yake ya mwisho kabla injini haijadondoka chini na kumpondaponda vibaya sana. Majirani walijitokeza na kumsaidia kumtoa chini ya injini hiyo ambayo ilikuwa bado ikinguruma. Alikuwa akipumua, lakini hakuwa mtu wa kuishi. Uso mzima ulikuwa umepondeka, kichwa na kiwiliwili vikiwa kama vimeachana.

Sikupata kuona kitu cha kutisha kama kile maishani mwangu. Nilitetemeka mwili mzima huku machozi yakinitoka. Nilitetemeka zaidi pale nilipokumbuka kuwa mimi ndiye niliyetakiwa kuwa chini ya gari lile. Kwa maneno mengine, mimi ndiye ambaye ningekuwa taabani, nusu maiti. Nilishukuru

pale nilipohisi mtu mmoja akinishika mkono na kuniongoza taratibu hadi katika chumba changu cha nyumba ya wageni na kuniketisha kitandani.

“Pumzika. Ikiwezekana lala. Usitoke kwenda kula nje hadi masuala yote ya kumshughulikia marehemu yatakapokwisha,” alisema.

“Ame... amekufa!” niliropoka.

“Kwa vyovyote vile.”

Nikainua macho kumtazama mfadhili wangu huyu. Hakuwa mwingine zaidi ya yule mshauri wangu wa masuala ya madini, ambaye mara ya mwisho nilipuuza kumsikiliza. Alikuwa akinitazama kwa huzuni, lakini nilihisi macho yake yalikuwa yakinicheka na kunidhihaki kama yanayosema, “Si unaona? Nilikuambia nini!”

Kwa sauti alinieleza kile ambacho alidai alitaka kunieleza toka awali, lakini, ‘nikampuza!’ kuhuza sifa mbaya za mzee Ayubu, “Ni mtu hatari sana. Ni mshirikina kupita kiasi. Marehemu Kalinga ni mtu wa tano aliyepoteza maisha katika mazingira ya ajabuajabu katika ajali.”

“Kwa vipi?” nilimuuliza. “Inakuwaje mambo hayo?”

“Ushirikina.”

“Ushirikina?”

Akaamua kunifafanulia. “Inaaminika mzee Ayubu alipata utajiri wake kwa njia ya ushirikina. Kabla hajawa na kitu alifiwa na mkewe katika mazingira ya kutatanisha. Mara akaibuka na kununua magari kwa mpigo. Kipindi fulani alionekana kulegalega kiuchumi mtoto wake mkubwa naye akafa kiajabuajabu. Akaibuka tena na kuongeza magari. Lakini kwa kuwa mali ya haramu haidumu magari yake nayo yaliandamwa na mkasa huu na ule. Mara yapate ajali, mara yaharibike. Mawili yalipata kuibuka bila sababu yoyote.”

Nilimsikiliza kwa mshangao. Nikayakumbuka yaliyonikuta mimi mwenyewe kule Sumbawanga ya Mmanyema kudaiwa kutaka kunigeuza ndondocha.

“Hivi ni kweli mambo haya yapo?” nilimuuliza.

Swali hilo ambalo lilimfanya anitazame kama mdudu kwa dharau. “Unauliza ni kweli? Huna hakika! Hujui kuwa ni wewe uliyekusudiwa? Kalinga amekufa kwa bahati mbaya tu. Wewe ndiye hasa uliyehitajika!” alisisitiza.

“Mimi! Kwa nini mimi?”

“Kwani hukumbuki mara ngapi umenusurika?” alinijibu kwa swali jingine. “Ni wewe uliyekuwa chaguo lake. Damu za wengine wote waliokutangulia hazijafaa. Wewe toka alipokutia machoni alishajua u chaguo lake,” alinijibu.

“Alijuaje kuwa damu yangu itamfaa?” nilisisitiza.

Aliendelea na mtindo wake wa kunijibu swali kwa swali, “Kwani hujui?” alinihoji. “Unataka kusema kuwa hujui kuwa una alama?”

“Alama! Alama gani?” Nilihoji kwa mshangao uliochanganyika na hofu.

Akaangua kicheko. baadaye alisema taratibu., “Usijifanye mtoto kuliko ulivyo. Una alama ya shari. Iko wazi usoni mwako kwa kila mjuzi wa mambo atakayekutazama usoni mara moja. Hapo ulipo una elimu ya kutosha lakini haikusaidii! Una nyota lakini haing’ari! Wewe si mtu wa kuhangaika kama unavyohangaika. Unahitaji kusafishwa, kufutiwa alama hiyo. Vinginevyo, maisha yako yataendelea kuwa kama ya mbwa koko asiye na mwenyewe.”

Niliyatafari maneno na hoja zake. Chembechembe za ukweli zilikuwa nyingi kuliko uongo. Kwa mara ya kwanza nilijikuta nikipatwa na hofu kubwa juu ya maisha yangu, hofu ya kufa *Kama mbwa koko* kama alivyonielea. Leo niko

hapa kesho niko pale! Kila ninachoshika hakishikiki! Nadhani machozi yalinilengalenga au kunitoka bila taarifa, kwani nilihisi mkono wa jamaa yangu huyo ukiwa begani kwa namna ya kunifariji; kitendo ambacho kilifuatiwa na sauti yake yenye huruma aliponiambia, “Usijali mdogo wangu, nitakusaidia.”

“Utanisaidiaje?” nilinong’ona.

“Nitakupeleka mahala, utasafishwa vizuri. Baada ya hapo utaona milango yote uliyofungiwa ikifunguka.”

Bado nilikuwa na wasiwasi. “Utanipeleka wapi?” Nilimuuliza.

“Kilwa.”

“Kilwa?”

“Naam. Kuna wajuzi wa mambo haya na gharama zake ni nafuu. Utaoshwa utasafishwa na kukaangwa upya. Hakuna atakayekugusa.”

* * *

Mipango ya safari ya Kilwa ilianza mara baada ya mazishi ya dereva Kalinga. Yalikuwa mazishi yaliyoudhuriwa na takribani kila mkazi wa Mbeya, waliomfahamu na wasiomfahamu. Wakati wote wa msiba hadi matanga lilisemwa hili na lile kufuatia muujiza ule wa kifo chake. Jina la mzee Ayubu lilikuwa mdomoni mwa kila mtu. Wako waliomwita ‘mchawi’ wengine walimwita ‘mshirikina.’ Lakini walikuwepo wengine waliokuwa wakimtetea kwa madai kuwa anarogwa na watu wenye kijicho kwa mali na jitihada zake. Mradi kila mmoja alikuwa na lake la kusema.

Mzee Ayubu mwenyewe alikuwa mtu wa kuhurumiwa sana. Katika kipindi chote hicho cha msiba alikuwa mkimya muda wote akiwa kajiinamia. Haikuwa rahisi kujua iwapo minong’ono na macho ya kusengenya ya waombolezaji wengine

ilihusiana na ukimya wake au la.

Nilimhurumia zaidi pale nilipomwita chemba na kumuarifu kuwa kazi kwake basi. Alishtuka kama aliyeguswa na waya wa umeme. Nilihisi machozi yakimlengalenga pale aliposema, “Unajua ni wewe ninayekutegemea? Nakuhitaji sasa zaidi ya wakati mwingine wowote ule. Kuondoka kwako itakuwa sawa na kuondoka kwa roho yangu.”

Nilitamani kumsikiliza. Nilitamani kufutilia mbali uamuzi wangu na kurudi kazini kwa kumhurumia. Lakini nilijihurumia pia, zaidi ya nilivyomhurumia yeye. Nikapiga moyo konde na kuung’ang’ania msimamo wangu. Hakuwa na la kufanya zaidi ya kunilipa madai yangu kisha tukaagana bila kuangaliana machoni.

Mfadhili au mshauri wangu mpya, ambaye sasa nilimfahamu kwa jina kuwa aliitwa Bushiri Mtanashati, alinipongeza kwa uamuzi wangu wa kiume. “Ni muhimu sana kwa mtoto wa kiume kujua na kusema ‘ndiyo’ au ‘hapana’. Ukishindwa hilo utaishia kuwa hamnazo.”

Akili yangu ilikwisha hama kabisa toka Mbeya sasa ilikuwa Kilwa. Nilikuwa nikitafakari kile ninachofahamu juu ya mji huo ambao una historia kubwa kote duniani.

Kufika kwangu Kilwa kungefanya nifike Pwani na kuiona bahari kwa mara yangu ya kwanza, bahari maarufu ya Hindi ambayo jiografia inaonyesha kuwa ndiyo inayolinganisha bara letu la Afrika na lile la Asia. Bahari hiyo naambiwa ina maji mengi lakini hayanyweki kwani yana chumvi tofauti kabisa na maji ya maziwa yetu kama Nyanza na Tanganyika ambayo yanafaa kila aina ya matumizi.

Kihistoria Kilwa ni miongoni mwa miji michache katika Pwani ya Bahari ya Hindi ambayo ilikuwa na idadi kubwa ya watu walioishi pamoja. Hali hiyo ilisababisha uwe mji wa

kwanza kibiashara katika nchi yetu. Historia hiyo ilijengeka zaidi April 15, 1497 pale inapodaiwa kuwa mtu mweupe wa kwanza alipokanyaga ardhi ya Tanganyika, kupitia Kilwa katika jitihada zao za kutafuta biashara. Juni 2, mwaka uliofuata Mreno aliyeitwa Vasco da Gama, akiongoza kundi kubwa la watu walifika Pwani ya Tanganyika. Tamaa na uroho wa da Gama vinaaminika kuwa chanzo cha ukoloni wao nchini. Hivyo ilipofika mwezi wa Julai, tarehe 16, mwaka 1500 wakazi wa Kilwa walikuta bendera ya utawala wa Kireno ikipepea juu ya vichwa vyao. Miaka miwili baadaye wakazi hao wa Kilwa waliamriwa kuanza kulipa kodi ya kichwa kwa serikali ya Ureno na hivyo kuufanya mji huo kuwa koloni la kwanza la wageni katika Tanganyika.

Utawala wa Wareno haukuja kwa urahisi kiasi hicho. Baada ya da Gama lilifuata kundi la pili, lililoongozwa na Pedro Cabral, kamanda katika jeshi la wanamaji. Waliuvamia mji kwa mizinga, kusambaratisha wakazi na wengi kuuawa kabla ya kufanikiwa azma yao. Baada ya hapo walimwekea gavana wao wa kwanza, Antonio Fernandes kama mtawala wa kwanza wa Wareno nchini Tanganyika.

Miaka iliyofuata Kilwa iliondokea kuwa lango kuu la biashara. Biashara iliposhamiri sana hapa miaka ya 1901 hadi 1914, ingawa ilipigwa marufuku tangu 1873, ilikuwa ile ya utumwa. Lakini pia biashara za meno ya tembo, dhahabu, vipusa na simbi zilifanyika kwa kasi mjini hapo zikivuta wafanyabiashara toka nchi mbalimbali za dunia kama China, Uarabuni na India.

Mzunguko huo wa biashara pia uliwezesha mazao mbalimbali kama mahindi, viazi na korosho. Aidha, matunda kama vile mapera na mapeasi na mananasi ni sehemu ya ujio

huo wa Wareno waliopo nchini. Pamoja na vyakula athari za Mreno katika utamaduni wa Tanganyika hazitaweza kufutika. Kwa mfano, katika lugha ya Kiswahili maneno kama gereza, meza, lesa, karata, mvinyo na mbolea yana athari kubwa ya lugha ya Kireno.

Kwa mujibu wa kumbukumbu zangu maeneo mengi ya Kilwa ni vivutio vikubwa kwa macho ya mwanadamu. Kwa wapenzi wa mazingira kitu cha kwanza kitakachonasa macho yake ni ile delta kubwa ya mto Rufiji. Delta hii ya aina yake inapambwa zaidi na miti aina ya mikoko iliyoizunguka miti, miti ambayo huota majini na hivyo mashina yake yenye mizizi kuwa maficho na mazalio ya samaki aina mbalimbali hasa kamba.

Kwa mwanahistoria delta hii ni hadithi ya pekee. Ni humo ambamo nguvu za Mjerumani katika Tanganyika zilipata pigo lake la kwanza pale manowari yake ya kivita, *Konigsberg* ilipopatwa na mkasa wa kuharibika na hivyo kuruhusu kipigo ambacho hawatakisahau. Magofu ya Kilwa Kivinje, Kilwa Visiwani, visiwa vya songo mnara, Songalungu, Sanje na Kati na Sanje ya Majoma, mapango ya Chetasui, Mkondaji, Mbagi, Kiinja na Maloho, Jiwe la Mzungu, Kilola Mbani ni miongoni mwa maeneo ambayo mwanahistoria angesisismkwa sana kuyaona kwa macho yake.

Na mwana utamaduni naye atavutiwa na ule mchanganyiko wa tamaduni za makabila mbalimbali ya eneo hilo kama Wamatumbi na Wangino na ule wa Waarabu na kuzaa kitu ambacho baadhi ya watu hupenda kukiita 'waswahili'. Makabila hayo makuu pamoja na na yale ya Wasongo, Wambana, Wambamula, Wamasoko na Washirazi ni sehemu ya utamaduni wa Kilwa. Wengine ni Wamachinga,

Wamakonde, Wayao, Wamera na wengineo. Wengi kati yao wamerithi dini na mila za kiarabu kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, ndani kabisa ya mioyo yao wengi wao bado ni watu walewale, wenye imani na tamaduni zilezile za asili yao.

Kwa mfano, wakati kwa Waarabu watu wa Kilwa wamerithi utamaduni ule ambao hufanya mtoto wa baba mkubwa na wa baba mdogo waweze kuoana bila pingamizi lolote, bado taratibu zao za jadi katika masuala kama jando na unyago ni za asili zaidi. Mtoto wa kiume hupelekwa *itani*, yaani *jandoni* afikapo umri wa kati ya miaka kumi na kumi na nne. Baada ya hapo hupelekwa *utagoni*, ambako hukaa muda mrefu wakifundwa mila, tamaduni na wajibu wao kwa jamii. Hatua ambayo inapokamilika hufuatwa na sherehe maalumu yenye chakula maalum *ngando* ambacho huandaliwa kwa majani ya mti maalumu, *mfulu*, ambao umefanana sana na vidole vya ndege wanayemwita *kituku*, kwetu akiwa ni njiwa.

Masuala hayo ya jando huenda sambamba na yale ya unyago kwa wasichana. Hata hivyo unyago hauna mambo mengi sana. Siku ya kwanza binti ambaye amefikia hadhi ya *mwali* hukamwatwa na kufungiwa ndani akiitwa '*kukujike*.' Siku ya pili hutapishwa kwa dawa maalumu, chini ya uongozi wa *kungwi* mkuu. Siku ya tatu hurudishwa nyumbani kwao ambako huogeshwa, kupakwa mafuta na kuvishwa kanga mpya. Toka hapo yuko huru kwa mchumba yeyote anayestahili kumposa.

Hiyo ndiyo Kilwa, Kilwa ambayo niliifahamu vilivyo kinadharia, baada ya kusoma na kusikiliza simulizi za watu mbalimbali juu ya mji huo wa kihistoria, mji ambao siku mbili tatu zijazo ningeutembelea na kujionea kwa macho yangu mwenyewe siri ya umaarufu huo. Siri hiyo ingesaidia

kuniondolea ‘alama’ katika uso wangu.

Maandalizi ya safari yalikuwa yakiendelea vizuri. Rafiki na mshauri wangu mpya, Bushiri Mtanashati, alikuwa mtu wa kushughulika kinyume kabisa na siku za awali ambazo nilimwona akiwa amekaa bure muda mwingi. Alienda huko na huko kufanya utafiti wa njia bora zaidi, gari lipo na lini linaondoka. Mara mbili alichukua pesa kwangu kwa maelezo yaleyale ya *‘Maandalizi ya safari.’*

Nilikuwa na pesa za kutosha na nilitaka ‘alama’ iondolewe haraka katika paji langu la uso. Hivyo, sikuwa mtu wa kusita kila nilipotakiwa kutoa. Lakini pale alipokuja kwa mara ya tatu, akiwa amelewa, na kuniomba nimpe pesa zaidi nilianza kumtilia mashaka. “Leo unataka za nini?” nilimuuliza.

“Maandalizi.”

“Yapi?”

“Kwani hujui?” aliuliza kwa sauti yenye hasira kidogo “Hii ni safari ndefu. Safari ngumu lakini muhimu sana kwako. Kivuli cha kifo kinakufuata popote uendapo. Usipokiondoa huna uhai, pesa unazotafuta hutazifaidi.”

Sikupenda kubishana naye. Nikampa, shingo upande. Siku hiyo sikumwona tena hadi kesho yake akiwa mchovu sana, bila shaka kwa ulevi. “Safari imewiva. Kesho mchana tunaondoka. Usiwe na wasiwasi mdogo wangu,” aliniambia akijilaza juu ya kitanda changu na kupitiwa na usingizi.

Wasiwasi nilikuwa nao. Bushiri alinitia wasiwasi. Tabia yake, maneno yake na sasa vitendo vyake vilianza kunipa picha tofauti kabisa na ile ya awali, kabla hajautia mkono wake katika mfuko wangu. Alikuwa ameshinda amekaa, ghafla amekuwa hapatikani. Alikuwa halewi, mara amekuwa mlevi! Nilimtazama wakati kalala chali, akikoroma kama nguruwe

aliyejeruhiwa. Karatasi mbili tatu katika mfuko wake wa shati zilikuwa zikichungulia nje. Nikashawishika kuzichomoa ili kujua kama zilikuwa tiketi au la. Haikuwa tiketi. Moja ya karatasi hizo kilikuwa kipande cha kodi ya kichwa cha miaka miwili iliyopita. Ni jina kwenye cheti hicho ambalo liliniacha hoi zaidi. *Abdallah Jonga! Mkazi wa Kisarawe!* Sio Shubiri Mtanashati tena! Wala hatoki tena Newala ambako alisema ni jirani sana na Kilwa!

Nikakumbuka alivyonieleza kwa taabu sana jina na historia yake fupi baada ya kumsaili mara wa mara.

Mimi: Unajua hujapata kunitajia jina lako?

Yeye: Hivi sijakutajia? Naitwa ... Bushili.

Mimi: Bushili au Bushiri?

Yeye: Bushiri

Mimi: Kabila lako?

Yeye: M-makonde

Yeye: Mmakonde wa wapi? Wa Msumbiji?

Yeye: (*Akicheka*) Hapana. Wa Tanganyika hapahapa. Ingawa nina wajomba wengi huko Nampula, Msumbiji. Mimi natoka Newala. Ndiyo maana Kilwa naijua vizuri sana.

Mie: Mimi nilidhani wewe Mnyakyusa, Mbungu au Muandali wa hapahapa Mbeya.

Yeye: (*Akacheka tena*) Hapana. Wengi wanafikiri hivyo. Wengine wananiita Mmalila, wengine Msangu, wengine Mbungu. Sijui kwa nini. Mimi Mmakonde bwana.

Mie: Mbona huna *ndonya*? Wamakonde wengi wana *ndonya*.

Yeye: Nilinusurika. Sikukulia kule sana. Hata kilugha naongea kwa taabu sana.

Maongezi hayo sasa niliyatilia mashaka kutokana na

kulibaini jina lake jingine kwenye cheti hicho. Karatasi ya pili ilikuwa bili ya vinywaji ambavyo ama alikunywa ama anadaiwa. Senti hamsini! Fedha ambazo zilitosha kununua shati jipya, suruali mpya na viatu! Nikaweka nadhiri kutompa hata senti yangu moja bila uthibitisho wa kile ninachokwenda kufanya.

Safari ya kesho, ambayo tayari niliitilia mashaka, ilipatwa na pigo jingine. Tajiri yangu wa zamani, mzee Ayubu alikufa ghafla. Maiti yake ilikutwa ikining'inia kwenye kamba, juu ya mwembe uliokuwa nyuma ya nyumba yake. Alikuwa amejinyonga. Nilisikitika sana na kujikuta nikilia kama mmoja wa jamaa zake wa karibu.

Mara baada ya mazishi jambo jingine, kubwa zaidi, lilitokea na kubadilisha kabisa ramani ya safari yangu iliyokuwa kichwani.

SURA YA KUMI

Tanga, kama Manamba

Kosa langu, ambalo nililifanya bila kukusudia ni kujisahau. Kwa maneno mengine, ni kuyafumbia macho mabadiliko ya umri na maumbile yangu kwa muda mrefu. Ni kosa hilo lililoniletea matatizo ya kisheria, dhidi ya serikali ya Mwingereza na mfalme wao George.

Nilikuwa nimebadilika. Nilirefuka kiasi cha watu wengi wanaoitwa warefu kulazimika kunyanyua nyuso zao ili kunitazama usoni. Sikupata kuwa mnene, lakini mwili wangu ulijaza vizuri na kunipa ukakamavu na kila dalili ya afya njema. Nadhani sura yangu ilivutia, kwani nilipata hisia kuwa wasichana wengi walipenda sana kuzungumza na mie, wakati mwingine bila sababu za msingi. Na pale nilipowakazia macho wengi wao waliinama kwa aibu kuyakwepa macho yangu.

Rafiki zangu huko mtaani nao walinishangaza. Walianza kunipisha kila nilipotokea, huku 'shikamoo,' zikiwatoka baadhi yao. Heshima hizi zilinifanya nisite kuzipokea kwa ukunjufu huku nikijawa na mshangao ulioambatana na maswali tele. Yakoje mambo haya? Au mavazi mazuri ninayovaa na usafi wa mwili wangu vinachangia kunipa heshima?

Lakini ni jana tu nilipoweza kupata majibu ya fumbo hilo. Nilikuwa nimetoka kuoga, tayari nimepaka mafuta na sasa

najikagua kwenye kioo chenye ukubwa wa kiganja changu. Niliridhishwa na nywele zangu nyeusi, zilizosheviwa vizuri. Nilivutiwa na sura yangu ang'avu, yenye pua lililochongoka kiasi cha baadhi ya watu kunifananisha na Watutsi. Mara macho yangu yakavutwa na kitu kigeni katika uso wangu huo. Kwenye kidevu changu, chini ya mdomo, palikuwa na vijinywele vitatu ambavyo havikupaswa kuwa pale. Nilidhani ni nywele zilizokatika toka kichwani wakati nachana, lakini pale nilipovikung'uta kwa kidole na kuona haviondoki ndipo nilibaini kinachotokea. *Ndevu! Nimeanza kuota ndevu!* Hatua ambayo ilikuwa na tasfri moja tu; *Nimekua!*

Sina budi kukiri hapa kuwa kubaini hilo kulinishtua sana. Sikuona kuwa ilikuwa habari njema kwangu kuingia katika safari ya utu uzima bila kutarajia. Sikuwa nimejiandaa, si kielimu si kiuchumi. Bado nilikuwa na ndoto za kurudi shule na kujipatia elimu ili niweze kupata ajira yenye hadhi na wajibu mkubwa zaidi, ambao kwa kawaida huambatana na malipo makubwa zaidi. Kwa kuona dalili za kuzeeka zikianza, nilianza kupata mashaka iwapo nitakaa niyafikie matumaini hayo.

Mawazo hayo yalitembea kichwani mwangu jana tu, leo nilipata majibu. Tulikuwa nje ya hoteli yangu, tukibishana na Bushiri Mtanashati, au Abdallah Jongo, juu ya kumpa fedha zingine za kile alichokiita 'kukamilisha' mikakati ya safari. Nilimkatalia katakata na kumwambia wazi kuwa hata safari yenyewe naifikiria kwa mara ya pili.

Alinitazama kwa macho yake makali, yaliyowekwa katika hali ya kunitisha na kunihurumia pamoja. Kisha, kwa sauti ya upendo aliniambia, "Mdogo wangu naona hujipendi. Hizo fedha zitakusaidia nini kama kila uendako unafuatwa na

kivuli cha mauti? Angalia, utakufa siku si zako.”

Mie pia uvumilivu ulianza kunishinda. “Hivi wewe ni nani hasa hata uwe na kauli juu ya kifo au uhai wangu?” Nilimuuliza. “Wewe ni nani?” niliongeza, “Mungu au Shetani?”

Kauli yangu ilimshangaza kuliko kitu kingine chochote kile. Macho yake yalibadilika na kuwa makali kama simba aliyeona kila dalili ya windo lake kupokonywa. Alifungua mdomo wake kutaka kutamka jambo. Lolote alilotaka kusema lilitoweka pale tulipowaona tarishi watatu wa bomani, walipotujia na kusimama kwa namna ya kutuzingira.

“Toeni vipande vyenu,” tarishi mmoja kati yao aliamuru baada ya kutuuliza majina yetu.

Nilimwona Bushiri Mtanashati akitetemeka. “Vipande gani?” aliuliza.

“Vipande vya kodi,” alifafanua.

“Kodi?” niliropoka. “Ilikuwa mara yangu ya kwanza maishani kuulizwa kodi. Ni hapo nilipobaini kuwa utoto ulikwishanitoka na nimeingia ukubwani. “Lakini mimi sijaanza kulipa kodi,” nilijitetea.

“Kwa nini?” Yule msemaji wao alihoji.

“Mimi bado. Umri haujafika. Isitoshe mimi ni mwanafunzi.”

Askari huyo na wenzake waliangua kicheko.

“Umri bado!” mmoja wao alisema.

“Mwanafunzi!” mwingine alitamka “Mwanafunzi!” aliongeza yule msemaji wa kwanza. “Tunakuona mwaka mzima hapa unafanya kazi mbalimbali, leo umekuwa mwanafunzi! Pita huku!” Nilielekezwa upande ambao kulikuwa na watu wengine kadhaa, bila shaka mateka kama mimi.

Nikaenda na kujiunga nao.

“Na wewe?” walimgeukia Bushiri Mtanashati.

Huku akitetemeka alijishikashika mifukoni na kuchomoa pochi yake ambayo ilikuwa na vyeti na nyaraka zake kadhaa. Alitoa mojawapo kwa wasiwasi na kuitazama. Akataka kuirejesha mfukoni. Tarishi mmoja akawa mwepesi wa mkono. Aliipokonya pochi hiyo na kutoa nyaraka hizo ambazo alizisoma taratibu na kisha kumtazama Bushiri kwa mshangao.

“Inaonekana umelipa kodi mara ya mwisho miaka miwili iliyopita,” alimhoji.

Bushiri alikubali kwa kichwa.

“Halafu,” tarishi huo aliongeza akiwa kamkazia macho, “Umesema jina lako ni nani vile?”

Bushiri alibadilika. Niliona akitokwa na jasho huku miguu yake ghafla ikionyesha kukosa nguvu za kukibeba kiwiliwili chake. Alifunua mdomo kutaka kutamka neno ambalo halikutamkika au kusikika.

Tarishi alimkazia macho. “Hujui jina lako?” alimuuliza tena.

Tarishi wengine walivutiwa na mjadala huo. Wakakiomba kitambulisho hicho na kukitazama kwa zamu. Kila mmoja alitikisa kichwa huku akimtazama Bushiri.

“Za mwizi arobaini,” mmoja wao alisema. “Arobaini za leo zimetimia. Unajiita Bushiri Mtanashati wakati jina lako ni Abdallah Jongo! Jongo tunayemfahamu sisi, ambaye anatafutwa kwa miaka miwili sasa ni mhalifu aliyemwibia mwajiri wake fedha nyingi kule Pangani. Kumbe muda wote umejificha hapa? Twende,” walisema wakimkamata na kumtia pingu.

“Naomba nizungumze faragha na mdogo wangu,” Bushiri au Abdallah alisihi akinitazama mimi.

“Nani mdogo wako? Huyu?” Waliuliza.

“Mimi siyo mdogo wako” niling’aka mara moja. “Nimemfahamu hapahapa, tena kwa jina la Bushiri Mtanashati. Hatuna uhusiano wowote wa damu wala kabila.”

“Mtanashati sio?” Tarishi mmoja alisema akicheka. “Basi atafanya utanashati wake akiwa jela. Wewe suala lako ni dogo. Tutakupeleka bomani ukalipie kodi ya faini. Kama huna utapelekwa manamba, Tanga, ukajifunze kutafuta fedha kwa kukata mkonge.”

Safari ya Kilwa ilikufa. Safari ya Tanga ikazaliwa. Nilikuwa katika kundi la watu wasiopungua arobaini, wenye umri tofauti, waliokuwa wakiisubiri safari hiyo. Nadhani mimi nilikuwa mdogo kuliko wote kiumri. Lakini kwa ajili ya umbile langu niliweza kujumuika katika kundi hilo bila ya yeyote kunishuku.

Sikuwa na sababu kubwa ya kuwemo katika kundi hilo. Nilikuwa na fedha ambazo zingetosha kulipia kodi na bado nikabakiwa na akiba. Aidha, barua ile ya Chifu Masanja na madaftari yangu toka shule yangu ya awali Uhayani, ambayo niliyatunza kama roho yangu, vingetosha kumwonyesha mkubwa wa hapo bomani na angeniachia mara moja. Lakini sikufanya hivyo. Sikuona haja yoyote ya kubakia kusini, ambako sikuwa na kazi wala mipango yoyote inayoendelea kiuchumi au kielimu. Hivyo, sikuona ubaya wowote kusafiri bure, ukihudumiwa chakula na matibabu, hadi katika nchi mpya maishani mwako. Si kuna mhenga mmoja aliyepata kusema kuwa bahati ya mwanaume iko kichwani, miguuni na mikononi mwake? Huwezi jua, pengine huko ambako miguu yangu inanielekeza ndiko iliko bahati yangu.

Hilo ni moja. La pili lililofanya nipokee masaibu hayo ni umbali wa huku nyumbani. Lakini habari za watu wengi wa kutoka kwetu waliokwenda huko kwa njia na mazingira kama haya zilikuwa nyingi. Wengi wao wakiwa wamelowea hukohuko na kufanya makazi ya kudumu. Hivyo, uhakika wa habari na hata uwezekano wa kusafiri toka huko hadi nyumbani ulikuwa mkubwa sana.

Ni kwa mtazamo huo ndipo niliufyata ulimi wangu nisiweze kujitetea na baadaye kukusanya vitu vyangu vyote ambavyo ningesafiri navyo kuelekea Kaskazini Mashariki ya Tanganyika.

Tulisubiri safari kwa takribani wiki nzima, tukiwa tumefungiwa katika ukumbi mmojawapo wa Bomani. Mtu mmoja ambaye sikupata kumfahamu alikuwa ameingiza nakala mbili tatu za magazeti ya *Ngurumo* na *Mamboleo* ambayo hayakuwa na msomaji zaidi yangu. Gazeti jingine la lugha ya kiingereza, *Tanganyika Standard*, ambalo lilikuwa limeanza mwaka 1930 niliweza kupata nakala yake ya miezi kadhaa iliyopita. Ingawa nililisoma kwa taabu kidogo kutokana na kiwango changu cha lugha ya Kiingereza bado nililielewa na kunivutia kwa habari zake.

Bila mwenyewe kuwa na habari, tabia hiyo ya kujisomea kwangu ilivuta macho ya mateka wenzangu pamoja na watekaji wenyewe. Afisa mmoja Mzungu alipotembelea makazi yetu kukagua afya zetu aliponikuta nimejiinamia nikisoma *Tanganyika Standard* alishangaa sana. Alishangaa zaidi pale aliponihoji maswali mawili matatu kwa Kiingereza na nikamjibu vizuri. Akaniuliza kwa nini niko pale. Nilipomjibu kuwa ni tatizo la kodi alitikisa kichwa kwa masikitiko na kuondoka zake. Baada ya tukio hilo nilianza kupewa jukumu la ukarani kwa kuratibu mambo mbalimbali ya manamba wenzangu,

kuwaelekeza wagonjwa matumizi ya dawa walizopewa na wakati mwingine ukalimani kwa wageni ambao hawakufahamu kiswahili.

Sikubahatika kumwona tena bwana Bushiri Mtanashati au Abdallah Jongo. Tangu pale alipotiwa pingu na kuburuzwa huku akinitupia jicho la 'kwa heri' lililoonyesha chuki na hasira dhidi yangu kwa kile alichokichukulia kama kumsaliti, alitupwa gerezeni kusubiri safari ya pwani kujibu tuhuma dhidi yake. Kwa jumla, nilishukuru kutengana naye, kwani nilihisi kuwa angenielekeza shingoni badala ya kileleni. Ndiyo, alinishauri mengi juu ya masibu katika maisha. Lakini gharama ya ushauri wake ilikuwa kubwa kuliko mahitaji halisi. Kwa vyovyote vile, kama ningeendelea naye ningejikuta katika lindi kubwa la umasikini pengine na madeni pia badala ya faraja aliyoniahidi. Kubainishwa kwake mapema kuwa ni mtu wa aina gani kuliniokoa na mengi.

Safari ilianza alfajiri ya siku ya nane toka tulipokamwatwa. Tulisafirishwa kwa lori kuukuu, ambalo mlio wake ulinikumbusha lori la hayati Ayubu ambalo nililitumikia kama kondakta kwa muda mrefu. Sasa tulikuwa zaidi ya watu tisini baada ya wengine kuletwa siku mbili kabla ya safari. Tulijazwa nyuma ya lori hilo, watu na mizigo yetu na kung'ang'ania kuta za bodi ili kujiepusha na kuanguka kwa kuyumba kwa gari kulikosababishwa na ubovu wa barabra. Ilikuwa safari yangu nyingine ngumu, ndefu na ya kukatisha tamaa. Lakini Mungu si Athumani, siku ya nne tangu tulipoanza safari tulifika Muheza ambako tulishushwa ili kusubiri kugawanywa katika mashamba ya mkonge.

* * *

Umepata kulisikia kabila la Wandorobo? Hawa kwa kiasi fulani ni watu wa porini. Wanapenda kuvaa kiutamaduni, pande la ngozi ya nyama (Lusira) au kaniki, ikiwa imefunikwa sehemu tu ya mwili wake. Nywele zao huwa ndefu na hupendelea kuzivuta kwa nyuma. Kwa wanaume mara zote utamwona akiwa ameshika upinde, podo la mishale ubavuni na kishoka, ambacho wenyewe hukiita 'kitodyo' mkononi.

Kwa kawaida Wandorobo ni watu wa kuhamahama, mara msitu huu mara ule. Chakula chao kikuu ni nyama za porini, mizizi na asali. Aidha, ni watumiaji wa matunda ya porini yatokanayo na mimea kama *ngabaito* na *olugumu*. Wakati wa mvua Wandorobo hujisitiri kwa kujenga mabanda ya ngozi za wanyama, mfano wa mahema.

Watu hawa ni mashujaa wa aina yake. Si waoga, hivyo hawapendi au kujali sana umoja. Mtu na mkewe wanaweza kukaa porini kwa miaka bila hofu wala kuhitaji msaada wa watu wengine. Inaaminika pia kuwa wana uwezo mkubwa wa kutumia miti shamba kuyatawala mazingira yao kiasi cha wanyama wakubwa kama simba, chui na majoka kuwakimbia.

Kuna hadithi nyingi za miujiza ya watu hawa. Moja ni ile inayosimulia juu ya wawindaji saba walioingia katika msitu mmoja mkubwa kwa matarajio ya kupata wanyama. Si kwamba hawakufanikiwa tu, bali pia walipotea mchana kutwa wasiweze kujua njia ya kurudi kwao. Ulipofika usiku, wakiwa wamekata tamaa waliona mbuyu mkubwa wenye pango kwenye shina, ambalo lingetosha kuifadhi watu kumi na wa tano au zaidi. Wawindaji hao waliingia katika pango hilo kwa matarajio ya kupitisha usiku. Ikatokea kuwa pango hilo lilikuwa makazi ya joka kubwa aina ya chatu. Lilirejea na kuingia pangoni humo. Wawindaji wale, kwa hofu kubwa walitimka mbio kila mmoja akikimbilia anakokujua, kuokoa roho yake.

Kumbe muda wote ule alikuwepo Mndorobo mmoja aliyekuwa akiwatazama. Mndorobo huyo aliwaita na kuwataka watulie. Kisha akaenda kwenye pango lile la mbuyu na kutamka maneno kadhaa. Mara kwa mshangao wa wawindaji wale joka lile lilitoka taratibu na kutokomea porini. Mndorobo akawataka wawindaji kurejea pangoni na kulala bila wasiwasi wowote. Walilala na kesho uake wakafanikiwa kupata njia ya kurudi kwao.

Pengine jina hili la Wandorobo lilitokana na tabia yao katika ulaji wa uwindaji. Ni hodari sana kwa kutumia mishale. Mshale mmoja wa Mndorobo huua wanyama wawili kwa mpigo si jambo la ajabu. Mara nyingi, wanapowinda uwalenga zaidi wanyama wanaonyonyesha. Mara wanapomwona mnyama wa aina hiyo humpiga mishale na anapoanguka hukimbilia na kunyonya maziwa yake na damu yake kama mdudu aitwaye Ndorobo anavyonyonya damu ya binadamu na mifugo. Huanza kwa kunyonya maziwa. Akitosheka hutafuta mshipa unaotoa damu na kuinyonya hadi ashibe. Baada ya hapo ndipo huchukua kibuyu chake wanachokiita *ululu* na kukijaza kwenye ziwa. Baadaye Mndorobo hurudi nyumbani ambako humchukua mkewe na wanawe na kurudi kwenye windo lao ambalo hulichuna na kulila wakitunza ngozi, mafuta na mifupa kwa matumizi ya baadaye.

Watu hawa, ambao kwa viwango vya dunia ya sasa ni masikini sana, kwani hawana tabia ya kuweka akiba ya chakula wala mifugo, hawajengi wala kulima, hawatilii maanani suala la elimu wala kujishughulisha na masuala ya serikali kwa namna yoyote, wanaaminika kuwa ndiyo wakazi wa asili wa Tanga. Tabia yao ya kuhamahama pia inawafanya wapatikane katika maeneo ya Arusha na Manyara na Singida.

Simulizi za kale zinaonyesha kuwa makabila maarufu ya sasa mkoani Tanga, maarufu kama Waseuta lilipata msaada mkubwa toka kwa Wandorobo hata wakawashinda Wareno na kuweza kuanzisha himaya yao. Simulizi hizo zinaanza kwa mfalme mkuu Seuta. Waseuta walianza ugomvi na Wareno kule Vumba, wakakimbilia Sonjo na Nguu. Baadhi walitimka hadi Kondoa Irangi.

Seuta anaelezewa kutawala Waseuta ambao ni mjumuiko wa makabila ya Wazigua Wanguu, Wabondei, Wakilindi wa Waluvu. Katika makabila hayo awali, lilikuwa moja kabla ya kutawanyika, kila ukoo ukishika njia yake, na kuibuka katika mazingira na lafudhi tofauti, ingawa wote wanalichukulia jina la Seuta, mfalme wao kuwa ni mzimu wao unaowaepusha na balaa na kuwafanikishia masuala yao pale wanapomtambikia.

Seuta alianza kutawala akiwa na miaka kumi na miwili tu. Alizaliwa eneo liitwalo Nguu (Kilindi) baba yake akiitwa Kuba Kaluli. kwa msaada mkubwa wa mishale aliyopewa na Wandorobo, Seuta aliweza kuwateketeza Wareno waliokuwa wakiwaandama. Mbinu nyingine ilikuwa ile ya kuwaachia Wareno vijiji, huku wakiwa tayari wemeteketeza au kuharibu mahitaji yote muhimu kama chakula na maji jambo lililowaacha hoi Wareno. Na wakati wakihangaika ndipo mishale ya Waseuta iliwanyeshea kama mvua na kufanya bunduki zao zishindwe kutimiza malengo yao. Wachache walionusurika walirejea Pwani, ambako huko nako balaa lilikuwa likiwasubiri. Waarabu toka Oman waliwashambulia na kuwafanya waikimbie kabisa Pwani ya Afrika Mashariki.

Hao ndio Waseuta na hiyo ndiyo Tanga. Mkoa mwingine uliobahatika kuwa katika Pwani ya Bahari ya Hindi, kwenye wilaya za Handeni, Lushoto, Korogwe, Muheza, Kilindi na

Tanga yenyewe. Nje ya makabila ya Waseuta makabila mengine ni pamoja na Wadigo, Wasegeju na Wadaiso.

Lakini hadithi ya Tanga katika vita na mapambano hiishii hapo. Mjerumani na mikiki yake alipoingia Tanganyika ghafla aliipenda Tanga. Mwaka 1889 akaiteua kama ngome yake ya vita. Pendekezo lililorasimishwa miaka miwili baadaye. Tanga ilionja kali ya vita kuu novemba 4, 1914 pale mapambano makali yalipoibuka. Mwingereza ambaye alitokea Kenya alitandikwa.

Majeshi yake yaliyokuwa na wapiganaji wapatao 8,000 ambao hawakuwa na ujuzi wa kutosha yalisambaratishwa na kukimbilia maporini, ambako huko nako walishambuliwa na kundi kubwa la nyuki hata vita hivyo vikaitwa ‘vita vya nyuki.’

Lakini ilipofika julai 7 mwaka huohuo, baada ya kujizatiti Mjerumani alizidiwa hata kamanda wa Wajerumani, Von Lettow – Vorbeck, akiwa na bendera nyeupe akamfuata jemedari wa Waingereza, Arthur Aitken na kumwangukia. Jambo hilo liliokoa maisha ya majeshi yake na likampa hadhi kubwa nchini Ujerumani.

Naam, hiyo ndiyo Tanga. Tanga niliyoifahamu kupitia vitabuni na simulizi za wazee walioshiriki vita hiyo kwa hali na mali. Tanga ambayo sasa nilikuwa sehemu ya wakazi wake, nikiishi Pangani, kilometa zipatazo arobaini na tano toka mji mkuu.

Niliandikishwa kazi katika shamba la Mgiriki mmoja, bwana Nicodemus, ambalo halikuwa mbali sana toka mji mdogo wa Tongwe ambao ulibahatika kuwa kando ya barabara inayotokea Mzungu, inavuka mto Pangani na kwenda hadi Majongo na hatimaye Tanga mjini. Tongwe ilikuwa na bahati nyingine kubwa. Reli. Ni ile inayotoke Pwani na kuelekea

Tanga, kabla ya kuchepuka pale Korogwe ambako inaenda hadi Kilimanjaro na Arusha.

Kazi ya kilimo cha mkonge sio mchezo. Inahitaji ujuzi na maarifa kuliko mtu anavyoweza kufikiria. Wageni ambao hawakuwa na ujuzi wa kutosha katika wiki mbili zao kwanza walitaabika sana na baadhi kuugua kwa kuchomwa na ncha ya katani au kudondokewa na maji yake ambayo yanawasha sana. Hali ambayo pia ilichangia kuwanyima mapato.

Mimi, kama kawaida yangu, nilijihisi mwenye bahati. Nadhani tajiri huyo alidokezwa jambo juu yangu, kwani mara tulipoanza kugawiwa majukumu mimi nilifanywa mnyapala na karani wa shamba moja wapo. Jukumu langu lilikuwa pamoja na kutoa ripoti ya kiwango cha kazi ya kila kibarua, kusimamia utendaji wao na kumwandalia tajiri taarifa za malipo ya kila wiki. Haikuwa kazi rahisi kama mtu mwingine anavyoweza kufikiri. Kukimbia hapa na pale, kugombana na huyu au yule, huku muda wote tajiri akiwa nyuma yako akifoka na hata kutukana pasipo sababu za msingi ni miongoni mwa mambo yaliyofanya niichukie tangu siku ya kwanza ya ajira.

Nikaanza kupanga namna ya kutoroka.

Hata hivyo, azma yangu haikutimia hadi mwaka mmoja na nusu baadaye. Kipindi ambacho kilinipa uenyeji wa kutosha wa mkoa huo. Kwa mfano, ni huko Pangani ambako kuliniwezesha kutimiza ile ndoto yangu ya kuona Bahari ya Hindi kwa mara ya kwanza maishani mwangu, ndoto ambayo awali nilitarajia kuitimiza katika ile safari yangu ambayo haikuwa ya kwena Kilwa.

Niliona kile nilichokuwa nikisikia toka utotoni juu ya tabia ya bahari kupwa asubuhi na kurejea jioni. Kwa macho yangu nilijionea eneo la bahari likiwa kavu kana kwamba

halikupata kuwa na maji lakini jioni bahari ikarejea na kulifanya sehemu ya bahari. Majahazi ya wavuzi na wasafiri wakitembea juu yake kama kawaida.

Nilijionea, kuwafahamu na kuwaonja samaki wa maji chumvi; pweza, samaki mtamu mwenye miguu lukuki na kichwa ambacho mgeni wa Pwani huwezi kufahamu ni kipi. Samaki wengine walionitoa macho kwa mshangao nilipodokezwa kuwa waliliwa pia ni kasa ambaye alifanana na kobe na nguva anayefanana umbo na binadamu, hasa mwenye jinsia ya kike, kwa umbile lake. Sikupata kumtia machoni samaki huyo wa ajabu. Lakini picha nilizopata kuona na simulizi za watu zilifanya niamini kuwa nguva ana maziwa kama mwanamke. Wale vibua, kolekole, changu, kamba, ngisi na hata kaa niliwaona na kuwala kama kawaida.

Jambo jingine ambalo lilinivutia macho Pangani ni minazi. Hapana, sio mnazi kwa maana ya urefu wa mti wake, La hash! Walionishangaza ni wakwezi wa mnazi. Mimi nilizaliwa na kukulia porini. Kupanda miti na hata kuruka toka tawi hili au lile lilikuwa jambo la kawaida kwangu. Lakini wakwezi wa minazi ya Pangani, mti mrefu takribani futi 30 au zaidi, ukiwa hauna tawi lolote la kushikilia, kulifanya niwatazame kwa mshangao mkubwa wakwezi hao waliofuata nazi na madafu au kugema mnazi huko angani. Kila nilipomwona mtu akikwea mnazi sikuchoka kumtazama kwa hofu hadi nilipomwona akishuka akiwa salama.

Sitaisahau Pangani wa sababu nyingi. Kubwa ni kunipa fursa ya kumwona kwa macho yangu mwenyewe yule mshairi gwiji, aliyekuwa akiwanyanyasa wakoloni kwa mafumbo yake mazito katika beti za tungo zake. Mtu huyu alitamba sana katika magazeti mbalimbali kama *Ngurumo*, *Kiongozi* na *Lipuli*. Kwa jina aliitwa Shaaban Robert.

Mtu huyu alinisisimua kwa mengi, kubwa likiwa hekima zake ambazo zilichongwa na kufichwa vilivyo katika lugha ya kiswahili, aya baada ya aya, tenzi baada ya tenzi huku zikimsuta mkoloni na kumshawishi Mtanganyika kujiandaa kuichukua nchi yake. Isingekuwa kwa utaalumu huo wa kucheza na lugha Shaaban Robert asingeweza kuajiriwa na serikali hiyohiyo aliyokuwa akiipiga vita kama karani wa Forodha katika kituo cha Pangani kwa miaka kumi na minane kabla ya kuhamishiwa Tanga mjini.

Msisimko wangu kwake, hasa ulitokana na kubaini kuwa elimu yake ilikuwa ya muda mfupi tu darasani, nikiwa nimemzidi kwa miaka miwili, lakini upeo wake wa kufikiri, kuchambua mambo na kuitumia vilivyo lugha ya Kiswahili upeo na uwezo wake uliwazidi kwa mbali watu wengi wenye shahada. Kwa mujibu wa maandishi yake mwenyewe, Shaaban alisoma katika shule ya msingi ya Msimbazi iliyoko Dar es salaam kati ya mwaka 1922 hadi 1926.

Titi la mama ni tamu

Japo liwe la Mbwa,

Ni moja kati ya beti za mashairi yake ambayo kamwe hazijapata kunitoka akilini.

Jambo jingine lililonisisimua katika uhai wangu wa Pangani na Tanga kwa ujumla ni kule kujikuta katika mazingira tofauti kabisa na yale ya kwetu na sehemu nyingi nilizozipitia. Mazingira ya Kiswahili kile nilichokuwa nikisoma na kusikia, kwamba Waarabu walifika miaka nenda rudi katika Pwani ya mwambao mzima wa Afrika Mashariki, sasa nilikiona kwa macho yangu. Wanawake wengi walijificha nyuso zao kuonekana. Wanaume wengi walivaa kanzu na vilemba au baragashia. Idadi kubwa ya wakazi walikuwa Waislam huku tamaduni na hata lafudhi zao zikiwa za Kiarabu

zaidi. Watoto walipenda madrasa wakiwa bado wadogo na wengi wao waliondokea kuwa hodari wa Koran kuliko hata Waarabu wenyewe. Familia nyingi, isipokuwa kwa ajili ya rangi, wangeweza kabisa kuwa sehemu ya wakazi wa Oman, Baghdad au Cairo.

Moja kati ya familia hizo ni ile ya Sheikh Msa. Yeye na wanawe hawakupata kukosa sala hata moja. Kila mmoja, hadi yule mjukuu wa miaka kumi na tatu, tayari alikuwa na 'sijida' katika paji lake la uso inayoonyesha jitihada za uadilifu wake katika kumcha Mungu.

Ilitokea bahati nikafahamiana na mzee huyu. Alikuwa kazini kwangu akiwa na barua ya Kiingereza ambayo alitaka nimsomee. Barua hiyo iliondokea kuwa fomu iliyotakiwa kuijaza ili kupata uthibitisho wa ushiriki katika vita vikuu vya kwanza. Ni katika kumjazia niliposhangaa alipodai kuwa asili yake ni Kigoma.

"Kigoma! Kigoma ipi?" Nilimuuliza

"Kwani kuna Kigoma ngapi, Sheikh?" alinijibu kwa swali vilevie. "Kigoma ni moja tu ya Wamanyema na Waha."

"Wewe ni Mmanyema?" Nikahoji tena.

"Hapana, Muha, ingawa huku tunaruhusiwa kuitwa Wamanyema..."

Nikazidi kuvutiwa naye, "Muha wa wapi?"

"Kasulu, baba alipotea maeneo ya Nyamasovu, akalowe huku." Ikawa zamu yake kushangaa. "Siye tunafahamu unatokea Mbeya! Kumbe 'mwanangu' allah akbar!"

"Ni hadithi ndefu," nikamjibu "Nyumbani hasa ni Buha. Kwenda Mbeya na kufika hadi huku ni katika jitihada za kutafuta maisha."

"Allah akbar" alisema tena akiwa amenikodolea macho ya mshangao.

Tulizungumza sana na mzee huyo maongezi ambayo yalikolea pale nilipomtazia jina la babu yangu na akajikuta amemkumbuka mara moja.

“Wewe ni mjukuu wa Kionambali? Oh ni mwanangu kabisa!” alimaka. Akanieleza alivyokutana na babu katika vita kuu ya kwanza, walipochukuliwa kama wapagazi, wakaishia kupewa bunduki. “Babu yako alikuwa mkorofi sana. Hakupata kumfyatulia adui bunduki hata mara moja. Wajerumani wakamfanya mpishi. Huko nako alikuwa na vituko vyake vingi tu. Halafu akatoweka. Nadhani Wajerumani walimwua. Walikuwa katili sana.”

Nilihisi machozi yakinilengalenga kwa simulizi hiyo ambayo babu hakupata kunisimulia hata mara moja. Mzee alishangaa zaidi pale nilipomwambia kuwa yuko hai, alirejea Buha zamani sana.

“Sishangai. Ni mtu wa miujiza sana babu yako. Hatabiriki!”

Nikawa nimepata ndugu, udugu ambao ulipelekea mzee huyu anitazame kwa jicho tofauti na lile la kawaida, kabla hajasema taratibu, “Mwanangu una nini? Kwa kila hali hustahili kuwa hapa ukifanya kazi hizi za kitumwa. Umesoma una busara, na una afya tele. Kuna kitu kimepungua au kuzidi katika nafsi yako. Ni hicho kinachofanya uwe mtu wa kutangatanga. Ama nyota yako imefifia. Inahitaji kusafishwa.”

SURA YA KUMI NA MOJA

Kwa jahazi hadi Bagamoyo

Kwa mara ya kwanza niliitumia bahari kusafiri. Kwa ushauri wa mzee wangu na mshauri wangu mpya kwa masuala yanayohusu maisha, Sheikh Msa, haikuwepo haja ya kutumia barabara ambayo gharama yake ilikuwa kubwa zaidi na magari yalipatikana kwa shida sana. Bahari ya Hindi ilitosha.

Safari yangu ilikuwa ya kwenda Bagamoyo, dhamira ya safari ikiwa ileile iliyotaka kunipeleka Kilwa, kusafisha nyota yangu kwa kuondoa ‘wingu’ la mkosi ambalo lilifunika bahati yangu, safari ambayo ilitokana na maelekezo ya mzee Msa, baada ya maongezi marefu baina yetu toka siku ile alipoishuku nyota yangu kuwa na kasoro.

Sikuwa na sababu yoyote ya kutomwamini mzee huyu. Akiwa mtu mwenye heshima zake, mtu anayejiweza kiuchumi kwa kumiliki mashamba na vyombo vya uvuvi, huku watoto wake wanne wakishindana kumletea mahitaji mbalimbali; asingekuwa na sababu yoyote ya kunihujumu kama alivyokusudia yule Bushiri Mtanashati, hapana. Nilimsimulia mkasa mzima wa safari yangu, toka zilipoibuka fununu za kunitoa kafara kwa ajili ya mvua hadi safari yangu ya nchi ya

Wahaya kutafuta elimu na hata kupotea kwa hirizi niliyopewa na babu.

“Unaona? Unaona? Nilijua zamani una jambo mwanangu. Sasa lazima usafishwe, uoshwe. Hirizi yako lazima irudi,” kauli ambayo ndio hasa iliyozaa safari hii ya Bagamoyo.

Naikumbuka vizuri tarehe ya kuanza kwa safari yangu. Ilikuwa tarehe 7 Januari, 1938. Sikuwa na namna ya kuisahau kwani ni siku hiyo serikali ya Mwingereza, kwa kauli ya gavana wake nchini, wakati huo bwana H.A Mac Michael, alipoitazama rasmi eneo la Pangani kuwa wilaya kamili.

Safari ilianza alfajiri, mara baada ya pepo za kusi toka kaskazini kuanza kuvuma. Tulisafiri kwa jahazi litumialo matanga yaliyopokea upepo vizuri sana na kwa ujuzi wa naodha wetu aliyekuwa akitoa maelekezo kwa mahabaharia wake haikuchukua muda kabla ya jahazi letu kushika kasi likifuata mwambao wa bahari kukelekea kusini. Tulipepepa hadi Mwera, tukaacha na kuingia Mkwaja, tukaipita hadi Saadani kabla ya kutia nanga Bagamoyo mjini saa kumi na moja za jioni.

Pamoja na uzoefu wangu wa mambo ya majini sina budi kukiri hapa kuwa nilifika Bagamoyo nikiwa taabani. Upepo wa kusi ambao tulianza nao safari ulikuwa ukibadilikabadilika mara kwa mara. Ziko sehemu ambazo tulipambana nao, ukituelekeza takribani hukohuko tunakotoka, lakini kwa uhodari wa naodha chombo hakikupata kwenda mrama. Ziwa Nyanza lina mawimbi. Lakini mawimbi yale na haya niliyopambana nayo baharini ni vitu viwili tofauti kabisa. Kama wimbi la ziwani ni kubwa kama nyumba la bahari liliweza kuwa kubwa kama mlima. Chombo chetu kilipaa na kushuka juu ya mawimbi hayo kama unyoya, huku naodha wa baharia

wetu wakifanya hili na lile kuhakikisha usalama.

Harufu ya maji chumvi nayo ilikuwa kero nyingine. Ilikuwa harufu aina fulani, kavu, ambayo ilishawishi kutapika. Hata hivyo, sikuthubutu kukubali kushawishika. Hakuna aibu katika safari za majini kama kutapika. Wazee wengi husema kuwa hayo ni maradhi ya wanawake.

Jahazi hilo lilikuwa na abiria wawili tu, mimi na Ramadhani, mtoto wa nne wa mzee Msa, ambaye aliteuliwa kunisindikiza. Awali, ilikuwa Msa mwenyewe anilete Bagamoyo, lakini siku mbili kabla, alibanwa na mshipa wa ngiri, uliofanya ashindwe hata kutoka kitandani kuniaga. Hivyo, Ramadhani ambaye tulikaribiana kwa umri akabebeshwa jukumu hilo la kuniongoza. Na alianza kwa kunifikisha salama mikononi mwa mjomba wao aliyekuwa akiishi hapohapo Bagamoyo. Tulikaribishwa vizuri, tukapewa chakula na malazi hata kabla ya kueleza kiini cha safari yetu.

Kesho yake Ramadhani alinitambulisha kwa mjomba wake huyo kama ‘ndugu yetu’ ambaye mola kamleta mikononi mwetu ili kumnusuru na pepo mbaya aliyemkumba.’ Akaeleza kwa ufasaha kila alichelekezwa na mzee Msa kukieleza.

“Hilo mbona tatizo dogo tu.” Mwenyeji wetu, ambaye baadaye nilibaini kuwa ni Imam wa msikiti mashuhuri wa hapo Bagamoyo, alisema. Kwa jina aliitwa Al Haji Suleiman. Sikupata kuuliza kama Al Haji ni jina lake au wadhifa ambao muislam hupata baada ya kutimiza nguzo mojawapo muhimu ya dini ya kwenda Hijja.

“Tatizo ni dogo sana,” aliongeza. “Kesho pia pumziken. Kesho kutwa nitawapeleka Mlingotini, kwa Sheikh Mahmoud. Atamsafisha mara moja na kama kuna mkono wa mtu, mtu huyu ana bahati mbaya sana.”

Nilikuwa nimechukua likizo ya wiki mbili kazini kwangu. Hali ya mfuko wangu kifedha pia haikuwa mbaya. Hivyo, mapumziko hayo ya siku moja kabla ya kukutana na ‘mtaalam’ wa kusafisha nyota niliamua kuyatumia kwa kuvinjari vilivyo Bagamoyo.

“Unafahamu kuwa pamoja na mambo mengine kufika hapa Bagamoyo peke yake ilikuwa ni moja ya ndoto zangu kubwa maishani?” nilimwambia Ramadhani.

“Kwa nini?” alihoji.

“Huu ni mji wa kihistoria,” nilimwambia. “Wataalamu wa historia na mambo ya kale wanaamini mji huu ni wa kale kuliko yote Afrika Mashariki. Wanaamini ulikuwepo kabla ya kalenda tunayoitumia sasa, yaani kabla ya Issa bin Mariam hajazaliwa kule Nazareth. Huoni kama ni bahari ya pekee kuwa katika mji huu leo na kujionea kwa macho yako kile ambacho umekuwa ukisimuliwa na kujisome?”

Ramadhani alikuwa na tabia moja ambayo sikuipata kuipenda. Tabia ya kuiminye midomo yake kila unapomwambia jambo ambalo anahitaji kulitafakari. Tabia hiyo huchukua nafasi yake ya kutabasamu, kucheka na kununa. Ndivyo alivyofanya nilipomweleza jambo hilo. Sikujua kama anatabasamu au amenipuuza. Nilisubiri kwa dakika nzima kabla ya kuipata kauli yake. Hivyo, nikaamua kumwambia, “Kama wewe hupendi kutembea nitakwenda peke yangu.”

Aliiminye tena midomo yake kabla hajasema, “Uwe mwangalifu sana.”

“Kwa nini? Nitapotea?” nikamuuliza.

“Si afadhali upotee!” alisema. “Hii ni Bagamoyo ndugu yangu. Jina halisi la hapa ni ‘Bwaga moyo’ maana ukifika hapa sahau kwenu, sahau yote unayojivunia. Hapa ni mwanzo na

mwisho wa maarifa.

Sikumwelewa. “Kwa hiyo,” nikamuuliza.

“Kwa hiyo, maana yake ni kwamba uwe makini sana na nyendo zako. Usione paka ukampiga jiwe. Utashangaa anageuka binadamu na kukuliza, ‘wanipigia nini? Nikikupiga miye utaamka weye?’

Nikaangua kicheko.

“Usicheke,” Ramadhani alinionya. “Sikutanii. Haya ni mambo ya kawaida hapa. Vilevile usithubutu kutamani mwanamke. Ukimtamani mke wa mtu utarudi kwenu umeota busha la tende. Na ukikutana na msichana mzuri ukamtaka, utashangaa atakavyokuchangamkia hata kukushawishi ufike nae kwao. Huko utakuta nyumba nzuri, vijakazi tele na utalazwa kwenye kitanda murua kinachonukia manukato. Lakini utakapomka kesho utajikuta umelala makaburini, peke yako.”

Hadithi zake ziliniyunja nguvu. Hazikuwa hadithi mpya. Lakini zinakuwa na uzito wa pekee pale zinapozungumzwa ukiwa juu ya ardhi ya Bagamoyo, mzungumzaji mwenyewe akiwa mtu anayekuongoza kwenda kwa mnganga. Kwa kweli, zilipunguza sana ari yangu ya kuvinjari mji wa Bagamoyo.

Nadhani Ramadhani aliyasoma mawazo yangu. Nilimwona akiuvuta tena mdomo wake. Nikahisi kuona dalili za kicheko au tabasamu katika macho hayo, dalili ambazo zilifuatiwa na kauli yake aliyoitoa kwa sauti ndogo “Usiogope. Nenda katembe. Mimi najisikia uchovu bado. Natamani kulala usingizi mchana.”

* * *

Wafanyabiashara wa Kihindi na Waarabu ni sehemu moja ya kihistoria ya Bagamoyo. Wajerumani na Wamisionari wa dini ya kikristo ni sehemu ya pili ya mji huu wa kale wa Bagamoyo. Historia ilianza rasmi kunukuu kuwepo kwa mji huu toka karne ya kumi na tatu, wakazi wake wengi wakiwa wavuvi na wakulima. Mnamo karne ya kumi na nane familia kadhaa za kiislam, za ukoo wa mtu aliyejulikana kama Shamvi la Magimba aliyeishi Oman zilihamia Bagamoyo na kuifanya makazi yao. Wakaanza pia kuwatoza wenyeji kodi. Wakati huohuo biashara za chumvi, shanga na nguo zikishamiri. Biashara ambazo zilifuatiwa na ile ya watumwa wa pembe na za ndovu toka sehemu za ndani ya nchi kama Morogoro, Kigoma na hata Kongo. Wakati biashara ya utumwa ilipigwa marufuku rasmi mwaka 1873, mjini Bagamoyo biashara ilishamiri hadi mwishoni mwa karne ya kumi na tisa.

Hayo niliyafahamu kinadharia.

Sasa nilikuwa nikiyaona kwa macho yangu mwenyewe. Nilianza kwa kwenda kaskazini mwa mji huo ambako kulikuwa na eneo la Wamisionari wa kikatoliki. Lilikuwa eneo kubwa lenye majengo kadhaa likiwemo kanisa, shule, karakana za ufundi na miradi ya kilimo. Kwa mujibu wa kumbukumbu zangu misheni hii ilianzishwa mwaka 1868 kwa waislam kutoa ardhi hiyo kwa wakristo. Jambo hilo linaelekezwa kuwa lilizusha upinzani mkubwa toka kwa wenyeji, Wazaramo, ambao hawakuridhika wageni kugawa ardhi kwa wageni wengine ili waanzishe dini ngeni ambayo ilipingana na maadili yao.

Nilitembea nje ya majengo hayo, nikichungulia hapa na pale na kuvutiwa na kila nilichokisoma. Wafanyakazi wa misheni walikuwa katika pilikapilika zao, wanafunzi

wakiwa madarasani. Kwa mbali, nilimwona padri mmoja akitembea taratibu, rozali mkononi. Mara nikayakumbuka maisha niliyoyaacha katika misheni kama hiyo kule Kagera. Nikaikumbuka nafasi ya elimu niliyoipoteza. Kisha nilikumbuka hirizi yangu, hirizi ambayo niliamini kupotea kwake ndio chanzo cha mikosi na mikasa iliyoniandama. Nilihisi machozi yakinilengalenga. Nikageuka na kurudi nyumbani taratibu.

“Mbona mapema?” Ramadhani aliniuliza. “Hamu yako ya kuiona Bagamoyo imeisha mara hii?”

Badala ya kumjibu niliiminya midomo yangu kama ilivyokuwa kawaida yake. Nadhani alinieleva, kwani kwa mara ya kwanza nilimwona akiangua kicheko. Mie pia nikaangua kicheko. Tulicheka pamoja kwa dakika moja au zaidi bila sababu za msingi. Mimi nikimcheka yeye na yeye akinicheka mimi; tukio dogo, ambalo lilinifanya nijisikie karibu zaidi na ndugu yangu huyu. Nadhani naye alijisikia hivyo kwani toka hapo alikuwa rafiki zaidi kuliko ule udugu wetu wa awali.

Kesho yake Alhaji Suleiman alituamsha alfajiri, ili tujiandae kwa safari ya Mlingotini. Tulioga, tukapata kifungua kinywa na kisha kuanza safari hiyo ya miguu tukielekea kusini mwa mji. Nusu saa baadaye tulikuwa mbele ya nyumba ya Sheikh Mahmoud. Tulikaribishwa vizuri sana na mkewe na kukaribishwa kahawa kwa kashata na tende, ambazo nilizifurahia sana. Lakini pale mwenyeji wetu alipomweleza mama huyo haja yetu ya kumwona mzee, nilijiona nilivyokuwa mtu mwenye bahati mbaya.

“Hayupo,”

“Kaenda wapi?”

“Kasafiri. Tena kaondoka alfajiri ya leo tu. Wamekuja watu toka Darisalama kumchukua, akawasidie. Kama

mngejua, jana kashinda hapa hana kazi yoyote.”

Wote watatu tulitazamana kwa zamu. Kisha mwenyeji wetu akamgeukia mama Mahmoud na kumuuliza, “Atarudi lini?”

“Hakusema. Lakini huwa hakai nje muda mrefu. Anaweza kurudi kesho au kesho kutwa. Ningeshauri mje tena kesho au kesho kutwa, huenda akawepo.”

Tulishukuru tukaaga na kuondoka.

Mimi sikurejea nyumbani mara moja. Niliwataka udhuru wenyeji wangu kuwa ningependa kuendelea kuvinjari maeneo ya kihistoria ya Bagamoyo. Jiografia yangu ilionyesha kuwa toka hapo Mlingotini haikuwa umbali mrefu kuyafikia magofu ya Kaole, mji ule wa kale ambao kitendawili chake bado hakijateguliwa hadi leo.

Walindiruhusu. Wakashika hamsini zao nami nikashika hamsini zangu.

Nilipenya katika vichaka hadi kuyafikia magofu ya mji huo. Ilibidi kukaza macho ili kuweza kuona mabaki ya majengo ambayo yalionekana kama misikiti na majumba ya watu. Baadhi ya majengo hayo tayari yalifunikwa na ardhi na mimea kuota juu yake. Lakini kuta kubwa za mawe, milango yenye nakshi ya aina yake na sakafu imara zilitoa kila dalili ya maendeleo au ustaarabu wa watu walioishi mji huo. Kitu kingine kilichovuta macho yangu ni wingi wa makaburi yaliyojengwa kando ya majengo hayo. Ilionyesha kuwa wakazi hao ama hawakupenda kuwazika wafu wao mbali, ama mji huo ulikuwa maalum kwa ajili ya mazishi.

Mji wa Kaole machoni mwa wataalamu ni kama kitendawili kwa sababu kadhaa. Kwanza, kwa kila hali unaonyesha kuwa ulikuwa mji mkubwa uliokaliwa na watu

wengi. Lakini hadi sasa hakuna mtaalamu yeyote ambaye alipata kubaini bila mashaka nini kiliutokea mji huo na wakazi wake walikwenda wapi. Baadhi ya wataalamu hupata hisia kuwa huenda yalitokea maradhi mabaya ambayo yaliwateketeza wenyeji wote. Hisia hizo hupingwa mara moja kutokana na utafiti ambao haujapata kuonyesha mafuvu au mifupa ya watu iliyozagaa kuthibitisha tukio la aina hiyo.

Baadhi ya watafiti katika mji huo waliwahi kuchimbua sarafu iliopata kutumika katika karne ya kumi na mbili. Sarafu ya Kilwa inaaminika kuwa ni moja ya zile za Sultan Ali Hassan ambaye alitawala Kilwa katika kipindi hicho. Uthibitisho mwingine unaoashiria kuwa Kaole na Kilwa ziliwasiliana kibiashara miaka hiyo.

Nilitembea katika magofu hayo moja baada ya jingine. Viumbe pekee hai niliowaona wakiwa ndege, mijusi na digidigi wawili niliowakurupusha. Nilipojiridhisha kuwa nimetimiza wajibu wangu kutembelea eneo hilo nilirejea nyumbani.

Kesho yake Alhaji Suleiman alikuwa na wageni. Alituruhusu mimi na Ramadhani kwenda peke yetu kwa Sheikh Mahmoud. Tuliarifiwa kuwa hajarudi.

“Jaribuni tena kesho,” mkewe alituelekeza.

Asubuhi hiyo mimi niliendelea na safari zangu. Nilitembelea lile jengo maarufu ambalo awali lilikuwa soko kuu la watumwa, binadamu wakipigwa mnada kama mifugo, jengo imara lenye kuta pana zilizopanda juu ambazo pia ziliweza kuhimili silaha hafifu za enzi hizo.

Wajerumani walipoitawala Tanganyika waliitumia ngome hii kama makao yao makuu ya jeshi. Hata hivyo, mwaka wa kwanza tu wa vita vikuu vya kwanza wajerumani walisalimu amri na kuikimbia Bagamoyo pale majeshi ya

Uingereza walipowamiminia mabomu toka katika mizinga yao ya melini.

Nilishuhudia kwa macho yangu makovu ya mabomu hayo na kushika kwa mkono wangu, mmoja wa mizinga ya Mjerumani iliyotekwa. Nikafurahi sana kwa fursa hiyo.

Kesho yake tuliamkia tena kwa Sheikh Mahmoud.

“Hajarudi. Hatujui kapatwa na nini maana si kawaida yake,” mkewe alisema sura yake ikiwa na dalili za wasiwasi na mashaka.

Niliendelea kuvinjari Bagamoyo. Kwa ushauri wa mmoja wa vijana mjini hapo nilitembea hadi eneo la Mbegani ambako nilishangazwa na wingi wa wanyama mbalimbali wa porini, wengi wao wakitembea hadi Pwani ya bahari kama mifugo. Walikuwa twiga, swala, korongo na pundamilia. Ndege wa aina mbalimbali pia waliipamba burudani hiyo ya aina yake kiasi cha kufanya nijione kama natazama picha ya sinema badala ya hali halisi.

Toka hapo nilitembea hadi mdomo ambao mto Ruvu uliingiza maji yake katika bahari, upande wa pili mji wa Bagamoyo. Hapo pia kuna burudani yake, kuona maji ya mto yanavyoshindana na yale ya bahari na bahari ikasalimu amri. Yakiwa maji yanayopita maeneo mbalimbali, maji haya yalibeba aina mbalimbali za taka ikiwa pamoja na udongo ambao ulifanya rangi ya maji eneo hilo hadi baharini ibadilike.

Nilirudi nyumbani nikiwa taabani kwa uchovu. Kesho yake nilichoka zaidi pale tulipokwenda tena kwa Sheikh Mahmoud na kukuta pana msiba, akina mama wakilia ndani, watani wakipita na kusema hili na lile bila kujali huzuni ya wafiwa.

“Kuna nini?” mmoja wetu aliuliza.

“Mzee Mahmoud amefariki.”

“Lini?”

“Hatujapata uhakika. Kafia Darisalama. Maiti imeletwa leo alfajiri.”

Nilipigwa na butwaa. Nguvu zikaniisha. Nikamkodolea macho Ramadhani ambaye pia alionekana kuduwaa, hajui lipi ni lipi.

Baadaye tulipata nusu ya ukweli toka kwa mtani wao mmoja Mluguru ambaye aliinuka na kuangua kicheko kabla hajasema, “Yako wapi? Siku zote nilimwambia akawa mbishi. Alijitia yeye bingwa wa kutoa majini na roho za watu. Mbona hili limemshinda? Achezee majini ya Kizaramo siyo ya Kimanyema. Amekwenda Darisalama, amelitania jini limemshikisha adabu. Yako wapi?”

Nilishtushwa sana na uzito wa maneno ya mtani huyo, ukizingatia kuwa hata maiti alikuwa yungali ndani. Ndugu wa marehemu walikasirika lakini hawakuwa na la kufanya. Hali ambayo ilifanya mtani huyo aongeze vijembe.

“Mnajua alitoa roho ngapi mzee wenu huyu? Mnajua kila roho inamngojea huko aendako na kijinga cha moto mkononi? Toka leo yeye ni mtu wa kuungua tu, usiku na mchana,” aliongeza huku akionyesha jinsi marehemu atakavyokuwa akirukaruka kwa maumivu ya moto.

Haikuwa rahisi kujizuia. Hata baadhi ya wafiwa walicheka.

Mazishi yalifanyika mchana huohuo. Alhaji Suleiman aliendesha ibada ya mazishi msikitini na baadaye kwenye mazishi. Alisoma dua kadhaa hadi marehemu alipolazwa katika mwanandani. Tukatawanyika. Wana ndugu na majirani wakienda kulala matanga. Siye wengine tukirudi majumbani.

Mimi binafsi niliduwa. Kitu fulani kilinifanya nishuku kuwa kifo hiki ni katika jumla ya mateso na mikasa dhidi yangu. Vinginevyo, kwa nini afe ghafla? Kwa nini afe hata kabla sijamtia machoni na kusikia ambacho angeongea juu ya masaibu yangu? Kitu gani hasa kinanitokea?

Mawazo hayo yalinitinga kiasi kwamba alinisemesha mara mbili bila ya kumsikia. Aliporudi kwa mara ya tatu nilisikia sauti yake bila ya kumwelewa. Nikamtaka radhi.

“Naona uko mbali sana,” alisema. “Nilikuwa nikikwambia kuwa wajuzi wa masuala yale wako wengi. Usivunjike moyo kwa kifo cha Sheikh Mahmoud. Kesho tu Alhaji atatupatia mtaalamu mwingine.”

Sikujua kama bado nilikuwa na hamu ya wataalamu zaidi, baada ya kifo cha kutatanisha cha mtalaamu huyu.

SURA YA KUMI NA MBILI

‘Mgeni’ Siku Ya Tatu.

Kesho yake ilikuwa Jumapili. Niliamka alfajiri, kabla ya mtu yeyote mwingine katika nyumba ya Alhaji Suleiman. Nikachukua ndoo ya maji toka kwenye pipa la maji ya akiba na kuibeba hadi maliwatoni ambako nilioga. Nikarudi ndani na kuvaa nguo zangu safi, nikachana nywele zangu, kisha huyoo; nikaondoka zangu.

Kwa kweli, sikuwa na pa kwenda. Haja yangu ilikuwa kupata nafasi ya upweke ili niweze kuifikiria hatma yangu kwa kina. Upekee huo niliupata ufukweni, nilipoketi juu ya gogo la mnazi ulioanguka nikiitazama bahari. Macho yangu yaliweza kuiona mitumbwi ya wavuvi wawili watatu waliokuwa baharini wakitafuta riziki zao. Niliweza pia kuviona visiwa vya Zanzibar na Unguja, ambavyo kutoka hapa Bagamoyo ni mwendo wa kilomita thelathini tu kuvifikia.

Nikapata wazo. Kwa nini nisiachane na imani za kishirikina za kuwekwa alama au nyota kuchafuka na kuijaribu bahati yangu katika biashara? Kipindi nilichokaa hapo Bagamoyo nilikwisha sikia na kujionea mwenyewe biashara mbalimbali zilizokuwa zikiendelea baina ya mji huo na visiwa vile. Biashara kubwa iliyonivutia ni ile ya chumvi.

Uzalishaji wa chumvi, toka katika mabwawa mengi

yaliyochimbwa kandokando mwa bahari nje kidogo ya mji wa Bagamoyo ilikuwa imeshamiri sana na iliuzwa maeneo mbalimbali ya pwani na bara. Nilichukulia kama biashara isiyo na madhara sana kwani kila mtu anahitaji chumvi katika chakula chake na ni bidhaa ambayo haiharibiki haraka kama nyanya au samaki. Kwa kuwa bado nilikuwa na akiba yangu ya fedha nilishawishika kumshauri kiongozi wangu wa msafara, Ramadhan, tuifanye kazi hiyo kwa muda kabla ya kurejea Pangani.

Wazo hilo lilinipa uhai mpya. Nikajiona nimechangamka. Nikainuka na kuanza kurandaranda juu ya mchanga wa bahari, ambao maji yake yalikuwa hayajarudi.

Mara nikasikia kengele ya kanisa ikilia kwa mbali. Ikanizindua. Nikakumbuka kuwa nilikuwa sijahudhuria ibada kwa muda mrefu sana, toka lilipotokea lile tukio la hirizi na kukimbia kwangu. Kuna ubaya gani nikienda kanisani? Nilijiuliza. Sikuhitaji jibu. Niligeuka na kuanza kutembea, kuelekea kwenye kanisa ambalo linadaiwa kuwa la kwanza Afrika Mashariki. Nilikuwa miongoni mwa waumini wa kwanza waliofika kujumuika na wenzao katika kumcha bwana.

Kana kwamba padri alijua kuwa katika waumini wake alikuwemo mmoja ambaye yuko njia panda kati ya imani ya bwana na ushirikina, mahubiri yake yalielekea katika kulaani vitendo hivyo na kumtegemea Yesu. “Alizaliwa kama mmoja wetu, akasulubiwa, akafa na siku ya tatu akafufuka. Damu yake ilitusafisha na laana ya asili. Tumefunguliwa minyororo yote ya dhambi. Jina lake ni dawa na jibu pekee la kila tatizo letu.” Padri alisema. Kuna wakati nilihisi kama alikuwa amenikazia macho mimi, kana kwamba anaisoma roho yangu kupitia katika macho yangu.

Mwisho wa ibada nilifikiria kumfuata padri ili niungame, lakini nikasita. Nitaungama kwa lipi? *'Baba nimetenda dhambi! Nilipoteza hirizi ya babu! Nikamsukuma padri na kukimbia! Sasa naona mambo yangu yanakwenda mrama. Baba nisamehe!'* niliwaza. *Atanielewa kweli?* Niliwaza nikicheka mwenyewe kimoyomoyo.

Baada ya kutoka katika eneo la kanisa niliona bado ni mapema kurejea nyumbani. Nikaamua kurudi ufukweni na kuvinjari taratibu kuelekea kusini. Nilipita nikiitupia macho mikoko iliyonawiri katika maeneo mbalimbali ya mwambao huo wa bahari. Bila kutegemea nilijikuta nimefika tena Kaole. Nikachepuka na kuingia katika eneo lenye magofu yale ya kale, nikichungulia hapa na kupapasa pale kana kwamba nilitarajia kitendawili cha mji huo kiteguke, nijue ni watu gani hasa walioishi hapo, walianza kuishi lini na masaibu gani yaliwakuta.

Mawazo yangu yalisitishwa na mlio wa kitu kama chuma kilichogongana toka upande wa pili wa jengo la msikiti niliokuwa nikiukagua. Nilishtuka sana, nywele za utosini zikanisimama. Nikatulua na kusikiliza kwa makini. Zaidi ya nyimbo za ndege wa angani na milio ya wadudu wasiofahamika, palikuwa na ukimya mkubwa. Nadhani masikio yangu yamenidanganya; Niliwaza nikianza tena kutalii. Mlio ule ukasikika tena. Safari hii ukifuatiwa na sauti ya mtu aliyekohoa. Huku nikiwa na hofu, nilinyata kuelekea upande ule. Nikawaona. Watu wawili, mwanamume na mwanamke, walikuwa wameinamia gari wakihangaika kulitengeneza. Nadhani, kwa maelezo ya mwanamume, mwanamke aliingia ndani na kuwasha. Mlio uliosikika ulionyesha kuwa gari hilo lisingewaka kamwe. Mafuta yalikuwa hayaingii kwenye kabreta. Nikawasogelea.

Waliponiona wao pia walishituka kama mimi. Lakini baada ya kuniona kuwa ni mtu wa kawaida, sio mmoja wa mizimu ya watu wa kale, walichangamka na kunisalimu kwa Kiswahili chao cha mashaka. Niliwaitikia, baadaye nikawauliza kwa Kiingereza changu ambacho nadhani kwao kilikuwa cha mashaka pia, “Kuna tatizo gani?”

Walichangamka zaidi kuona naongea lugha yao. Mwanamume akaeleza. Gari lilikuwa linawaka, halipandi mafuta. Na joto lilikuwa likipanda kwa kasi kiasi kwamba gari isingeweza kutembea kwa dakika kumi kabla ya kuishiwa maji. “Unamjua fundi?” waliuliza.

Sikuwa mgeni wa magari mabovu. Uzoefu wangu wa lile gari la mzee Ayubu Kilole kule Mbeya na malori ya shambani mwa bwana Nicodemus Pangani vilinifanya nijue wapi pa kuanzia kabla ya kumhitaji fundi. Nikawaomba nichungule kidogo. Wakanipisha. Nikafunua tenki la maji. Yalikuwa yamekauka. Nikafunua gudulia la maji yatokayo kwenye injini. Lilikuwa limejaa pomoni. Nikayachukua na kuyamimina kwenye lile tenki la kupozea injini. Kisha nikakagua na kugundua mpira mmoja wa kupitisha hewa ambao ulikuwa umechomoka. Nikaurudishia. Nikaingia ndani ya gari na kuliwasha. Likawaka. Nikaiendesha kidogo kabla ya kusimama na kuwakabidhi ufunguo wao.

Hawakuamini. Walinikodolea macho ya mshangao huku mwanamke akitangulia, “Wewe ni nani?” aliuliza. Kisha akajitambulisha haraka. “Sisi ni mume na mke. Mimi naitwa Mary Leakey. Mume wangu ni Dkt. Louis Leakey. Tunatoka Uingereza. Lakini muda wetu mwingi tunautumia kufanya utafiti wa mambo ya kale. Hapa tunatafuta chochote ambacho tunaweza kupata juu ya masuala hayo.”

“Kwa kweli tunajihusisha na mambo ya kale zaidi ya haya,” mume wake aliingilia kati. “Tunatafuta ushahidi juu ya binadamu, kwamba aliishi Afrika Mashariki miaka milioni nyingi iliyopita. Hapa tumekuwa kama kupitia tu. Tunafanya shughuli zetu zaidi huko Kondo la Irangi katika Bonde la Ufa.” Mumewe aliongeza.

“Wewe ni nani?” mkewe alirudia swali.

Walikuwa wakiongea Kiingereza kwa haraka sana. Lafudhi yao ikiteleza kiasi kwamba niliwaelewa kwa taabu. Nikajitahidi kuwajibu kwa Kiingereza changu cha kujikongoja. Nikawatajia jina langu na kazi yangu ya ukarani katika mashamba ya mkonge.

Mke alimtazama mume kama anayesubiri atamke neno fulani. Mume alimwelewa. Akanigeukia na kuniuliza, “Kwa nini usifanye kazi na sisi? Mikono yako ina miujiza kwenye mashine za gari. Bila shaka unajua kuendesha pia. Na unazungumza Kiingereza kwa ufasaha. Utatusaidia katika ukalimani pia.”

Mke akaongeza, “Hatuna pesa nyingi. Tunaishi kwa michango ya watu wengine pamoja na kujitolea. Lakini tuna hakika utakachokipata kitakuwa bora kuliko hicho unacholipwa huko kwa Wagiriki.”

Huku nikitabasamu, niliwashukuru kwa kunifikiria. Hata hivyo, niliwaambia, “Nimeamua kujaribu bahati yangu katika biashara.”

“Biashara gani?” Mmoja wao aliniuliza.

“Ya chumvi” nilimjibu.

“Ina faida kweli?” mwingine aliuliza.

“Nadhani. Watu wengi wanaifanya...”

“Hakuna kosa kubwa katika biashara kama kudhani,” Leakey mwanamume alinikatiza. “Biashara ni mahesabu.

Fanya hesabu zako kwa makini, toa gharama zote, jumuisha muda wako na uione faida kabla hujatumia fedha zako. Kinyume na hivyo ni hatari sana,” aliongeza.

Mkewe akadakia, “Nadhani unahitaji kulifikiria pendekezo hili. Tuko hapa siku mbili zaidi. Tutakuonyesha mahala tulipofikia. Kama utabadili mawazo tutakupokea kwa furaha.”

Tulirejea wote mjini. Kwa namna niliyoichukulia kama majaribio zaidi, akina Leakey walinitaka niendeshe mimi. “Lakini sina leseni,” nilijitetea, utetezi ambao hawakuafikiana nao. Nikawafikisha nyumbani kwa afisa mmoja wa Kiingereza, ambaye alitajwa kuwa mtaalamu wa masuala ya samaki wa baharini na uvuvi, nikawaacha. Nikatembea taratibu hadi kwa wenyeji wangu.

* * *

Kuna ule wimbo au shairi maarufu kwa wakazi wa Pwani, ambalo lilipendwa sana hapo Bagamoyo. Kama nakumbuka vizuri beti za shairi hilo zinasema;

*Mgeni siku ya kwanza,
mpe mchele la panza,
Mtilie kifuuni,
Mkaribishe mgeni.*

*mgeni siku ya pili,
Mpe maziwa na samaki,
mali ikizidia,
mzidishie mgeni.*

*Mgeni siku ya tatu,
Nyumbani hamna kitu,
Mna vibaba vitatu
pika ule na mgeni.*

*Mgeni siku ye nne,
mpe jembe akalime
akirudi muagane
ende zake mgeni!*

*Mgeni siku ya tano,
Mwembamba kma sindano
Nyumbani haiishi mnong'oni
atetwa yeye mgeni.*

*Mgeni siku ya sita,
mkila mnajificha,
muingie vipembeni,
afichwa yeye mgeni.*

*Mgeni siku ya saba
si mgeni; ana baa!
Hata moto mapaani
Atia yeye mgeni !*

*Mgeni siku ya nane
Njoo ndani tuagane!
akitoka nje;
kwa heri, nenda mgeni.*

*Mgeni siku ya kenda,
Enenda bwana, enenda!
Usirudi nyuma,
Usirudi mgeni!*

*Mgeni siku ya kumi,
Kwa mateke na magumi,
hapana afukuzwaye,
Afukuzwa yeye mgeni.*

Nilipata hisia kuwa wenyeji wangu, nyumbani kwa Alhaji Suleiman walikuwa wakiniimbia wimbo au shairi hilo nyuma ya kisogo. Hisia hizo ziliniingia akilini kuanzia Jumapili ya jana tu, mara baada ya kurudi toka kanisani na matembezini ambako nilikutana na akina Leakey.

Nilirejea nyumbani hapo kama saa tisa hivi. Ramadhani hakuwepo, Sheikh alikuwa chini ya mwarobaini, kando ya nyumba yake akisoma msahafu. Akina mama na watoto walikuwa katika pilikapilika zao kama kawaida. Hakuna mtu yeyote aliyeonekana kunichangamkia kama awali. Zaidi, hakuna yeyote aliyezungumza chochote juu ya chakula. Mie njaa ilikuwa ikiniuma, chango likinguruma tumboni kudai chochote. Nikatupa jicho la upelelezi jikoni. Jiko nalo lilikuwa limenuna. Halina dalili ya moto wala moshi. Nikadhani pengine nyumbani hapo hamkuwa na chakula siku hiyo. Hivyo, nikatoka

taratibu hadi sokoni ambako nilinunua changu wakubwa wanne, kilo kumi za mchele, nyanya, vitunguu na mchicha. Nikajitwisha mfuko wangu na kuupeleka nyumbani, ambako niliutua jikoni bila kupokelewa na mtu yeyote. Nikatoka tena na kutembeatembea ili nikirudi chakula kiwe tayari.

Nilirejea mida ya saa kumi na mbili. Jiko lilikuwa bado limenuna.

Nikalala na njaa yangu. Ramadhani alichelewa sana kurudi, akakuta tayari nimelala. Kesho yake nilipoamka kwenda maliwatoni nilishangaa kuwaona wale samaki wazuri niliowanunua wakiwa wametupwa katika pipa la taka. Sikuelewa. Mtoto mmoja wa kike wa Alhaji alikuwa akifagia uwanja. Nikamsogelea na kumuuliza kisa cha samaki wale kutupwa.

“Mama alisema walishachina, wasingefaa kuliwa.”

Sikuamini maneno yake. Ndiyo, mimi ni mzaliwa wa bara lakini si mshamba wa samaki wala mgeni wa mambo ya pwani. Maisha yangu katika ziwa Nyanza na katika Bahari ya Hindi pale Pangani yalikwishanitoa kabisa katika ugeni wa mambo hayo. Sikuwa mtu wa kununua samaki aliyeharibika.

“Mbona hamkuniambia niwarudishe?” nilimhoji mtoto huyo.

“Sijui mwenyewe mama,” alinijibu.

Ni hapo wimbo ule wa watu wa Mafia uliponirudia akilini.

‘Mgeni siku ya kwanza...’ nikaingia maliwatoni. Nilipotoka nilimwamsha Ramadhani na kumuuliza kulikoni. “Ukarimu wa wenyeji wetu umetoweka ghafla. Hata chakula nilichonunua kimetupwa. Waswahili mnamsemo kuwa *‘Akufukuzwaye hakuambii toka,’* nisingependa kuamini hivyo,

lakini kuna dalili, kulikoni?”

Ramadhani alisita kwa muda, kisha akanitaka nimsubiri naye aoge ili twende tukazungumze faragha. Tulikwenda hadi kwenye kijimgahawa ambako kwa njaa niliyokuwa nayo nilikunywa vikombe vitatu vya chai na chapati sita. Ramadhan alikunywa kikombe kimoja kwa chapati mbili.

“Ni kosa lako mwenyewe.” Baadaye alisema.

“Kosa langu! Kosa gani?”

“Kwa nini ulikwenda kule?”

“Kwenda wapi?”

“Kanisani.”

Nikashangaa. “Kwani kuna ubaya gani kwenda kanisani?” Nikamuuliza. Ramadhan aliiminya midomo yake kama ilivyo kawaida yake kabla hajatoa hotuba yake fupi, “Kwako wewe hakuna ubaya wowote. Lakini si kwa Alhaji Suleiman. Yeye dini haiko rohoni mwake pekee. Iko akilini na katika damu yake. Ukizingatia kuwa ameutumia muda wake mwingi kukutafutia maalim ambaye anagekusaidia, akijua fika kuwa wewe ni mwislam safi, taarifa za kuonekana kwako kanisani zilimsononesha sana. Kwa bahati mbaya hata mimi sikujua hilo. Nafikiri hata baba hakujua wala kupata kufikiria kuwa wewe si mwislam!”

Nikazidi kushangaa. Kwa nini mtu amezwe na dini kiasi hicho? Sisi wote ni viumbe wa Mungu. Suala la imani ni la mtu binafsi. Wengi wetu tumerithi dini toka kwa wazazi wetu ambao nao walirithi kwa wazazi wao. Suala la kuwa dini fulani ndiyo hasa inayokubalika na Mwenyezi Mungu ni midahalo ileile ambayo haijapata na haitokaa ipate ufumbuzi. Nilitamani kumwambia hayo Ramadhan, lakini nilisita. Yasingenisaidia mimi wala kumsaidia yeye kwa lolote lile.

“Kwa hiyo, sina budi kuondoka,” nilimwambia.

Alitafakari kidogo kabla ya kuuliza, “Lini?”

“Leo.” Nilimjibu. “Haifai kuishi chini ya paa la mtu ambaye unamkera na kumkinaisha.”

“Leo hakuna jahazi la kurudi Pangani. Kesho lipo,” alinidokeza.

Nilimshangaza pale nilipomwambia kuwa sina mpango wa kurudi Pangani haraka. Nikamweleza nia yangu ya kumshirikisha katika biashara ya chumvi kati ya Bagamoyo na Zanzibar. “Tutapata hela za kutosha. Tutarudi pangani tukiwa matajiri.”

Ramadhan aliyatafari maneno yangu kwa makini. Nilihisi akishawishika. Lakini kitu fulani kilimfanya asite. Nilishuku kuwa kitu hicho kilitokana na mkasa wa dini ambao uliibuka kati yetu na kujenga ukimya ambao haukuwepo. Baada ya ukimya mrefu aliniambia kuwa lazima arudi Pangani, asingefanya shughuli yoyote bila idhini ya baba yake.

Kwa hiyo inabidi tuagane,” nilisema nikitia mkono wangu mfukoni na kutoa fedha ambazo nilizichambua na kumkabidhi sehemu ya fedha hizo.

“Za nini?” Aliuliza kabla hajazipokea.

“Zitakulinda njiani. Lolote laweza kutokea.”

Akazipokea. Macho yake yalionyesha masikitiko makubwa. Mie pi nilinyong’onyea kumpoteza ndugu na rafiki ambaye nilikuwa na ndoto za kufanya naye mambo mengi.

Tuliporejea kwa Alhaji tulikuta tayari ametoka. Nikamshukuru mkewe na wanawe na kuwataka radhi kwa lolote nililowakosea. Niliwaona wakiyakwepa macho yangu. Nikaingia ndani na kuchukua kilicho changu, kisha huyoo, nikatokomea katika mji wa Bagamoyo. Sikutaka kuisubiri siku

ya kumi kama yule mgeni wa kale. Ya tatu tu ilitosha.

Wakati nikitafuta nyumba ya wageni nilifikiri harakaharaka. Wazo la biashara ya chumvi lilianza kunitoka. Niliona wazi kuwa nisingeweza kuifanya peke yangu; kubeba, kupakia na kupakua magunia ya chumvi nzito. Pia, sikuwa na mwenyeji ambaye kwake pangukuwa kituo changu cha biashara. Chumvi si biashara ya kuweka katika vyumba vidogo vya wageni. Hivyo, nikafikia uamuzi wa kuacha. Wazo la kurudi Pangani kuendelea na kazi ya unyampala katika mashamba ya mlonge niliachana nalo. Licha ya mshahara duni kazi yenyewe haikuwa ya kimaendeleo. Sikuwa na jipya la kujifunza wala matarajio yoyote kukua kitaaluma. Ni hapo nilipowakumbuka wale Wazungu na kuamua kuipokea kazi yao ya ajabuajabu.

Jioni hiyo niliwafuta na kuwaarifu juu ya uamuzi wangu. Walifurahi sana.

* * *

Tulianza safari kesho yake. Haikuwa safari ya Kondoa moja kwa moja. Leakey aliamua tupite Dar es Salaam ambako alitaka gari lipate matengenezo makubwa. Pia alikuwa na nyaraka fulani ambazo alihitaji kuziwasilisha.

Safari ya Dar es Salaam ilinisisimua sana. Nilikuwa nimesikia mengi juu ya mji huo. Mji mkuu wa nchi ambao ulikuwa na bandari maarufu katika mwambao huu wa bahari. Chimbachimba zangu katika vitabu vya historia zinaniambia kuwa Dar es Salaam ni mji wa kale pia ingawa ni sawa na Kilwa au Bagamoyo. Kwamba, mji huo asili yake ni kijiji kidogo cha wavuvi kilichoitwa Mzizima, ambacho haikujulikana kilianza vipi au lini. Kumbukumbu za maandishi juu ya Dar

es Salaam zinaanzia mwaka wa 1865 pale Sultan Sayyid Majid wa Zanzibar alipoitembelea Mzizima. Alivutiwa sana na shughuli za uvuzi na biashara zilizokuwa zikifanyika hapo kwa amani na utulivu. Akaamua kuhamishia himaya yake hapo na kupaita Bandur ul Salam. Jina hilo lilibadilika taratibu na kuwa Dar es Salaam kwa maana ileile ya bandari salama.

Kama ilivyokuwa kawaida ya Waarabu wengi enzi hizo, Sultan aliifanya Dar es Salaam kituo kikubwa cha kupokelea biashara haramu ya watumwa, mizigo na pembe za ndovu. Bidhaa hiyo zilisafirishwa hadi Zanzibar na baadaye nchi za mbali. Sultan huyo alifariki mwaka 1870.

Mrithi wake alikuwa na mapenzi na Bagamoyo zaidi ya Zanzibar. Mashua nyingi za biashara zikahamishiwa huko. Umaarufu wa Dar es Salaam ulipungua zaidi baada ya mwaka 1873 pale jitihada zilizosimamiwa na Waingereza za kuteketeza biashara ya utumwa zilipozaa matunda. Lakini uhai huu ulirejea tena 1887 pale Wajerumani walipoipokonya Tanganyika na kuanzisha ujenzi wa bandari ya Dar es Salaam kwa kasi. Na mwaka 1912 pale ujenzi wa reli ya kati ulipoanza kwa kishindo Dar es Salaam ilizidi kushamiri. Dar es Salaam ilitamalaki zaidi baada ya vita kuu ya pili, pale Mwingereza alipomshinda Mjerumani na kuifanya Dar es Salaam makao makuu ya serikali yake.

Safari ya Dar es Salaam, toka Bagamoyo ni fupi sana. Ni umbali wa kilometa zipatazo sabini na tano hivi kwa ajili ya uduni wa barabara, ikiwa na mashimo mengi, sehemu nyingine mchanga na hata makorongo ilituchukua masaa manne kuwasili katika mji huu. Tulipita vijiji mbalimbali vyenye watu na nyumba chache; Kaega, Bunju, kunduchi na vinginevyo. Njiani mito ya msimu kama Mpiji, Tegeta na

Kunduchi ambayo yote, nyakati za masika huendeleza tabia ya asili kumimina maji yake yote, hadi tone la mwisho, katika bahari, ambayo kamwe haitosheki.

Leakey na mkewe ni watu ambao hawakujua kitu kinachoitwa uchovu. Mara baada ya kufika kwa mwenyeji wao, kula na kuoga waliamua kuingia mjini kuendelea na shughuli zao. Mie waliniruhusu kupumzika. Lakini mie pia sikuwa mtu wa kupumzika. Nilifuatana nao. Leakey aliendesha gari kwa uangalifu zaidi, kwani tofauti na Bagamoyo hapa hazikupita dakika tano kabla ya kupishana na gari jingine. Kwa maelekezo ya mwenyeji wake alilipeleka gari lake Kariakoo, kwa fundi wa Kigoa, ambaye aliaminika zaidi.

Kariakoo, enzi hizo ikiwa kama kijiji ndani ya mji, ilikuwa na sifa zote za mji. Eneo maarufu zaidi lilitemwa kando kidogo ya soko kuu zamani pakiitwa ‘pombe shop’ ambapo mamia ya watu walijumuika kila jioni kunywa pombe ya mnazi, kahawa kucheza bao na pilikapilika nyingine tele. Bendi mbalimbali za muziki pia zilitumbuiza siku za sikukuu na mwisho wa wiki.

Eneo jingine lililotamba likiwa lile la kilabu cha wazee walioshiriki vita kuu. Jengo lao likiwa kandoni mwa barabara iendayo Morogoro, likiwa na ukubwa wa ukumbi wa muziki, eneo la kuuzia ‘mnazi’ na vinywaji vingine lilikuwa fahari kubwa ya wakazi wa Dar es Salaam. Hadithi za matukio ya vita zikisimuliwa, waliopotea vitani wakikutana na kubadilishana mikasa, waliopoteza maisha walikumbukwa, umaarufu wa eneo hilo ulikuwa mkubwa.

Fundi huyo na wasaidizi wake walilivamia gari kama nzige. Huyu alishika spana hii na kufungua pale, huyu alifunua kile, huyu alilala chini ya gari dakika kumi baadaye injini nzima ilikuwa imefumuliwa. Fundi mkuu alikagua

kifaa baada ya kifaa na kutuagiza kurudi baadaye ili awe ameandaa orodha ya vifaa vitakavyohitajika kununuliwa na vipi vitafanyiwa matengenezo. Nilitumia fursa hiyo kuagana na akina Leakey kwa maelezo ya kukutana nao hapo kwa fundi baadaye.

“Angalia usipotee. Hapa siyo Bagamoyo.” mkewe alitania.

Nikacheka kabla ya kumjibu, “Kama kupotea ningepotea zamani. Nimekuwa mtu wa kiguu na njia toka utotoni.”

Mara tu walipoondoka niliuliza lilipo soko la Kariakoo. “Shuka hapa, mtaa ule ingia kushoto, utalionna,” mmoja kati ya mafundi wasaidizi wa Goa alinielegeza. Nikayafuata maelekezo yake.

Soko lilikuwa pale, likinisubiri. Pilikapilika tele za biashara za nafaka, dagaa, samaki, nazi, matunda na kila unachoweza kufikiria zilikuwa zikiendelea kama kawaida. Kwa mara nyingine nikawa shahidi wa historia ya yote niliyopata kusikia juu ya soko hili.

Toka hapo niliomba kuelekezwa iliko shule ya Msimbazi. Haikuwa mbali kutoka hapo. Nilienda na kujionea mwenyewe majengo ambayo yalimhifadhi Shaaban Robert kwa miaka minne na kumpa ule ujasiri wa aina yake. Yalikuwa pale. Na wanafunzi wengine walikuwa pale, pia waliandaliwa au kujiandaa kuyakabili maisha yao ya baadaye.

Kelele za wanafunzi waliokuwa nje ya madarasa, usafi wa sare zao na utulivu wa wale waliokuwa madarasani, vitabu vilifanya, kwa mara nyingine tena niyakumbuke maisha ya shule na kuyatamani. Nikayakumbuka hata madaftari niliyoyaacha Pangani, ambayo sikupata kutengana nayo kwa miaka nenda rudi iliyopita. Ndoto za kurudi shuleni zikanirudia

huku nikijinong'oneza. *Umeshakuwa mtu mzima Mtukwao. Huoni 'shikamoo' zinavyokuandama?*

Haikua uongo. Kama ilivyokuwa Pangani, Bagamoyo na sasa Dar es Salaam nilipokea heshima. Nami nikajifunza kuitoa kwa kila aliyeonekana kunizidi umri. Kwa wale ambao hirimu yetu ilionekana moja tulipeana 'Assalaumaleikum' au 'Saballakheri' kabla ya maongezi zaidi. Tabia hiyo nilijifunza hasa kule Pangani baada ya tukio moja lililonitia aibu. Kuna jambo nilitaka kuuliza; ama njia ama kumuulizia mtu. Mzee mmoja mwenye upara na ndevu nyingi nyeupe aliketi juu ya kiti mbele ya nyumba yake. Nilimsogelea na kumuuliza hicho nilichotaka kumuuliza. Alinikodolea macho kama mtu ambaye hanisikii. Nilirudia swali langu mara tatu bila mafanikio. Nikamwacha na kwenda nyumba ya jirani. Baada ya kuwauliza hicho nilichotaka kuuliza niliwahoji iwapo yule jirani ni bubu.

"Hapana kwa nini?" Walihoji kwa mshangao.

"Maana namsemesha hajibu," niliwaeleza.

Wakacheka, kisha mmoja wao akaniuliza kama nilimwamkia kabla mzee Yule.

"Hapana." Nilikiri.

"Unaona?" Alisema akicheka. "Mzee yule kama hujamwamkia hata umwulize mara ngapi hakujibu."

Niliporejea gereji akina Leakey walikuwa hawajafika. Niliketi na mafundi ambao tayari walimaliza kazi yao wakimsubiri. Walikuwa katika ubishi, juu ya mechi ya mpira ambayo ingechezwa mwishoni mwa wiki ijayo. Ilielekea kuwa kati ya mafundi hao walikuwemo washabiki wa klabu moja waliyoitaja kama Yanga na ya pili waliyoiita Sunderland. Yanga ilitajwa kama timu kongwe zaidi ya Sunderland. Sikuwa mjuzi wa masuala ya mpira wa miguu, hivyo sikufatilia sana mdahalo huo.

Akina Leakey waliporudi walionyeshwa vifaa vilivyohitaji kununuliwa. Wakatoa pesa, tukaondoka kwa ahadi ya kulichukua gari hilo kesho yake jioni. Hali hiyo iliyonipa nafasi nyingine nzuri ya kuendelea kuvinjari Dar es Salaam ya enzi hizo. Niliwaomba akina Leakey na wakaniruhusu kulala mjini, katika nyumba ndogo ya maeneo hayohayo ya Kariakoo, badala ya kufuatana nao Oysterbay.

Jioni hiyohiyo nilianza kufaidi Pwani ya Dar es Salaam. Nilikuwa nikipita katika moja ya mitaa ya kitongoji hicho. Macho yangu yakavutwa na kundi kubwa la watu, wengi wao wakiwa wanawake na watoto ambao walikuwa wakitembea huku wakicheza na kuimba. Mchezo wao ulikuwa wa kulisimua sana. Wakiongozwa na mdundo wa ngoma, ambazo wapigaji wawili walizipiga kifundi wachezaji walikuwa wakichezeshwa viungo vyao, miguu ikipiga hapa na pale huku wakirusha viuno ambavyo vilifungiwa kanga iliyokunjwa. Nyimbo zao pia zilikuwa za kulisimua, sehemu mchanganyiko wa beti za ngonjera, mashairi na sehemu zilizojaa mafumbo na ucheshi. Wimbo mmoja ulisema;

Nimeinama, nimeinuka,

Nimeokota kidude.

Wachezaji walicheza huku wakionyesha ishara za kuinama na kuinuka. Kila ngoma ilipokolea msafara ulisimama kwa dakika mbili tatu na kuwaburudisha watazamaji kabla ya kuendelea tena. Hali iliyopelekea watu wengi zaidi kutoka majumbani mwao, kuja kushangilia, huku wengi wao wakijiunga na msafara huo wa kushiriki katika kucheza na safari ambayo ni wachache waliojua ambako ingeishia.

“Mdundiko huo kijana,” mzee mmoja aliniambia. Yeye alikuwa hatazami ngoma. Alikuwa akinitazama mimi, bila

shaka akiwa amevutwa na mshangao aliouona katika macho yangu. “Mdundiko mwanangu,” aliongeza. “Ngoja ya Kizaramo, ingawa Wandengereko, Wakware na makabila yote ya Pwani yanaicheza.”

“Inaashiria nini?” nilimuuliza.

“Mambo mengi. Inawezekana mwali anatolewa nje mahala fulani au msichana anachezwa unyago,” aliongeza.

“Mbona kila mtu anacheza?”

Alicheka, “Mdundiko haina uchoyo. Ni ngoma pekee duniani ambayo haina mwenyewe. Kila mtu ana uhuru wa kuiburudisha roho yake kwa kujimwaga uwanjani na kuonyesha uwezo wake. Ngoma hiyo inaweza kwenda hadi Ilala na hata Temeke bado ikawa na umati mkubwa hivyo hivyo. Ikiisha utasikia taarifa za watoto na hata watu wazima kupotea, kwani wengi huifuata bila kuangalia wanakotoka au wanakokwenda,” aliongeza.

Wakati huo ngoma ilikwishatuacha na kuendelea na hamsini zao. Nami nikashika hamsini zangu kwa kuendelea kukata mitaa. Nilitembea taratibu na kuiacha Kariakoo, kwa kuifuata barabara ya Morogoro hadi nilipofika bandarini.

Bandari ya Dar es Salaam kweli ni ‘Bandari Salama.’ Jiografia yake inathibitisha hivyo. Bahari kuu ikiwa nje ya bahari hiyo, upo mdomo wa bahari ambao unawezesha meli kuingia na kutoka bandarini humo kama mtu anavyoingia ndani ya nyumba yake baada ya misukosuko mingi ya baharini kama dhoruba za upepo mkali pengine pamoja na viumbe kama papa ambao hawawezi kuvumilia maisha katika eneo finyu kama hilo.

Nilitembea kuifata pwani hiyo hadi mbele ya mdomo wa bahari hiyo, ambayo ulitenganisha mji na sehemu

niliyodokezwa kuwa inaitwa Kigamboni kwa eneo la takriban meta mia mbili. Eneo ambalo lilikaliwa na wavuvi wengi. Nikiwa nimesimama hapo, nilipoambiwa kuwa panaitwa Magogoni, niliweza kuona mitumbwi ya wavuvi ama ikijishughulisha na uvuvi au kuvusha watu toka upande mmoja hadi mwingine.

Niliamua kupoza kiu yangu kwa kunywa maji ya dafu baada ya kumwona muuzaji akipita karibu yangu na tenga la madafu juu ya baiskeli yake.

“Unataka gumu au laini?” Aliniuliza.

“Kwani kuna tofauti gani?”

“Gumu ni lenye nyama na maji matamu zaidi. Laini halina nyama, maji yake kidogo yana chumvi.”

Niliomba laini. Nikanywa maji na kufaidi ujiuji wake badala ya gumu ambalo nyama zake mara nyingine hufanana na nazi.

Wakati nikirejea, juu kidogo ya Pwani hiyo ya Magogoni nilionyesha jengo ambalo nilidokezwa kuwa ni makazi na ofisi ya Gavana. Sikuweza kuvumilia, nikachungulia. Macho yangu yalivutwa na bustani kubwa ya miti mbalimbali iliyootesha, mingi ikiwa ya asili. Niliweza kuiona miti kadhaa, ambayo babu alipata kunitajia majina yake wakati tukisafiri kwa miguu miaka ile iliyopita.

Kitu kingine kilichonivutia katika Ikulu hiyo ni ndege. Ilionekana kama shamba la wanyama kutokana na ndege aina mbalimbali waliokuwa wakiruka, kuimba na kucheza toka mti huu hadi ule, tawi hili hadi lile. Ndege walionivutia zaidi ni tausi. Walikuwa wengi, waliimba na kutembea kwa maringo kana kwamba wao ndio walikuwa wafalme na malkia wa bustani hiyo. Tausi mmoja, mwenye mkia mrefu na rangi ya kuvutia, alinizawadia kwa kunifunulia mkia wake na kuufanya

ugeuke kuwa mfano wa mzuri wenye mchanganyiko wa rangi ya dhababu, almasi na lulu.

Ningeendelea kuduwa hapo kama askari mmoja asingetokea na kunifukuza. Nikaondoka na kuifuata barabara inayotokea hapo Ikulu, ambayo nayo ni burudani tosha kwa miti asilia tele, iliyootehwa kila upande na kuipa barabara kivuli na hewa murua tofauti kabisa na maeneo mengine ya mjini ambayo hayakutofautiana sana na jangwa.

Sikuwa na haraka. Nilitembea taratibu nikitazama hapa na pale. Nilipita katika bustani ya Mnazi mmoja, yenye maua na miti ya vivuli. Nikaiacha na kufika maeneo ambayo hayakuwa na watu hadi nilipofikia hoteli yangu. Ilikaribia saa mbili za usiku.

Wakati tayari nimeoga na kupiga mswaki nikijiandaa kulala mtaa wa pili zilisikika kelele za muziki. Sikuwa mpenzi sana wa muziki. Lakini ile midundo na tungo zao mara nyingi zilinisisimua. Hivyo, sikuhitaji kuambiwa kuwa muziki huo ulikuwa wa mwanamuziki mahiri, Hamisi Machapti aliyekuwa akiongoza *Dar es Salaam jazz*, bendi kongwe iliyozaliwa mwaka 1933.

Nilimsikiliza kwa muda kabla ya usingizi kunichukua.

SURA YA KUMI NA TATU

Ya akina Kingalu wa Morogoro

“Petro!”

Nilishtuka kidogo lakini sikugeuka. Nani ananifahamu mimi katika mji huu wa Dar es Salaam? Zaidi, nani ananifahamu kwa jina hilo la Petro ambalo sina tabia ya kulitumia mara kwa mara? Nikaendelea na hatua zangu, moja baada ya nyingine; nikiwafuata kina Leakey ambao walikuwa wamesimama nje ya gari lao, tayari kwa safari yetu ndefu.

“Petro!” Sasa mwitaji alikuwa nyuma yangu. Pumzi yake, wakati akiniita, ikikifikia kichogo changu. Nikahisi mkono wake ukinigusa bega. Kwa sauti ya kujiamini zaidi nilimsikia akisema, “Wewe ni Petro Kionambali. Sidhani kama nitakuwa nimekosea.”

Nikageuka kumtazama. Aliyesimama pale alikuwa mtu ambaye kamwe nisingeweza kumsahau, mtu ambaye alisababisha safari yangu ya kielimu ivunjike mwanzo tu wa safari. Mtu huyo ndiye chanzo cha mikasa na masaibu yote yanayonipata. Nikamkodolea macho ya mshangao.

“Usiniambie kuwa hunikumbuki?” alisema akitabasamu. “Wewe si yule Petro wa hirizi”

“Ndiye” nikamjibu “Na wewe nakukumbuka vizuri sana.

Unaitwa Byabato. Tulikuwa wote kule Kagera.”

“Naam halafu ukapoteza hirizi yako,” akakumbushia.

“Naam, na wewe ukaiokota.”

“Kabisa. Nikaipeleka kwa faza Backhove akaamua kuichoma moto hadharani...”

“Mie nikaikwapua na kukimbia nayo.”

Tulipofika hapo Byabato akaangua kicheko kisha akasema huku akiendelea kucheka, “Ikakuponyoka tena. Nikaiokota tena. Nikamrudishia faza. Akiwa amekasirika sana faza aliichukua na kuitumbukiza ndani ya moto kwa mkono wake mwenyewe.”

Taarifa yake ya mwisho ilikuwa habari mpya kwangu. Kumbe hirizi yangu ilipatikana na ikatiwa moto? Nikamtazama kwa macho yenye maswali mengi ambayo aliyasoma na kuyajibu baadhi.

“Hirizi haikuungua,” alisema.

“Haikuungua? Ilikuwaje?”

“Ilikataa kuungua!”

“Ilikataa kuungua! Kwa vipi?” nilizidi kushangaa.

“Ilikataa tu. Ilikuwa hirizi ya ajabu sana na imeacha historia kubwa. Kila ilipotupwa katika moto ilidunda na kuchupa kama chura hadi nje ya moto huo. Tukio hilo lilirudiwa zaidi ya mara tano, lakini hirizi haikukubali kuungua. Kila mtu alishangaa. Padri akaamua ikatupwe ziwani, mbali kabisa ya nchi kavu. Nadhani walifanya hivyo, ingawa baadhi ya wanafunzi wanadai padri alihiifadhi ili ipelekwe kwao ikafanyiwe uchunguzi wa kina.

Hirizi yangu ilikuwa na maajabu hayo! Niliwaza kwa mshangao. Nikamkazia macho Byabato kuona kama alikuwa akisema ukweli au uongo. Siku zote shuleni pale alijulikana

kama mwanafunzi mzushi, mchangamshi na mwongo lakini kwa hili alionekana kuwa alikuwa akisema ukweli.

Nikamtazama kwa makini. Zaidi ya kuwa mnene zaidi na mweusi zaidi hakuwa amebadilika sana. Alikuwa amevaa nguo za kuvutia. Viatu vyeusi, suruali nyeusi na shati jeupe ambalo liling'ara zaidi kutokana na tai nyekundu iliyokuwa ikining'nia shingoni mwake. Sauti yake pia ilikuwa ya kujiamini zaidi.

Yeye pia alikuwa akinitazama kwa makini. Alivutiwa na suruali yangu ya kijivu, shati la buluu na jaketi la kahawia nililovaa. Miguuni nilikuwa na viatu vya bei ya kuridhisha. Nilimwona akiwa na dalili zote za kuridhishwa na hali yangu ya kiuchumi.

“Haya, ulipata wapi?” alihoji ghafla.

“Nini?”

“Hirizi ile. Unajua haikuwa hirizi ya kawaida uliipataje ile?”

“Achana na mambo yale.” Nilimwambia. “Yamepitwa na wakati.”

Akacheke kabla hajaongeza swali jingine. “Halafu kwa nini ulikimbia?”

“Ilikuwa utoto tu.” Nilijibu na mimi na kumtupia swali harakaharaka. “Na wewe kwa nini ulipoikota uliipeleka kwa padri badala ya kunirudishia mwenyewe?”

“Ilikuwa ni utoto vilevile.”

Jibu lake lilinifariji kiasi. Nikamchukulia kuwa amekuwa kiakili na kitabia hivyo, nikataka kujua mengi zaidi juu yake. Nikamuuliza anafanya nini hapo Dar es salaam.

“Naishi huku. Huu mwaka wa tatu sasa. Niko shule ya Minaki. Naendelea na kidato cha tano.” Alisema kwa sauti ya

majivuno kidogo. “Na wewe?”

Nilifikiri kidogo kabla ya kumpa hadithi yenye uongo kidogo iliyochanganyika na ukweli mwingi. “Mie nilipowaachia ile shule yenu nilienda Uganda. Kule nilimaliza kidato cha nne na sasa nipo mwaka wa pili wa Chuo Cha Makerere. Nipo hapa na maprofesa wangu. Wale pale wananisubiri. Tuko katika utafiti wa mambo ya kale. Hivi unanvyoniona tumetokea Bagamoyo kwenye magofu ya Kaole na tunaelekea bonde la ufa kwa ajili ya utafiti wa mtu wa kale.”

Kama kuna mtu aliyepigwa na butwaa siku hiyo hakuwa mwingine zaidi ya Byabato. Alipogeuka na kuwaona wazungu wale wakiwa wamesimama nje ya gari lao katika hali ya kunisubiri pengine pamoja na ubora wa mavazi yangu aliamini mara moja. “Unajua tulidhani umeliwa na fisi kule porini ulipokimbilia?” Baada ya muda alisema.

“Fisi au mamba wa ziwa Nyasa?” Nilihoji nikicheka. “Hapana. Niko hai. Tuko pamoja katika kuitafuta elimu ili tuweze kuitumia vyema kuitumikia nchi yetu mara mkoloni atakapoondoka.” Nilisema kwa kujiamini huku nikimtaka radhi ili niwawahi ‘Maprofesa’ wangu.

Nilimwacha kasimama palepale. Macho kayakodoa kwenye gari hadi ilipowashwa na kuondoka kwa mwendo wa kasi.

* * *

Gari lilikuwa limepona. Mlio wa mashine ulidhihirisha hivyo, ukiulinganisha na ule wa awali, kabla ya matengezeto ambao haukutofautiana na ule wa ng’ombe mgonjwa anayevutwa kupelekwa malishoni kwa nguvu. Tuliteleza tukaiacha Kariakoo, Ubungo na hatimaye kibaha. Toka

hapo tulifika Chalinze ambako tulisimama kidogo, akina Leakey wakibisha iwapo tuelekee kaskazini kwa kuifuata njia inayoelekea kaskazini ambayo ingetupeleka hadi Kilimanjaro na Arusha kabla ya kwenda Kondoa Irangi au ile ya moja kwa moja ambayo ingetufikisha Morogoro, Dodoma na hatimaye Kondoa. Waliafikiana tuifuata ya Morogoro.

Ilikuwa safari yangu nyingine ya kuvutia. Mazingira yaliyoizunguka barabara yalikuwa na rasilimali tele za kuisisimua. Uwanda mpana wa mto Ruvu. Ambao ulitosha kuwa malisho murua ya ng'ombe ulikuwa pale, umetulia tuli kama bustani ya aina yake, iliyokuwa ikisubiri kutumiwa. Bustani ambayo kwa wakati huo ndege kama yangeyange na korongo walikuwa tele mbele ya macho yetu wakiifaidi.

Milimaya Uluguru, ambayo ilitulaki ilikuwa imeusimamia mji kama inayoulinda, ilikuwa burudani nyingine ya kuvutia. Ukiwa unameremeta kwa rangi ya kijani, iliyotokana na msitu mkubwa uliousingira, mlima huo uliashiria kila dalili ya kuwa chanzo cha mvua kubwa, mbolea na utajiri wa kila aina ya mti, wanyama, ndege na wadudu waliojihifadhi humo. Nilikumbuka kusoma mahala fulani kuwa msitu huo, ambao unaangukia upande wa pili wa mji, unakisiwa kuwepo kwa zaidi ya miaka milioni ishirini na tano. Waluguru wengi hadi leo wanadaiwa kuendesha matambiko yao kimila ndani ya msitu huo.

Licha ya msitu, Morogoro ilijaliwa mito na mabwawa mengi kama mto Wami, bwawa la Mindu, Kidatu na Kihansi ambayo si kwamba huwapatia wavuvi mahitaji yao tu, bali pia pamoja na nguvu za umeme ambazo sehemu kubwa ya nchi inazitegemea.

Mama Leakey hakuweza kujizuia. Mara kwa mara alishuka kwenye gari na kupiga picha za maeneo na matukio

mbalimbali, huku uso wake ukiwa na furaha tele.

Tulisimama kidogo hapo Morogoro ili tupate mlo wa mchana. Tulisimama mbele ya hoteli moja ndogo, katika eneo la Kinole. Kwa mshangao wetu tulikuta hoteli hiyo imefurika, kitu kama sherehe za kikabila zikiendelea.

“Kuna nini hapa?” Leakey aliuliza.

“Nipe dakika tano nitakuwa na jibu,” niliwaambia wakiketi katika viti ambavyo meza yake ilikuwa tupu.

Mimi nilijichomeka katika kundi la watu waliokuwa wakiimba na kushangilia jambo. Katikati ya umati huo, waliketi watu watatu, mmoja kati yao ambaye alionekana kijana zaidi alionekana kama mgeni rasmi wa shughuli hizo.

“Kuna nini?” nilimuuliza jirani yangu mmoja ambaye alikuwa akichekelea kila tukio kwa macho, meno na hata mikono yake.

Mtu huyo alinitazama kwa macho ya mshangao uliochanganyika na dharau kiasi kabla hajaniuliza kwa sauti ya juu kuliko nilivyotegemea, “Hujui kuna nini hapa leo?”

“Sijui,” nikakiri.

“Una maana kuwa hata yule aliyeketi pale humjui?” aliniuliza akielekeza mkono wake kwa yule kijana.

“Simjui.” Nikakiri tena.

Alinitazama kwa namna ya kunisikitikia. Kisha akaamua kunielimisha, “Yule pale ni Kingalu.”

“Kingalu ndiye nani?”

Alinisikitikia zaidi, “Kingalu rafiki yangu, huko kwenu ni Chifu au Mtemi. Sisi Waluguru tumewaita Kingalu. Huyu hapa ni Kingalu mwana wa wa Banzi mpya. Amerithi wadhifa huo majuzi tu. Alipoamua kutembelea hoteli hii ambayo ni ya mwanafamilia, watu waliosikia habari, wameamua kuja

kumwona, kumpa heshima yake na kupokea baraka zake.”

Maongezi yaliyofuata baada ya hapo yalikuwa matamu zaidi.

Nilisimuliwa historia ya kabila la Waluguru. Kwamba baadhi ya watu wanaamini kuwa Mluguru alitokea kusini, katika mipaka ya Msumbiji na Ruvuma na kupita Mahenge, Kilosa hadi Kasanga na hatimaye Morogoro mjini ambako Kingalu Mkuu aliweka makao yake rasmi.

Kingalu Banzi, aliyekuwa akishangiliwa hotelini hapo, niliarifiwa, alikuwa mmoja kati ya akina Kingalu Banzi wengi ambao walipata kushika wadhifa huo kabla ya kuurithisha kwa wengine. Ikiwa na maana kuwa jina hilo ndio hasa la ukoo na kila mrithi aliwajibika kulitumia. Akiwa Chifu Mkuu, Kingalu alikuwa na machifu wengine wengi wa koo mbalimbali kama akina Chifu au Chifu Kingo. Wote walifanya kazi zao za kusimamia masuala ya koo, kuamua kesi, kusimamia matambiko na mara nyingine kutoa baadhi ya dawa za asili zenye miiko maalum.

Machifu hawa, kama Kingalu, hawafanyi kila kitu peke yao. Ama hukasimu madaraka kwa watu wengine, ama huwatumia wasaidizi wao maalumu, wanaoitwa ‘Wandewa’ kwa tafsiri ya Kiswahili ‘Waheshimiwa’ ambao kwa sasa tunaweza kuwalinganisha na baraza la mawaziri au madiwani.

Kwa mujibu wa mwalimu wangu huyo wa masuala ya Waluguru, Mluguru ni mali ya mama zaidi ya alivyo baba. Kwamba chanzo cha utamaduni huo kinaendana na historia ya kale ya kabila zima la Waluguru. “Kama nilivyosema tunaaminika tulitokea kusini. Mababu wanatuambia kuwa ujio wetu ulitokana na ugomvi wa ndugu wawili katika familia. Waligombana sana hadi mmoja wao akaamua kuondoka hapo

na kwenda eneo la mbali kuanzisha makazi yake mapya. Hakupenda kuondoka peke yake. Alimchukua dada yake na kuondoka naye. Kumbe dada yake huyo alikuwa mjamzito. Haikujulikana ujauzito huo ulikuwa ni wa nani, jambo lililopelekea mtoto huyo awe mali ya mama. Na kwakuwa mtoto huyo aliyezaliwa ndiye aliyekuja kuwa chanzo cha ukoo na hatimaye kabila la Waluguru utamaduni wa kuwaenzi wajomba zaidi umeendelea kushamiri.”

Mwenyeji wangu huyo, ambaye sasa tuliketi kwenye viti, mimi nikila wali na kuku wa kienyeji, yeye akinywa bia niliyomnunulia, aliendelea kujibu hata maswali yale ambayo sikupata kumwuliza, bila hiyana.

“Unajua sababu ya majina ya akina Mkude na akina Mbena kuwa mengi kwa Waluguru?” aliniuliza na kujibu mwenyewe. “Ni majina ya ukoo. Mimi hapa naitwa Mbena. Ukoo wa mama yangu ni Mwenda. Hivyo, nikipata mtoto wa kike ataitwa jina la ukoo Mwenda. Japo kama baba naweza kumpa jina jingine lakini jina litakalotambuliwa na ukoo mzima ni lile la Mwenda. Mwenda akizaa mtoto wa kiume atamwita Mkude. Majina hayo vilevile yana maana nyingi. Kwa mfano jina la Banzi lina maana ya kibanzi cha kuni. Jakka lina maana ya kibanzi kilekile cha kuni lakini kinachowaka. Chinga ni kibanzi kikubwa zaidi. Bonzo ni kibanzi kikubwa zaidi ya vyote.”

Nilipomaliza chakula changu nilikishushia kwa chupa ya fanta baridi, kisha nikamshukuru kwa ukarimu wake na kujiunga na akina Leakey ambao nao walikuwa tayari. Tukaendelea na safari yetu. Njiani nilisimulia kila nilichoweza kukielewa juu ya Chifu au Kingalu na kabila lake.

Niliongeza kile nilichojua juu ya Morogoro na vitongoji vyake. Niliwatajia makabila ya Wapogoro, Wakaguru na

Wasagara kuwa ni baadhi ya makabila ya eneo hilo.

Shughuli za kiuchumi? Nje ya uvuvi niliwaambia kuwa wakazi wengi zaidi ni wakulima. Mazao kama nyanya, uwele, mpunga, cocoa, simsim na muhogo na baadhi ya kilimo cha Morogoro. Niliwakumbusha pia kilimo cha miwa na katani ambacho kilishamiri sana katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo uliojaliwa rutuba na mvua kwa takriban mwaka mzima.

“Kwa mfano, upande wa pili wa mlima wa Uluguru ni pori na msitu mkubwa uliojaa wanyama aina aina. Msitu huo umeambaa hadi kuungana na mto Rufiji ambao nao ni habari nyingine kubwa.” Nilimweleza kwa kujigamba.

Nilitamani kuwaeleza pia kuwa miujiza ya Mlima Kolelo, ulioko kusini mwa mji wa Morogoro katika eneo liitwalo Mvuha. Simulizi za mababu toka enzi zao hadi sasa zimejaa hadithi za vituko vya kususimua toka ndani ya mapango ya mlima huo.

Ukiwa mlima mwingine ulio katika himaya ya Waluguru, Kolelo unatumiwa na wazee kwa tambiko na tiba kwa matatizo mbalimbali. Kwa mfano, Uluguru inapokumbwa na ukame wa muda mrefu wazee huenda mlimani, wakatoa kafara na kuomba mvua, hazipiti siku mbili kabla ya mvua kubwa kunyesha na kurutubisha ardhi. Kwa upande mwingine wanandoa wanapojikuta wameishi muda mrefu bila kupata ujauzito. Hata hivyo, watoto wa aina hiyo wanakuwa na miujiza yao; akikosa usimpige wala kumkaripia kwa hasira nyingi, atakufa ghafla. Aidha, mtoto huyo akiugua usimpe dawa za hospitali wala mitishamba unayoifahamu wewe. Mpeleke mlima Kolelo atambikiwe, kesho anakuwa mzima kana kwamba hakupata kuugua.

“Mna bahati kubwa sana Watanganyika.” Mama Leakey alisema.

“Kwa nini?” Nilimuuliza.

Nchi yetu kubwa sana na ina kila kitu. Wengine wana nchi kubwa, lakini sehemu kubwa ni jangwa ambalo si mnyama wala binadamu anayeweza kuishi. Wengine eneo kubwa la nchi zao ni milima isiyopitika au iliyofunikwa na barafu kiasi cha kutishia uhai wa viumbe hai wa huko. Nyie sivyo. Ardhi yenu imejaa rutuba. Ndani ya ardhi kuna kila dalili za madini. Mmezungukwa na mito, maziwa na bahari, jambo ambalo linafanya kamwe msijue shida ya maji wakati huohuo mkila samaki wa kila aina. Maana mapori na misitu iliyofurika wanyama na ndege wa kila aina. Hali ya hewa hapa kwenu ni nzuri kabisa kwa maeneo tofauti. Mungu awape ni zaidi?” aliuliza.

“Atupe uhuru,” nilimjibu.

“Uhuru wa ...”

Kutumia rasilimali zetu, nguvu na akili zetu kwa faida yetu. Kwa sasa hatuna uhuru huo. Mwarabu alikuja akatuvuruga kwa biashara zake za utumwa. Mreno na udikteta wake akafuatia. Wakati tunajipanga kupambana naye akingia Mjerumani na sera zake za kikatili. Ndiyo, alifanya mengi ya maendeleo kama kusomesha watu wapatao laki moja katika shule zake na kutujengea reli. Lakini hakupata kutushirikisha kikamilifu katika mipango ile. Aliwafanya babu zetu vijakazi na watwana, jambo ambalo lilipunguza ufanisi. Na ilipokuja vita kuu babu zetu walilazimishwa kushiriki bila hata kujua wanapigania nini. Wakafa, wakaparanganyika, uchumi wa nchi ukadidimia. Kisha akaja Mwingereza. Naye alikuwa na yake, kwa faida yake. Hadi leo hatujapewa nafasi ya kujipanga na utamaduni na uwezo wa kutumia rasimali zetu kwa faida yetu,” nilimjibu.

Ilikuwa moja ya hotuba zangu ndefu nilizopata kuzitoa. Nadhani ilikuwa hotuba ya maana kwani nilimwona Mary akinitazama kwa namna ya kuniunga mkono. Kupitia kwenye kioo cha dereva nilimwona pia mume wake, Leakey, ambaye alikuwa akiendesha gari, akitikisa kichwa huku tabasamu dogo likiwa limechanua usoni mwake.

“Uhuru una matatizo yake,” Mary alinichokoza tena.

“Bila shaka. Lakini hilo tutahangaika nalo baada ya kupata uhuru, sio kabila.”

Leakey hakuweza kujizuia. Aligeuka na kunitazama usoni kwa muda kana kwamba ndiyo kwanza ananiona maishani hivyo angependa kunifahamu zaidi. Kama angekuwa mtumishi wa serikali nilikuwa na hakika kuwa msimamo huo ungefanywa nitupwe jela kwa miaka kadhaa na viboko tele kwa tuhuma za uchochezi. Kwa bahati akina Leakey hawakuwa wa aina hiyo. Walikuwa na yao.

Wala mimi sikuwa mwanasiasa. Nilikuwa na uchungu tu wa kuiona nchi yangu ikiwa chini ya wageni, tena ambao hawakuujua wala kuuthamini utu na utamaduni wetu. Walijipa amri ya maisha yetu na kujichukulia madaraka juu ya uchumi wetu. Watu ambao kwao, kwa mujibu wa vitabu na habari za redio na magazeti walijitawala wenyewe huku wakichota rasilimali zetu na kuzipeleka kwao kwa ajili ya maendeleo ya nchi na watu wao.

Msimamo wangu huo ulikuwa ukichochewa na sauti za watu, akina Nkurumah kule Ghana na Wamarekani weusi ambao walianza kupiga kelele wakitaka watu weupe waondoe kwato zao Afrika.

SURA YA KUMI NA NNE

Wagogo Na ‘Idodomya’ Yao

Gari lilitafuna ardhi kwa kasi ya wastani. Dakawa, Magole, Gairo. Tukaingia katika ardhi ya Dodoma eneo la Kongwa.

Sura ya Dodoma kwa ile ya Morogoro ilitofautiana kama samaki na panya. Tulipokelewa na dalili nyingi za jangwa, isipokuwa kwa mti mmojammoja aina ya ‘mikungu’ ambayo iliota hapa na pale, tofauti kabisa na ile ya Morogoro iliyokuwa na misitu mikubwa na mapori yaliyoashiria neema. Milima ya hapa Dodoma pia ni jambo jingine la kuchekesha. Mingi ilikuwa midogo midogo, iliyoumbwa kwa mawe au majabali ambayo hayakuwa na mpangilio maalum.

Ukame au umbile hili la nusu jangwa limemwezesha mpita njia kuona mbali sana ya eneo alilopo. Hivyo, tuliweza kuona nyumba mbalimbali za Wagogo zikiwa zimejengwa hapa na pale. Majengo yao ni hadithi nyingine ya kusisimua. Wakati makabila mengi hujenga nyumba za kuta za udongo na paa la majani, au kuta na paa za majani matupu Wagogo zao zilikandikwa na udongo juu na chini, paa zao zikiwa za tambarare kama sakafu. Nyumba hizi fupifupi kiasi cha kumlazimisha mtumiaji kuinama anapoingia au kutoka na kuketi au kulala muda wote anapokuwa ndani. Ujenzi huo

ulishawishiwa na uhaba wa miti na nyasi katika eneo lao, pamoja na vipindi virefu vya ukame na mvua ndogo ambayo isingekuwa na madhara makubwa kwa majengo yao.

Katika maeneo mbalimbali tuliyopita, hasa eneo la Masalato, lililo karibu zaidi ya mji wa Dodoma tulikutana na mashamba kadhaa ya zabibu, wakulima waliendelea na shughuli zao.

Nilibaini baadaye kuwa Dodoma ni nchi pekee duniani ambayo zabibu hulimwa kwa misimu miwili ndani ya mwaka mmoja bila kuhusisha kilimo cha umwagiliaji. Kwa eneo ambalo mvua zake ni rasharasha na msimu wa ukame ni wa muda mrefu, toka Aprili mwanzoni hadi Disemba mwishoni, uzalishaji huo wa zabibu niliuchukulia kama moja kati ya ile miujiza midogomidogo ya dunia.

Tulitafuna kilometa zote 486 za safari toka Dar es Salaam na kuingia Dodoma. Tukatafuta mahali pa kulala, kwani akina Leakey walionyesha dalili ya uchovu. Tulipata hoteli ndogo lakini safi kuliko tulivyotegemea. Ukiwa mji mdogo sana enzi hizo, Dodoma ilikuwa haina pilikapilika nyingi licha ya ukweli kuwa ramani ya barabara ilionyesha kuwa Dodoma kilikuwa kituo muhimu cha safari toka nchi ya Misri hadi Afrika Kusini bado uchangamfu wake haukufika ule wa Dar es Salaam wala miji mingine niliyopata kuitembelea.

Akina Leakey walioga, wakala wakanywa mvinyo kidogo, kisha wakaingia chumbani kwao kulala. Mimi sikufanya hivyo. Niliamua kuitumia nuru ndogo ya jua ambalo lilikuwa likielekea kuzama magharibi mwa nchi na kuvinjari kidogo katika mitaa ya mji huo. Nilipenda sana kusikia lafudhi za makabila. Hapa niliwasikia Wagogo na Wakaguru wakizungumza. Ingawa sikuelewa wanazungumza nini bado

nilifurahi pale nilipozilinganisha lafudhi hizo na zile za makabila mengine niliyopata kukutana nayo. Lugha za baadhi ya makabila zilifanana sana hata nikaweza kuokota maneno mawili matatu na kuyatafsiri kwa Kiswahili.

Kiza kilipoanza kuingia nilirejea hotelini na kuketi na baadhi ya wageni wenzagu ambao walijipumzisha nje ya jengo hilo.

Mabadiliko ya hali ya hewa yalinishangaza. Lile joto la mchana lilitoweka ghafla na hali ya ubaridi ulioambatana na upepo wa kipupwe ikachukua nafasi. Nilijikuta nikitetemeka kidogo.

“Mbukwenyi!” alinisalimu mtu mmoja. Sikuwa mgeni sana wa salamu hizo za Kigogo.

“Mbukwa,” nikamjibu huku nikigeuka kumtazama.

Alikuwa mzee mmoja. Aliketi pia nje ya hoteli hiyo akinywa chai. Alikuwa ameona ninavyohangaika kwa baridi, “Hujapata kufika Dodoma?” aliuliza.

Nikamwambia kuwa hiyo ilikuwa mara yangu ya kwanza.

“Pole sana,” alisema. “Hali ya hewa ya Dodoma inadanganya sana. Mchana joto usiku baridi. Ukijidanganya kwa joto la mchana uje hapa bila koti wala blanketi utaadhirika na kuathiri afya yako.”

Lafudhi na umbile la mzee huyu ni mambo ambayo hayakuhitaji kuambiwa kuwa yeye ni mwenyeji wa hapohapo Dodoma. Pamoja na kuvaa nguo za kileo, koti, tai, na suruali nzuri bado alikuwa na alama mashuhuri, ambayo huonekana mara nyingi katikati ya nyuso za Wagogo walio wengi.

Wenyewe wanaiita ‘*nindi*.’ Katika enzi za kale jamii ya Wagogo waliitumia na kuamini kuwa ilikuwa kinga na tiba ya

tatizo la maradhi ya macho, tatizo ambalo ama kwa ajili ya pepo nyingi za kipupwe, ama uhaba wa maji, ama yote mawili, lilishamiri sana katika eneo hilo.

Niliingia ndani nikavaa sweta juu shati langu kisha nikatoka na kuketi tena na mzee yule. Nadhani sura yangu imekaa katika hali ya kupenda kusikiliza zaidi ya kuzungumza. Kwani hata kabla sijakaa vizuri mzee huyu alianza kuzungumza. Mazungumzo hayo kwangu yalikuwa somo la kususimua.

“Unajua kwa nini hapa panaitwa Dodoma?” alianza kwa kuniuliza.

“Sijui.”

Akacheka kabla hajaendelea, “Kwa kweli, hata kuitwa hivyo nimekosa tu. Wageni, hasa Wazungu wanaposhindwa kutamka jina fulani huishia kulitamka kivyao na kuliandika hivyohivyo. Hapo jina hasa ni ‘Idododmya.’

Haikuwa habari jema kwangu.

“Unajua jina hilo lilitokeaje?” aliuliza tena.

“Sijui.”

Akacheka tena, “Zamani sana.” Akaeleza, “Enzi za mababu wa mababu zetu, palikuwepo na bwawa kubwa ambalo wakati wa mvua lilitoa maji mengi kiasi cha kuitwa mto. Bwawa hilo lilikuwa kando ya mti mkubwa wa mkikuyu, hali iliyosababisha bwawa hilo litwe mto Mkikuyu. Enzi hizo wanyamwa walikuwa wengi na walitembea ovyo. Tembo, mmoja ambaye bila shaka alikuwa na kiu, alitembea hadi katika bwawa hilo kwa nia ya kukata kiu yake. Mara akaanza kudidimia. Tembo alihangaika sana kutoka kujiokoa lakini wapi. Watu wengi walikuja na kushuhudia tukio hilo. Walimwona tembo akizidi kudidimia hadi akatoweka machoni mwao. Kwa enzi hizo, ambazo matukio kama hayo yalikuwa machache hiyo

ilikuwa habari kubwa, ikaenea na kubadili kabisa jina la eneo na kuwa 'Idodomya' au Dodoma kama mnavyoita leo.”

Haikuwa hadithi jema masikioni mwangu. Hata hivyo, nilimzawadia kwa kujifanya nimeshangaa sana. Hali iliyompendeza na kufanya aanze simulizi nyingine juu ya Dodoma mara moja. “Ulipata kusikia chochote juu ya mtu aliyelitwa Mburumatare au Stanley?”

“Naam, nimemsoma katika vitabu vya kihistoria,” nilimjibu. “Naam, ameandikwa sana na aliandika sana vitabu vinavyohusu safari yake. Moja ya safari hizo ilimfikisha hapa Dodoma. Ni yeye aliyekuwa mgeni wa kwanza kuliweka jina la Dodoma katika maandishi.” Alitulia midogo, akameza mate. “Huo ulikuwa mwaka 1874” aliendelea kueleza. “Aliporejea tena mwaka 1886 Stanley aliliangalia eneo la Wagogo kwa tamaa. Hakuweza kujizuia, akaandika, “Nilikaa pale kwa miezi sita. Nilikuwa na hakika Ugogo ingeweza kufanywa ya kupendeza na tulivu, kuwa mahala pa rehema kwa wakazi wake na wagine. Hakuna nchi katika Afrika iliyonipendeza sana kuliko hii.”

“Mgeni mwingine mashuhuri,” mzee huyo aliendelea. “Jenerali Cameron alipata kupumzika Dodoma mnamo 1873 katika safari yake ya miguu katika bara la Afrika alisema ‘katika majira ya mvua mambo yote ni tofauti, nchi yote ni kijani, yenye uhai. Mapande makubwa makubwa ya ardhi yamefunikwa na mtama, maboga na tumbaku...”

Hali hiyo ya mabadiliko makubwa ya kimaumbile mwaka baada ya mwaka, raha na karaha zikipokezana, ilikuwa na athari zake kwa wagogo. Koo nyingi zilitawanyika na kuhamahama kutafuta ardhi yenye rutuba na malisho ya mifugo yao, hali iliyosababisha pasiwepo na utawala wowote

mkubwa, wa kudumu ambao ulijumuisha kabila zima.

Lakini jiografia ya Ugogo ilikuwa hazina tosha. Ikiwa katikati ya nchi, kwenye njia kuu iliyotokea pwani hadi ziwa Tanganyika, watu na biashara zote toka pande zote zilipitia hapo. Baadhi ya misafara iliyosheheni bidhaa za chumvi, meno ya tembo, nguo, silaha za watumwa ilisimama hapa kwa siku kadhaa wakijipanga kabla ya ngwe ya pili ya safari.

Pamoja na kutokuwa na himaya yenye nguvu Wagogo hawakukubali ardhi yao itumiwe bure. Watemi mbalimbali waliwatoza wageni hao ushuru mdogomdogo ambao Stanley aliulalamikia sana na kuuita 'kero' na kuongeza "Utaweza kufikiria kama ilikuwepo shule mahala fulani nchini Ugogo ya kuwafunza ujanja mdogomdogo na ubaya wa machifu ambao ni mabingwa wa kazi hii."

Lakini msafiri mwenzake, Cameron alitofautiana naye. Alisema kama ungekuwepo utaratibu maalum malipo hayo yangekuwa ya halali kabisa kwani kama Wagogo wasingelikuwa wanaishi katika eneo hilo, wakilima na kufuga, pamoja na kutunza vyanzo vya maji eneo hilo lisingepitika kamwe.

Lakini unyama uliofanywa na Mjerumani mmoja, Carl Peters, dhidi ya msimamo huo wa Wagogo kamwe hautafutika katika kurasa za historia ya unyama wa baadhi ya watu weupe dhidi ya wageni. Mtu huyu, ambaye aliacha nyayo za damu kila alikopita, toka nchi ya Wamasai, alifika Ugogo mnamo 1890. Alifika katika kijiji cha Mtemi mmoja aliyeitwa Makenge. Alipiga kambi yake bila ridhaa. Alipotakiwa kutoa ushuru alikataa na kutema cheche za vitisho vingi. Baada ya ugomvi wa maneno alifika mjumbe wa Mtemi aliyemwambia, "Sultani anataka amani nawe. Atakupa ushuru wa pembe za ndovu na ng'ombe dume." Kwa maneno yake mwenyewe Carl Peters

anaandika hayo na jibu alilotoa akisema, “Sultani atapata amani. Itakuwa ni amani ya milele. Nitawaonyesha Wagogo, Wajerumani ni watu wa aina gani.”

Ndipo, kwa maelezo yake mwenyewe alipoanza kutekeleza mpango wa kuteketeza na kuiteka sehemu hiyo, “Nilisonga mbele dhidi ya kijiji cha mwanzo. Wagogo walijaribu kujilinda, lakini baada ya wengi wao kupigwa risasi walitimka ovyo kupitia lango la kusini. Kijiji kikawa mikononi mwetu.”

“Teka nyara kijijini humo, choma nyumba zote, vunjavunja kila kitu ambacho hakikuweza kuungua... walijitahidi kukimbiza mifugo yao lakini tuliweza kupora ng’ombe mia mbili au tatu, huku tukiwapiga wale waliokimbia. Bunduki yangu ilikuwa ya moto sana kutokana na kupiga risasi kila mara hata ikawa shida kuishika.”

“Asubuhi yake zilipokelewa ripoti za kuuawa zaidi ya watu hamsini. Makenge akaomba tena amani. Peters alijibu, “Mwambie kuwa sitaki amani naye. Wagogo ni waongo, lazima waangamizwe kabisa duniani. Lakini ikiwa Sultani atataka kuwa mtumwa wa Wajerumani hapo tena yeye na watu wake wataweza kuishi.” Baada ya maneno hayo aliomba na kupewa ushuru wa ng’ombe dume, kondoo, mbuzi, maziwa na asali. Kisha akaahidi kuwapelekea bendera ya Ujerumani.

Unyama huo wa Peters ulifanyika pia Mpwapwa na sehemu nyingine ambako Chifu mmoja aliyeitwa ‘Muniama,’ Chifu wa Kigogo wa Kogollo, aliwaua wapagazi wake wawili. Peters alihakikisha anamuua yeye na watu wake na kuteka silaha zake ikiwemo bunduki aina ya *mauser*.

Lakini utawala wa Wajerumani Dodoma ulikuwa na sura tofauti. Wakati wa ujenzi wa reli, june 2, 1910 ilipotolewa amri ya kuchukua eno fulani la ardhi kwa ajili ya kupisha

majengo ya serikali watu mbalimbali waliokuwa na majengo na mashamba katika eneo husika walilipwa fidia. Miongoni mwao ni bwana Ndogwe aliyelipwa fidia ya rupia 27. Bwana mwingine aliyeitwa masala alipokea rupia 15. Kweche na Kihale kila mmoja alilipwa rupia kumi.

“Wajerumani pia walianza mchakato wa kuhamisha makao makuu ya Tanganyika hapa Dodoma tangu wakati ule,” alieleza mzee huyo kwa sauti ya majigambo.

Aliutaja mwaka 1921 kuwa ulikuwa na mengi yaliyofanyika kwa ajili ya azma hiyo ambayo haikupata kuwa baada ya himaya ya Mjerumani kutimuliwa nchini.

Kwangu, maelezo hayo lilikuwa somo kubwa la kisheria. Somo ambalo si rahisi kulipata toka katika kumbukumbu za mtu mmoja. Hivyo, nilimtaazama mzee huyo na kumuuliza, “Wewe ni mwalimu?”

Alicheka kabla hajasema, “Hapana. Mengine nimeyaona kwa macho yangu, mengine nimesimuliwa na baba na babu yangu. Yaliyobakia nayasoma katika vitabu. Nakuhakikishia mwanangu ipo siku na haiko mbali sana utukufu wa Idodomya utakumbukwa na mji utakuwa na kustawi kuliko unavyoona leo.

* * *

Umbali wa safari toka Dodoma hadi Kondo haikutofautiana sana na ule wa Dar es Salaam hadi Morogoro. Hata hivyo, ilikuwa safari ndefu na ngumu zaidi. Barabara haikuaminika sana, katika sehemu nyingi ilitulazimu kupita kwa uangalifu mkubwa kutokana na makorongo yaliyotafuna nusu ya barabara na madaraja mabovu ya hapa na pale.

Toka Dodoma kuja Kondoa ilitulazimu kupita kwa uangalifu mkubwa kutokana na makorongo yaliyotafuna nusu ya barabara na madaraja mabovu ya hapa na pale.

Toka Dodoma hadi Kondoa ilitulazimu kubadili mwelekeo. Badala ya kuelekea Magharibi kama tulivyofanya toka Dar es Salaam sasa tulielekea Kaskazini. Tulipita vijiji mbalimbali ambavyo sikuweza kushika majina yake yote isipokuwa Melamela, Babaiyo Nafakwa. Hapo tukavuka Mto Mbu na kuingia kwa Mtoro, eneo lenye maajabu yake.

Kwa Mtoro lilikuwa eneo kame zaidi. Ardhi yake ilitawaliwa na mchanga mwingi. Ungeweza kumwona mtu aliye umbali wa kilometa hadi tatu bila kuhitaji darubini wala jitihada za ziada. Kwa mtazamo wa harakaharaka ungeweza kudhani kuwa eneo hilo lisingeweza kuwa na watu. Lakini watu walikuwepo. Nyumba moja mbili, aina ya tembe, zilionekana hapa na pale, wenyeji wake wakionekana kwa nadra sana. Na kila aliyetokea alionekana nusu mtupu kwa mavazi duni waliyovaa. Aidha, karibu kila mmoja alionekana kupauka kwa vumbi na jua kali. Hilo halikupata kunishangaza sana. Kwani sikuwa nimepata kuona dalili ya maji ya kisima wala bwawa katika umbali mrefu wa safari yetu. Hata kile kilichoitwa mto mara nyingi yalielekea kuwa makorongo tu, ambayo hupata maji kwa vipindi vifupi vya mvua kabla hayajakauka tena.

“Wanaishije watu upande huu wa dunia?” alihoji Mary Leakey akitazama huku na huko.

“Wanayo namna yao ya kuishi,” mumewe alijibu. Jibu ambalo lilithibitika pale tulipofika mahala na kukuta watu wawili wakichimba katika mkondo wa mto mmoja uliokauka

ili kupata maji kwa matumizi yao na mifugo yao “Unaona?” Leakey alimwonyesha mkewe.

Tulisimamisha gari, nikashuka ili kuwauliza jambo. Ni hapo nilipokutana na mwujiza wangu wa kwanza katika eneo hilo. Watu hao, wakiwa weupe zaidi ya weupe wa kawaida kwa Mwafrika walisimama na kunitazama kwa mshangao. Kila dalili ikionyesha kuwa hawakuelewa lugha yangu.

“Nawasalimu, hamjambo?” Nilirudia tena. Nilipoona bado hawanielewi nilirudia salamu hizo kwa lugha ya Kigogo ‘*mbukwenyi*’ niliwaona wakitabasamu, dalili ya kuelewa. Kazi ilikuwa pale mmoja wao aliponijibu. Ilikuwa mara yangu ya kwanza kuisikia lugha kama ile. Kwanza nilihisi kuwa anaondoa kitu mdomoni mwake kwa ulimi pale alipobandika ulimi wake kwenye fizi na kutoa sauti mnato.

Aliporudia tena, na baadaye kupokewa na mwenzake kwa namna ileile ndipo nikabaini kuwa wanajaribu kuniambia kitu kwa lugha yao, ambayo nadhani haiyandikiki kwa herufi hizi za kizungu tunazotumia.

Wasandawe! Nikakumbuka. Kwa kiasi fulani nililinganisha lugha yao hiyo na ile ya Wamang’ati au Wandorobo ambao si Wabantu. Sikuwa na la kufanya zaidi ya kugeuka na kurejea kwenye gari, tukaendelea na safari.

Dalili za neema katika ardhi hiyo zilianza kujitokeza pale tulipofika mji wa Kondoa. Ulikuwa mji mdogo lakini watu wengi na pilikapilika nyingi kuliko nilivyotegemea. Kulikuwa na nyumba ya wageni, maduka mawili ya Waarabu na kituo kidogo cha afya. Hii ilikuwa nchi ya Warangi, ambao ni Wabantu zaidi. Aidha, wengi wao walizungumza Kiswahili

kwa ufasaha, lafudhi ya Kiarabu ikiwa imetamalaki katika matamshi yao. Dini ya Kiislam pia ilijikita zaidi, kwani hata kabla hatujatulika tulilakiwa na sauti ya ‘wahadhini’ ambao walikuwa wakiwakumbusha waumini kwenda msikitini kwa sala ya jioni.

Tulipata nyumba tukapumzika. Kesho yake pia tuliamua kupumzika. Leakey aliandaa ratiba ya pilikapilika zake za safari, mimi nilivinjari katika mitaa na vitongoji vya Kondoa. Fursa ambayo iliniwezesha kuona na kujua mengi juu ya mji huo. Kwa mfano niliweza kubaini kuwa kihistoria haukuwa mji mdogo kama unavyofikiriwa. Ulikuwa na sehemu yake, kubwa tu katika kurasa za kihistoria ya vita kuu zilizohusisha Tanganyika.

Kondoa ni mji mdogo lakini una mengi ya kusisimua. Kinyume na Dodoma, Kondoa ilikuwa na sehemu yake katika historia ya vita kuu. Pale wakazi wa eneo hilo walionja makali ya vita hivyo kuliko wale wa Dodoma, jambo lililofanya Wajerumani waiweke Kondoa katika hifadhi ya kumbukumbu zao za matukio muhimu ya vita ile.

Kiutamaduni Kondoa pia ina nafasi ya pekee. Wakati wakazi wa Dodoma wakisubiri maji kwa msimu Kondoa wao mizimu ya babu zao iliwazawadia maji ya kudumu yanayotoka hadi hivi leo.

Ntomoko ni jina la mlima wenye chemchem ya maji safi yanayotoka kwenye jiwe kubwa lililoko kwenye mlima huo. Mlima huo ni mkali na uhitaji ushujaa mkubwa kuupanda. Kuna maelezo kuwa jina hilo la Ntomoko, kama ilivyo ‘Idyodoma’ lilitokana na mapigano kati ya Warangi na Wamasai. Kwamba

Wamasai walikuwa wakivizia mara kwa mara na kuwaibia Warangi ng'ombe. Hali hiyo iliwachosha Warangi ambao waliishi juu zaidi ya kilima hicho. Hivyo siku moja walizingira kilima chote na kuanza kuwashambulia Wamasai kwa mikuki na mishale. Wamasai wakawa wakikimbia kwa kujirusha katika kichaka kilichokuwa na miti mingi bila kujua kuwa pale kulikuwa na chemchem. Kila aliyejirusha hapo alididimia na kufa. Warangi walipoona hali hiyo ndipo wakaliita eneo hilo 'Ntomoko' kwa maana ya mahala ambapo watu hutokomea.

Baadaye Wamasai walilifanya eneo hilo mahala pa tambiko kwa kuwakumbuka wahanga waliotokomea katika eneo hilo. Inadaiwa kuwa tambiko hilo liliambatana na kumpeleka ng'ombe aliye hai na kumfungia. Wanaporudi baadaye hukuta ng'ombe huyo kachinjwa na kuchunwa. Nusu ya nyama hiyo waliila nusu wakiiacha hapo kwa ajili ya mizimu.

Awali, kabla ya kuhusishwa na teknolojia ya kisasa katika chanzo hicho cha maji zilikuwepo taarifa nyingi za miujiza. Ilielezwa kuwa mtu aliyekwenda hapo ghafla bila kuhusisha wazee wafanye tambiko alijikuta akipakwa kinyesi cha binadamu bila kujua nani kampaka. Usiku zilisikika sauti za ngoma na watu wakicheza lakini hawakuonekana. Wakati mwingine unapokaribia maji, maji hayo yalibadilika rangi ghafla na kuwa kama maziwa au yaliyojaa tope. Mara nyingi saa za usiku wakazi walidai kuona mlima ukiwaka taa. Hali iliyopelekea wazee wa Kirangi kufanya tambiko hapo kwa kupeleka kondoo mweusi kila mwaka ili maji yasikauke.

Kiongozi mmoja wa serikali aliamua kwenda Haubi,

kilipo chanzo cha maji. Alipoona maji hayo yanavyotoka kwa wingi alitamka kuwa anadhani kama ungechimbwa mfereji mkubwa maji hayo yangeweza kuhudumia watu katika maeneo mengi zaidi ya Kondoa. Kwamba mara baada ya kauli yake hiyo maji yalibadilika ghafla na kuwa machafu. Wazee wakashauri kufanya tambiko. Baada ya tambiko maji yakarejea hali yake ya kawaida, ikiwa ishara kuwa mizimu iliafiki wazo lake. Miaka kadhaa baadaye mradi mkubwa wa kuchimba mfereji wa kufikisha maji hayo katika vijiji vipatavyo kumi na vinane vya Irangi nchini. Baadhi ya vijiji hivyo ni Busi, Mairinya, Kirere cha Ng'ombe, Goima, Chandama na vinginevyo. Watu wapatao 30,000 wakinufaika na huduma hiyo.

Siku mbili baadaye Leakey aliniarifu kuwa alikuwa tayari kwa kile alichonilezea kama 'maandalizi' ya kazi yake. Maandalizi yalikuwa magumu kuliko hata kazi yenyewe. Kwa msaada wa mzee mmoja wa Kirangi, Msii, ambaye alipewa ajira ya muda tulikuwa watu wa kusafiri katika maeneo mbalimbali ya Kondoa, safari nyingi zikihusisha kutembea kwa miguu katika mapori, majangwa, milima na mabonde ambayo Leakey aliyapendekeza kutokana na ramani yake. Mara kwa mara tulishinda porini, mara kadhaa tukilala huko huko ili tuweze kuamka alfajiri na kuendelea na kazi. Haukupita muda mrefu kabla mzee Msii hajatutoroka na kutoweka bila hata ya kuchukua ujira wake.

Safari hizo zilitufikisha Serya, Mondo, Goima, Sombwa, Mnenya na baadaye Kolo ambako kwa mara ya kwanza niliona Leakey akitoa tabasamu lake la kwanza. Ilikuwa baada ya kugundua mapango na majabali kadhaa yaliyokuwa na michoro

ya ajabuajabu. Michoro ambayo baada ya kuichunguza sana Leakey na mkewe waliniambia kuwa ilichorwa na watu wa kale.

“Leo ni siku ya kihistoria. Nina hakika makazi ya kale zaidi ya watu wa kale. Michoro hii inaweza kuwa na umri wa miaka isiyopungua elfu thelathini hadi leo,” alisema kwa furaha akiyumba huku na kule kama mtu aliyegundua machimbo ya dhahabu.

Mingi kati ya michoro hiyo ilikuwa ya wanyama hasa swala na nyati. Mengine ilikuwa ya watu waliokuwa katika mawindo, silaha zao mishale au mawe ikiwa mkononi tayari kuua mnyama. Vifaa walivyotumia kuchora ndivyo vilivyoniacha zaidi ya michoro yenyewe. Ilikuwa aina fulani ya rangi ambayo iliweza kuingia kwenye jiwe na kudumu kwa miaka mingi ikistahimili jua, mvua na misukosuko mengine tele ya kimaumbile.

Tulikaa katika eneo hilo kwa wiki mbili. Mary akiitumia kamera yake kupiga picha kila mchoro na kila kifaa walichokishuku kuwa ni cha kale. Tulifanya pia, kazi ya kuchimba hapa, kufukua pale. Kazi hiyo iliwezesha kukusanya vifaa vingi kama silaha, mawe ya kusagia, mabaki ya mifupa ya wanyama walioelekea kuuawa na binadamu na vitu vingine tele. Dalili ambazo zilizidi kuthibitisha hisia za Leakey na mkewe kuwa mtu wa kale zaidi ya duniani aliishi hapo au maeneo hayo.

Hisia ambazo zilithibitishwa na wenyeji pale alfajiri moja tuliposhangaa kuwaona wazee watatu, mmoja wa kike waliovaa kimila wakija katika eneo hilo na kuendea moja ya

jabali yenye michoro na kuanza tambiko la kimila. Waliimba na kucheza kabla ya kumwaga mchele na vyakula vingine kama zawadi kwa wahenga.

Baadaye tulibaini kuwa eneo hilo hutumiwa na wenyeji tangu enzi za mababu zao kwa ajili ya matambiko ya kuita mvua au kujiepusha na maafa mbalimbali kama mlipuko wa maradhi au vita. Kwamba ilikuwa nadra sana matambiko katika eneo hilo kutojibiwa kwa neema.

Eneo hilo lililojaa miamba, ardhi yake ikiwa nusu jangwa kama ilivyokuwa sehemu kubwa ya ardhi ya Dodoma iliashiria kuwepo kwa ardhi nzuri, yenye miti, majani na wanyama tele miaka mingi iliyopita.

“Mtu wa kale aliishi hapa,” Leakey alisisitiza akitazama huko na huko. “Naweza kusema kuwa aliishi hapa miaka milioni mbili iliyopita. Naamini uchunguzi wa kimaabara kwa baadhi ya vifaa hivi tulivyopata utathibitisha hivyo,” aliongeza.

Nilimtazama kwa kumpongeza. Pia, nilijipongeza kwa kuwa sehemu ya mafanikio ya uvumbuzi huo.

SURA YA KUMI NA TANO

Bonde la Ufa na Morani wa Kimasai

Sikumbuki niliishi na akina Leakey kwa muda gani. Hazikuwa siku wala miezi. Wala haukuwa mwaka. Niliishi nao kwa miaka, tukihangaika pamoja katika mapori, miamba, mito, milima na mabonde mbalimbali ya Bonde la Ufa.

Tulichimba hapa, tulifukua pale, tuliokota hiki, tulitupa kile ilimradi mtu asiyejua tunachokifanya angeweza kutufananisha na genge la wendawazimu.

Haikuwa kazi nyepesi. Ilihitaji vifaa na watu wa kutosha. Mara kwa mara tulilazimika kutoa ajira za muda kwa watu ambao walitusaidia kwa shughuli hizo ngumu. Hali kadhalika, hatukuwa na kituo kimoja. Tulipiga kambi katika miji na vijiji mbalimbali vya Babati, Mbulu, Manyara na kwingineko. Kupokea na kusikiliza kwa makini simulizi za wazee na hata hadithi za mapokeo ilikuwa sehemu ya kazi yetu kwa ajili ya utafiti tuliokuwa tukiufanya.

Eneo la kazi nalo lilikuwa pana sana. Bonde la Ufa ni uwanja mrefu sana. Unakadiriwa kuwa na urefu wa kilomita 6,000 ukiwa umeambaa toka nchi ya Syria, Lebanon, Jordan, Israel, Kenya, Tanganyika hadi Msumbiji. Mto Jordan ambao hupeleka maji yake katika bahari mfu na Galilaya, milima ya

Virunga na Luenzori, maziwa kama Tanganyika, Nyanza na Magadi au Nakuru ya Kenya ni sehemu ya Bonde la Ufa. Baadhi ya milima kama Kilimanjaro, mlima Kenya na mengineyo inaaminika kuwa ilikuwa ikipata milipuko ya Volcano miaka ya nyuma. Mlima Oi Doinyo Lengai hadi sasa hupatwa na mlipuko huo wa volkano.

Katika Bonde hilo la Ufa ndimo lilimo eneo la Olduvai Gorge, wenyeji wakiliita 'Oldupai.' Likiwa katika uwanja wa Serengeti, ambao pia una wanyama wengi kuliko mahali popote pale duniani, lilikuwa na mito, milima na maziwa madogo kwa makubwa. Moja ya maziwa hayo likiwa Olduvai. Maumbile ya eneo yalionyesha dalili za kuwepo kwa jambo kubwa kama tetemeko kubwa la ardhi na jambo jingine kubwa zaidi ambalo lilitikisa dunia na kufanya ididimie katika Bonde hilo la Ufa huku maeneo mengine yakiwa yameathirika zaidi. Bonde la Olduvai. Pia liko katika maeneo hayo.

Zipo hisia kitaalamu kuwa eneo ilo lilikaliwa na watu, takribani miaka milioni mbili iliyopita. Dalili nyingi zilithibitisha hivyo. Ni humo ambalo Leakey aliendesha utafiti wake kwa muda mrefu na kuchimbua vitu mbalimbali ambavyo vilizidi kuashiria hilo.

Jitihada hizo zilizaa matunda siku ile alipogundua fuvu la kichwa cha mtu wa kale. Fuvu ambalo lilipopimwa kwa njia za kisasa zaidi lilibainika kuwa lilikuwa la mtu wa kale zaidi duniani. Kwa maneno mengine, mtu wa kale zaidi duniani aliaminika kuishi katika maeneo ya Tanganyika. Ugunduzi huo ulimpa Leakey sifa kubwa miongoni mwa wataalamu wa masuala ya mambo ya kale. Hali hiyo ilimsababisha awe mtu wa safari nyingi sana, katika nchi mbalimbali za dunia. Aliudhuria warsha na semina nyingi hapa na pale,

alikaibishwa katika vyuo vikuu mbalimbali kutoa miadhara, alitembelea majumba ya kumbukumbu za mambo ya kale huku na kule na kuendesha mikutano mingi ya kuchangia fedha ili zimwezeshe kuendelea na utafiti wake mrefu na mgumu.

Safari hizo zilinifanya niwe mtu wake wa karibu zaidi Tanganyika, mara kwa mara nibakie kuwa kiongozi na msimamizi wa shughuli zake. Nilikuwa na uwezo wa kuajiri na kufukuza. Nilihifadhi nyaraka na kumbukumbu za utafiti. Kwa kweli sikuwa tena mtu mdogo kama yule kondakta wa gari bovu kule Mbeya au Mnyampala wa mashamba ya katani kule Pangani.

Posho au mshahara wangu haukuwa mbaya, aidha matumizi hayakuwa mengi. Muda mwingi uliishia maporini ambako sikuhitaji kutumia fedha zozote. Hali iliniwezesha kufungua akaunti benki na kujiwekea akiba kidogo kidogo. Hiyo ni faida nyingine niliyoipata katika ajira yangu kwa akina Leakey.

Lakini faida kubwa ilikuwa elimu. Sikubahatika kupata elimu ya darasani. Ndoto ya kurudi shule zilikwishayoyoma tangu niliposahau madaftari yangu kule Pangani na kwenda Bagamoyo, baadaye Dar es Salaam hadi huku. Nilitafuta elimu vitabuni. Leakey na mkewe walikuwa watu wa vitabu. Walisoma kila kitu; toka historia, sayansi, jiografia hadi riwaya. Walisoma vitabu vya dini, majarida na makabrasha ya kila aina. Walipobaini kuwa mimi pia nilikuwa ‘mgonjwa’ wa vitabu waliniruhusu kusoma kitabu chochote nilichokitamani. Ingawa sikuwa na kiongozi wa kunielekeza kile ninachokisoma bado nilijifunza mengi na kupata ufahamu wa kutosha.

Lugha ya kiingereza ni jambo jingine ambalo nilinufaika nalo kwa kuwa nao. Mara kwa mara, walizungumza nami

kwa lugha yao, hali iliyopelekea niondoe hali ya kutojiamini na kuwajibu bila kujali kama nakosea au la, kama ambavyo wao pia waliongea Kiswahili bila kujali kama wanapatia au la. Taratibu nikajikuta naimudu vizuri lugha yao. Hata pale nilipokutana na watu wengine, wawe wageni wasiojua kabisa Kiswahili, au wasomi wa vyuo mbalimbali, niliweza kuzungumza nao kwa ufasaha hata wakashindwa kuamini kuwa elimu yangu haikuvuka daraja la kati.

Habari ulikuwa ugonjwa wangu mwingine. Pamoja na ukweli kuwa muda mwingi niliutumia maporini, ambako redio nyingi hazikuweza kusikika na ilikuwa ndoto kuona magazeti, bado kila niliporejea mijini niliyafuta hata yale ya mwezi mmoja uliopita. Nilisoma habari, makala, matangazo, hadithi na mashairi. Gazeti jipya la *Mwangaza* lililoanzishwa Mei 10, 1951 na lile la kwetu la tangu 1943 likihaririwa na Chifu Thomas Mareale II (OBE) ni miongoni mwa magazeti ya Kiswahili ambayo pamoja na upatikanaji wake wa nadra bado yalininufaisha sana kuelewa mtazamo wa mtu mweusi katika nchi yake.

Habari ya Pangani kufanywa wilaya (Janua 7, 1938), samaki wa aina ya sangara kupandikizwa katika ziwa Nyanza, ambalo sasa liliitwa Victoria (1950), Laurian Rugambwa kuteuliwa kuwa askofu wa kwanza Mwafrika nchini Tanganyika (Desemba 13, 1951), kuanzishwa kwa Chama cha TAA kikidai haki za watu weusi (1949). Amri ya serikali kuitangaza rasmi Serengeti kuwa hifadhi ya taifa (April 20, 1948 na kadhalika).

Vyombo hivyo vya habari viliniwezesha pia kufahamu kuwa sensa ya mwaka 1948 ilionyesha kuwa Tanganyika ilikuwa na idadi ya watu 7,744,600 kati yao 183,860 au

asilimia 2.4 pekee wakiishi mijini. Idaidi ambayo miaka tisa baadaye (1957) ilibadilika na kuwa watu 9,087,6000 nchi nzima, 364,070 au asilimia 4.0 wakiishi mijini.

* * *

Alfajiri moja nilipata mtihani wangu wa kwanza wa kiutamaduni nikiwa kama mkuu wa kambi ya Leakey. Tulikuwa tumepiga kambi katika maeneo ambayo hayakuwa mbali sana na ziwa Manyara. Akina Leakey walikuwa nje ya nchi kwa miezi kadhaa. Usiku huo mzima ngoma za Wamasai ambazo wenyeji zaidi yangu walizitambua kama ‘Omorata’ ambayo huchezwa majira ya tohara, miezi hiyo ya julai zilitumbuzwa. Niliamshwa toka usingizini kwa kelele za mtu aliyekuwa akilia nje ya hema langu kwa sauti huku akiita kwa nguvu, “Nisaidie. Baba nisaidie...” nilipotoka nilikuta msichana mdogomdogo akiwa hapo nje, kapiga magoti, akilia na kutetemeka kwa hofu.

Alikuwa msichana wa Kimasai. Alipambwa kwa shanga kwenye kichwa chake chenye nywele fupi, shanga nyingine tele shingoni, masikioni, mikononi na miguuni. Alivaa vazi la buluu, lililomfunika hadi miguuni. Hakuwa na viatu. Nadhani msichana huyu alitegemea zaidi kumwona mtu mweupe akitoka humo ndani badala ya mweusi kama mimi, kwani niliona dalii za kukata tamaa katika macho yake. Hata hivyo aliendelea kupiga magoti huku akisema “Nisaidie baba... naomba unisaidie.”

“Kuna nini?” niliuliza.

“Na... niko naogopa...” alisema kwa Kiswahili chake cha shida.

“Unaogopa nini?”

“Naogopa. Naogopa sana. Kufa ...”

“Kufa!”

“Ndiyo... kufa. Ndito mmoja kafa jana. Damu... damu nyingi. Naogopa,” aliendelea kusema huku mara kwa mara akigeuka nyuma alikotokea kwa dalili za hofu.

Ndipo nikaelewa. Msichana huyu alikuwa akikimbia tohara, jambo ambalo wasichana wote wa Kimasai, kabla ya kuolewa, hutakiwa kufanyiwa. Kwa maana hiyo msichana huyu alikuwa Ndito. Alikuwa hajafikia hadhi ya kuitwa kokoo. Yeyoo au Shangiki ambazo ni hadhi maalumu za wanawake wa kimasai waliopitia hatua mbalimbali za kimila na kimaisha.

“Wewe unatoka wapi?” nilimuuliza.

“Enkang,” alinijibu, akiwa na maana ya boma lao.

Mimi nilitaka kujua kama anatokea Kenya au Tanganyika. Nikamuulia hivyo.

“Hapana.”

“Hapana? Hutoki Kenya?”

“Ndiyo.”

“Kwa hiyo wewe n Mtanganyika?”

“Hapana.”

Nikashangaa. “Kwa hiyo wewe ni raia wa nchi gani?”

“Siye ni Wamasai,” alinijibu.

Ilinibidi nicheke kidogo. Alinikumbusha tabia ya Wamasai ya kujiona kuwa wao ni raia wa nchi hizo mbili. Tabia hiyo ilijengeka katika fikra zao kutokana na kukulia katika utamaduni wa kuahama hama wakifuata malisho ya mifugo yao bila kujali kama wameruka mpaka au la.

“Nisaidie... wanakuja...” alisema akiinuka na kukimbia ndani ya hema langu. Nilipotanabahi, nilikuta hema zima limezingirwa na vijana wa Kimasai wapatao ishirini, wakiwa na ngao zao mikononi, mkuki mkono wa pili. Walikuwa tayari

kwa lolote. Tayari kwa vita, tayari kwa mauaji.

“Iko naficha yeye wapi?” mmoja wao aliniuliza. Nikamtazama. Alikuwa ‘Layoni’. Mwenyewe akiwa bado hajatahiriwa, hajaua simba wala kuoa lakini hawaogopi isipokuwa wakati wao bado.

Walikiri kuwa nikweli msichana mmoja alifariki usiku huo katika kufanyiwa tohara. Lakini walilielezea tukio hilo kuwa la bahati mbaya tu, ambalo hutokea kwa nadra sana. Wakasisitiza msichana huyo kufanyiwa tohara ili aweze kuwa mtu mzima, abebe majukumu ya kifamilia.

“Ataolewaje bila emorata? Atapataje watoto na familia? Ndito lazima apitie mila zote alizopitia mama na bibi yake,” mmoja wao alisisitiza.

“Lakini huyo hataki,” nilijaribu kutetea.

“Siyo suala la kutaka au kutokutaka. Ni suala la ukoo. Akikataa atatengwa na jamii nzima. Atafukuzwa kila anakokwenda. Hataolewa milele. Huoni kama hilo pigo kubwa kwake kuliko kifo?” alinihoji kijana huyo wa Kimasai.

Kama wenzake alivaa nguo nyekundu. Nywele zake ndefu zilizosukwa vizuri kurudi nyuma zilipambwa kwa rangi au udongo mwekundu. Mikononi na miguuni alivaa bangili za shanga ambazo zilifanya kila hatua aliyopiga wakati tukizungumza itoe mlio ambao nadhani huchangia kumchanganya hata simba kwa wale waliopata kupambana nao.

Wamasai ni watu wanaothamini utamaduni wao kwa kiwango kilekile wanachotamani ng’ombe wao. Ujenzi wa maboma yao, ambayo nilipata kuyatembelea mara kwa mara unathibitisha hilo. Vijiji vinavyoitwa ‘Enkang’ hujengwa kwa mduara, ng’ombe wao wakilala katikati ya duara hilo ili

kuwaepusha na wanyama wakali pamoja na wezi wa mifugo. Vijiji huwa havidumu sana kwani mara malisho ya mifugo yao yanapoonyesha dalili za kupungua, au kifo kinapotokea katika eneo hilo huondoka mara moja na kuhamia sehemu nyingine.

Maamuzi mengi ya Wamasai hufanywa na 'Laibon,' ambaye ni kiongozi na pia kuhani wao kwa mungu wao, wanayemwita 'Enkai'. Kutoboa masikio pili aweze kuvaa bangili, kung'oa watoto meno ya mbele ili aweze kulishwa uji wakati akiumwa na kuhakikisha mtoto wa kiume anapotahiriwa hapigi kelele za kuogopa maumivu ni baadhi ya mila za Kimasai ambazo zimedumu miaka nenda rudi. Lugha yao 'maa' pia wanaithamini sana kiasi kwamba kuwa hawafanyi jitihada za haja za kujua lugha za watu wengine.

Tofauti na makabila mengi nchini, kazi za ujenzi wa nyumba zao hufanywa zaidi na wanawake wakati wanaume wakijihusisha na ulinzi wa makazi na mifugo.

Kwa Wamasai tohara ni tukio la aina yake. Ndilo ambalo humtoa msichana au mvulana katika hadhi moja kwenda ya pili. Hivyo, tukio hilo huambatana na mbwembwe nyingi, zikiwemo ngoma maalumu ambazo huchezwa miezi ya Julai na kufuatiwa na tukio lenyewe ambalo hufanyika alfajiri, kabla jua halijachomoza. Tukio hufanyiwa karibu na zizi, moto mkubwa huwashwa na ng'ombe mmoja kuchomwa mkuki shingoni. Damu ya ng'ombe huyo hukingwa na kuhifadhiwa katika kibuyu maalumu kiitwacho 'Eng'oti'. Damu hiyo huchanganywa na maziwa na watahiriwa wote kunyweshwa kabla ya tohara.

Kilimo ni moja ya mambo ambayo hayawavutii sana Wamasai. Chakula chao kikuu ni nyama ama kupika ama ya kuchoma. Nyama za kupika zina maadili yake. Huchanganywa

na dawa mbalimbali. Kwa mfano dawa ya ‘Okiritaraswa’ humfanya mtu awe na hasira sana. Dawa nyingine ni ‘Orumukatani’ ambayo nayo hupikwa na humpa mtumiaji nguvu. Mara nyingi watumiaji wa dawa hizi ni wale walio tayari kwenda vitani au kupambana na simba. Dawa ya tatu, ‘Orokirotiti’ humfanya mtumiaji kuwa na hamu ya kula pamoja na kuwa mchangamfu. Nyingine ni dawa za kuondoa mafuta mwilini, kujikinga na maumivu ya misuli na kujenga mwili.

Hawa ndio Wamasai. Watu wanaojipenda na kujithamini. Watu wanaoupenda na kuuthamini utamaduni wao kiasi kwamba ujio wa wageni mbalimbali nchini, toka makabila yaliyoingia toka kila upande wa nchi, Waarabu waliotoka mbali na ujanja wao, Wazungu na hila zao na wengine hawakupata kuwatikisa Wamasai na imani zao. Watu wa aina hiyo ambao walikuwa tayari kwa lolote, ikiwa pamoja na kutoa uhai wao, ili kulinda hadhi yao, mimi ni nani hata nibadili imani yao katika muda wa saa moja? Niliwaza nikiingia ndani ya hema kwa dhamira ya kumtoa dada yao.

Nilimkuta akibubujikwa na machozi huku akitetemkea mwili mzima. “Tafadhali, usiwaruhusu wanichukue. Naogopa... Nitakufa!” alinisihi akipiga magoti miguuni mwangu.

Nilipatwa na huruma. Nikahisi machozi yakinilengalenga hasa pale nilipomtazama usoni na kuona alivyonitumbulia macho ya huzuni kama mfamaji aliyekata tamaa, anayetegemea msaada wangu pekee.

Huko nje Morani walisikiliza wakianza kupiga kelele. Nadhani walihisi kuwepo kwa jambo linaloendelea humo ndani. Mara wakaanza kuimba nyimbo zao zinazoashiria vita huku wakirukaruka kulizingira hema langu. Ghafla mmoja mmoja akaingia ndani ya hema, mkuki wake ukiwa umetangulia.

Mwingine akafuatia, sime mkononi. Walimwendea *ndito* moja kwa moja na kuanza kumvuta nje. Msichana akazidi kulia akinitazama kwa macho yake yaliyoloa machozi.

Sikufikria mara mbili. Nilichupa na kuichukua bunduki ya Dakta Leakey na kuilekeza kwao huku nikifoka, “Mwacheni!”

Hawakuamini macho yao. Walinitazama kwa mshangao na hasira kali.

“Tokeni!” Nilifoka tena.

Yule mwenye sime alipandwa na hasira. Akamwachia msichana na kunifuata huku akichomoa sime yake. Lakini mwenzake alimshika na kumnong’oneza jambo.

Nadhani alikuwa hajasahau maafa ya risasi kwa miili yao. Pengine alikumbuka tukio la kinyama la mamia ya watu wao waliouawa na Stanley walipopambana naye kwa mikuki na sime zao. Mwezie alimsikiliza. Kama kondoo, waligeuka na kutoka nje ambako waliwashawishi wenzao kuondoka. Lakini haikuwa kabla ya kunitupia jicho kali, la kisasi, ambalo hadi leo sijapata kulisahau katika njozi zangu za usiku na mchana.

Mara walipoondoka, nilimrudia msichana yule na kumtaka yeye pia aondoke. “Nenda zako, wakirudi hapa hawatafikiria mara mbili,” nilimhimiza.

Aliinuka, akanitupia jicho la shukrani kisha kwa sauti ndogo alisema, “Umesaidia mimi sana. Ahsante Laibon.”

Laibon! Heshima aliyonipa haikuwa ya kawaida. Nilimtazama akigeuka na kuondoka taratibu. Nje ya hema alitazama huko na huko kabla ya kuondoka akielekea upande wa pili wa walikoelekea wabaya wake.

Wasaidizi wangu walunifuata baadaye, mmoja akinipongeza wa pili yule anayejua Kimasai akinipa pole.

“Pole ya nini?” Nilimwuliza.

“Hujui? Unadhani Mmasai ni mtu wa kuvumilia kitendo ulichokifanya? Kwao umedhalilisha kabila zima. Lazima watataka kulipa kisasi. Kama si leo kesho, kama si kesho keshokutwa au hata mwakani,” alinifafanulia.

Kwa kuamini kuwa Wamasai wasingependa kucheza na risasi, hasa baada ya kuona bunduki mikononi mwangu, niliipuuza hofu yake. “Enzi zile zimepita ndugu yangu. Sasa wanajua bunduki, wanajua utawala wa sheria,” nilimweleza.

Hakuonekana kuafikiana na fikra zangu, ingawa hakutia neno jingine. Niliamini hivyo jioni hiyo aliponitaka ruhusa ya kwenda nyumbani kwake kuitazama familia yake. Hakukuwa na kazi nyingi. Hivyo nilimruhusu. Msaidizi wa pili alitoweka bila kuaga. Bila shaka kwa hofu ileile.

Usiku huo nilijikuta peke yangu katika kambi, katikati ya uwanda mpana wenye jangwa na majani hafifu.

Sina budi kukiri kuwa kwa kiasi fulani nilishikwa na hofu. Nilikusanya magogo na kuwasha moto nje ye hema langu kwa dhamira ya kutishia wanyama wakali waliozowea kutembelea makambi yetu hasa nyakati za usiku. Ulipofika wakati wa kulala niliweka bunduki yangu kando ya kitanda na kujilaza chali na huku nikijiambia kuwa nisingeruhusu usingizi unichukue.

Usingizi ulinichukua. Tena ule wa pono.

Nadhani nililala kwa masaa manne au matano kabla ya kuzinduka ghafla kwa hisia ambazo sikufahamu zilitokana na nini. Nilihisi kuwepo kwa mtu au kitu cha ziada hemani humo. Nikafumba macho na kutazama kwa makini huku mkono wangu ukiwa tayari kuichukua bunduki yangu.

Kweli kulikuwa na kitu. Hapana, mtu! Kwa nuru ndogo iliyotokana na moto uliokuwa ukiendelea kuwaka pale nje,

niliweza kuona kiwiliwili cha binadamu kikipenya kimyakimya, kama mzimu, kunifuata kitandani. Niliinuka mara moja na kusimama huku nikianza kuinua bunduki yangu

“Shhhh! Hapana kelele,” ilinong’ona sauti ya mtu huyo. Ilikuwa sauti ya kike! Sauti ya yule msichana aliyetoka hemani humu asubuhi hii.

“Kuna ni...” Nilijaribu kumuuliza. Lakini kwa mara nyingine alinizuia kuzungumza, safari hii kwa kuniziba mdomo kwa kiganja chake cha mkono wenye baridi.. Kitendo kilichofuatiwa na sauti yake ya mnong’ono vilevile ikisema, “Haraka... Ondoka. Wanakuja kukuua.”

“Nani?” Nilinong’ona kama yeye.

“Morani. Wanakuja...” Hata kabla hajamaliza kunifafanulia. Nilisikia hatua za watu wanaotembea kulifuata hema. Nilipochungulia nje, niliona viwiliwili vya miili ya watu wapatao ishirini, silaha mkononi, wakitembea kulifata hema langu.

“Kimbia!” Alisema akinisukuma kutoka nje.

“Wewe?”

“Acha mimi... nitakufa... peke yangu. Wewe hapana.” alinong’ona.

Sikuafikiana naye. Nilimshika na kumvuta mkono kutoka naye nje, huku tukiwa tumeinama. Nje ya hema tulinyata taratibu kuelekea upande wa pili, kulikokuwa na vichaka na miti miwili mitatu.

Hata kabla hatujafikia vificho hivyo, Morani walikwishafika kwenye hema na kulizingira. Walipita huko na huko wakikagua hema baada ya hema. Walipobaini kuwa mahema yote hayakuwa na watu, waliutumia moto niliouwasha mwenyewe kuteketeza mahema yote. Walifanya

hivyo huku wakiimba nyimbo za kivita au za ushindi, wengine wakirukaruka juu kama waliopagawa.

Bila ya msichana yule kunishikilia, ningeweza kurudi waliko ili kupambana nao. Moto, ambao niliushuhudia ukiteketeza mahema hayo, kwangu ulikuwa pia ukiteketeza ndoto na matumaini yangu ya maisha.

Achilia mbali vitabu na nyaraka zangu binafsi, nyaraka zote za Dakta Leakey na mkewe, baadhi ya vifaa vyake katika shughuli zake za utafiti na kumbukumbu mbalimbali za muhimu zilizotafunwa na moto huo. Kama mchezo wa kuigiza. Ilikuwa dhahiri kuwa nisingeweza kuwa naye, kwani nisingeweza kumweleza chochote ambacho angekielewa.

Nadhani nilitokwa na machozi kama mtoto. Nadhani miguu yangu iliishiwa nguvu, kwani nilijikuta nimeketi chini huku mikono ya msichana huyo mdogo ikiwa imenikumbatia kwa namna ya kunifariji. Yeye pia alikuwa akilia. Bila shaka akijiona chanzo cha mkasa huu mzito katika maisha yangu.

Nilimtazama, mara nikajikuta nikimuonea huruma badala ya kujionea huruma mimi mwenyewe. Nilimwona katika nuru tofauti. Si kama msichana aliyekimbia tohara bali shetani au malaika aliyetumwa kuvuruga maisha na matarajio yangu kama ilivyokuwa ada katika maisha yangu. Nikainuka na kisha kumwinua.

Aliinuka kwa taabu.

“Twende!” Nilimwambia.

“Wapi?” Alinong’ona kwa sauti yenye kwikwi .

Wapi! Nilijiuliza vilevile. Ndio kwanza ikanipambazukia kuwa toka muda huo sikuwa na mahala pa kwenda. Nilikuwa nimerudi nilipoanzia; Mtu wa kutangatanga kama ndege asiye na makao maalum.

Niende wapi? Nilijiuliza tena. Ningeweza kwenda polisi kutoa taarifa ili Morani wale watafutwe na kuadhibiwa, lakini hilo lisingesaidia. Ni vigumu sana kuwapata Morani katika uwanda huo mpana. Kesho wanaweza kutorokea Arusha, kesho kutwa wakawa Kenya. Zaidi ya hayo sikuona vipi adhabu hiyo ingeweza kunisaidia. Kamwe isingerudisha chochote kati ya yote yaliyoteketea.

Nilimvuta taratibu kuelekea nje ya eneo hilo. Tulitembea taratibu, tukikurupusha wanyama hapa na pale hadi tulipofikia mti mmoja mkubwa. Msichana yule alininong'oneza jambo akielekeza kidole chake kwenye mti ule. "Unasemaje?" Nilimhoji.

"Jana nashinda juu ya mti ule. Nalala juu yake hadi nasikia ngoma ya vita. Nakuja ita wewe," alisema

Nilimwelewa, nikawa nimepata jibu la swali lililokuwa likinisumbua, la kutaka kufahamu alijuaje kuwa ndugu zake walikusudia kunidhuru. Ukiwa juu ya mti huo mkubwa, unaweza kuona hadi mbali. Na ukiwa msikivu, unayezifahamu mila zako, hutashindwa kujua ngoma inayopigwa kwa mbali inaashiria nini.

Alinishauri tulale juu ya mti ule.

Nikaafiki.

Tulipata tawi kubwa, lililofanya tuketi bila hofu kubwa ya kuanguka. Kwa ajili ya baridi kali, usiku huo, pengine na hofu ya uzito wa matukio, binti huyo aliniegemea kifuari, usingizi ukamchukua. Joto lake na uwepo wake ulinifariji. Lakini sikuweza kupata usingizi. Jogoo wa kwanza alipoanza kuwika, nilimuamsha taratibu. Aliamka kiasi akishikwa na aibu kwa jinsi alivyonikumbatia. Mimi sikuwa huko. Akili zangu zilikuwa mbali maili nyingi nje ya eneo hilo.

“Nadhani nianze safari ya kuondoka.” Nilimwambia.

“Wewe nakwenda wapi?” aliniuliza akifikicha macho yake kutoa usingizi.

“Sijui ninakokwenda lakini sihitaji kukaa hapa. Nitakwenda popote.”

Alinitazama kwa makini kabla hajatamka taratibu, “Nakwenda na wewe.”

“Unakwedna na mimi! Wapi?”

“Sijui. Popote nakwenda wewe mimi nakwenda,” alisema.

“Mimi sijui nakwenda wapi.” Nilimwambia.

“Hata mimi yenyewe sijui. Nabaki hapa itaniua. Wewe nasaidia mimi. Hapana acha iniue.”

Niliishiwa nguvu. Nikaduwa

Jogoo wa pili walianza kuwika. Sikutaka alfajiri inikute hapo. Nikashuka kwenye mti na kuanza safari. Msichana wa Kimasai alishuka na kunifuata.

SURA YA KUMI NA SITA

Na ‘Mzigo’ Wangu Hadi Singida

Kuna fasihi simulizi nyingi nchini ambazo zamani nilidhani zilikusudiwa kumsisimua msikilizaji wake peke yake. Nyingi kati ya hizo ziliwalenga watoto. Baadhi zilikuwa hadithi za kulisimua au kutisha sana kiasi cha kuwatoa machozi wasikilizaji wake, wengine zikiwakosesha usingizi.

Moja ya hadithi hizi ni zile za kubeba ‘mzigo’ ambao mhusika alishindwa kuutua kwa urahisi, kwa mfano, kuna ile inayosimulia kijana ambaye alikuwa akitembea porini peke yake. Kwamba alifika mahala penye mto ambao alitakiwa kuuvuka. Kando ya mto huo alikuta msichana mdogo, mzuri sana aliyetaka kuvuka vilevile lakini alikuwa akiogopa mkondo mkali wa mto huo. Hivyo alipomwona kijana huyo msichana aliangua kilio akimsihi amsaidie kuvuka. Kwa huruma zake, kijana alikubali. Akambeba binti huyo mgongoni na kuogelea naye hadi upande wa pili ambako alijaribu kumtua. Lakini msichana huyo alikataa. Alipotanabahi kijana huyo alibaini kuwa alibeba kikongwe ambacho kilimng’ang’ania mgongoni usiku na mchana hadi mvulana akakosa nguvu.

Nyingine inayofanana na hiyo, ni ile ya mvulana mwingine aliyekuwa akivuka mto vilevile. Yeye alielezewa

kukuta kikongwe kikilia kando ya mto huo kikiomba msaada wa kuvushwa. Kilikuwa kibibi kichafu kinachonuka na kutoa tongotongo na kamasi muda wote. Mhusika alikihurumia. Akakitia mgongoni na kukivusha. Kinyume na mhusika wa kwanza, huyu mara tu alipokitua, alibaini kuwa kikongwe kile kilikuwa msichana mrembo sana, mwenye uwezo wa *kimalaika*. Walipendana, wakaoana. Maisha ya mvulana huyo yakiwa yamebadilika toka kwenye ufukara na kuwa tajiri na mtu maarufu sana nchini kwao.

Awali sikupata kufikiria uzito wa falsafa iliyokuwemo katika simulizi hizo. Sasa nikiwa na matukio yale, nilizichukulia kwa uzito unaostahili. Tatizo ni kutokujua nilikuwa katika nafasi ipi kati ya wahusika wale wawili.

Hayo yalipita akilini mwangu baada ya kumtazama kwa mara nyingine yuleyule msichana wa Kimasai aliyeniganda kama kupe. Jitihada zangu zote za kumwacha ashike hamsini zake nami nishike zangu hazikupata kuzaa matunda. Nilijaribu kumtelekeza hapa na pale lakini machozi yalimtoka na macho yake yenye huruma aliyonikazia yalinipokonya ujasiri. Hali iliyopelekea nijikute nikipanda naye lori la kwanza lililopita barabarani alfajiri hiyo

“Mnakwenda wapi?” Dereva aliniuliza.

Sikuwa na pa kwenda. Nilichohitaji ni kuondoka eneo hilo kuelekea popote. Sikuwa tayari kuwaona wale vijana wa Kimasai tena. Kwani kama wasingeniua mimi ningewaua wao au mmoja wao.

Pia sikuwa tayari kutazamana na akina Leakey macho kwa macho, iwapo wangerejea ghafla kutokana na hasara niliyowatia.

“Wapi?” Dereva alihimiza.

“Kwani nyie mnakwenda wapi?”

“Singida, kupitia Babati,” Sikuhitaji kumjibu. Niliparamia gari lake. Msichana alifanya hivyohivyo. Tukaondoka. Tulipumzika kwa muda. Nilitumia mapumziko hayo kumvuta kando na kumtaka abakie hapo na kuwatafuta ndugu zake wengine. Alikataa katakata kwa maelezo kuwa toka alipokataa tohara tayari amekataa ndugu wote hivyo hana mahala pa kwenda.

“Kwan nini usikubali kupata tohara?” Nilimhoji.

“Naogopa.” Lilikuwa jibu lake.

“Unaogopa?”

“Kufa. Mwenzangu alikufa jusi tu.” Alisisitiza.

“Lakini mimi sina pa kukupeleka. Mwenyewe sijui nitakwenda wapi, nitalala wapi. Huoni kuwa unanipa mzigo juu ya mzigo?” Nilijaribu kumshawishi. Badala ya kunielewa aliangua kilio. Kwa mara nyingine ushujaa ulinitoka, ubinadamu ukachukua mkondo wake.

Kwa bahati nzuri nilikuwa na tabia ya kutembea na akiba yangu yote ya fedha mfukoni, isipokuwa zile zilizokuwa benki peke yake. Hivyo, mkasa huo ulinikuta nikiwa na vijisenti ambavyo vingeweza kuniweka hai kwa wiki mbili tatu kabla ya kuanza kutaabika kwa njaa. Nilitumia sehemu ya senti hizo kulipia nauli na kula chakula cha mchana kabla ya kuanza tena safari ya Singinda.

Mzee mmoja tuliye kuwa naye safarini humo. Nadhani alisoma sura yangu iliyojaa mashaka na ule uso wa Kimasai uliolowa machozi. Aliniuliza kulikoni. Nilihitaji sana ushauri hivyo sikusita kumsimulia kila kitu, toka mwanzo hadi mwisho wa mkasa. Kwa mshangao wangu nilimwona akiangua kicheko baada ya kunipa pole.

“Sioni kama kuna jambo la kuchekesha hapo,” nilimwambia kwa sauti ndogo iliyoficha hasira zangu dhidi ya kitendo chake hicho.

Mzee alinishika bega kabla ya kuninong’oneza ili msichana yule asisikie. “Nacheka kwa kuwa unasumbuliwa na jambo dogo sana,” alinieleza.

Sikumwelewa. “Dogo kivi? Mtoto wa watu hana pa kwenda kwa sababu ya uzembe wangu. Mimi mwenyewe sina pa kwenda kwa sababu ya uzembe uleule. Unaliita jambo dogo?” nilimwuliza.

“Dogo sana.” Alisema. “Nitakusaidia mara tutakapofika Singida. Naitwa Kingu. Halfan Kingu. Kwa hilo ondoa wasiwasi mwanangu.”

Nilishusha pumzi. Kwa muda nilisahau matatizo yangu na kuifurahia safari kwa kuyaruhusu macho yangu kuburudishwa na mandhari mbalimbali za mazingira kando mwa barabara hiyo. Mbuga pana zilizojaa ndege na wanyama ainaaina zilitulaki, majabali yaliyosimama katika maumbile ya kulisimua yalitushangaza, majangwa yasiyo na msitu wala nyasi nayo yalikuwa sehemu ya mazingira hayo.

Tulifika Singida jioni sana. Wakati huo tayari roho yangu ikiimba tenzi na mashahiri juu ya Singida niliyoifahamu kupitia simulizi za kihistoria na maandishi ya vitabuni.

Kwa mfano, nilipata kusoma juu ya reli iliyojengwa enzi za vita kuu inayounganisha mji huo na reli ya kati kupitia Manyoni. Leo nilikuwa nimepata fursa ya kuiona kwa macho yangu mwenyewe reli hiyo.

Singida, nchi ya mwanamke pekee shujaa katika historia ya mapambano ya Watanganyika dhidi ya ujio wa wakoloni. Mwanamke huyu Leti Kidanka, kati ya mwaka 1903

hadi 1907 aliongoza majeshi ya Wanyaturu kupambana na yale ya Wajerumani hata wakaelekea kusalimu amri. Kama isingekuwa kwa ajili ya silaha zao kali na nyingi Wajerumani wale wasingefanikiwa kumkamata, wakamchinja na kuondoka na kichwa chake kama walivyofanya kwa Mkwawa.

Niliweza kuyaona majengo ya kale, boma la kilimatinde walilojenga Wajerumani hao kati ya mwaka 1880 na 1890 na lile la mkoloni lililojengwa 1900 hadi 1911. Boma ambalo lilikuwa makao makuu, ofisi, gereza, makazi ya maafisa wao na eneo la kunyongea watu. Nilishangaa kuona mti uliokuwa ukitumika kunyongea watu toka enzi zile ukiwa hai hadi leo.

Mzee Kingu ambaye tulifuatana naye katika safari hiyo ya mjini baada ya kuhusika kwenye gari alitabasamu kila aliponiona nikivutiwa na hiki au kile.

“Laiti ungefika Iramba,” alisema na kuongeza “Kuna vivutio tele ambavyo kwa udadisi wako vingekusisimua sana. Kuna mapango kama yale ya Kondoa Irangi na majabali yaliyoubwa kwa namna ya binadamu,” alisema.

“Unaifahamu Sodoma na Gomora?” Aliniuliza ghafla.

“Naam. Imesimuliwa katika Biblia na Koran,” nilimjibu.

“Unafahamu chochote juu ya mwanamke aliyegeuka mwamba wa chumvi baada ya kugeuka nyuma kuutazama mji wa Sodoma ukiteketea kinyume cha maelekezo waliyopewa?”

Hili pia nililifahamu, “Mke wa Lutu sio?”

Mzee Kingu alitikisa kichwa kuafikiana nami. “Kwa taarifa yako sanamu ya mwanamke yule aliyeganda na kugeuka nguzo ya chumvi iko huku kwetu. Ukienda Iramba, uingie maporini utaikuta. Na chumvi inapatikana hadi leo kama ilivyoandikwa,” aliongeza.

“Wewe ulipata kuiona?” Nilimuuliza.

“Sijapata lakini wazazi wangu walinihakikishia. Wao walikuwa wakienda huko katika safari zao za uwindaji.”

Sikuweza kumkubalia wala kumkatalia. Tulikuwa tukitembea mjini. Yeye mbele, mimi kati, msichana wa Kimasai nyuma. Ilikuwa safari iliyobuniwa na mzee huyo kwa maelekezo kuwa ni ya kunisaidia. Hata hivyo, alikuwa hajaniambia tunakwenda wapi.

Vivutio vya mji wa Singida havikuwa na mwisho. Maziwa yaliyojikita katikati ya mji, Singidani na Kindai ni miongoni mwa mambo ambayo yasingekosa kumvutia mgeni yeyote. Sehemu fulani tuliwaona wavuzi wakitafuta riziki zao katika maziwa hayo, huku ndege kama bata maji na yangeyange nao wakijishughulisha na yao.

Safari yetu iliishia mbele ya jengo moja lililokuwa na maandishi yaliyosomeka EVANGELICAL LUTHERAN AUGUSTANA SYNOD. Kingu aliniambia kuwa hiki kilikuwa kitengo cha kanisa ambacho kilijishughulisha na kusomesha watoto yatima na wale wasiojiweza. Aliniambia kuwa wasingesita kumpokea msichana huyo na kumlea, hasa baada ya kuonyesha msimamo wake wa kupingana na mila potofu za jamii yake.

Nilimweleza hivyo msichana yule. Nilishukuru kuona akiipokea habari hiyo kwa utulivu. Tulikaribishwa ndani. Mtumishi aliyetupokea hakushangazwa na maelezo yetu hata kidogo. Alimshika msichana yule mkono kwa dalili zote za upendo kabla ya kumwuliza umri wake.

Hakujua ana miaka mingapi. Kwa kukadiria kwangu hakuzidi miaka kumi na miwili. Mchungaji wao hakuwepo. Hivyo alitutaka mimi na Kingu kuondoka kwa maelezo kuwa msichana huyo alikuwa katika mikono salama.

Tuliinuka. Nilishangaa kuona msichana huyo naye akiinuka na kunifuata. Nilimtazama kwa macho makali yenye maswali mia moja na moja. Hata hivyo, nilipumua pale nilipomuona akitabasamu na kisha kusema kwa kiswahili chake kibovu, “Taka kushukuru. Yenyewe imeokoa maisha yangu.”

Alinikumbatia. Machozi yakimlengalenga machoni.

Kitendo chake kiligusa ile sehemu laini katika moyo wangu. Mie pia nilihisi machozi yakinilengalenga. “Hapana ni wewe uliyeokoa maisha yangu,” nilimwambia. Ulikuwa ukweli toka katikati ya moyo wangu.

“Hapana kweli... mimi haribu maisha yako,” alijitetea.

Sikutaka kuendelea na mjadala huo. Hivyo nilijikwanyua taratibu toka katika mikono yake na kuanza kuondoka, huku nikijitahidi kuyaepuka macho yake.

Hutaki kujua hata jina langu? Nilihisi swali hili katika macho yake. Nikajikuta nikitokwa na swali hilo.

“Mimi naitwa Nashifa,” alisema.

“Vizuri sana Nashifa. Mimi naitwa Petro. Petro Kionambali,”

* * *

Kuutua ‘mzigo’ ilikuwa mwisho wa tatizo moja. Tatizo la pili, langu binafsi lilikuwa palepale. Sikujua usiku huo na siku zinazofuata ningekitua wapi kichwa changu wakati nikianza upya kufikiria hatma ya maisha yangu, baada ya miaka kadhaa ya kuzungukwa na akina Leakey katika Bonde la Ufa na miji au vijiji vya jirani.

Nadhani kwa mara nyingine Kingu aliweza kuusoma moyo wangu. Ni pale nilipomsikia akianza kujinadi ghafa

kwamba anatoka katika ukoo unaoheshimika na usio na njaa. “Wanyaturu wote wananifahamu. Natoka katika ukoo wa Machifu. Huyu unayemsikia Chifu Said Gwao mdogo wangu upande wa baba. Kwangu utalala, utakula bila wasiwasi wowote.”

Nikashtuka. “Hayo yametokea wapi tena?” nilimwuliza.

“Naona unasumbua kichwa chako kufikiri leo utalala wapi,” alinijibu. “Hilo achana nalo kabisa mwanangu. Fikiria mengine.”

Nilimtumbulia macho ya mshangao uliochanganyika na aibu. “Nisingependa kukusumbua zaidi. Tayari umenisaidia sana. Kunipatia makazi ya yule msichana lilikuwa tatizo langu kubwa. Mengine sioni kama yatanisumbua,” nilimweleza.

“Huwezi kulala nje. Huwezi kutupa pesa katika vyumba vya wageni kwa ajili ya kulala tu. Utakuwa mgeni wangu. Leo, kesho na keshokutwa. Utakaa hadi hapo utakapoamua vinginevyo.”

Sauti yake iliashiria kufunga mjadala. Akiwa mtu mwenye umri mkubwa, bila shaka zaidi ya baba yangu, ingawa hakumpata babu, nililazimika kumsikiliza. Tukaongozana kuelekea kwake. Yeye mbele mimi nyuma.

Mzee Kingu alikuwa akiishi nje kidogo ya mji. Kauli yake kuwa hakuwa mtu mwenye njaa ilidhihirika mara tulipofika nyumbani kwake. Kwa kweli haikuwa nyumba bali majumba. Alikuwa na kijiji! Nyumba kama nane hivi, zikiwa katikati ya shamba la ekari zipatazo tano au zaidi, za matama na alizeti. Tatu zilikuwa nyumba za wake zake, nne za wanawe na moja niliyoambiwa kuwa ilikuwa maalumu kwa ajili ya wageni. Pembeni alikuwa na zizi kubwa la mifugo. Milio ya ng’ombe na mbuzi ilisikika.

Tofauti na alivyokuwa safarini, mcheshi na mzungumzaji sana, hapa nyumbani alikuwa mtu mwingine kabisa. Tulifika yapata saa mbili za usiku. Mji huo ulikuwa umechangamka kwa kelele za watoto, sauti za redio na pilikapilika za akina mama. Hali ambayo ilibadilika mara mzee alipotia mguu katika himaya hiyo. Wajukuu walipunguza kelele, kila mmoja akirejea kwa mama yake. Watoto walimfuata na kumsalimu, lakini katika hali ambayo haikuwa tofauti sana na salamu za askari na afande wake. Walibadilishana maneno mawili matatu, ya juujuu, kabla ya watoto hao kuteleza kila mtu akienda anakokufahamu. Hali haikuwa tofauti sana na wake zake wadogo. Ni mke mkubwa pekee ambaye baada ya kumsalimu aliketi na kumwuliza habari za safari. Hata hivyo, baada ya dakika moja tu yeye pia alijikuta hana cha kuzungumza. Aliketi pale kwa utulivu kama anayesubiri amri, ambazo zilianza kumiminika mara moja.

“Huyu ni mgeni wangu. Chumba chake kimeandaliwa?”

“Wale ng’ombe wawili wagonjwa wamepatiwa dawa?”

“Nina mashaka kama mmekumbuka kurekebisha lile ghala linalovuja...”

Mkewe ambaye tayari alikuwa mama wa makamo alijibu kila swali kwa ufupi na umakini mkubwa kama mwanafunzi kwa mwalimu wake.

Muda mfupi baadaye chakula kililetwa. Hakikuwa chakula cha watu wawili wala watatu. Ulikuwa mlo ambao watu sita wangeweza kula na kusaza. Ulikuwepo mguu wa mbuzi wa kuchoma, kuku wawili waliopikwa, sinia kubwa la wali na bakuli la matunda. Wakati mimi niliishia kula mapaja mawili ya kuku na wali kidogo mzee Kingu alitekeleza robo tatu ya chakula kile. Alikula nusu ya matunda na kushushia kwa birika zima la maji.

“Endelea kula.” Alinihimiza “Mimi nimechoka. Unajua utu uzima tena! Watakuonyesha sehemu ya kulala,” alisema akiondoka bila kusubiri shukrani zangu.

Mie pia uchovu ulikuwa umenishika. Hivyo, mara alipoondoka nilinawa mikono, nikamshukuru bi mkubwa ambaye muda wote alikuwa pale. Kisha niliomba nielekezwe yalipo malazi yangu. Mvulana mmoja alinipeleka kwenye nyumba ya wageni. kiasi ilijitenga na nyumba nyingine na hivyo kutoa uhuru wa kutosha kwa wageni. Taa ya chemli ilikuwa ikiwaka chumbani, kando ya kitanda kilichotandikwa kwa blanketi na shuka mbili safi. Mara tu kijana huyo alipotoka nilivua nguo zangu na nikafunga mlango na kisha kujibwaga kitandani.

Mkesha wa siku hiyo, uchovu wa safari ya miguu na gari pamoja na purukushani za siku nzima vilifanya usingizi unichukue mara tu nilipokitua kichwa changu juu ya mto. Ulikuwa usingizi wa pono. Nililala hadi saa tisa au kumi za alfajiri nilipoamshwa na kitu fulani. Sikufahamu ni kitu gani lakini hisia zilifanya nishuku jambo. Sina tabia ya kukoroma, bado niliamini kuwa nilijisikia kama nakoroma usingizini. Nilitulia kimya nikijaribu kufikiri kitu gani kiliniamsha. Sikuelewa. Wakati usingizi ukianza tena kunichukua hisia zilezile za kukoroma zilinireja. Hapa, hazikuwa hisia. Ilikuwa sauti halisi ya kukoroma tena ikitoka chini ya kitanda.

Nilishuka toka kitandani, nikapandisha mwanga wa taa na kuchungulia uvunguni. Nilishangaa kuona kitu kama tochi mbili zikininmulika toka chumbani humo. Tukio ambalo lilifuatiwa na mguno mzito kama ule wa mbwa anayehisi kuhatarishiwa uhai wake.

“Fisi!”

Niliripoka baada ya kutazama vizuri. Fisi mkubwa kabisa alikuwa amelala uvunguni humo, chini ya kitanda changu! Nilitetemeka. Nikaruka kuendea nguo zangu ambazo nilivaa harakaharaka na kutoka mbio.

Mbio ambazo ziliishia mbele ya nyumba ambamo nilimuona mzee Kingu akiingia kulala. Kabla hata sijagonga niliona mlango ukifunguliwa, mzee akiwa amevaa kikoi, kifua wazi. Alitoka. “Kuna nini?” alihoji kwa sauti kali kidogo.

“Fisi yuko chumbani kwangu.” Nilimjibu.

Mzee akaangua kicheko. “Hilo tu?” alinihoji baadaye. “Yule pale hana neno. Zaidi anakulinda kama anavyoulinda mji huu.”

Sikumwelewa. “Hana madhara! Kwa hiyo nikalale na fisi?”

Mzee alicheka tena. Kisha akasema, “Kumbe wewe bado mtoto mdogo sana sio? Unadhani himaya hii utailinda vipi bila kuwa na vitu kama vile? Yule amefugwa. Anatii amri zangu zote na hafanyi jambo lolote bila maagizo yangu. Isitoshe ni mtumishi mzuri anayebeba mzigo na hata kunibeba mimi mwenyewe katika safari zangu za usiku.”

Nilizidi kuchanganyikiwa. *Nazungumza na binadamu au shetani? Anazungumzia kufuga fisi kama kufuga mbwa!*

“Binadamu anawezaje kumfuga mnyama kama yule?” nilimwuliza bila kutarajia.

Na bila kutarajia vilevile alinijibu. “Ujuzi tu mdogo wangu. Nyie mnaita uchawi lakini ni ujuzi. Ukipata jino la fisi unaweza kumfuga fisi. Ukipata la mamba unaweza kummiliki mamba. Vivo hivyo kwa simba, chui na hata nyoka. Watu wanawafuga binadamu wenzao washindwe kumfuga mnyama?” alisema. Sasa nilikuwa na hakika kuwa sizungumzi na binadamu

wa kawaida. Sikuona kama nilihitaji kuendelea kumsikiliza. Alizisoma hisia zangu. “Nenda kalale,” akaniamuru.

Nikageuka kuondoka. Mara akaniita tena, “Kijana,” alisema. “Kitu kimoja kinanisumbua. Umekula nini wewe?”

“Nimekula nini? Una maana gani?” sikumwelewa.

Maana wenzako wote hulala na fisi wangu hata kwa mwezi bila kumwona wala kumsikia. Wewe umetafuna nini?”

Sikumjibu. Niliondoka. Wala sikurudi kwenye banda lake la kuchangia na fisi. Nilipitiliza kuifuata njia iliyonifikisha katika mji huo. Nilitembea taratibu hadi mjini. Alfajiri ilinikuta nikipitapita katika mitaa ya mji huo. Jua lilipochochoza lilinikuta nimeketi kando ya ziwa Singidani nikitazama pilikapilika za wavuvi.

Sikuwa na wazo jingine zaidi ya kutafuta gari litakalonipeleka kokote kwenye usalama. Sikuwa tena na hamu ya kuendelea kuvinjari Singida.

Niliuliza mahala wanapopandia magari ya kwenda mikoani, nikaonyeshwa. Sikusita kulipia nauli ya kwenda Kilimanjaro na kuianza safari mara moja.

SURA YA KUMI NA SABA

Kilimanjaro, Paa la Afrika

Nilikuwa nimesikia mengi ju ya Kilimanjaro, mlima mrefu kuliko wote barani Afrika. Hali kadhalika, nilisoma mengi na kutazama picha nyingi zilizoonyesha mlima huo. Lakini katika yote hayo niliyosikia au kuona kwenye picha hakukuwepo lolote lililoniacha nisiweze kupigwa na butwaa huku nikiwa siyaamini macho yangu pale nilipoutia machoni mlima huu. Kwa kweli, ni mlima ambao lazima uuone, kusimuliwa pekee kulikuwa hakutoshi.

Ilikuwa ndio kwanza nashuka toka katika basi lililonileta mjini hapo, macho yangu yalipopokelewa na utukufu ule. Ujio wangu Kilimanjaro ukiwa umefanyika bila matarajio baada ya yale mapokezi ya kutisha niliyoyapata Singida. Mapokezi ya kulazwa chumba kimoja na fisi.

Ni mawazo hayo yaliyofanya Singida kama nuksi nyingine iliyokuwa ikinisubiri. Hali iliyopelekea baada ya siku mbili tatu za kuzurula mjini hapo nipande basi lililonileta Kilimanjaro, kwa matarajio ya kupata kazi au biashara yoyote ambayo ingeniwezesha kupata chochote ili nitimize azma yangu ya kurudi nyumbani. Azma ambayo umuhimu wake uliongezeka siku baada ya siku.

Mlima ulisimama pale kwa kiburi na fahari zote. Ulikuwa

peke yake, ukiwa umechomoza hadi juu ya mawingu, kiasi cha kujionyesha vizuri popote uliposimama katika eneo la miji kama Moshi, arusha na vitongoji vyake. Ukiwa umepambwa kwa theluthi iliyokuwa ikimeremeta kileleni, Kilimanjaro ulisimama pale, peke yake, kama mfalme aliyevalia taji lake ambaye hakuwa na mpinzani. Hapana, alionekana zaidi kama malkia mwenye majivuno, aliyevalia mapambo yake yote, ambaye hakupenda kujichanganya na watu wengine. Sijui ningeukodolea macho kwa muda gani mlima huo kama nisingehisi kushikwa bega huku sauti ya mtu mmoja ikisema, “Angalia, yasije yakakukuta yaliyomkuta Rebmen kwa kuushangaa mlima huo.”

Nikazinduka. Nikayaondoa macho yangu toka kileleni na kumtazama msemaji. Alikuwa mpita njia tu, mvulana aliyevaa mavazi ya shule, mfuko wa madaftari yake ukiwa kwapani. Alikuwa akitabasamu.

“Rebmen gani?” nilimuuliza.

“John Rebmen. Yule Mjerumani aliyekuwa Mzungu wa kwanza kuutia machoni mlima huu,” alifafanua.

Nikalikumbuka jina hilo. Nikakumbuka pia tarehe na mwaka ambao Rebmen aliuona mlima huo kwa mara ya kwanza. Ilikuwa Mei 11, 1848.

“Rebmen alifanya nini?” niliuliza.

“Hukumbuki?” mwanafunzi huyo alinihoji. “Hukumbuki yaliyompata? Hukumbuki kuwa aliibiwa mfuko wake uliokuwa na fedha zake, nyaraka zake na kumbukumbu zote za safari yake? Ulivyokuwa umeduwaa pale wewe pia ungeweza kuporwa huo mfuko wako bila kujijua”

Nikacheke. Nilikumbuka kusoma tukio hilo kwenye kitabu cha mwandishi mmoja. Nadhani alikuwa Rebmen

mwenyewe aliyeandika. Kwamba akiwa Kilimanjaro, maeneo ya kibosh, aliibiwa mfuko wake uliokuwa na fedha zake zote na nyaraka zake zote muhimu. Siku hizi watani wa Wachaga, hasa Wapare, hulitumia tukio hilo kuwadhihaki Wachaga kuwa kwa ajili ya tukio lile Rebmen aliyekuwa mmisionari aliwalaani hata wakawa watu wa kupenda na kuabudu sana pesa kuliko utu. 'Mchaga mzuri ni aliyekufa tu,' ni moja ya kauli zinazoendana na utani huo.

Ingawa sikumbuki kama kweli Rebmen aliibiwa wakati akiushangaa mlima lakini bado nisingeweza kumlaumu. Kwa mtu kama yeye, aliyetoka mbali sana na ambaye hakupata kusikia wala kuona picha ya mlima huo kama mimi, kuduwa kiasi cha kuibiwa begi lake kamwe lisingekuwa jambo la ajabu. Kitendo cha ardhi kuchomoza hadi meta 5894 juu usawa wa bahari, huku ukiwa umesimama peke yako siyo jambo la kawaida. Aidha, ile theluji kileleni na historia ya milipuko ya volkano katika vilele vyake vitatu vya Kibo, Mawenzi na Shira ni sababu nyingine za kihistoria ambazo zitamfanya mtazamaji aukodolee macho hata kuweza kuporwa begi lake.

Hata hivyo, kauli ya mtoto yule wa shule ilinifanya nianze tena kutembea mitaani, begi mkononi, macho yakiwa hayakomi kurudi kwenye kilele cha mlima mara kwa mara.

Mji huu wa Moshi, ulio mbali kwa kilomita 580 toka Dar es Salaam na 76 toka Arusha, uko kilomita 890 toka usawa wa bahari. Hesabu ya watu wa mwaka 1948 ilionyesha kuwa mkoa mzima wa Kilimanjaro ulikuwa na idadi ya watu wapatao 267,700.

Hiyo ilikuwa sehemu ya akiba yangu ya kumbukumbu juu ya Kilimanjaro. Sehemu nyingine ilikuwa juu mkazi mkuu wa mkoa huo, Mchaga. Wakati watu wengi walifahamu

kuwa Wachaga ni kabila moja, linaloongea lugha moja, mimi nilikuwa na taarifa tofauti. Wakiishi kusini mwa mlima Kilimanjaro Wachaga ni mkusanyiko wa makabila mbalimbali, wanaozungumza lugha mbalimbali wakiwa wametoka katika maeneo mbalimbali kwa nyakati mbalimbali. Watu hawa, ambao kwa bahati wote ni wabantu, baadhi yao wanafananishwa na Wakamba wa Kenya kwa siha na lafudhi. Wengine wanafaninishwa na wataveta na hata watu wa Niger na Kongo. Wataalamu wanahisi watu hawa walivutwa na hali ya hewa, mbali na utajiri wa misitu kwenye mteremko wa mlima tangu karne ya kumi na saba. Hali iliyowawezesha kuwa wakulima wakubwa wa mibuni kama zao la biashara na migomba kwa ajili ya chakula.

Miongoni mwa makabila yanayounda Wachaga ni pamoja na Warombo, Wamachame, Wavunjo na Wamarangu. Inaaminika kuwa katika zama zile za kuhamia Kilimanjaro makabila haya, ambayo yalikuwa na falme tofauti kama zilivyo lugha na tamaduni zao walipigana vita mara kwa mara. Kabila jingine maarufu Kilimanjaro, Wapare, lilitumia fursa hiyo kwa manufaa yao kiuchumi. Inaaminika Wapare walikuwa wafua vyuma mashuhuri ambao koo mbalimbali za Wachaga ziliwategemea kuundiwa silaha mbalimbali kama mikuki mishale na mapanga kwa minajili ya kujipatia ushindi dhidi ya koo nyingine.

Nilijikumbusha hayo wakati nikitembea taratibu toka kituoni hapo nikifuata barabara ambayo sikuifahamu, wala sikuwa na haraka ya kuifahamu. Nilikuwa nimejikumbusha nguo zangu za kazi, kaptula na shati la kaki murua ya Marekani, viatu vizito vya dhoruba na soksi nyeusi. Nywele zangu, kama kawaida, zilikuwa fupi zilizochongwa vizuri. Nadhani

nilionekana mrefu kuliko watu wengi eneo hilo. Nadhani pia ngozi yangu ya maji ya kunde, usafi wa mwili wangu na utulivu wangu wakati nikivuta hatua moja baada ya nyingine kutoka kituoni hapo ni miongoni mwa vitu vilivyovutia macho ya wapita njia dhidi yangu. Niliona nikitazamwatazamwa kuliko kawaida, baadhi ya watu walinong'onezana huku vidole vikielekezwa kwangu.

Halafu likatokea jambo ambalo halikupata kutembelea fikra zangu. Kundi kubwa la kinamama liliibuka toka mahala fulani kituoni hapo na kunifuata mbio. Waliponifikia walianza kuimba huku wakipiga makofi na vigelegele.

Babaaa baba huyoo....

Babaa baba huyo.... Baba...

Sikuelewa. Nilisimama na kugeuka huku na huko nikitazama nani anapokelewa na kushangiliwa kiasi hicho.

Hakuwa mwingine zaidi yangu. Walikuwa tayari wamenizingira, mfuko wangu ukapokonywa na mama mmoja kuamua kuubebea yeye. Waliendelea kuimba.

“Karibu sana baba,” mmoja wao alisema huku akinikumbatia.

Nilizidi kuchanganyikiwa. *Ama wana wazimu ama mimi napata wazimu!* Niliwaza nikijaribu kujibabadua toka katika mikono ya mama huyo.

“Vipi... kuna nini?” nilijaribu kuuliza. Sikusikika. Kelele zilikuwa nyingi. Yule aliyenikumbatia kwanza aliwageukia wenzake na kuwaambia, “Mnaona? Niliwaambia ni mtu mwenye haya sana.” Akawageukia vijana wa kiume waliokuwa kando na kuwauliza, “Mbona hamchangamki? Mpokeeni kishujaa shujaa wetu.”

Kauli hiyo ilifuatiwa na vijana hao wa kiume kunivamia,

wawili kati yao wakaniinua na kunibeba juu wakiniongoza njia kunipeleka walikokujua. Katika maongezi yao nilisikia mmoja akisemea, “Nilidhani Nyerere ni jitu kubwa, linalotisha na kuwatetemesha wakoloni. Kumbe ni mtu wa kawaida...”

Ndipo nikaeleka. *Walikuwa wamenifananisha na Nyerere!*

Wakati huo vuguvugu la kudai uhuru likiwa linazidi kupamba moto majina ya akina Julius Nyerere, Oscara Kambona, Bibi Titi Mohamed na wengineo yalikuwa yametawala sana katika vyombo vya habari. Nyerere, ambaye wakati huo alikuwa mwalimu wa shule moja ya sekondari kule Tabora alifahamika zaidi kutokana na maandishi yake katika vyombo vya habari hasa magazeti akiwa msomi aliyefika hadi Makerere, Uganda. Nyerere aliwaandaa Watanganyika kujitawala. Alisema na alisikika sana.

Sikupata kufikiria kama ingetokea siku mimi, *Kiguu na Njia* nikapokelewa kwa heshima kiasi hicho. Hivyo, lazima nikiri kuwa kwa kiasi fulani nilifurahia nafasi hiyo ya kubebwa. Lakini pia, kwa ajili ya kelele na imani yao kuwa nina haya nilijua wasingeamini chochote ambacho ningewaambia. Nikaamua kutulia tuli juu ya mabega yao nikicheka kimoyomoyo.

Msafara huo uliishia katika nyumba moja ya wageni, mtaa wa tatu kutoka katika kituo hicho. Nilipelekwa moja kwa moja katika chumba maalum kilichoandaliwa kwa ajili ‘yangu’. Kilikuwa na bafu na choo chumbani humo. Mfuko wangu wa safari tayari uliwekwa juu ya meza, salama salimini. Yule mama aliyejipa uenyeji zaidi yangu alisema, “Baba, oga upumzike kidogo. Bibi Titi alifika jana. Nitamwarifu juu ya ujio wako, pengine mtapenda kuteta kidogo kabla ya kuanza safari ya Machame. Chifu Abdieli Shangai atakuwa tayari

amewasubiri.”

“Lakini mimi sio Nyerere,” nilimwonya. “Naitwa...” hakusubiri hata nitaje jina langu. Badala yake aliangua kicheko, akipuuza alichokichukulia kama mzaha wangu. Akatoka huku akiufunga mlango nyuma yake.

Sikuwa na jinsi. Nikaoga. Nikapaka mafuta na kuvuta zile nguo zangu za safari. Nikavaa suruali na shati safi. Nikatia tai na koti juu. Nilifanya hayo kwa uangalifu mkubwa bila kuchafua bafu wala kuvuruga kitanda ili mweye chumba chake halisi atakapotokea akikute kikiwa kisafi.

Wakati nikijiandaa kutoka, nikiwa na dhati ya kuwahakikishia kuwa mimi sikuwa Nyerere, mlango uligongwa nikaufungua. Bibi Titi Mohamed alikuwa pale. Sikuhitaji kutambulishwa. Alikuwa mwanamke mfupi, mnene, mwenye macho maangavu.

“Julius, umeruka kwa ndege? Nilidhani ungefika hapa jioni,” alisema kwa sauti yenye mamlaka. Sauti hiyo ilififia ghafla aliponitazama usoni na kubaini kuwa mimi sikuwa Julius Nyerere waliyekuwa wakimtegemea.

“Nimejitahidi sana kuwaambia mimi sio Nyerere, hawakukubali,” nilijitetea. “Ni kama nimetekwa nyara na kuletwa hapa,” niliongeza.

Bibi Titi aliangua kicheko. Aligeuka kuwatazama wenyeji wetu waliosimama nyuma yake kunisubiri. Kicheko chake kilizungumza kila kitu. Akageuka tena kunitazama, “Pole sana bwana. Ni kweli umefanana sana na mwalimu. Kwa mtu asiyemfahamu vizuri kuwafananisha si ajabu.”

Sikumjibu. Sikuwa na la kujibu zaidi ya kutabasamu.

“Ulikuwa ufikie wapi?” aliniuliza.

“Nilikuwa natafuta mahali pa kupanga.”

“Basi unaweza kulala hapa,” aliniambia. “Malaika wako amekwishakukuongoza hadi chumbani humu, huna sababu ya kupingana naye. Pumzika, baadaye tutakaa tuzungumze. Si ajabu mola kakuleta mikononi mwetu kwa sababu maalum.”

Sikuwa na sababu ya kukataa.

* * *

Kwa mujibu wa maelezo niliyoyapata baadaye, vuguvugu la wagombea uhuru nchini, chama cha TANU ambacho kilikuwa kimeanzishwa kutokana na TAA kulikuwa na matatizo katika kanda hiyo ya mashariki, hasa Kilimanjaro. Kwa mujibu wa maelezo hayo, matatizo hayo hayakuhusiana na chama kukubalika au kutokukubalika eneo hilo bali yalitokana na mvutano ndani ya Wachaga wenyewe.

Baada ya ule mvutano na mapigano ya makabila mbalimbali yanayounda Uchaga ulifika wakati pamoja na kukubaliana kuwa kitu kimoja. Uamuzi huo ulifuatiliwa na kumteua Mangi mkuu kama msimamizi na msemaji rasmi wa masuala ya Wachaga. Mangi mkuu huyu aliyekuwa na makao yake huko Marangu aliwekwa juu ya viongozi wengine wote wa kikabila.

Hata hivyo, ule mzimu wa chuki na kutokutamaniana miongoni mwao, ingawa ulizikwa, bado haukufa. Ni kama ulizikwa hai. Ujio wa Mjerumani, ambaye alifuata nyayo za mpelelezi wao Rebmen, ulifanyika Kilimanjaro iwe chaguo lao la awali, wakati machifu wengine wakisita kuwapokea. Mangi Sina wa Kibisho, miaka ya 1890 akiwa amejizatiti kiuchumi kwa kilimo na ufugaji, alikuwa pia ameimarisha jeshi lake ambalo lilikuwa kero kubwa kwa utawala wa wajerumani. Awali ya hapo Wajerumani hao, chini ya uongozi wa Karl

Peters, waliendesha utawala wa kinyama na ukatili mkubwa Kilimanjaro, hali iliyopelekea April 25, 1897 gavana huyo katili afukuzwe kazi na serikali yake.

Lakini miaka mitatu baadaye, Machi 2, 1890 Wajerumani hao waliwanyonga hadharani, mjini Moshi, viongozi tisa wa kikabila. Viongozi mashuhuri kati ya waliopoteza maisha siku hiyo wakiwa Mollelia wa Kibosho, Ngalami na Meli wa Moshi. Madai ya Wajerumani kwa kitendo hicho yakiwa kwamba viongozi hao walikuwa wakiwavurugia jitihada za uongozi wao Kilimanjaro.

Hivyo, mkataba ambao Mangi Rindi wa Chaga aliingia na Mjerumani miaka mitano kabla ya kitendo hicho cha kikatili, na kuufanya mji wa Moshi kuwa kituo kikubwa cha biashara ya ndovu na watumwa kati yake na Zanzibar, lilikuwa pigo jingine katika jitihada za kuifanya Kilimanjaro kuwa na sauti moja.

Ujio wa vuguvugu la kupigania uhuru kukawa kama msumari wa mwisho kwenye jeneza la jitihada hizo. Wakati huo tayari yakiwepo malumbano makubwa ya iwapo kulikuwa na uhalali na haja ya Mangi mkuu kuendelea kutoka katika ukoo na kabila moja na cheo hicho kiende kwa kupokezana au la. Mangi mkuu, wakati huo Chifu, Thomas Mareale na kambi yake walishikilia msimamo wao. Kwa upande mwingine, machifu kama Abdiel Shangali walilipinga hilo kwa vitendo. Wasomi wengi wakiwa nyuma yake, Shangali alitumia fursa hiyo ya mparanganyiko kuunga mkono TANU na kuwekeza kimsimamo mikononi mwa mkewe Solomon Eliofoo, aliyekuwa ametokea masomoni Uingereza na Marekani na kurudi na kuazishwa tawi la TANU Machame.

Lilikuwa tatizo zito kwa Chifu Mareale. Jitihada zake za kuwekeza kwa Petro Njau hazikuzaa matunda yaliyotarajiwa, hali iliyopelekea uhusiano wake na TANU ulegelege. Ingawa yeye binafsi aliwasiliana sana na Nyerere na wakati fulani kumtaka aje Kilimanjaro kuzungumza na Machifu wote bado alionekana kama mtu aliyekuwa njia panda. Hali ambayo baadaye ilishusha umaarufu wake, lakini hadhi yake na nafasi yake katika historia kamwe haikupata kufutika.

Kwa upande mwingine, Kilimanjaro haikuwa na njaa sana ya uhuru kama zilivyokuwa sehemu nyingine za Tanganyika. Kiuchumi alikuwa mbali zaidi. Kilimo cha mibuni kilikuwa kimeanzishwa katika eneo hilo tangu mwaka 1919 na kushika kasi 1930 na kuendelea. Hali hiyo iliambatana na kuanzishwa kwa vyama vya ushirika, ikiwa nchi ya *Kwanza Afrika* kuwa na mfumo huo. Hali ya hewa na ujio wa mapema wa wakoloni katika maeneo hayo pia ilikuwa neema nyingine kwao. Walipata shule nyingi na bora zaidi mapema.

Huduma za matibabu, barabara na maji pia walizijua kabla ya maeneo mengi ya nchi kufikiriwa.

Hivyo, inaweza kueleweka pale ‘Mshumbue’ Mangi mkuu Thomas Lenana Mlangi Mareale II aliponukuliwa akishuku kuwa Nyerere ‘alikuwa akinikwepa,’ na kwamba alimsahau katika harakati za uhuru. Hata hivyo, Mangi mkuu huyu aliendesha harakati mbalimbali za kisiasa ndani na nje, ikiwa pamoja na kumlipa wakili ambaye alimtetea Kenyatta wa Kenya hadi akaachiwa toka kifungoni wakati akituhumiwa kujihusisha na Mau Mau.

“Hivyo, ni sehemu fupi ya historia ya uchagani kaka yangu,” Bibi Titi Mohamed alisema baada ya maelezo hayo ambayo niliyaunganisha na kujaribu kuyaweka katika mtiririko

mmoja baada ya huyu kusema hili, huyu lile nikijumuisha na yale yaliyokuwa katika kumbukumbu zangu.

Tulikuwa katika ukumbi wa hoteli hiyo. Watu wapatao wanane, wakiwemo wanawake watano, Bibi Titi na wawili wengine kati ya wale walionipokea pale kituo cha mabasi. Nilionekana kama muujiza. Nadhani hata kama angekuwa Nyerere mwenyewe hangepata idadi kubwa ya watu waliokuwa wakiingia na kutoka kwa nia ya kumwona ‘mtu aliyefanana na Nyerere’. Wingi wa watu hao wakiwa kina mama ambao walicheka na kujicheka sana kwa kosa la kunichanganya na kijana huyo aliyekuwa akitajwatajwa sana. Nadhani kwa namna fulani walidhibitiwa, kwani baadaye tuliketi na kuingia katika maongezi marefu, yaliyoongozwa zaidi na Bibi Titi, mwanamama msemaji sana, mwingi wa vichekesho huku akiwa pia msikilizaji mzuri.

“Wachaga wana historia tofauti na sehemu nyingi za nchi,” Bibi Titi aliongeza. “Sisi watu wa Pwani tuna historia inayotofautiana kwa kiasi kikubwa na wao. Nadhani wageni wengi waliotembelea makwetu toka enzi za enzi waliacha athari nyingi miongoni mwetu zaidi ya Uchagani ambako ni mbali kutokea Pwani.”

“Nadhani,” niliunga mkono. “Maana toka Waarabu, Wareno, Wajerumani na baadaye Waingereza wenyeji wao wa awali ni nyie tu.”

“Bibi Titi alitabasamu. “Tuyaache hayo,” alisema. “Hebu na wewe tuambie yako tukusikie. Ilikuwaje ukafananishwa na bwana Julius?” alinihoji.

“Kwa kweli sijui. Simjui Julius wala sijapata kumtia machoni labda imetokea tu tukafanana maana duniani wawili wawili,” nilimjibu.

“Huna udugu naye?”

“Hata kidogo.”

“Wewe ni Mzanaki?”

“Wala.”

“Kumbe nini basi.”

“Mie Muha. Natokea kigoma.”

Hufanani na Waha. Utakuwa Mmanyema.” Bibi Titi alidai. “Lakini hilo halina haja kwa sasa,” aliongeza. “Kama hutajali, tuambie wewe ni nani, unatokea wapi na unaelekea wapi.”

Nikawatajia jina langu. Nilitaja pia kazi niliyowahi kufanya ambayo sasa sikuwa nayo. Walivutiwa na taarifa ya safari za hapa na pale katika miji na vijiji mbalimbali vya Bonde la Ufa pamoja na mbuga za wanyama.

“Hujapata kufikiria kujiunga na harakati za kupigania uhuru?” Bibi Titi aliuliza. Akaongeza, “Maana wewe unaonekana ni mtu wa watu. Halafu, unatembea sana. Lakini la muhimu zaidi ni kwamba tungependa kupata mtu wa kwenda kuhamasisha harakati hizi huko kwenu. Ndiyo kuna watu tayari, lakini hawatoshi. Kumg’oa mkoloni siyo mchezo. Inahitajika kila silaha na kila askari.”

Wazo hilo halikupata kunitembelea akilini. Sikuwa na hakika kama mimi ni mtu wa kupanda jukwaani, mbele ya kadamnasi na kuanza kujinadi kuwa mimi ni bora zaidi ya wengine, au kumnadi mtu mwingine kwamba anafaa kuliko mwingine. Kwa ujumla sikupata kuwa na ndoto ya kuwa mwanasiasa maishani mwangu.

Bibi Titalisoma hayokatika machoyangu. Akatabasamu. “Ni jambo linalohitaji kulifikiria.” Alinena. “Harakati zetu bado ni changa. Hakuna fedha za kulipa mtu wala kulipwa. Kwa

ujumla tunajitolea. Tunachopigania ni uhuru. Ukipatikana kila mtu atakula matunda ya uhuru.”

Alisita, akaitazama saa yake. “Nadhani basi alilopanda Mwalimu linakaribia kufika. Nisingependa akina mama wakampokee mtu mwingine wa watu na watu. Naenda mwenyewe kumpokea. Atafikia hoteli hiihii. Nitakukutanisha naye, pamoja na Kambona, ili uzungumze nao. Nadhani utakuwa tayari umefanya uamuzi.”

Akainuka na kuondoka, alifuatana na wale kina mama wengine na wanaume wawili.

Nilibakia na watu wawili mmoja alikuwa mtu mfupi, mweupe, ambaye kama si kwa ajili ya mvi mbili tatu kichwani ungeweza kumfikiria kuwa ni mtoto mdogo, ingawa umri wake ulizidi wangu kwa mbali sana. Hakuonekana kuwa Mchaga. Na hakuchelewa kunithibitishia hilo pale alipozungumza na mara moja nikabaini lafudhi yake kuwa ya Kipare zaidi.

“Nikwelimimini Mpare,” alijibuswalilangu. “Nimeungana hawa watani wangu wajanjawanja, katika harakati hizi za kupigania uhuru. Tatizo ni hapo utakapopatikana huo uhuru. Mchaga atapenda kuuteka nyara uwe wake, maana Mchanga mzuri ni yule aliyekufa tu.” Alisema akimtazama Mchaga.

Yule Mchaga akachekeka. Yeye pia alinizidi umri. Alikuwa amevaa suti ya kijivu, tai shingoni na alishikilia mkoba wa nyaraka mkononi. Uso wake uliojaza ulipambwa na miwani. Hali iliyompa sura ya usomi.

“Achana na wajukuu wetu hao,” aliniambia. “Hao wameshindikana kabisa. Mpare anapata kesi ya kuku, ama kwa kuiba au kuibiwa. Atauza hata ng’ombe ili ashinde kesi hiyo. Kuna mtu hapo?”

Mie pia nililazimika kucheka.

Waliagiza vinywaji. Wao walikunywa bia mimi nilikunywa soda.

“Bia?” alihoji mmojawao.

“Sinywi.”

“Kwa nini? Unaumwa?”

“Hapana. Sijawahi kunywa toka nizaliwe.”

Walinitazama kwa mshangao kana kwamba nimewaambia jambo la ajabu kuliko yote waliyopata kuyasikia.

“Kwa umri huo?” Yule Mchaga aliuliza, “Huo ni umri wa kunywa vitu vya kiutu uzima.” Aliongeza.

“Tatizo ni kwamba sijapata kuitamani wala kuifiria. Halafu bei yake kubwa mara tatu kuliko soda.” Nilijitetea.

“Acha ubahili wa Kipare,” Mchaga alisema akicheka.

Mpare alicheka pia. Lakini aliamisha maongezi na kunitaka nimsimulie juu ya safari zangu za maporini. “Huko ulikokwenda kuna wanyama?”

“Wengi tu.” Nilimjibu “Unaweza kukutana na kundi la nyati wengi kama Ng’ombe wanaofugwa, kundi la twiga utadhani wako kwenye maonyesho na pundamilia kana kwamba wana sherehe.”

“Tembo?”

“Wengi kupita kiasi”

“Vifaru?”

“Wengi tu.”

“Umepata kuwaona kwa macho yako?”

“Mara nyingi tu.” Nilimjibu.

Mchaga alijaribu kuingilia kati, lakini Mpare alimkatisha kwa maswali yake juu ya wanyama na maeneo tuliyotembelea. Nilipomtajia kuyafahamu kwangu vyema maeneo ya Manyara, Ngorongoro na Tarangire alionekana kuvutiwa zaidi. Nilihisi

kuona dalili za udenda zikielekea kudondoka toka mdomoni mwake. Sikuwa na hakika kama niliona vizuri.

“Itabidi tuzungumze kama wanaume baadaye,” aliniambia. “Unatarajia kuondoka lini?”

“Sina haraka,” nilimjibu. “Nitapenda kufika Arusha pia kabla ya kurejea maporini,” niliongeza.

“Nitakupeleka.” Alidakia. “Mimi ni mwenyeji Arusha kuliko hapa Moshi. Hutohitaji kulala au kula hotelini.”

Mchaga aliangua kicheko cha dhihaka, kicheko kilichofuatiwa na “Ndugu yangu umekwisha. Mpare ajitolee kukupeleka Arusha, akupe malazi na chakula! Kuna jambo hapo,” alisema.

“Atakwisha yeye,” nilijibu, “Maana siye Wamanyema tuna historia ya kula watu. Nitamla mzimamzima kabla yeye hajanila,” kauli ambayo iliniangusha kicheko kirefu.

“Lakini Wapare unawajua vizuri? Wana maradhi yasiyo na dawa ya uchoyo. Wewe na yeye mtakufa njaa hata kabla hujafikiria kumla, huku mkiwa na fedha mfukoni,” aliongeza na hivyo kuongeza kicheko. Sikujua mengi juu ya Wapare zaidi ya ukweli kuwa ni kabila jingine kubwa la Kilimanjaro, wanaishi katika miteremko ya milima ambayo ni sehemu ya mlima Kilimanjaro, na kwamba wao pia wamegawanyika katika sehemu kuu mbili, Wapare wanaozungumza Kingweni, wanaoishi kaskazini na Wachasu waishio Usangi, Kusini. Lugha zao zina aina fulani ya kulandana na zile za Wataveta na Asu wa Kenya.

Enzi za kale Wapare walisifika kwa uganga wa mvua na uhunzi. Uhakika kuwa kabila hili ni la kale ni pale nilipowahi kuona kitabu kitakatifu cha Biblia iliyoandikwa kwa lugha ya Kipare, kilichochapishwa mwaka 1910. Pamoja na ujio huo

wa dini za kisasa Wapare waliendelea na tiba mbalimbali za asili kama maziwa ya Konda badala ya mama kumtibu mtoto mwenye *wintu*, maradhi ya sangasi yaliyoharibu vinywa vya watoto, majani yaliyoitwa more yaliyotibu ‘Kirumu,’ ‘kiruti’ au ‘kinyoka’, maradhi ya macho kwa watoto wadogo.

Historia ya dini za kigeni Upareni inaanza na mmisheni Jakob Janssen Dannholz, Mjerumani wa madhehebu ya kiluteri ambaye mwaka 1908 alianzisha ‘kazi ya bwana’ huko Mbagu, Upare ya kusini. Aliishi hapo hadi mwaka 1907 alipokamatwa na kuchukuliwa na Waingereza kama mfungwa wa kivita hadi katika kambi yao ya Misri ambako alifariki mwaka mmoja baadaye. Alifariki na umri wa miaka arobaini lakini kazi aliyoianzisha iliishi, ikakua na inaendelea kukua hadi leo.

Kinyume na makabila mengi nchini, wanawake wa Kipare walikuwa mstari wa mbele, pengine kuliko wanaume zao, katika harakati za kupigania uhuru na haki zao. Kumbukumbu zangu toka vitabuni zilinikumbusha mwaka 1946, kule Usangi, pale maelfu ya akina mama walipoibuka na kuanzisha vurumai kubwa wakipinga kulipa kodi. Tukio hilo liliibuka pale Chifu mmoja alipotembelewa na mkuu wa wilaya kwa ajili ya majadiliano. Umati wa wanawake wapatao mia tano waliizingira nyumba hiyo kutaka ufafanuzi juu ya utaratibu wa kodi ambao hawakuafikiana nao. Mkuu huyo alipojaribu kuondoka bila kuwapa ufafanuzi walipandwa na hasira, walianzisha nyimbo huku wengine wakiipiga mawe nyumba hiyo ya Chifu. Tukio hilo lilifuatiwa na maelfu ya wanawake kujiunga katika vuguvugu hilo ambalo lilitikisa serikali ya mkoloni.

Kama Wachaga, Wapare pia walikuwa katika mstari wa

mbele katika kuiunga mkono TAA na baadaye TANU katika mapambano ya kudai kujitawala. Hali hiyo inachukuliwa kuwa ilisaidia kuondoka wazo la kuibuka kwa chama cha kikabila ambacho kingeweza kuwa chini ya 'PARE UNISI' ambayo ilikuwa na nguvu nyingi kutokana na mchango wa kiuchumi iliyotokana na kilimo cha mibuni, katani na chai.

“Unasemaje?”

Mpare alinizindua. Nikamtazama.

“Naona uko mbali sana,” aliongeza. “Nilikuuliza unadhani tuondoke lini kwenda Arusha?”

“Nilikuambia sina haraka, kwani hatuonani tena baada ya leo?” nikamuuliza.

“Tutaonana. Bila shaka yoyote.”

Mara akina mama walikwenda stendi kumpokea mwalimu wakaanza kurudi, mmoja baada ya mwingine. Hawakuwa na furaha kama ile waliyoonyesha wakati wakinipokea mimi. Hatukuchelewa kuelewa sababu.

Mwalimu Nyerere hakutokea.

Mchaga aliyekuwa kimya muda mwingi, akishughulikia kinywaji chake alitabasamu kidogo akinitazama. Kisha akasema, “Maadam Nyerere hakuja, na wewe umefanana naye, tutaendelea kukuita Nyerere. Unasemaje?”

Sikumbuki kama nilimjibu.

SURA YA KUMI NA NANE

Pilikapilika Za Moshi Na Arusha

Moshi na Arusha ni miji jirani sana, ikiwa imetenganishwa kwa umbali wa kilometa 75 tu na hivyo kufanya safari toka mji huu hadi ule iwe takriban dakika sitini kwa gari lisilo na matatizo.

Safari ya Arusha na Moshi ni burudani tupu. Japo barabara haikuwa nzuri sana, lakini kule kupita katikati ya mashamba makubwa ya mibuni na migomba, vijiji vichache vikichomoza hapa na pale ilikuwa burudani ya macho. Ilikuwa alfajiri moja tulivu na angavu sana. Anga lilitakata pasi ya wingu lolote. Jua lililokuwa likichomoza Mashariki liliufanya mlima Kilimanjaro ambao tuliupa kisogo usimame pale, taji lake jeupe kichwani, juu ya kiwiliwili chake cha kijani, ukiwa umetuinamia kama mzimu au malaika aliyekuwa akitutakia heri katika safari yetu. Sikuchoka kugeuka mara kwa mara kuutazama uzuri huo wa pekee.

Hata kabla Kilimanjaro haujatokomea nyuma yetu, ulijitokeza mlima mwingine mbele yetu. Kama Kilimanjaro, ulisimama kando ya mji wa Arusha, kwa maringo na utukufu wa aina yake. Japo mbele ya Kilimanjaro mlima huu ulikuwa kama mtu na mdogo wake, bado utukufu wake ulikuwa palepale. Sikuhitaji kuambiwa kuwa huu ulikuwa mlima

Meru, fahari nyingine ya Tanzania. Ukiwa umepanda juu ya usawa wa bahari kwa mita 4565 mlima huu ulimwaga hewa safi yenye ubaridi mwanana uliopenya katika miili ya wakazi wa Arusha na vitongoji vyake hadi kuitikisa mifupa ya wageni wa mandhari hiyo.

“Naona tayari umeanza kumsahau mrembo mmoja umeanza kumtamani mrembo mwingine. Vipi, unafikiria kumpanda?”

Nikazinduka na kumtazama msemaji. Alikuwa rafiki yangu mpya, yule Mpare, ambaye toka tukio lile la mimi kufananishwa na Nyerere na kumsimulia kwa ufupi maisha yangu ya maporini aliniganda kama kupe. Siku zote tatu nilizokaa mjini Moshi alikuwa nami kama kuku na vifaranga vyake. Sikupata kujiuliza nani alikuwa kuku nani kifaranga kati yetu. Lakini ile tabia yake ya kuwa nami bega kwa bega, tukiachana wakati wa kulala, nikiamka tayari ananisubiri, nilianza kupata hisia pamoja na yeye kujifanya kuku ilielekea kuwa yeye ni kifaranga asiyetaka kumpoteza mama yake.

“Mrembo gani?... Kumpanda nani?” nilimuuliza kwa mshangao.

“Mrembo Kilimanjaro, dada mtu. Mara tu ulipomwona mdogo wake, Meru, tayari umehamishia mapenzi yako kwake. Hilo liko wazi katika macho yako. Ukipenda tunaweza kufanya mipango tuupande. Sio mrefu kama Kilimanjaro,” alijibu.

Niliyatafakari maneno yake kwa muda. “Kama ningepata fursa hiyo ningeitumia kupanda mama wa milima yote Afrika, mwenye sifa zote za pekee duniani, Kilimanjaro; ili nipate kitu cha kuwasimulia wajukuu zangu pale nitakapozeeka,” nilimweleza.

“Wajukuu! Uliniambia hujaoa.”

“Iko siku nitaoa. Nitapata watoto na baadaye wajukuu,” nilimjibu, jibu ambalo lilifanya mada hiyo iishie hapo.

* * *

Arusha ilinisisimua kwa mengi. Mji mdogo ndiyo, lakini ulikuwa na pilikapilika nyingi, wageni wengi. Ukiwa mji wa mpakani, ukiwa umetenganishwa na Nairobi kwa kijiji mashuhuri cha Namanga. Wageni wengi walioitembelea Arusha walikuwa wafanyabiashara, watalii na wataalamu mbalimbali wakiwa katika pilikapilika hii na ile. Wahindi wachache walikuwa na biashara zao lakini sehemu kubwa ya biashara ilishikwa na wenyeji, Wachaga, Wapare na Waarusha wachache.

Wamasai walinisisimua pia. Ingawa kiasili wao ndio wenyeji hasa wa mji huu lakini kama wanavyoishi mbungani ndivyo walivyokuwa wakiishi hapa. Siku zote walionekana wageni wa mji, wakifanya kazi yao nje kabisa ya mji ambako wao na ng’ombe wao walijiona huru zaidi. Hata ujio wao mjini kwa mahitaji muhimu kama chumvi na vipande vya nguo walivyozowea kuvaa, bado vaa yao, upande mmoja wa mwili ukiwa wazi, sime kiunoni kana kwamba muda wote wako vitani huku kiswalhili na lugha nyingine zinazotumiwa na wengi kikiwapiga chenga. Kuwepo kwao mjini kulifanya waonekane kama watu waliopotea njia.

Mpare, wakati fulani aliponiona ninavyowashangaa, alinisisimulia kisa kimoja cha kuchekesha juu ya Wamasai. Kwamba katika jitihada za kuwalazimisha kuvaa nguo za kisasa serikali ilipata kutoa amri ya wauzaji wote wa maduka kutomuuzia kitu Mmasai ambaye hakuvaa ama suruali ama kaptula ndani ya shuka lake.

Hatua hiyo iliwaudhi sana Wamasai. Hata hivyo, ili wapate huduma hizo kijiji kilibuni mbinu ya kununua kaptula moja ambayo kila aliyekuwa na shida mjini aliazima. Kwa aibu, kaptula hiyo ilivaliwa nje kabisa ya kijiji. Na baada ya manunuzi anaporejea nyumbani Mmasai aliivua kaptula hiyo nje ya kijiji kabla ya kuirejesha.

Sikushangazwa kabisa na habari hiyo, kwa jinsi nilivyowafahamu Wamasai.

Kama ilivyokuwa Moshi, Mpare hakuwa Mpare wa kawaida Arusha vilevile. Hatukulala hotelini. Alinipeleka kwa ndugu zake, maeneo ya Kaloleni ambako alinitambulisha kama rafiki yake ‘mpenzi.’

Alinitembeza maeneo mbalimbali ya mji, Oljoro, Kijenge, Mianzini na kwingineko. Alinifikisha hadi Namanga, Mpakani, ambako alijaribu kuomba ili turuhusiwe kuvuka mpaka na kuikanyaga ardhi ya Kenya walau kwa dakika kumi, tukakataliwa. Wakati tukirejea, kwa hasira zake za kukataliwa kuvuka mpaka aliamua kubadili uelekeo wa safari yetu. “Twende zetu Ngurdoto, tuburudishe macho yetu,” alisema.

Nimetembea sana katika mbuga, misitu mito na ziwani. Nimeona wanyama na ndege wengi sana. Lakini sikupata kuona wanyama wa kuvutia kama tumbili weupe, lino wekundu, mbega na ndege wengi kama niliowaona Ngurdoto. Niliwaona kereng’ende, kibeti, aina mbalimbali za vibisi, kicheleko na wengine wengi ambao waliifanya Ngurdoto kuwa mahala pa kuisimua.

Mandhari ya eneo hilo pia ni kitu kingine cha kuvutia. Ikiwa karibu kabisa na mji wa Arusha, katikati ya milima mikubwa maarufu ya Kilimanjaro na Meru Ngurdoto ilikuwa zawadi nyingine ya asili kwa nchi na vizazi vyake.

Tulirejea mjini jioni sana. Kwa ushauri wake tulikula chakula cha usiku hotelini. Tukashushia kwa vinywaji. Yeye bia za moto, mie fanta mbili za baridi. Kama ilivyokuwa katika mambo mengine, alisisitiza kulipia vinywaji na chakula hicho peke yake. Nikakataa katakata na kulipia. Kisha nilimwambia, “Nadhani umefika muda wa kuzungumza ana kwa ana kama wanaume wawili. Umekuwa mwema kwangu kwa muda mrefu. Umelazimisha urafiki na udugu hadi nikaukubali. Niambie, unahitaji nini sasa kutoka kwangu?”

Mpare alitazama huko na huko kuona kama tulikuwa katika faragha. Hakuridhika. Akanishauri tuhamie katika kona ya baa hiyo iliyokuwa na meza mbili tatu zisizo na watu. Tukahama. “Nataka tuwe marafiki,” alisema baada ya kuketi.

“Nadhani tumeshakuwa.”

“Nataka tuwe ndugu,” aliongeza.

“Nadhani tumeshakuwa,” nilimjibu tena.

Alisita kwa muda kabla hajasema, “Nataka tuwe wasiri. Kwa mwanamume udugu na urafiki havitoshi. Tuwe kitu kimoja. Langu liwe lako, lako liwe langu. Tuafikiane hilo kwanza, kisha tuchukue hatua ya pili.”

Nilimtaazama kwa mshangao uliochanganyika na mashaka. Alikuwa akizungumza kwa makini na msisitizo kuliko ilivyokuwa kawaida yake.

“Hatua ya pili ni ipi?” Nilimuuliza.

“Nataka tutafute pesa. Nataka tuwe matajiri. Mimi nawewe,” alijibu mara moja.

“Kwani hatutafuti?” Nilimuuliza.

Swali hilo lilimfanya aangue kicheko. “Tunatafuta ndiyo. Lakini tunazotafuta ni fedha za kula tu, fedha za kubadili mboga na mashati. Mwanamume anahitaji fedha zilizotakata.

Unaona maghorofa yake yanayopanda?” aliuliza akinielekeza nje ya dirisha ambako jengo la ghorofa nne lilikuwa likijengwa.

“Lile linajengwa na binadamu kama mimi na wewe. Nataka miaka miwili ijayo tuwe na majengo kama yale. Tuwe na magari ya maana. Tuweze hata kununua ndege.”

Nikacheke.

“Usicheke. Hii sio ndoto. Nyota yangu na yako zinafanana. Naona waziwazi mimi na wewe tukiogelea katika bahari ya pesa. Tunajenga... tunalimisha mashamba makubwa... tunakwenda kutembea Ulaya...”

Alizungumza huku akitazama angani, macho kayakodoa kama anayekiona hicho anachozungumza. Nilitamani kucheka tena, lakini kitu fuani kilinizuia. Kitu ambacho sikuweza kukipambanua kati ya hofu na mashaka juu ya rafiki yangu huyo.

“Nitakusimulia hadithi moja,” alisema ghafla. “Sio hadithi ya kupendeza sana, lakini itakufanya uelewe kwa nini nahitaji fedha za maana. Yuko bwana mmoja,” alianza hadithi yake. “Alizaliwa katika familia moja masikini sana. Kwa bahati mbaya sana, familia hiyo ilizungukwa na familia yenye kipato kikubwa, familia ambazo zilisomesha watoto wao nje ya nchi, zilijenga nyumba za maana na kushindana katika kubadili magari na mavazi. Masikini na huyu na ndugu zake wote waliishia kuajiriwa katika mashamba ya majirani hao ambao waliwanyanyasa na hata kuwapiga makofi hadharani. Hali hiyo ilimfanya jamaa huyu asononeke na kukosa raha.”

“Siku moja bwana huyu masikini alikuta baba yake akiwa amepiga magoti mbele ya mtoto wa tajiri yao mmoja, huku akisihi na kubembeleza. Kisa? Masikini baba yake alikuwa amefukuzwa kazi kwa kushindwa kufika kazini

jana yake kutokana na maumivu ya mgongo. Baba alikuwa akijaribu kumsihi mtoto huyo wa tajiri abadili uamuzi wake na kumruhusu kuendelea na kazi ya shamba. Kijana huyo hakukubali, badala yake alimtukana kwa kila neno chafu alilolifahamu hata masikini mzee akawa akitokwa na machozi.”

“Ilikuwa picha ya kusikitisha sana kwa yule kijana. Alimfuata baba yake na kumwinua huku akimwambia, “Kufukuzwa kazi sio mwisho wa dunia. Nenda nyumbani kapumzike,” kauli ambayo yule mtoto wa tajiri aliisikia.

Akageuka na kumwambia, “Na wewe pia umefukuzwa kazi. Toka leo msikanyage katika mashamba yetu.”

“Masikini kijana yule maisha yakawa magumu sana. Alikuwa ndio kwanza ameo na kupata watoto wawili mapacha. Alishindwa kuwalisha. Watoto wakapata utapiamlo na kufa mmoja baada ya mwingine. Mama wa watoto alishindwa kuvumilia. Alilia kwa wiki mbili. Asubuhi moja ya wiki ya tatu mama huyo alikutwa aking’inia kwenye paa la nyumba yao. Alijinyonga kwa kamba ya katani.”

“Uchungu, aibu na hasira vilimfanya baba huyo aondoke nyumbani na kwenda mjini kutafuta kazi. Hakuwa na elimu ya kutosha, hakuwa na ndugu mwenye madaraka, hivyo suala la kazi likawa ndoto. Masikini aliishia kuambulia vibarua vya hapa na pale, ambavyo havikumsaidia sana. Wakati akihangaika huko mjini alipokea habari mbaya moja baada ya nyingine. Mama yake alikuwa amefariki kwa malaria. Hakwenda, kwa aibu ya kwenda mikono mitupu. Baba yake naye akafa. Hakwenda, kwa sababu zilezile. Familia yao sasa ilibakiwa na watu watatu tu, bibi mzaa baba, kikongwe ambaye kila usiku ulipoingia waliamini kuwa kesho asingeamka kutokana na malalamiko ya maumivu ya miguu na mgongo

yaliyokuwa yakimsumbua. Wengine walikuwa wadogo zake wawili, msichana aliyekuwa kiwete na mvulana ambaye ndiye aliyekuwa akichangia kuleta walao vibaba vya unga vilivyowawezesha kuvuta siku.”

“Yule bwana, masikini, hadi leo anahangaika mijini akijaribu kushika ama hiki ama kile bila mafanikio,” alimaliza hadithi yake na kunikazia macho.

“Hii ni hadithi ya kweli,” baadaye alisema. “Na wahusika wake ni wa kweli. Mhusika mkuu ni mmi.”

“Wewe?” Niliuliza kwa mshangao.

“Naam, mimi mwenyewe. Na, kwa kweli, hicho ulichokisikia ni moja ya kumi tu ya mateso na aibu zitokanazo na umasikini ambazo nimepata kukutana nayo. Kinachoitesa roho yangu sana ni huyo bibi na wajukuu zake ambao wanaishi kwa kudra ya mwenyezi mungu. Tatizo lolote linalohusiana na pesa linaweza kumfanya yeyote kati yao au wote wapoteze maisha kama mende au kunguni mikononi mwa binadamu.”

Sikupata kujua kama nilikuwa na huruma. Lakini nilipohisi machozi yakinilengalenga kwa simulizi hiyo nilijua kuwa nimeshikwa na huruma. Akili ikahama na kunifanya niifikirie familia yangu huko Buha. Pengine ina hali kama hiyo. Pengine haipo tena, wote wamekufa kwa shida hii au ile! Choji moja liliteleza ghafla na kulifikia shavu langu. Nililifuta mara moja kwa kiwiko cha mkono na kisha kutoa lesa yangu ambayo haikutoka mkononi mwangu kwa muda mrefu.

Tulipigwa na kimya cha muda mrefu, kimya ambacho Mpare alikiondoa pale aliposema baadaye, “Ninaposema nimejaribu kila kitu maana yake ni kila kitu. Nimejaribu biashara lakini bila mtaji ni biashara gani utafanya? Nimejaribu kutafuta kazi. Bila elimu utapata kazi gani ya maana? Lilipokuja

vuguvugu la siasa na kupigania uhuru nilikuwa mstari wa mbele kujiunga, kwa matarajio kuwa nitakuwa mmoja wa wachache watakaowahi kula matunda ya uhuru. Lakini humo pia nimekata tamaa. Elimu yangu ya *ngumbaru*, niliyoipata kwa taabu haikufua dafu mbele ya wenzangu ambao tayari wamejipanga vizuri. Hata pale unapokuwa na wazo la maana bila elimu au pesa kamwe hutasikia wala kusikilizwa.” Alisita kwa muda. Alipozungumza tena ilikuwa kama aliyenisahau, na kuzungumza peke yake. “Nimepoteza watoto niliowapenda. Nimempoteza mke niliyempenda. Nimepoteza wazazi. Siwezi kupoteza tena nafasi ya kutajirika.”

Akanigeukia ghafla na kusema, “Nitakuwa tajiri. Nitafuta aibu zangu zote. Wewe utanisaidia. Tutapaa kama mlima Kilimanjaro. Wote waliokuwa wakitupuuza watainua nyuso zao kutushuhudia.”

“Ulisema juu ya tatizo la mtaji. Umeshaupata?” nilimuuliza.

Kwa mara ya kwanza katika kipindi kirefu nilimwona akitabasamu. “Naam, mtaji ninao tayari,” alijibu baadaye.

“Uko wapi?”

“Wewe ni mtaji.” Alijibu.

“Mimi! Nilishangaa “Unajua sijakuelewa?”

Akatabasamu tena kabla hajasema, “Utanielewa. Ni rahisi sana. Kwa ujuzi wako wa mambo ya porini, kwa uzoefu wako wa masuala ya mbugani na msimamo ambao nauona katika macho yako, naamini tukishikana ni mtaji tosha.”

Bado sikumwelewa.

Akafafanua, “Tunahitaji bunduki moja tu na risasi tano. Risasi moja ikilenga shabaha tayari tumetajirika. Bunduki ninayo, risasi ninazo. Kitu gani kitanizuia?”

Bado sikuwa nimemwelewa. Nikamtumbulia macho ya kumtaka ufafanuzi.

“Nadhani nizungumze kwa tuo. Nisikilize kwa makini, tafadhali,” alisema akijiweka vizuri juu ya kiti na kukivuta karibu yangu zaidi.

* * *

Niliwapenda wanyama wa porini. Niliwapenda sana. Kukururu, kakara, tumbili na nyani wakicheza juu ya miti, mara waruke toka tawi hadi tawi au toka mti hadi mti, kwangu ilikuwa burudani safi sana. Niliwahusudu chui, ngozi zao za madoa yanayopendeza na mwendo wao wa maringo porini, pasi ya kishindo, kana kwamba wao ni malkia wa nyika ni mambo ambayo yalinisisimua sana. Nilivutiwa na simba, wafalme wa mwituni, kwa ubabe na jeuri yao hasa wale wa Serengeti ambao hupanda miti na kupumzika juu yake kama chui. Niliwapenda twiga na shingo zao ndefu, niliwapenda hata fisi wala mizoga. Kwa ujumla, niliwapenda wanyama wote.

Niliwapenda pia ndege, tai mvumilivu ambaye anaweza kumfuata mnyama na hata binadamu mgonjwa kwa siku kadhaa hadi atakapozidiwa na kukata roho ndipo humvamia na kumla, njiwa ambao huburudisha kwa sauti zao nzuri, korongo na jamii zake zote, korongo mfuko shingoni, korongo uso mwekundu na wengineo. Nilimpenda pia bundi na hadithi zake zenye mapokeo anuwai.

Samaki wa majini, wadudu wa ardhini pia ni viumbe niliowapenda. Kila mmoja ambaye ungemtazama kwa makini na kufuatilia nyendo zake, kama unazo fikra usingekosa kujifunza jambo toka kwao. Nyuki na malkia wao, ambao kwa umoja wao hujengwa himaya kubwa na kutuwezesha kupata

asali. Mchwa ambao pamoja na udogo wao hujenga vichunguu, kinyonga mwenye uwezo wa kubadili rangi ya mwili wake kama anavyojisikia, jongoo menye miguu elfu moja na moja lakini asiyeweza kukimbia, nyoka asiye na mguu hata mmoja, mwepesi wa kuteleza maporini kama mshale.

Zaidi ya wanyama niliyapenda mazingira yanayowawezesha kuishi: misitu murua yenye mimea na vivuli wanavyohitaji, mito na mabwawa yanayowapatia maji na hifadhi kwa wale waishio majini, mawe, milima na mabonde ambayo ni sehemu ya maisha yao na kadhalika. Licha ya mazingira haya hifadhi ya wanyama bado ni kivutio muhimu cha watalii, ambao kutembelea kwao nchini kuna maana ya kuleta pesa. Aidha, mazingira ni urithi wa watoto na wajukuu wetu ambao wana haki ya kufaidi kama tunavyofaidi sasa.

Niliwaza yote hayo nikiwa chali kitandani, usingizi ukiwa umenikimbia usiku kucha. Ilikuwa baada ya Mpare, ambaye jina lake halisi lilikuwa Daniel Mbonea.

Alikuwa ameibuka na wazo la mradi wa hatari, unaoshawishi na kutisha pamoja, mpango wa kunitaka tushirikiane katika uwindaji wa wanyama pori na kujipatia nyara ambazo zingetupatia utajiri wa harakaharaka.

“Kila kitu katika wanyama ni pesa,” alikuwa amesisitiza. “Ukimwua tembo pembe zake ni pesa. Ukimwua chui na hata mamba ngozi zao ni pesa. Lakini tunayemtaka zaidi ni kifaru. Ukiwaua wawili tu, umasikini kwa heri. Wako wengi huko mbungani. Lazima tuwatafute.”

Wazo hilo sikupata kulifikiria. Kwa kila namna lilinitisha, nikijua kuwa si kazi ya hatari kwa maisha yetu tu, bali kwa vyovyote vile ni kinyume na sheria. Nilimkumbusha hilo. Lakini Mpare alicheka tu, kisha akaniuliza, “Hivi unafahamu

hawa waliotajirika wamefanya kazi gani?”

Nikamjibu kuwa sijui.

“Huwezi kujua. Hutapata kujua. Na wao hawatajua utajiri wetu umetoka wapi. Mwanamume anahitaji kuthubutu. Hii ni nafasi yetu ya pekee.”

Nilikuwa na mengi ya kufikiri. Awali ya yote lilikuwa lile pendekezo la akina Bibi Titi Mohamed la kunitaka nirudi nyumbani nikaanzishe tawi la TANU ili kujiandaa kwa uhuru ambao alisisitiza kuwa ‘umenukia.’ Kimsingi nilikuwa tayari nimeafikiana naye. Si kwa ajili ya kwenda kufanya siasa pekee. Nia yangu kubwa ilikuwa kufika nyumbani kwetu kuwajulia hali wazazi wangu. Akiba yangu ya pesa haikuwa ndogo. Ningeweza kabisa kuwajengea nyumba bora zaidi, kuwanunulia mavazi mapya na kumpatia baba baiskeli. Nilimwambia hivyo Mpare. Lakini alinicheka tena kabla ya kuniuliza, “Baada ya kujenga hiyo nyumba?”

Sikumjibu haraka. Akaamua kujibu kwa niaba yangu. “Baada ya nyumba utarudia kwenye umasikini wako. Hutakuwa na kitu tena. Kwa maana hiyo ni kwamba huna kitu. Lazima tutafute pesa zilizotakata. Achana na vijisenti ambavyo havitabadili maisha yako.”

Ndipo nikamwomba aache nilifikirie wazo lake hadi kesho, fikra ambazo zilifanya nipoteze usingizi wangu kucha na kubakia nikitapatapa kitandani kuubembebeza.

Nilishawishika.

* * *

Kuwinda sio lelemama. Sio kuingia porini, kuona mnyama, kuelekeza bunduki na kuifyatua peke yake. Ni zaidi ya hapo. Kuwinda kuna miiko na maadili yake. Mimi sikuwa

mwindaji. Lakini sehemu kubwa ya maisha yangu nikiwa nimeitumia maporini nilikuwa nimeona mengi na nimejifunza mengi, mengi tosha kunipa ujanja na maadili ya porini.

Kwa mfano, usiku mmoja tukiwa katika barabara moja mbovu, ya mkato katika maeneo ya Makuyuni, nilishangaa kuona njia imeziba ghafla. Nikasimamisha gari na kumuuliza mmoja wa abiria wangu kuna nini mbele yetu. Aliangalia mara moja tu na kuniambia “Tembo.”

Kumbe tembo mkubwa alikuwa amesimama katikati ya njia akitutazama. Baada ya muda alianza kutusogelea taratibu. Nikaweka gari ya kurudi nyuma na kuanza kurudisha gari taratibu. Tembo alizidi kutusogelea. Kwa wasiwasi nilijikuta nimerudisha gari vibaya na kuingia shimoni. Tembo aliendelea kuja taratibu. Mara nikamsikia abiria wangu mwingine akiuliza kama kulikuwa na mtu mwenye kiberiti. Nilikuwa nacho. Nikampa. Kwa mshangao wangu alishuka nje ya gari na kuwasha sigara. Moshi na harufu ya sigara ulipeperushwa na upepo kuelekea aliko tembo, tulimwona akisita. Kisha tembo yule aligeuka na kuondoka zake taratibu kama alivyokuwa akija.

Tembo hapendi harufu ya sigara.

Katika tukio jingine niliwahi kulala ndani ya hema langu mapumzikoni, huko Ngorongoro. Nyakati za alfajiri nilipata hisia kuwa mambo si shwari. Nikafungua macho kutazama nje. Pazia la hema langu lilikuwa limefunguka. Simba wawili, dume na jike waliketi pale mlangoni wakinitazama. Walipoyaona macho yangu waliinuka na kuondoka zao polepole. Niliwatazama hadi walipotokomea porini.

Wanyamawanajuabinadamunidhaifu, hawamshambulii bila sababu.

Nilimsimulia hayo Mbonea. Hayo na mengine mengi. Nilimwambia kimaadili ni mwiko kumuua mnyama mwenye mtoto au watoto.

“Hutakuwa umeua mnyama mmoja tu, bali wengi. Baadhi ya wanyama wachanga huweza kutembea dakika tatu tu baada ya kuzaliwa. Wanamhitaji mama kwa maziwa na ulinzi. Ukimwua mama umewaua wao pia,” nilimfafanulia.

“Binadamu tunamwogopa sana simba, pengine na chui,” nilimweleza. “Lakini wanyama wote ni hatari. Nyati, kwa mfano, ni mnyama mwenye hasira na hila nyingi. Ukimpiga risasi ukamwona ameanguka usije ukamsogela. Wakati mwingine hata ukiwa umemkosa au kumjeruhi atajiangusha chali na kujifanya kafa. Ukimsogelea unakufa wewe. Kifo cha nyati ni mpaka pale utakapoona amejikojolea.”

“Mkojo huo wa nyati akiwa hai ni silaha kali sana.” Niliongeza. “Kama utakuwa umepambana na nyati halafu unamkimbia na kupanda juu ya mti atakachofanya ni kuukojolea mkia wake na kisha kurushia mkojo huko aliko. Mkojo wake unawasha sana. Ukikupata kwa vyovyote utaachia mti na kuanguka chini, ambako utamkuta akikusubiri. Atakusagasaga kwa miguu na pembe zake hadi ahakikishe umekufa.

Mpare Mbonea alishangaa. Ilikuwa dhahiri kuwa hilo hakulijua.

“Tembo hata kama hujampiga risasi, ukimwona kaanguka usimwogope. Tembo akianguka haamki, huwa ndio mwisho wa maisha yake. Ndiyo maana tembo hata akilala hulala wima, ama kwa kujiegemeza kwenye mti au kwa tembo wawili kuegemeana.”

Hilo pia Mbone hakulijibu. Alizidi kuduwaa.

“Huyu tunayemwinda ni mkali zaidi na wa hatari zaidi,” niliongeza. “Kwa bahati hana akili nyingi. Kifaru ana nguvu nyingi sana na kasi ya ajabu. Akikuona unatishia maisha yake atainama na kukujia kwa kasi, macho kayafumba, kwa lengo la kukuchoma lile pembe lake. Ukiona hivyo ondoka haraka sana eneo hilo. Wawindaji wajanja hulipata pembe lake kirahisi sana kwa njia hiyo. Wao husimama mbele ya mti mkubwa. Faru anapokuja huondoka mara moja kwa hasira zake na hujikuta amechomeka pembe lake katika shina la mti huo na kulididimiza. Katika jitihada za kuitoa mara nyingi pembe hiyo hung’oka, kifaru hutokwa na damu nyingi na baadaye kukata roho.

Mwindaji hujipatia hitaji lake kwa urahisi kabisa.” Mbonea alinisikiliza kwa makini sana, kana kwamba nilikuwa nikimfundisha namna ya kuingia katika ufalme wa mbinguni. Alinisikiliza. Lakini sina hakika kama alikuwa akinisikia, kwani mara alipopata nafasi ya kwanza aliivunja kanuni ya kwanza kabisa ya uwindaji. Kitendo hicho kiliniua kwa mara ya pili katika maisha yangu.

SURA YA KUMI NA TISA

Pembe Za Faru

Wanasema ‘za mwizi arobaini’. Sisi hatukuzihitaji arobaini hizo. Siku ya tatu tu, toka tulipoanza shughuli hizo, ilitosha kabisa kututia hatiani.

Tukio hilo lilianza hivi;

Baada ya kufika na Mbonea, aliniacha Arusha na kwenda Kilimanjaro. Aliporejea jioni hiyohiyo, akiwa na ‘vifaa’ vyake; viatu aina ya safari, suruali na shati la kaki, mfuko wa ngozi na zaidi ya yote silaha. Alikuwa na bunduki kuukuu ambayo aliielezea kama hazina yake pekee itakayomtoa katika lindi la umasikini. “Hii ndio baba, ndio mama. Nina hakika haitaniangusha,” alisema wakati akiitoa katika mfuko wake na kunikabidhi ili niikague.

Alfajiri ya siku iliyofuata tuliua mji wa Arusha, tukiifuata barabara ya Dodoma. Tulivipita vitongoji vya Ngarenaro, Sombetini na Majengo. Tukafika Kisongo na kuiacha njia ya Monduli kulia hadi tulipofika Makuyuni. Hao tungeweza kuelekea kulia vilevile na kufika Mto wa Mbu, Karatu na hatimaye Ngorongoro ambako nilitarajia tuanzie shughuli zetu. Tulipita kwa chini na kuliona ziwa Manyara kwa mbali kabla ya kuingia Magugu na hatimaye Babati.

Mbonea alisisitiza sana juu ya kuwatafuta vifaru kabla ya wanyama wengine. “Pembe zao ni almasi!” “Zinatafutwa sehemu mbalimbali za dunia.” Tukiipata walao moja tu....”

Nilitamani kucheka. Kwangu mimi kifaru ni mnyama mwenye sura mbaya na umbile lisilovutia kuliko wanyama wengine wote. Alivyokuwa na bahati mbaya zaidi pembe zake hizo kubwa na ndogo, zinazodaiwa kuwa za thamani zimeota juu ya pua, katikati ya uso wake. Wataalamu wanasema pembe hiyo ni mkusanyiko wa aina fulani ya nywele, zinazoota toka kwenye fuvu lake la kichwa jambo ambalo hupelekea kupoteza pembe hizo apoteze pia uhai wake.

Mbonea alinisikiliza kwa shahuku. Lakini nilihisi shahuku yake kubwa ilikuwa ni kumwona kifaru na kumpiga risasi, si vinginevyo.

* * *

Kifaru anaweza kuishi kati ya miaka 35 hadi 40, umri ambao humwezesha kufikia uzito wa tani moja na nusu hadi mbili. Pamoja na uzito huo anaposhambuliwa hukimbia kwa kasi kati ya kilomita arobaini na tano au hamsini kwa saa. Kifaru hana makuu. Pamoja na machachari yake yote chakula chake pekee ni majani, hata yale yenye miiba. Si msumbufu, kwani muda mwingi wa mchana hupenda kujipumzisha kando ya mito au mabwawa. Hali hiyo hufanya kazi ya kumwinda isiwe ngumu kama inavyotarajiwa.

Imani ya muda mrefu juu ya pembe zake hizo, kuwa hutengeneza dawa fulanifulani muhimu kwa binadamu pamoja na mapambo murua ni sababu iliyofanya aanze kuadimika sana duniani. Ukweli huo niliufahamu fika kupitia matangazo ya watetezi wa wanyama katika vyombo vya habari. Na hivyo

ikawa sababu mojawapo iliyonifanya kushiriki katika jukumu hili huku roho ikinisuta.

Lakini pindi maji ukishayavulia nguo huna budi kuyaoga. Sikuona kama ingekuwa uugwana kubadili uamuzi, hasa nikiwa tayari humo porini. Nilimwelekeza Mbonea maeneo yote ambayo yalikuwa na sifa za kuishi vifaruu. Nilimkumbusha mara kwa mara kuwa makini. “Macho ya kifaru ni dhaifu kidogo kuona mchana. Lakini pua zake ni makini sana. Akipata harufu yako kabla hujamwona na akishuku kuwa una nia mbaya ujue kuwa utakufa wewe badala yake,” nilimwambia.

Nikaongeza, “Lakini kifaru si wa kuogopa zaidi. Yupo askari wake. Huyu ni ndege ambaye muda wote hukaa juu ya miili ya vifaruu akidonoa wadudu wanaomsumbua. Wakati mwingine hata pale kifaru anapokuwa na jeraha ndege hawa huliongeza kwa kulidonoadonoa. Kifaru humvumilia. Pengine analazimika kumvumilia kwa kuwa hana la kufanya. Ndege huyo huona mbali sana na humshtua kifaru kwa mlio wake mara anapohisi dalili za hatari kwa *bosi* wake.”

Wataalamu wanakubaliana kuwa Ngorongoro ni moja ya miujiza kadhaa ya dunia. Wanaikadiria kuwa ni mwujiza wa nane duniani. Miujiza mingine ikiwa pamoja na ile ya yale majengo yaliyopo Misri. Piramidi, ambayo yalijengwa miaka ipatayo 4700 iliyopita lakini yangali hai hadi leo. Mojawapo ambayo yametumia mawe na miamba yenye uzio wa tani moja hadi mbili kila moja na kupaa juu urefu wa meta 140. Ikizingatiwa kuwa wakati huo hakukuwa na vifaa maalumu vya ujenzi kama leo, majengo hayo yaliyoandaliwa kama hifadhi ya miili ya farao yanamshangaza kila mtu anayeyaona. Sanamu ya mmoja wa miungu ya wagiriki, Zeus, akiwa amekaa juu ya kiti chake cha enzi, chenye ukubwa wa meta 12, ikiwa

imeundwa kwa meno ya tembo na kupambwa aina mbalimbali za madini ni mwujiza mwingine wa dunia.

Muujiza wa Ngorongoro unatokana na maumbile yake. Wakati eneo hili ambalo limo katika Bonde la Ufa linakadiriwa kuwa na ukubwa wa kilometa za mraba 8,300 zenye wanyama pori wapatao 300,0000 ndani ya eneo hilo kuna kilometa za mraba zipatazo 250 za kushangaza ziadi. Eneo hili, katika mabadiliko mbalimbali ya maumbile ya dunia lilididimia kwa kiasi cha meta 600 toka usawa wa ardhi. Humo ni shamba pekee la wanyama. Zaidi ya wanyama wapatao 20,000 wakiwemo vifaru weusi, nyati , pundamilia, tembo, fisi na wanyama wengine tele. Wamo pia ndege anuai na wadudu.

Ikiwa kama bustani ya aina yake, eneo hilo lenye maji tele, lishe ya kutosha na mazingira ya kuvutia limefanywa na wanyama hao kama makazi yao ya kudumu ingawa wanao uwezo wa kutoka na kuingia.

Kama ambavyo eneo hili humshangaza kila binadamu anayeliona kwa mara ya kwanza ndivyo lilivyomshangaza rafiki yangu Mbonea. Nilihisi kuona kitu kama machozi yakimlengalenga katika macho yake na dalili za udenda kumtoka pale tulipoingia na kuwaona wanyama mbalimbali wakiendelea na shughuli zao bila ya kututilia maanani. Twiga mmoja aliyekuwa akinyonyesha aligeuka kutuangularia kidogo kisha akaendelea kula juu ya kilele cha mti. Swala mmoja alikurupuka toka kichakani na kukimbia hatua kadhaa kabla hajasimama, kututazama kwa muda kabla na kisha kutokomea tena vichakani. Kwa mbali sana, tuliweza kuona kundi kubwa la nyati likipunga upepo huku vitoto yao vikiruka huku na huko katika michezo yao ya kawaida.

Mbonea alizidi kushangaa. Alishindwa kustahimili,

chozi likamdondoka. Alijaribu kulifuta harakaharaka, lakini haikuwa kabla ya kuliona, jambo lililofanya niangue kicheko. “Tunawatafuta faru,” nilimkubusha. “Sio kitoweo. Kwa hiyo, punguza papara.”

Tulizurura maporini humo kwa siku nzima. Tulipita katika mito ya layara, oljiro na Mungo. Tulipita kandokando mwa ziwa Makkat na katika bwawa la Mandus. Tuliingia hata katika msitu wa Lera. Tuliwaona wanyama wengi sana isipokuwa yule tuliyemwitaji, kifar. Ilikuwa siku mbaya.

Siku ya pili ilianza kwa namna ya pekee. Ilikuwa angavu sana na hata hali ya hewa haikuwa ya ubaridi mkali. Tulifuata barabara ya Lemaka iliyotupeleka tena kwenye ziwa Makkat ambako tulikuwa tumeona dalili za wanyama hao vikiwemo kinyesi na nyayo. Wakati tukiwa umbali wa kilometa moja toka ziwani hapa nilisikia milio ya ndege, askari wa vifar ikitokea vichakani. Kisha niliwaona ndege hao wakiruka angani na kutokomea.

“Wapo,” nilimwambia Mbonea. “Kwa bahati mbaya, wameshapata hisia za hatari. Lazima tuwe waangalifu sana,” nilimsisitizia. Hata hivyo, nilikuwa na mshangao kidogo. Ndege hao walikuwa wametuona sisi kweli au hatari nyingine? Maana tulikuwa mbali na pale walipotokea.

Tulitembea kwa hadhari kuelekea huko, mitutu ya bunduki zetu ikiwa imeelekezwa mbele, tayari kufyatuliwa iwapo lingetokea lolote lile. Tulipofika pwani ya ziwa tuliambaa nayo kuelekea upande wa kulia walikorukia ndege. Hata kabla hatujapiga hatua ishirini tulimwona kifar mmoja akiwa amesimama katika hali ya tahadhari akiangalia tunakotokea. Alikuwa na mtoto, kifar mdogo ambaye alisimama katikati ya miguu ya mtoto wake.

Mara nikamwona Mbonea akipiga goti chini na kulenga shabaha. “Usimwue... ananyonyesha...” nilijaribu kumwambia. Sauti yangu ikimezwa na mlio mkubwa wa ghafla kutoka kwenye bunduki yake. Alikuwa na shabaha ya pekee. Risasi ilipenya katika paji la uso la kifaruru huyo bila kuharibu pembe zake. Kifaruru alitapatapa kwa muda akipigania roho yake kabla hajaanguka chini. Risasi ya pili, iliyomwingia tumboni ilimfanya akate roho palepale.

“Umefanya nini?” nilimuuliza kwa ukali. “Nilikuonya mapema kuwa mnyama anayenyonyesha! Kinda yule atafanya nini peke yake katika mazingira haya?”

Mbonea alikuwa akitabasamu, tabasamu pana ambalo sikupata kuliona huko mbeleni katika uso wake. Badala ya kunijibu nilimsikia akisema, “Mmoja tayari! Bado wawili tu tumekuwa matajiri!”

Nilikuwa nimekasirika kiasi kwamba nilitamani kumlenga bunduki yangu na kuifyatua. Majuzi tu alikuwa akilalamika watoto wake pacha waliopoteza maisha kwa utapiamlo leo anaacha mtoto wa faru apoteze maisha kwa njaa, baridi au kukosa kiongozi wa kumsaidia mbinu za kuishi porini.

Mbonea alijua nimekasirika. Hakujua kama alinikasirisha zaidi pale aliposema “Toto la kifaruru litakufaa nini rafiki yangu. Hata pembe halina. Achana nalo, tushughulikie mali yetu.”

Wakati huo ‘toto’ hilo la kifaruru lilikuwa limehisi kuwepo kwa jambo baya lililomtokea mama yake. Lilionyesha kushangazwa na damu. Likamzunguka mama yake mara tatu na kujaribu kumtikisa kabla halijaanza kulia kwa sauti yake mabaya, sauti ambayo masikioni mwangu ilitia huzuni kubwa.

Sijui nini ambacho kingefuata baina yangu na rafiki yangu Mpare kama jambo jingine, kubwa zaidi, lisingetokea. Tulijikuta ghafla tumezingirwa na kundi la askari wa wanyama pori wasiopungua sita, kila mmoja akiwa na bunduki mkononi. Na kila bunduki ikiwa imetuelekea.

“Tueni bunduki zenu chini na muweke mikono yenu juu mara moja!” mmoja wao alitoa amri.

Tulitazamana na Mbonea kwa mshangao. Hatukuwa na namna yoyote ya kupambana nao wala kukimbia. Tukaziangusha bunduki na kuweka mikono yetu juu ya vichwa.

“Washenzi wakubwa nyie,” askari yule aliendelea kufoka. “Tumemlinda kifaruru huyu kwa miaka nyie mnamuua kama mchezo. Mtakuwa mfano mzuri sana kwa jamii. Kama hamjafungwa maisha, miaka ishirini kwa kila mmoja wenu haitamkosa.”

Walizichukua bunduki zetu. Wakatutia pingu za mikono kisha tukaanza kusukumwa kuelekea walikoificha gari yao. Tukatupwa ndani ya gari, ikatiwa moto na kuelekezwa mjini Ngorongoro ambako tulifungiwa katika kijichumba kidogo kwa siku tatu kabla ya kupelekwa Arusha. Tulifunguliwa mashataka.

* * *

Kabla ya kesi yetu kuanza kusikilizwa tulikaa rumande kwa wiki tatu nzima, tukiwa tumewekwa katika chumba cha watu hatari sana. Chumba hicho kilijumuisha watu watatu wa kesi za mauaji, watu watano wanaotuhumiwa kwa kujaribu kuvunja benki kwa nia ya kuiba, mmoja aliyekamatwa akimnajisi ng’ombe na wengine tele wenye tuhuma hii au ile.

Mmoja kati ya watuhumiwa hao nadhani alikuwa kichaa. Siku zote , wakati wote, alikuwa mtu wa kupiga kelele. Na kauli yake ilikuwa moja tu; ‘Nitaua mtu. Kama si leo kesho!’ Kauli hiyo ilitisha sana kwani sikujua alikusudia kumwua nani. Hakimumu anayesikiliza kesi yake, askari aliyemkamata au yeyote kati yetu mahabusu wenzake. Macho yake yalikuwa yanatisha, sura yake ikitangaza shari kama shetani mwenyewe. Kwa kweli alininyima raha na kufanya nijitahidi kila ilivyoweze kana kumkalia mbali.

Hiyo ndiyo jumuiya mpya niliyojiunga nayo, jumuiya ya wahalifu, jumuiya ya waasi wa sheria. Mimi, Petro Mtukwao Kionambali Kalimanzira tayari nilikuwa mmoja wao. Machoni mwa jamii nilikuwa mtu duni, asiye faa kuishi uraiani bali gerezani kusubiri hukumu kamili.

Ilinisikitisha zaidi pale watuhumiwa hao walipotupokea kwa furaha kana kwamba sisi ni mashujaa. “Jengo hili limejengwa kwa ajili ya wanaume kama nyie,” mmoja wao alisema. “Bila nyie, polisi na mahakimu wangekufa njaa, kwani hakuna mtu ambaye angekubali kuwalipa mishahara bure!”

Sikumwelewa.

Wala hakunijali. Aliendelea na mawaidha yake ya kishetani, “Wanaletwa hapa watu kwa makosa ya kitoto kabisa. Eti jitu zima limepiga hadi kumwua mkewe au mwanawe. Eti jitu na akili zake limeiba kuku wa jirani. Nyie wanaume bwana! Kuingia msituni, kupambana na wanyama hatari kama faru ili mpate zile pembe zake ni uanaume. Kukamatwa kwenu ni ajali kazini tu. Kama msingeshikwa mnekuwa matajiri wakubwa kutoka nchi hii.”

Hiyo ndiyo jela! Hakuna siri! Toka siku ya kwanza tulipoingia tayari tulikuwa gumzo. Kila mmoja alionyesha dalili

ya kutupongeza! Laiti wangejua nilivyokuwa najisikia moyoni! Nilikuwa taabani kwa aibu na kukosa raha. Sikutegemea kamwe maishani nifanye kitendo chochote, ama kwa makusudi ama kwa bahati mbaya, ambacho kingeniweka upande wa pili wa sheria. Nilikuwa na nilitegemea kuwa mtu mwaminifu na mwadilifu katika uhai wangu wote. Nilijuta kukutana na Mbonea. Nilijuta zaidi kumsikiliza. Nilitamani kumchukia maisha yangu yote. Nilitamani kumwambia hayo.

Hata hivyo, Mbonea hakuwa katika hali ya kuambiwa hayo. Toka tulipokamatwa muda wote alikuwa mtu wa kutokwa machozi. Mara nyingi, kwa sauti inayotetemeka, nilimsikia akinong'ona, "Bibi yangu kikongwe atafanya nini jamani... dada yangu kiwete ataishi vipi..." alisema huku akifuta machozi. Kwa muda huo mfupi Mbonea tayari alikuwa amekonda na kupungua uzito kwa zaidi ya kilo kumi. Hakupata usingizi. Alikula kwa shida baada ya ushawishi mwingi. Ndiyo, ni yeye aliyeniingiza katika mkasa huo. Lakini kwa jinsi alivyokuwa akitia huruma nilijikuta nikimhurumia kuliko hata nilivyojihurumia mimi.

Mbonea alikuwa na ndugu wengi. Alitembelewa na watu mara kwa mara na kujadiliana nao hili na lile. Nilishangaa alivyokuwa haonyeshi nia ya kunishirikisha katika maongezi hayo, ambayo nilitarajia yangelenga katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo letu. Sikuwa na la kufanya. Nikabakia na uyatima wangu nikiyaweka yote mikononi mwa Muumba.

Kabla ya kupelekwa mahakamani, tulihojiwa na watu mbalimbali, polisi, wanasheria na hata watuhumiwa wenzetu. Kila mmoja alikuwa na ushauri wake kwetu. Polisi na wanasheria wa serikali walinishauri kukiri kosa ili kupunguza uzito wa adhabu. Wanasheria wengine walinishauri kukataa

katakata kuhusika na suala hilo. Watuhumiwa na wenye uzoefu wa masuala ya kesi pia walinionya juu ya athari za kukubali kosa kubwa kama lile. Hali iliyofanya nijione kuwa nachangwanywa akili.

Tatizo jingine lilikuwa mshitakiwa mwenzangu. Kila nilipomtaka tukae na kuweka mkakati wa pamoja alikuwa akiishia kulia tu. Hatukupata hata mara moja kukaa na kuzungumza lolote kwa tuo. Mbaya zaidi ni pale ambapo tulikuwa tukihojiwa na hata kuandika maelezo kila mmoja kwa wakati wake. Sikujua amejeleza vipi na kuandikisha lipi, kama ambavyo niliamini yeye hakujua nilichoeleza.

Hatimaye, siku ya siku ikafika. Tulichukuliwa na lori la polisi toka gereza la Kilimwanga, tulilokuwemo na kupelekwa mahakamani mjini Arusha. “Pilato” alikuwa mzungu, mtu mfupi; mwembamba mwenye sura ya kitoto. Isipokuwa kwa miwani mizito na joho alilovaa isingekuwa rahisi kumfananisha na hakimumu. Nilikuwa nimepata sifa nyingi za hakimumu huko gereza. Nusu ya wafungwa wote ni yeye aliyewahukumumu. Nilikwishaambiwa mapema kuwa kama tungemkuta hakimumu huyo, ambaye gereza walimwita “Fisi maji” kwa ukali wake, gereza lisingeweza kutuepuka. Ajabu ni kwamba kwa sura hakuonekana katili kama alivyoelezewa.

Siku hiyo mahakama ilikuwa na kesi nyingi, kubwa na ndogo. Lakini nadhani kesi yetu ndiyo iliyomvutia zaidi maana niliona kesi nyingi akiziendesha harakaharaka. Zingine alizihairisha na nyingi alizitolea hukumu bila umakini mkubwa, huku mara kwa mara akitupa jicho upande wetu kama anayetusubiri kwa hamu.

Saa na hatimaye dakika ikawadia. Tukiitwa kwa majina, mmoja baada ya mwingine na kusimamishwa kizimbani. Mimi

nikitetemeka kidogo, mwenzangu akitetemeka na kupepesuka kama jani la mwembe.

Hakimu alivua miwani na kututazama kwa takribani dakika nzima, kabla hajaivaa tena na kusoma jalada la tuhuma zetu lililokuwa mbele yetu. “Petro Mtukwao Kionambali... Daniel Mbenea mnashtakiwa kwa kuingia katika hifadhi ya taifa ya Ngorongoro kwa makusudi ya kufanya vitendo vya uharamia. Kosa la pili, kwa makusudi vilevile mlimuua mnyama aitwaye kifarua kwa kumpiga huku mkijua fika kuwa kifarua huyo ni mmoja wa wale wanaolindwa na serikali kwa gharama kubwa ili kuifadhi viumbe hao walio hatarini kutoweka. Aidha, kosa lenu la tatu ni kumwua kifarua huyo huku mkijua na kuona wazi kuwa alikuwa na mtoto mchanga ambaye alimtegemea. Kwa maana hiyo mmehatarisha maisha ya kichanga huyo pia.”

Hakimu alivua tena miwani yake na kunikazia macho, “Petro Mtukwao Kionambali... ni kweli au si kweli?”

Nikageuka kumtazama mwenzangu. Alikuwa akinitazama pia, ingawa macho yake yalijaa machozi. Kwa namna fulani alikuwa kama anayenisihi jambo fulani. Sikujua ni jambo lipi. Nikainuka na kumtazama hakimu. “Ni kweli Mheshimiwa,” nilijibu.

Nilipata hisia kuwa kila mtu katika chumba hicho cha mahakama, ikiwa pamoja na hakimu mwenyewe, alipigwa na butwaa. Hakimu aliinama, akaandika jambo katika faili lake, kisha akainua tena miwani na kumkazia macho Mbenea. “Daniel Mbenea, mashtaka haya ni kweli au si kweli?”

“Sio kweli, Mheshimiwa,” Mbenea alijibu kwa sauti iliyokuwa na uhakika kinyume na hali yake.

Hakimu aliandika jambo. Akainua tena uso wake na kututazama kwa zamu kabla hajauliza, “Nataka kufahamu

kitu kimoja. Kati yenu nani aliyefyatua bunduki, ambayo risasi yake ilimuua kifarū yule?”

Tulitazamana tena na Mbonea. Alikuwa amebadilika tena. Anatetemeka na anapepesuka nusura aanguke chini. Macho yake yalijaa huruma na simanzi. Niliweza kuyasoma mawazo yake katika macho yake hayo; *bibi yangu kikongwe atafanya nini jamani... dada yangu kiwete ataishi vipi...* ujumbe ambao ulinifikia bila sauti. Ukanitia huruma. Bila kujua nilifanyalo, niliinua tena mkono wangu na kumjibu hakimu, “Ni mimi Mheshimiwa.”

Nilisikia sauti za kitu kama, “Ah!” zikiwatoka watu wawili watatu chumbani humo. Wengi wao walinikazia macho ya mshangao na kutoyaamini masikio yao. Hata hakimu alionekana kutoamini kile alichokisikia. Akaandika alichokuwa akikiandika. Kisha aliahirisha kesi kwa kupanga tarehe ya hukumu.

Tukarudishwa mahabusu. Huko nilikuwa gumzo kubwa. Kila mtu aliyesikia kilichotokea mahakamani alitaka kuniona kwa macho na kuisikia sauti yangu.

“Pole sana, mdogo wangu,” mzee mmoja aliyekaa rumande kwa miaka tisa sasa aliniambia. “Hivi hujaambiwa kuwa hata kukubali kosa ni kosa? Maana yake ni kwamba ulifanya kosa huku ukijua kuwa unafanya kosa. Adhabu yake ni kubwa sana. Humu, wewe anza kutafuta kona yako ambapo utalala kwa miaka ishirini. Halafu huonekani kama mtu wa kumudu chawa, kunguni na chakula cha ajabu kinachotolewa.”

Nadhani nilikuwa nimechanganyikiwa kwani haikuniingia akilini uzito wa mkasa uliokuwa mbele yangu hadi siku ya hukumu. Hakimu, akiwa mkali kama pilipili, alitumia zaidi ya dakika arobaini kuelezea athari za ujangili

kwa wanyamapori hasa wale adimu kama faru. Alitoa mifano ya nchi mbalimbali za dunia ambazo zimeweka sheria kwa ajili ya kuwalinda wanyama ambao wanazidi kutoweka siku baada ya siku.

“Tumeirithi nchi hii ikiwa na mazingira murua, wanyama na ndege tele. Tumerithi hayo kwa kuwa babu zetu hawakuwa waharibifu wala katili kwa wanyama. Tunahitaji watoto na wajukuu zetu nao warithi hali ile tuliyoikuta. Kwa bahati mbaya baadhi yetu wametia pamba masikioni mwao. Wanapuuza jitihada zote za serikali na dunia kwa matarajio ya maslahi yao binafsi. Hawa lazima wawe mfano kwa wengine kwa kupewa adhabu kali,” hakimumu alisema.

“Kesi iliyo mbele yangu inamhusu Petro Mtukwao Kionambali na Daniel Mbonea. Hawa walikamatwa na askari wa wanyamapori waliokuwa wakitelekeza jukumu lao la kumlinda kifaru huyu mwenye mtoto. Kwa ukatili mkubwa walimpiga risasi na kumwua.”

“Katika maelezo yao hapa mahakamani na hata yale ya awali, Mbonea alikataa kuhusika na mauji haya. Anasema kuwa alimtembelea rafiki yake huyo mbugani baada ya kufahamiana naye mjini Moshi na Arusha bila kujua kuwa kazi yake ni uwindaji wa vifaru. Kuwa kifaru yule mwenye mtoto alipotokea alimwona akiandaa bunduki na kutaka kumwua. Alimtahadharisha lakini Kionambali hakumsikiliza. Alifyatua risasi na kumwua kifaru yule. Kwa upande wake Kionambali mwenyewe katika maandishi na maelezo ya ana kwa ana mahakamani amekiri yote yaliyotokea. Hivyo, mahakama inamwachia huru Daniel Mbonea. Aidha, inamuhukumu Petro Mtukwao kifungo cha kwenda jela miaka ishirini na kazi ngumu na viboko kumi, ili awe mfano kwa wengine.”

Sikuelewa. Nilimwona Mbonea akibebwa juujuu na ndugu zake huku wakishangilia. Mimi nilitiwa pingu, nikasukumwa kuelekea kwenye gari la magereza ambako nilipandishwa na kurejeshwa Kilimanga ambako nilivuliwa mavazi ya uraiiani na kuvishwa yale ya gereza yenye namba na tarehe yangu ya kufunguliwa. Niliondolewa katika chumba cha mahabusu na kuelekezwa katika selo nyingine ambayo ingekuwa makazi yangu hadi mwisho wa kifungo changu. Kama ile ya mahabusu hii pia haikuwa na kitanda wala godoro. Nilipewa blanketi kuukuu na kuelekezwa mahala pa kulala. Juu ya sakafu ngumu. Kona moja ilikuwa na kijichumba kidogo chenye harufu kali ambacho kilitumiwa kama choo na bafu. Mlikuwa na bomba lakini halikupata kutoa walao tone moja la maji!

Nilitoka nje na kuketi mahala fulani nikiwa nimejiinamia. “Pole sana,” nilisikia sauti ikiniambia. Nikatazama. Alikuwa yule mzee wa miaka tisa mahabusu. “Nilikuuliza kama unamwamini mshtakiwa mwenzako hukupata kunijibu,” alisema na kuendelea, “Yule kakuuza rafiki yangu. Kesi yenu ilikuwa mbaya sana. Ilikuwa lazima mtu afungwe. Amekuchezea akili umefungwa wewe, yeye ametoka.”

“Kwa vipi?” niliuliza “Mbona mtu mwenyewe alikuwa mtu wa kulialia muda wote?”

“Kulia!” mzee alisema akicheka. “Kama alikuwa analia kweli basi yalikuwa machozi ya mamba. Alikuwa akikuchota akili huku akikucheka. Kwa bahati mbaya, wewe ulishiriki kumrahisishia azma yake kwa kukiri hili na lile. Hilo limemfanya atoke haraka kuliko alivyotegemea.”

Machozi ya mamba! Niliwaza kwa mshangao.

SURA YA ISHIRINI

Jela miaka ishirini

Mfikirie mtoto mdogo sana wa kiume, aliyeondoka kwao zamani sana kuiokoa roho yake, mtoto ambaye alifuatana na babu yake, wakavuka misitu na nyika, milima na mabonde, mito na mabwawa hadi nchi ya mbali. Huko mtoto aliona nuru mpya elimu. Akaanza kusoma huku akiwa na matumaini.

Mtoto huyu, ambaye kwa miaka nenda miaka rudi alikuwa hajazitia machoni sura za wazazi wake wapenzi, wala kuonana na babu yake kipenzi, majuzi tu alikwishafikia uamuzi wa kurejea nyumbani. Na alitarajia kupokelewa kishujaa kwani akiba yake benki ilikuwa ya kuridhisha. Angeweza kujenga nyumba ya kisasa na kutoa zawadi nyingine tele ambazo zingefanya ukoo mzima umshangilie. Lakini, kwa mara nyingine tena likatokea jambo jingine, kubwa kuliko yote yaliyopata kutokea. Na sasa yuko kifungoni. Hategemei kutoka kabla ya miaka ishirini! Hategemei kuwakuta wazazi wake wakiwa hai! Yeye mwenyewe hategemei kutoka akiwa hai!

Mtoto huyo ni mimi, Petro Mtukwao Kionambali. Tayari miezi miwili ilikuwa imepita toka nianze kutumikia kifungo. Miezi miwili! Ilibakia miezi isiyopungua mia mbili thelathini na nane, nikiwa ndani ya chumba hiki kinachonuka, nikilala juu

ya sakafu hili gumu na kula chakula chao kisikolika! Mara kwa mara wafungwa wenzangu walinishauri nijitahidi kuyazoea maisha ya jela, lakini yalikuwa hayazoeleki. Binadamu gani atazoea kula mlo mmoja, tena usioridhisha, kwa siku? Binadamu gani atazoea kula saa kumi na moja jioni, katika chumba kisicho na madirisha na kutoipata tena hewa ya nje hadi kesho yake?

Niliteseka sana kialikili zaidi ya kimwili. Nilitafakari kwa nguvu zangu zote na kushindwa kabisa kutambua kitu gani kinafanya siku zote niwe kondoo wa kafara. Sikuweza kuelewa kwa nini nilikwenda Kilimanjaro na kukutana na 'Mpare' Daniel Mbonea. Sikuweza kuelewa kwa nini nilikubali kushawishika hata nikafuata ushauri wake na kuahirisha dhamira yangu ya kurejea nyumbani Buha na badala yake kuingia naye porini kuwinda nyara za serikali. Zaidi sikuweza kuelewa kabisa sababu iliyofanya nijisikie kumhurumia kiasi cha kumlinda kwa kujitoa kuwa ni mimi niliyefyatua risasi ya kumwua kifaru kutokana na madai yake ya kutegemewa na bibi kizee na dada kiwete? Mie pia si nilikuwa na babu kizee na ndugu vilema wengi tu ambao walinitegemea. Machozi yake ya mara kwa mara? Mie pia ningeweza kutokwa na machozi siku nzima kama ningependa. Kwa kweli sikuweza kabisa kuelewa sababu.

Hisia za siku nyingi, ambazo nilianza kuzisahau zilinirejea. *Hirizi iliyopotea!* Nilianza kueleka kuamini kuwa chanzo cha balaa na mikosi yangu ni kuipoteza hirizi ile ambayo babu alinihusia kuitunza. *Una alama... alama ya shari...* Niliyakumbuka tena maneno niliyoambiwa kule Sumbawanga na Mbeya. Pengine ni kweli? Pengine alama hii ndiyo iliyomvuta Mbonea? Iwe kweli iwe uongo, niliwaza,

kwa vyovyote vile ilihusiana na hirizi yangu iliyopotea. Kama ningekuwa nayo, niliendelea kuwaza, mtu yeyote mwenye nia mbaya nami asingenisogelea. Kamwe nisingewekwa alama!

Majuto ni mjukuu! Niliwaza. Nilikuwa na miaka isiyopungua ishirini ya kuishi katika gereza hilo huku nikiwaza hayo. Mawazo ambayo yangeweza kunitia kichaa. Lazima nijifunze kuachana nayo. Lazima nipate jambo jipya la kuwaza badala ya kukodolea macho kalenda nikiitafuta siku ambayo ingechapishwa baada ya miaka ishirini.

Nilijitahidi pia kumfukuza Mbonea katika fikra zangu. Bwana huyu alikuwa mtu wa ajabu sana. Alikuwa mnaifi asiye na haya kuliko binadamu wote niliopata kuwafahamu. Siku tatu tu baada ya yeye kupata uhuru wake na mimi kuanza kutumikia kifungo alikuja gereza kuniona. Niliarifiwa kuwa nilikuwa na mgeni, sikuambiwa mgeni huyo alikuwa nani. Pengine nisingekwenda. Nikamkuta kakaa kitako akinisubiri. Alikuwa anang'ara mwili na mavazi, hali iliyofanya nijishuku kuwa nanuka jasho na uchafu wa nguo zangu.

Nilimwona akitafuta chozi la kunionyesha uchungu aliokuwa nao kwangu. Halikotoka. Sikuwa tena mgeni wa machozi yake ya mamba. Nilitamani kucheka. Hakunipa nafasi hiyo. Aliinuka na kunikumbatia bila ridhaa, kisha akanipa mkono wake wa kulia ambao muda wote alikuwa ameufumba. Nikaupokea na kubaini kuwa katika kunipa mkono huo alinipa kitu fulani kilichokuwa kiganjani. Nikaufungua mkono kutazama. Alikuwa amenipa kipande cha aina fulani ya jani.

“Nini hiki?” Nilimuuliza

“Jani.”

“Jani la nini?”

“Jani la isale,” alinijibu.

Nililifahamu jani hilo. Isale ni majani uhimu sana kwa Wachaga. Hutumiwa kupanda katika mipaka ya mashamba, kuepusha migongano. Lakini jani hilo pia hutumiwa kwa upatanishi. Mchaga anapomfuata mwenzie kwa suala zito kama kuombana radhi, kudaiana na hata ndoa huweka jani hilo mkononi na kumshikisha mwenzi huyo kabla ya mazungumzo ya siri. Mara nyingi baada ya kitendo hicho mazungumzo huwa ya amani na mafanikio kwa pande zote mbili.

“Unanipa isale ya nini?” nilimuuliza.

“Nataka kukuomba radhi kwa yote yaliyotokea,” alisema. “Nataka tuendeleo kuwa ndugu. Ndiyo, uko ndani niko nje. Nitautumia uhuru wangu huko nje kuhakikisha hukai ndani zaidi ya miezi mitatu. Nitahakikisha...”

“Umenipa isale ya nini?” nilimkatiza kwa ukali kidogo. “Mimi sio Mchaga na wewe sio Mchaga pia, kama ulikuwa ukisema ukweli.”

Mbonea alikohoa kidogo kabla hajanijibu akisema, “Ni kweli mimi sio Mchaga. Lakini sisi Wapare wa Ugweni tuna tamaduni nyingi zinazofanana na Wachaga. Moja ni jani hili. Tunalitumia katika upatanishi na mengineyo.”

Nilimtaazama kwa makini mtu huyu. Alikuwa Mbonea yuleyule mwenye sumu ya nyoka na hila za kinyonga. Sikuona sababu za kuendelea kumsikiliza. Nikamwambia, “Sikiliza Mbonea. Mimi sio malaika. Mimi sio Yesu Kristo ambaye aliwaelekeza wanafunzi wake wakipigwa shavu moja wakinge na la pili. Mimi ni binadamu kama wewe. Naomba uondoke. Naomba usikanyage tena hapa kwa niaba yangu.”

Nadhaini hakunielewa. Nilimwona kaduwaa, hajui lipi zaidi aseme. Nilimwacha katika hali hiyo na kurudi katika ‘utumwa’ wangu wa miaka ishirini.

Siku mbili tatu baadaye nilipata ugeni mwingine. Huyu alikuwa mwanamke. Alikuwa mnene, maji ya kunde. Sura yake nzuri haikuwa na dalili zozote za dhiki wala misukosuko ya maisha. Alifuatana na watoto wawili wa miaka saba au minane, mapacha.

“Mgeni wangu?” Nilimuuliza.

“Ndiyo. Wewe si Petro Kionambali?”

“Ndiye.”

Basi mimi ni mgeni wako. Nimetumwa na rafiki yako Daniel Mbonea nikuletee chakula. Ameniagiza nikutembelee mara mbili kila wiki na kukuletea mahitaji yako yote muhimu.

“Mbonea!” Nikaropoka. “Wewe ni nani kwake?”

“Mimi ni mkewe.”

Sikuyaamini masikio yangu, “Mkewe?” Nikauliza kuhakikisha. “Mke wa ngapi?”

“Kwani alikuambia anao wake wangapi?”

“Ninachofahamu ni kwamba hana mke. Mkewe alifariki zamani kwa kujinyonga.”

Ikawa zamu ya mama huyo kushangaa. “Mkewe alijinyonga?”

Kisha akaangua kicheko. “Bila shaka alikuwa akikutania. Tumeoana toka tukiwa vijana, sasa tunaelekea uzeeni. Hana mke mwingine, hana mke aliyepata kujinyonga.”

Niliduwa kwa muda. “Na hawa watoto? Unataka kuniambia kuwa ni wake?”

“Ndiyo. Ni watoto wetu. Alikuambia hana watoto?”

Nilishindwa kumwambia kuwa kwa mujibu wa Mbonea mwenyewe watoto wake pacha walikufa zamani kwa utapiamlo. Nilishindwa kuuliza juu ya bibi kizee na dada yake kiwete wanaomtegemea. Sikuhitaji kuhakikishiwa kuwa yote

aliyosema ulikuwa uongo, uongo mtupu, uongo uliokusudiwa kunitia huruma ili nishawishike kushirikiana naye katika dhamira yake chafu ya kutafuta utajiri.

“Mama, nashukuru sana,” nilimwambia. “Naomba umrudishie chakula chake. Halafu, tafadhali mwambie, sihitaji msaada wake wa aina yoyote si leo si kesho wala keshokutwa.”

Nikageuka na kuondoka zangu.

Nilimwacha mama huyo kaduwaa, haelewi kinachoendelea. Laiti angejua kuwa aliolewa na nyoka...

* * *

Gerezani kuna kiu. Kwangu kiu hiyo haikuwa ya vinywaji baridi au vinywaji laini. La, hashu! Ilikuwa kiu ya habari. Gerezani kuna njaa. Lakini njaa yangu mimi haikuwa ile ya chakula chao kibovu, ilikuwa ya kuona na kusikia kile kinachoendelea nje ya ukuta huo imara wa gereza la Kilimoanga. Kwangu hiyo ilikuwa adhabu kubwa zaidi na inayonitesa zaidi. Kwa nia ya kukidhi adha hiyo nilijenga urafiki na mfungwa mmoja kwa namna ya ajabu. Alikuwa na redio ndogo.

Kwa bahati mbaya, bwana huyu alipenda sana kusikiliza muziki. Mara kwa mara alitafuta stesheni zinazopiga muziki wa kina Mbaraka Mwinshehe na Salumu Abdallah. Nyimbo za ‘malaika’, ‘wanawake wa tanzania’, ‘mwanameka!’ ‘shida na Marijani Shabani’ zilikuwa mdomoni mwake kila dakika kufuatia mipigo redioni. Ilikuwa kazi ngumu kumshawishi mara chache aniruhusu kusikiliza taarifa za habari na vipindi vingine makini zaidi.

Ni kwa kupitia redio yake hiyo nilipofahamu kuwa Zanzibar, nchi ambayo ilitawaliwa na waarabu kwa muda mrefu, nayo ilikuwa ikiwaka moto kwa vuguvugu la kudai kujitawala.

Chama kilichoitwa Afro Shiraz kilikuwa kimeanzishwa na kuwapa taabu kubwa watawala.

Aidha, nilibaini kuwa hesabu ya watu ilifanywa mwaka 1957chini Tanganyika ilionyesha kuwa tulikuwa 9,087,6000 kati ya hao 364,072 au asilimia 4 tu wakiishi mijini.

Mwaka wa 1958 zikasikika habari za Julius Nyerere kushtakiwa mahakamani kwa kuandika katika gazeti la TANU, *sauti ya TANU*. Habari ambazo magavana wawili wa wilaya walidai kuwa ziliwadhalilisha. Nyerere alishinda shitaka moja na kutiwa hatiani kwa shitaka la pili. Adhabu yake ilikuwa kifungo cha miaka sita jela au faini ya shilingi 3,000/= alilipa faini. Kama asingelipa uenda tungejumuka naye gerezani humo.

Tukio hilo lilikuwa kama chachu ya matukio tele ya kisiasa yaliyoendelea kutumbuiza maisha yetu gerezani humo. Zilisikika habari za TANU kuchachamaa katika kudai uhuru. Zikasikika habari za chama kipya, ANC, kilichoongozwa na Zuberi Mwinyishehe Mtemvu, pia kiliomba ridhaa ya wananchi kuongoza serikali. Hatimaye, ikaja ile siku ya siku, desemba 9, 1961 tulikesha tukisikiliza redio, sauti ya Dar es salaam iliyokuwa ikitangazwa na bwana mmoja, Hamza Kasongo, kusheherekea uhuru. Ilipotimia saa sita za usiku tulisikiliza taarifa za bendera ya malkia wa Uingereza ikishushwa na ile ya Tanganyika ikipandishwa, Julius Nyerere akiwa Waziri Mkuu wa kwanza.

Pilikapilika hizo hazikuwa Tanganyika pekee. Kenya na Uganda pia kulikuwa kukiwaka moto. Lakini tukio lililongusa ni lile la visiwa vya Zanzibar, Unguja na Pemba. Huko nako kulikuwa na purukushani kali za kisiasa. Mtu mmoja aliyeitwa Abeid Aman Karume na chama chake cha Afro Shiraz alikuwa

akusuguana na vyama vya ZPPP na ZNP. Uchaguzi uliojaa hila ulifanyika na kutoa madaraka kwa vyama vile vilivyokuwa na ushawishi mkubwa wa Waarabu dhidi ya Afro Shiraz iliyoshindwa kwa asilimia 54.3 Januari 12, 1964 visiwa hivyo vililipuka, Waarabu wakatimuliwa, Karume na chama chake wakachukua uongozi.

Aril 21, 1964, pamoja na kuwa mfungwa nililala nikiwa Mtanganyika, kesho yake nikaamka nikiwa Mtanzania. Hiyo ilifuatia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao uliambatana na kubuniwa kwa jina jipya la nchi.

Nikiwa mfungwa kutokana na tuhuma za kuharibu maliasili na urithi wa taifa masikio yangu hayakuwa wazi kwa habari za kisiasa pekee. Nilitegemea siku hiyo habari zote zilizohusiana na mazingira, misitu na viumbe wake, maziwa na vyote vilivyomo na hata hali ya hewa. Kila nilipofanikiwa kupata gazeti nilifurahi zaidi na kulisoma lote, ikiwa pamoja na mashairi na kujaribu kujaza mafumbo.

Kupitia gazeti moja zile jitihada zilizobuniwa mwaka 1954, za kupandikiza aina mpya ya samaki katika ziwa Nyanza, ambalo sasa liliitwa Victoria, lilikuwa limetiliwa mkazo zaidi mwaka 1960 na kwamba jaribio hilo lilianza kutoa matunda. Hata hivyo, kulikuwa na malalamiko mengi toka kwa wana mazingira mbalimbali duniani kuwa samaki hao ambao ni wakubwa zaidi walikuwa wakiwateketeza samaki wa asili kwa kuwala. Hali ambayo ilielezewa kuwa iliashiria kuwa aina zipatazo hamsini za samaki wa ziwa hilo zilikuwa hatarini kutoweka.

Kwa upande mwingine nilijifunza kuwa serikali ilikuwa imeongeza jitihada za kuwalinda wanyama, miti na misitu asilia. Pamoja na Serengeti maeneo kama Ngorongoro, Ziwa Manyara,

Tarangire, Mikumi, Rubondo, Udzungwa na mengineyo tayari yalisajiliwa kama hifadhi maalumu za taifa. Maeneo mengine yalikuwa pamoja na Selow, Kilimanjaro, Gombe, Mahele na Katavi.

Hali kadhalika, mapori na misitu kadhaa ilihifadhiwa kwa ajili ya urithi. Selow yenye ukubwa wa takriban kilomita za mraba 50,000 ikiwa na maana kuwa inazishinda nchi kama Switzerland au Denmark kwa ukubwa lilikuwa eneo mojawapo. Ikiwa haina mtu anayeishi huko wala shughuli zozote za kibinadamu zinazofanyika, Selow inakadiriwa kuwa na tembo wapatao 60,000, nyati 160,000, viboko 40,000 na simba 5000. Pamoja na wanyama wengine anuai Selow inakisiwa kuwa na aina 440 za ndege. Ziwa Tagalala mto Rufiji, miti ya miombo na migunga pamoja na misitu inayoambaa na mito ni baadhi ya vivutio vinavyotajwa katika hifadhi hiyo.

Mapori mengine yaliyoifadhiwa yalikuwa pamoja na Moyowosi, Bugiri, Rungwa, Maswa, Kisiwa cha Saa Nane, Mkomazi na Ugala. Pia Usangu, Mpanga, Rukwa, Swaga, Ikorongo ni miongoni mwa mapori hayo.

Huko Zanzibar pia jithada tele zilikuwa zikifanyika kulinda mazingira ya nchi kavu na bahari. Pomboo, viumbe wa majini ambao wataalam hawapendi kuwaita samaki kwa kuwa wananyonyesha watoto wao, walikuwa wakitafutiwa namna ya kuwalinda. Vifo vya mara kwa mara vya viumbe hao, ambao ni wahamajihamaji vilikuwa vikisumbua sana vichwa vya wana mazingira. Viumbe hao, ambao wanafundishwa kwa urahisi hasa pale wanapochupa toka majini kama golikipa anayedaka mpira wanaweza kuwa kivutio kikubwa cha watalii.

* * *

Pamoja na ‘alama’, kama kweli nilikuwa nayo nyota yangu ya kupendwa na watu bado ilikuwa iking’ara, hali ambayo naamini ilichangia kufanya niweze kuyamudu maisha ya gerezani humo hadi mwisho wa kifungo. Wakati wenzangu wengi walipigwa kama ng’ombe, baadhi wakifa kwa kutiliwa maanani wanapougua, mimi hali ilikuwa tofauti. Nilipendwa na mkuu wa gereza. Nilipendwa na maafisa wake pia. Nadhani kale ka usomi kangu kalisaidia. Mara kwa mara nilipewa kazi ya ukarani, kujaza fomu, kurekodi matumizi au mahitaji, kuandaa taarifa za wafungwa wenzangu na kadhalika. Kazi hizo zilipokuwa finyu nilipewa udobi wa kunyoosha nguo za askari magereza. Mara nyingine nilipewa kazi ya kutunza bustani ya mkuu wa gereza ambazo ziliambatana na kudokolewa chakula cha binadamu toka jikoni mwake.

Sherehe za uhuru na zile zilizofuatana mara kwa mara ziliambatana na kuachiwa kwa baadhi ya wafungwa wenye makosa madogomadogo au ambao tarehe zao za kufunguliwa zilikaribia. Bahati hiyo mimi haikunipitia. Uzito wa kosa langu haukuruhusu kunijadili katika kundi hilo. Kama ungeruhusu naamini nisingekuwa na sababu ya kusubiri tarehe iliyobandikwa kifuani pangu.

Uhuru wenyewe ulianza kunitia mashaka kabla sijauonja. Tulitarajia uhuru ulikuwa mwisho wa kero zote za Mtanganyika, ambaye sasa aliitwa Mtanzania. Tulidhani uhuru ungekuwa mwanzo wa neema na faraja kubwa nchini. Haikuwa hivyo. Nyimbo za hali ngumu ya maisha toka huko uraiani zilitushangaza sana wafungwa. Tulishangaa zaidi pale kasi ya watuhumiwa waliokuwa wakiletwa gerezani ilipoongezeka badala ya kupungua, wengi wakiwa watu wenye makosa ya ovyoovyo yaliyoashiria jambo moja kubwa ‘njaa!’

huyu kampiga mke wake hadi kumwua kwa kupoteza shilingi mia! Yule kafungwa kwa kuiba kuku wa jirani. Na Yule? Yeye alitupa kitoto kichanga jalalani!

Kasi hiyo, ilifanya selo zifurike, tuanze kulala ‘mzungu wa nne’. Huyu aliweka kichwa huku yule kule. Chakula kiliongezeka ubaya, hata hewa katika selo ilibadilika na kuwa nzito kutokana na kutumiwa na watu wengi kuliko ilivyokusudiwa.

Nadhani ni hali hiyo iliyoibua tatizo jingine zito zaidi, ‘maradhi.’ Zamani kidogo ugonjwa mkubwa gerezani ulikuwa malaria. Mara yaliingia maradhi mapya ya kipindupindu. Ugonjwa hatari wa kuharisha ambao ulimchukua binadamu siku mbili tu kupoteza maisha.

Wafungwa wengi walipoteza maisha, kutwa watu sita au zaidi hadi ulipodhibitiwa kwa vidonge vya kufunga tumbo. Tuliambiwa ugonjwa huu hatari chanzo chake kilikuwa uchafu. Lakini kutokana na shida ya maji gerezani humo, naamin tuliobakia hai ilikuwa kwa kudra za Mwenyezi Mungu zaidi ya jitihada za kujikinga.

Habari za kipindupindu humo nje ya gereza pia zilivuma sana. Dar es salaam, Dodoma, Singida na kwingineko kipindupindu kiliteketeza maisha ya watu kama watu wa kusini wanavyoshambulia ‘dagaa nchanga’ au Wahaya wanavyowaonea ‘nsenene’. Sikuelewa hata kidogo kila nilipofikiria hilo. Watanzania tuteketee kwa uchafu kwa ajili ya uhaba wa maji! Nchi ambayo imezungukwa na maji kila upande, ikajaliwa mito, maziwa, mabwawa na chemchemi tele! Kwa kweli sikuweza kuelewa.

Wakati bado natafakari hilo, likaja jingine la kutisha zaidi, UKIMWI. Ugonjwa ambao wataalamu walidai kuwa

ulitokana na wadudu wanaoitwa HIV ambao hushambulia chembechembe nyeupe ambazo ni kinga ya mwili wa binadamu na kumwacha wazi kwa ugonjwa wowote kumtia mweleka wa mwisho. Niliwaona baadhi ya wafungwa wenye UKIMWI. Wanatisha kuliko chochote kile ulichopata kukiona. Nywele zao zilinyonyoka, mwili kuota mapele huku tumbo likiwa halina uwezo wa kuhifadhi chochote kutokana na kuharisha. Kama kipindupindu kiliogopwa kwa kuua haraka UKIMWI uliogopwa zaidi kwa kuchelewesha sana kumwua mteja wake huku ukimpa kila aina ya mateso.

Wajuzi wa masuala ya tiba walitueleza kuwa njia kubwa zaidi ya maambukizi ya UKIMWI ni katika kujamiiana bila kutumia kinga. Jambo ambalo mtu yeyote angeweza kulielewa mara moja na kujiepusha nalo. Lakini taarifa ya tatizo hilo huko nje lilikuwa kubwa na la kutisha kupita kiasi. Haikupita siku mbili bila kumsikia mfungwa mmoja wapo akiangua kilio. Kisa? Kafiwa na mdogo wake, mtoto wake, mke wake au rafiki yake. Taarifa za wasichana kujiuza katika majumba ya starehe, akina baba wenye pesa kuwarubuni wanafunzi, kuzagaa kwa mabaa na sehemu za starehe mitaani na vishawishi tele vya anasa ziliendelea kutufikia gerezani humo kwa kiwango kilekile cha kukua kwa kasi ya UKIMWI. Hali iliyoashiria kitu kimoja tu, hali ngumu maisha. Kwa lugha nyepesi; njaa!

Wakati huo tarehe yangu ya kumaliza kifungo ilizidi kukaribia. Siyo siri kwamba nilianza kuyaogopa maisha ya huko uraiani zaidi ya gerezani. Kama mazingira ya gerezani humo yangeweza kuboreshwa kidogo tu siyo siri, ningefikiria suala la kubaki gerezani humo wa makini zaidi.

SURA YA ISHIRINI NA MOJA

Mfungwa Asiye Na Mikono Toka Musoma

Wanahistoria wanatukumbusha kuwa adhabu ya kifungo, ambayo mimi na wenzangu gerezani humu tulikuwa tukiitumikia, ilianzishwa huko Ulaya yapata miaka 300 iliyopita.

Awali ya hapo mhalifu, au mtuhumiwa aliyepatikana na hatia ama alinyongwa ama alitoswa baharini au kuachwa katika visiwa vya mbali visivyo na watu.

Hapa Afrika pia tulikuwa na adhabu zetu mbalimbali. Mhalifu alilazimishwa kutoa baadhi ya mali zake kama adhabu, kutengwa na jamii yake hata kufukuzwa kijijini. Wakati mwingine alitungiwa nyimbo za mafumbo ambazo ziliimbwa katika sherehe na hivyo kumdhalilisha sana mbele ya jamii. Hali hiyo ilipunguza sana tabia ya uhalifu.

Hivyo, wageni walipoingia na kutushawishi kufuata dini na tamaduni zao kwa upande mmoja, upande wa pili walitushurutisha kutii sheria na adhabu zao. Moja ya adhabu hizo ni hili la gereza. Unakamatwa na mtu anayeitwa polisi, unapelekwa kwa mtu anayeitwa hakimumu, kufumba na kufumbua uko mikononi mwa bwana magereza; ukifanya kazi ambazo hulipwi na kupewa chakula ambacho hushibi.

Ni katika hali hiyo tuliposhangazwa siku moja alipoletwa

mfungwa asiye na mikono gerezani humo na kuanza kutumikia kifungo chake cha miaka thelathini. Gereza lilikuwa kubwa, lenye wafungwa tele, hivyo ilinichukua siku tatu nikisikia tu habari za mfungwa huyo bila kumwona kwa macho. Anakulaje? Anaogaje? Anavaaje na kuvua nguo zake? Nilijiuliza. Lakini swali kubwa zaidi lililonisumbua akili yangu ni pale nilipotaka kujua ni kitu gani kilimsibu mpaka akaipoteza mikono yake yote miwili. Kitu gani hasa kilimtokea? Gereza lilijaa simulizi tele juu yake. Mara anakula kwa kutumia miguu yake, mara hapana, anumia kinywa chake pekee na kadhalika. Mara aliiba, akakatwa mikono, mara hapana, alizaliwa kama alivyo.

Nilipokutana naye kwa mara ya kwanza nilishituka sana. Maumbile ya binadamu yana utaratibu wake. Akiwa na viungo vyake vyote binadamu anavutia macho. Akipoteza baadhi ya viungo vyake anatisha. Ndivyo nilivyomwona bwana huyu. Alionekana mrefu kupita kiasi, mwembamba kupita kiasi. Kwa ujumla, alionekana kama mnazi mrefu mweusi, unaotembea na kuzungumza. Uhai mkubwa zaidi katika umbo hili la kutisha ulikuwa katika sauti yake nzito na meno yake meupe ambayo yaling'ara sana kila alipozungumza.

Alikuwa akicheka!

Nilimkodolea macho ya mshangao, pale kwenye kundi la watu walioketi nao wakisikiliza simulizi ambazo sina shaka zilisisimua sana, kwani kila mtu alikuwa akimsikiliza kwa makini huku baadhi wakicheka. Alikuwa akitoa kichekesho. “Baba akamwambia mwanaye, ‘Toto jinga sana wewe. Kwa umri wako huo Idd Amin alishakuwa mkuu wa majeshi ya Uganda.’

“Mtoto akamjibu, ‘Na kwa umri wako huo alishakuwa Rais wa Uganda. Wewe mbona bado tarishi?’

Mie pia niliangua kicheko. Mchekeshaji huyo akageuka kunitazama. Akanikazia macho. Mara nikamwona akiachia tabasamu pevu zaidi huku akiinuka kunifuata.

“Petro!”

Aliniita. Sikuelewa. Nikamtolea macho ya mshangao.

“Petro, hunikumbuki?”.

Nilitikisa kichwa kukataa.

“Humkumbuki Umsolopogaas?”

“Umsolopogaas mwenyewe?”

“Naam, Mzulu halisi. Kiboko ya Wajivuni.”

“Kwa jina halisi Matayo Butiku?”

“Naam. Mathew Butiku halisi.”

“Mang’ana” nilimjibu.

“Mayia.” Alijibu akicheka.

Sijapata kupigwa na mshangao kama ule. Tuliishi na Matayo katika bweni moja tukiwa katika darasa moja kwa takribani miaka minne. Siwezi kusema kuwa alikuwa rafiki yangu, lakini hakupata kuwa adui yangu. Kwa kweli, alikuwa rafiki wa kila mtu. Utundu wake, ucheshi wake na vituko vyake ndani na nje ya darasa vilifanya awe rafiki wa kila mtu, walimu na wanafunzi, jambo ambalo nadhani lilimsaidia sana kushinda mitihani yake, kwani kidogo kichwa chake kilikuwa kizito kuelewa, lakini akawa mwepesi wa kuibia. Hata uifiche vipi kazi yako Matayo atapenyeza jicho lake na kuchopoa jibu.

Kipi kilimtokea? Nilijiuliza. Alikuwa kijana aliyekamilika, kwa miguu na mikono ambayo haikupata kutulia. Nakumbuka alipenda sana vitabu vya riwaya, hasa zile za mashujaa. Na alipenda kudandia majina ya wahusika wa riwaya hizo. Kuna wakati tulipewa vitabu vya someni bila shida, mara mwenzetu akaanza kujiita ‘Bulicheka, kiboko ya Wagagagigikoko.’

Tukaletewa *Safari ya Sindbad*. Mara mathayo akawa ‘Baharia Sindbad.’ Muda si mrefu akasoma *Alfu lela U lela*, akawa ‘Mfalme Harun Radhid wa Baghdad.’ Aliposoma hadithi ya *Allan Quatermain*, akavutiwa na yule mzee wa Kizulu, akaachana na jina la umbopa alilolipata katika *Mashimo ya Mfalme Suleiman* na kuwa ‘Umsolopogaas,’ jina ambalo naona amedumu nalo hadi leo. Hata kabati lake la shule aliweka vitu ambavyo vilipigwa marufuku shuleni hapo; panga, kisu, rungu na shoka ambalo aliliita *inkoskaaz*.

Aliponifikia, Matayo alitaka kunikumbatia. Haikuwa rahisi. Mikono yake iliyokatika juu ya viwiko ilichoweza kufanya ni kunipapasa kidogo tu mgongoni. Ni mimi niliyeweza kumkumbatia kikamilifu.

Tukaachana na kutazamana kwa muda.

“Nini kimetukia Matayo?”

Kwa mshangao wangu alicheka tena. “Ni hadithi ndefu,” alijibu na kuongeza. “Tutatafuta muda tukae mahala nikusimulie.” Akasita kumeza mate. “Na wewe kilikutokea nini?”

“Ni hadithi ndefu vilevile,” nilimjibu.

“Au ndio ile hirizi?”

“Hirizi gani?”

“Yako. Ile iliyopotea. Unajua iliokotwa ikachomwa moto lakini ikakataa kuungua? Nasikia mapadre wameipeleka Ujerumani kuifanyia utafiti.”

Nikajisingizia kutabasamu. Kichwani niliwaza jambo moja tu: Babyabato hakusema uongo. Hirizi yangu iliokotwa tena!

Wafungwa waliotuzunguka walionyesha kuvutiwa na taarifa hizo. Wakaanza kusogea ili kutusikiliza vizuri zaidi.

Nikasema, “Itabidi tutafute muda tukae na kusimuliana masaibu yetu kwa kituo.”

“Kuna ubaya gani?” Butiku alijibu.

* * *

Mkoa wa Mara unapakana na nchi ya Kenya kwa upande wa kaskazini. Mkoa huo ambao unachangia neema ya ziwa Victoria na mikoa ya Mwanza na Kagera, Mashariki umepakana na mkoa wa Serengeti. Mji wa Tarime, alikozaliwa Matayo Butiku, au ‘Umsolopogaas’ kama anavyopenda kujiita, uko mpakani na Kenya. Mji huu ni maarufu kwa pilikapilika nyingi kama ilivyo miji mingine ya mipakani kama Namanga, na Tunduma uko katika wilaya ya Tarime, kando kidogo ya mpakani, Sirari.

Mkoa huo una sifa zote ambazo nchi hii imejaliwa; mvua za kutosha, ziwa lililojaa samaki, ardhi iliyojaa rutuba na mbuga za wanyama kama Ikorongo, Nata na baba lao; Serengeti.

Mara una makabila mengi ya asili na wahamiaji. Ya asili ni Wakurya, Wazanaki, Wajita na Wajaluo ambao pia, kama Wamasai, wana mizizi yao nchini Kenya. Wahamiaji ni pamoja na wahindi, Wanyarwanda, Warundi, Wahangaza na wengineo.

Pamoja na sifa tele za neema katika nchi yao, watu wa Mara, hasa Wakurya wamerithi maradhi ambayo hadi leo tiba yake haijapata kupatikana; Ubabe. Mauaji na vita vinavyoitwa vya kikabila, ambavyo kwa kweli ni vita baina ya koo ndani ya kabila moja, vimekuwa vikitawala macho na masikio kupitia katika vyombo vya habari. Vijiji, kama Kubitarere, ni miongoni mwa vile ambavyo vimeathirika mara kwa mara na ubabe wa baadhi ya wanajamii wa ama Waachari ama Walyanchoka.

Kisa? Ama hawa wameshukiwa kuiba ng'ombe wa hawa, ama wamevamia shamba la hawa. Vita vitazuka, watu wanapoteza maisha, mashamba yanachomwa, nyumba zinabomolewa na uharibifu mwingine tele usio na kifani. Mara nyingi serikali, kupitia vyombo vyake vya usalama pekee ambayo huingilia vita hivyo na kuituliza. Lakini si kwa muda mrefu.

Ni mirathi hiyo ya hatari ambayo ilimgharimu rafiki yangu Matayo Butiku mikono yake yote miwili na kumpa kilema cha maisha.

Ilikuwaje?

Zilikuwa zimepita siku mbili toka nilipomtia machoni kwa mara ya kwanza akiwa katika hali ile. Tulipata wasaa wa kuzungumza, mimi nikifyeka majani yeye, aliyepangiwa kufyeka pia akipita hapa na pale huku akimwaga gumzo na vichekesho ambavyo nilibaini baadaye kuwa vilimsaidia sana kupatiwa huduma mbalimbali, ikiwa pamoja na kulishwa chakula.

“Tulipoachana pale shuleni mimi niliendelea kwa miaka miwili kabla sijaacha masomo na kurudi nyumbani ambako nilijiunga na shughuli za uvuvi katika ziwa Victoria. Baadaye niliacha kuvua na kuanza biashara ya kupeleka samaki Nairobi na Kampala.

“Unajua sangara hawaishi kuliwa tu?” aliniuliza ghafla. Sikumwelewa. Akafafanua, “Siku hizi sangara ni mali katika kila kiungo chake. Ngozi yake siku hizi ni mali ghafi inayotengeneza pochi murua za akina mama matajiri. Mifupa yake ni malighafi kwa viwanda vya mbolea na madawa. Siku si nyingi hata ile harufu yake itageuzwa manukato ya aina yake. Sangara ni almasi za ziwani.

“Nilipata fedha nyingi sana. Kwa viwango vya pale kijijini

nilikuwa tajiri. Nikajenga nyumba safi na shamba kubwa la miwa. Toka hapo ndipo mambo yalianza kwenda mrama.” Alisita kidogo.

Nikaitumia fursa hiyo kutumbukiza swali, “Ulikuwa hujabahatika kuoa?”

“Nini? Kuoa?” aliuliza huku akiangua kicheko. “Toka niko darasa la nne, wakati tukilala wote pale bwenini, mimi tayari nilikuwa na mke,” alisema.

Nikapigwa na butwaa. “Ulikuawa na mke!”

“Naam.”

“Ulio lini?”

“Sikuoa, niliozeshwa na ukoo wangu. Nilikuwa mtoto pekee wa kiume katika familia yangu. Dada zangu walikuwa kumi na mmoja. Walianza kuolewa. Tulipata ng’ombe wengi sana lakini wazazi hawakuridhika. Walihitaji mjukuu ili awe mrithi wa mali hizo na awapatie watoto wa kiume.”

“Uliwapata?”

“Watu gani?”

“Watoto wa kiume.”

Nikamwona Matayo, kwa mara ya kwanza, akipoteza tabasamu na kuonyesha dalili za masikitiko. Nusu dakika tu, mara alirudia sura yake ya kawaida na kunijibu akisema, “Kuo ni khiari, kuzaa ni majaliwa. Leo hii nina wake watano, hata mmoja hajanipatia mtoto wa kiume!”

Wake watano! Hata hivyo, sikushangaa sana. Matayo alikuwa mtu wa vituko na miujiza siku zote, muujiza wa kwanza ulikuwa ule wa kujiunga na shule akiwa ametuzidi umri wote darasani. Mwujiza wa pili ukiwa ule wa kuja shule na silaha zake zote. Sasa huu wa kwamba wakati wote alikuwa na mke!

“Hilo linakushangaza?” aliuliza baada ya kuyasoma mawazo yangu. “Kwa hiyo, utashangaa zaidi nikikwambia kuwa hata wakati tuko shule, kila likizo niliingia kwenye vita na kuwashikisha adabu adui zetu?”

Muujiza mwingine!

“Nilipigana sana. Na nilipata sifa tele za ushujaa. Adui zetu waliniogopa kuliko simba kwa njinsi nilivyokuwa hodari wa kupanga mashambulizi na kukwepa mishale na mikuki yao. Kwa kweli, jina la yule mzee wa Kizulu lilinistahili sana. Hadi leo sina mikono bado wananiogopa sana na kila vita niko mstari wa mbele nikiongoza mapambano. Kama nisingekamatwa na kushitakiwa wangenikoma.

“Ilikuwaje?”

“Nini?”

“Ilitokea nini Umsolopogaas akaishiwa ujanja na kukatwa mikono?” nilifafanua.

Akacheka. Kisha akasema, “ Naweza kusema ndege mjanja hunaswa na tundu bovu. Nilifanya kosa la kumdharau adui yangu. Mtoto mdogo sana, tena ambaye alikuwa hajapigana vita yoyote. Tulivamia kijiji chao, tukateka mifugo yote. Watu wazima wote walikimbia, mtoto huyu, wa miaka kumi na moja au mbili aliachwa nyuma akilia. Mkononi alikuwa na sime.

“Nilikatazama katoto kale. *Ka kiume!* Ningeweza kukaua, ningeweza kukavunja shingo. Lakini nikakahurumia. Kwangu mtoto wa kiume alikuwa lulu. Nikakaacha na kugeuka ili niondoke zangu. Mara waa! Mkono wangu wa kulia uliokuwa na sime ukaanguka chini. Maumivu makali yakanishika, lakini hayakunishinda hasira niliyoipata. Nikageuka kwa kasi. Waa! Nilikutana na pigo la pili ambalo lilidondosha mkono wangu

wa pili. Maumivu hayakuwa na kifani. Bila khiari nilianguka na kupoteza fahamu. Nilipozinduka nilijikuta niko hospitali, mikono yangu tayari imekuwa vibutu.

Na nilipopata nafuu nilishtakiwa kwa mauaji na uporaji na kupewa adhabu hii ninayoitumikia.

Ilikuwa taarifa ya kusikitisha sana. Nilimhurumia, sikuwa na uwezo wa kumsaidia. Nikaishia kumpa pole tena. Nadhani nilimhurumia. Lakini kutokana na vitendo vyake mwenyewe na msimamo wake hata baada ya kupoteza mikono nilishindwa kuamini kama kweli ninamhurumia au la.

“Haya na wewe niambie kulikoni hadi ukafika hapa,” alisema. “Si walisema ukijua kupokea ujue na kutoa? Ama ukiwa mroho usiwe mchoyo?” aliongeza.

Yangu yanaelezeka kweli? Nilijiuliza.

SURA YA ISHIRINI NA MBILI

Toka Gerezani Hadi Zanzibar.

Mfungwa hana kauli. Mfungwa hana hiari. Mara tu ukishahukumiwa wewe si wewe tena, ni mali ya mtu mwingine. Utafuata matakwa na hiari yake hadi mwisho wa kifungo chako.

Kwa mtu aliyekuwa na kifungo kirefu kama mimi, mfumo huo wa kanuni za mfungwa uliniathiri mara kwa mara, ingawa wakati mwingine athari hizo zilikuwa faraja kwangu kwa namna moja au nyingine.

Moja ya faraja hizo ni pale nilipobahatika kuwemo katika kundi la wafungwa walioteuliwa kwenda Zanzibar kusaidia kazi ya kuvuna karafuu. Kwa mujibu wa mkuu wa gereza karafuu zilipamba sana na zilikuwa zikielekea kuharibika. Vijana wa jeshi la kujenga uchumi wa huko walikuwa tayari wamepelekwa lakini hawakukidhi mahitaji.

Niliichekelea sana fursa hiyo. Kwanza ingenipa fursa ya kupumua hewa safi ya nje. Hewa asilia ya oksijeni itokayo katika mimea na kusambazwa na upepo badala ya hii tuliyokuwa tukiitumia ambayo sikujua ilitokea wapi. Lakini pia kufikia Zanzibar ilikuwa ndoto yangu ya muda mrefu. Toka nchi hizi zilipoungana na sifa za Karume za mapenzi kwa nchi yake zikiimbwa katika vyombo vya habari azma yangu ya

kukanyaga ardhi ya nchi hiyo ilikuwa ikiongezeka siku baada ya siku.

Toka wakati ule ningali *belubelu* bado, mkakati wangu wa kufanya biashara ya chumvi kati ya Zanzibar na Bagamoyo ulipokwama, niliishia kujifariji kwa kusoma na kusikiliza tu, kila kilichozungumza juu ya nchi hiyo. Nilijifunza kuwa ilikuwa moja ya nchi zenye historia pekee duniani. Kwa mfano, wataalamu wa historia wanaamini kuwa miji katika visiwa hivyo ni vya kale kuliko nchi nyingi za dunia. Inaaminika kuwa waanzilishi wa taifa hilo makabila ya Wahadimu na Watumbatu walianza kuishi katika visiwa hivyo, wakitokea katika pwani za Afrika Mashariki miaka 1000 iliyopita. Watu hao waliishi katika vijiji vidogovidogo vya ukoo, bila uongozi wa pamoja jambo lililofanya wakose uwezo wa kutetea haki yao ya umiliki pale walipoanza kuingia katika visiwa hivyo.

Wafanyabiashara toka nchi za Kiarabu hasa Iran na Iraq na Wahindi wanaelezewa kufanya biashara na nchi hiyo miaka nenda rudi. Katika karne ya 11 na 12 baadhi ya wafanyabiashara hao walianza kuifanya Zanzibar makazi yao ya kudumu wengi wao ikiwa pamoja na kuanza kuoana na wenyeji. Matokeo ya ndoa ni kuibuka kwa watawala kama Mwinyi Mkuu au Jumbe miongoni mwa wahadimu au mashaha miongoni mwa Watumbatu. Viongozi hao hawakuwa na nguvu nyingi. Lakini angalau walisaidia kulinda uhalisia katika makabila yao.

Yule naodha machachari wa Kireno, Vasco da Gama, alifika Zanzibar ,waka 1499 na kufungua njia ya wageni wa kutoka Ulaya nchini humo. Mwaka 1505 nchi hiyo ilifanywa koloni la Ureno pale walipoamua kuiteka kabisa.

Mwaka 1698 Zanzibar ikafanywa sehemu ya mali za Oman, hatua iliyofuatiwa na Sayyid Said bin Sultan al

Busaid ambaye akiwa na umri wa miaka 15, mwaka wa 1806 kuhamishiwa makao yake ya kifalme mjini humo. Baadaye utawala wa pamoja wa Zanzibar na Oman uligawanyika mwaka 1861 baada ya kifo chake, wanawe ambao walikuwa wakigombea madaraka walipofikia uamuzi wa Sayyid Majid bin Said alipochukua madaraka ya na Zanzibar na ndugu yake Sayyid Thuwaini kuwa Sultan wa Oman.

Baada ya hapo historia ya Zanzibar ina mlolongo mrefu wa kugombea au kupokonyana madaraka baina ya Waarabu na Waarabu, Wajerumani kwa Waingereza na hatimaye Waarabu kwa Waingereza. Ni pilikapilika za aina hiyo zilizofanya Zanzibar iingie katika historia kama nchi iliyovunja rekodi kwa kupigana vita fupi kuliko zote duniani. Vita hiyo ilipiganwa kwa dakika 45 tu. Ilikuwa baina ya majeshi ya Uingereza na yale ya Sultan Sayyid Khalid bin Bargash ambaye, alipokonya madaraka na kujitangaza Sultan wa nchi hiyo wakati Waingereza waliamini mtawala halali angekuwa Hamoud bin Mohamed. Waingereza walimwamuru Bargash kuachia madaraka; akakataa. Wakampa muda wa kuondoka huku manowari zao zikiwa baharini tayari kupiga mizinga iwapo angeendelea kukaidi. Muda waliompa ulipokwisha manowari hizo zililipua mizinga ambayo ililiharibu jengo la Beit al Hokum. Majeshi ya bargash yalijaribu kujibu kwa bunduki zao lakini hazikufua dafu. Dakika 45 baadaye Bargash alikimbilia katika ubalozi wa Ujerumani, vita ikasimamishwa na Maoud bin Mohamed akatawazwa kuitawala Zanzibar.

Utawala wa Mwingereza nao ulikoma katika kisiwa hicho mwaka 1963 pale nchi hiyo ilipotoa uhuru na uchaguzi ulipofanyika muungano wa ZNP na ZPPP uliposhinda kwa hila dhidi ya ASP ya wazalendo akina Abeid Aman Karume na kufanya Waarabu waendeleo kuwa madarakani. Utawala

huo haukudumu. Mwaka mmoja baadaye, Januari 12, 1964 wazalendo walipindua serikali hiyo na uongozi kuwekwa chini ya Karume.

Hayakuwa mapinduzi rahisi kama mtu unayeweza kufikiria Waarabu wengi wanadaiwa kuuawa, maelfu wengine wakitupwa gerezani. Aidha, Karume alitumia mapinduzi hayo kurejesha hadhi ya mtu mweusi kwa kutoa amri mwanamume kuoa mwanamke yeyote wa Kiarabu au Kihindi anayempenda. Amri chungu ambayo ilipigiwa kelele na baadhi ya nchi duniani, lakini kwa nchi iliyobobea kwa ukandamizaji, ambayo wakati fulani iliaminika kuwa robo tatu ya raia wake walikuwa watumwa wa Waarabu hatua ipi zaidi ingeweza kurejesha usawa na umoja haraka zaidi ya zile ndoa za lazima?

Misugvano ya ndani na vitisho toka nje kwa taifa hilo dogo ilikoma pale nchi hiyo ilipoungana na Tanganyika na kuzaliwa taifa jipya la Tanzania april 12, 1964 ikiwa miezi mitatu tu baada ya mapinduzi.

Hiyo ndiyo Zanzibar ya kale, ambayo kudra za Mungu ziliniwezesha kuwa safarini kuiendea.

Mfungwa hachagui njia, mfungwa hachagui siku ya safari. Yeye ni mtu wa kukurupushwa tu, kama mifugo. Ndivyo ilivyokuwa kwetu. Fununu za safari zilianza ghafla kwa minong'oni baina ya wafungwa. "Skochi jamani.... Skochi ya Zanzibar..." zilivuma taarifa hizo katika selo. Nadhani 'skochi' ni lugha moja ya zile lugha za *kijelajela* iliyokuwa na maana ya 'escort' kwa kiingereza kwani mfungwa haendi popote bila askari jela wa kuwasindikiza.

Sikujua Kama ningekuwa mmoja wa wateule hao hadi siku ya safari, jina langu lilipoitwa na kuamriwa kupanda karandinga. Tulikuwa kama wafungwa mia hivi na askari kumi wa kutulinda. Safari yetu ilianza asubuhi ya jumatatu

moja, tukaifuata barabara ya Dar es Salaam. Tulipofika Moshi tulisimama kwa nusu saa, mkuu wa safari aliposhuka kupata kifungua kinywa.

Nilitamani kuuona mji wa Moshi kwa mara nyingine, lakini niliishia kuuchungulia tu kupitia katika nyavu za waya za karandinga letu, hali ya hewa ilikuwa ileile, tamu inayosisimua. Mlima Kilimanjaro uliendelea kuinamia mji, kama unaolinda kwa maovu, kwa utukufu wake. Kitu kilichonivutia zaidi kwa mji wa Moshi ni usafi. Barabara zilikuwa zikimeremeta, majengo yaking'ara kwa rangi. Ilikuwa nadra sana kuona uchafu ukizagaazagaa mitaani kama ilivyo miji mingi niliyopata kuitembelea.

Safari ilipoanza tena nilikuwa tayari nimepata upenyo mzuri wa kuchungulia nje. Barabara safi, ya lami ilikuwa ikiteleza chini ya matairi ya gari letu kwa uhakika kabisa. Tulikuwa tukielekea Mashariki hadi tulipofika Himo ambapo kuna njia panda ya kuelekea Taveta nchini Kenya na ile ya Dar es Salaam ambayo kwa kiais fulani ilielekea Kusini. Tulipita Kifaru, tukaingia Mwanga. Toka hapo niliweza kuliona kwa mbali bwawa la nyumba ya Mungu. Tukateleza hadi Same, Hedaru, Mkomazi, Mombo na baadaye Korogwe ambapo tulipumzishwa katika gereza moja dogo ambalo sikubahatika kufahamu jina lake. Hapo tulipewa chakula na kutakiwa kumaliza haja zetu za kimaumbile, kubwa na ndogo kabla ya kuanza safari.

Tulifika Segerea na kuiacha barabara inayokwenda Tanga hadi Mombasa tukashuka na kuvuka mto Wami hadi Msata. Hapo viongozi wetu wa safari walisimama kwa muda kujadiliana, ama wafuate barabara ile ndogo isiyo na lami ambayo inachepuka hadi Kiwangwa, Kilola na hatimaye Bagamoyo au ile iliyozoeleka, lakini ya mzunguko, ambayo

ingetufikisha Chalinze, Mlandizi na Kibaha kabla ya kuingia Dar es Salaam. Kumbe safari yetu ya Unguja ilikuwa ianze Bagamoyo. Nadhani kwa usalama wao au wetu waliamua kupita njia ndefu ya Dar es Salaam.

Nilishangazwa na wingi wa watu na majengo niliyoyaona hasa kutokea Mlandizi, mara tu baada ya kuvuka mto Ruvu. Nilipopita kwa mara ya kwanza eneo hili lilikuwa pori la kutisha ambalo lilimilikiwa na nguruwe mwitu na ndege wa porini. Sasa lilijaa binadamu na majengo tele. Wakati huo ilikuwa usiku wa saa tatu hivi, lakini taa za umeme toka maeneo mbalimbali, wingi wa magari barabarani na watu tuliwapitia kando ya barabara uliashiria wingi wa watu na pilikapilika nyingine za kibindamu.

Pilikapilika hizo ziliongezeka maradufu mara tulipoingia Mbezi na hatimaye Kimara. Gari letu lilikwenda kwa mwendo wa kinyonga kutokana na msongamano wa magari. Kandokando mwa barabara, kulia na kushoto, nilishangazwa na wingi wa baa za pombe na wateja waliofurika kelele za muziki wa kileo, ambao baadaye niliambiwa kuwa unaitwa *Bongo flavour* ziliweza kusikika ndani ya gari hiyo kwa uwazi kabisa. Katika baa moja mwanamuziki mmoja alikuwa akicheza kwa nguvu zake zote;

Kuku kapanda baiskeli,

Bata kavaa raizoni...

Wimbo huo ulitufikia vizuri kabisa katika gari. Wengi wetu ambao tulizowea nyimbo za akina Marijani Shabani, Wema Abdallah au Mbaraka Mwishehe tuliishia kucheka kwa mapinduzi haya ya kisanaa. Hatukujua kama tunakwenda mbele au tunarudi nyuma katika fani hiyo ya muziki.

Zaidi ya nyimbo kitu kingine kilichotufikia ndani ya gari hilo ni harufu ya nyama choma. Yale mapande ya nyama,

mishikaki na kuku waliokuwa wakiokwa katika mabaa hayo yalisambaza harufu tamu ambayo ilitutia uroho wa nyama, mboga iliyopatikana kwa nadra sana gerezeni.

Tulifika Dar es Salaam yapata saa nne na robo usiku. Ule muujiza nilioutegemea ulijidhihirisha. Dar es Salaam haukuwa mji tena bali jiji. Majumba mengi yaliyopanda juu, watu wakiwa tele mitaani muda wote. Biashara ya baa ilishamiri karibu kila mahala. Nchi hii haina biashara nyingine?

Tulitoka Ubungo na kuelekezwa Mwenge. Gari likageuzwa na kuelekea Kaskazini tulikotokea tukifuata barabara ya Bagamoyo. Kwangu barabara hiyo ilikuwa muujiza mwingine. Tofauti kabisa na ile tuliyoitumia na akina Leakey miaka kadha wa kadha iliyopita hii ilikuwa barabara pana ya lami. Na ilifurika magari muda wote. Lile pori la wakati ule halikuwepo tena. Badala yake mji ulikuwa umemeza kila kitu kiasi cha kufanya kambi ya jeshi la Lugalo, ambayo zamani ilionekana kujengwa porini sasa iwe katikati ya mji wa kiraia, ambao ulisambaa hadi Pwani yake uwe hadi ufukwe wa Kunduchi. Vile vilivyojulikana kama vijiji vya Tegeta, na Bunju sasa ilikuwa sehemu ya jiji la Dar es Salaam ambalo lilibakiza kilometa mbili tu kuungana na mji wa Bagamoyo, Bagamoyo ambako tulifikishwa katika gereza la Kigongoni kusubiri safari ya Zanzibar.

Ulipata kusikia kuwa binadamu ana mkia? Kama ulipata, je ulipata kuona mkia huo? Ni watu wachache sana duniani waliopata kuuona; mimi nikiwa mmoja wao. Bahati au balaa hiyo nilikutana nayo katika gereza hilo ambalo ni maalum kwa kilimo.

Awali sikuyaamini macho yangu pale nilipowaona watu wa ajabu. Miili yao ilikuwa inatisha, ngozi ikiogofya. Fikiria ngozi ya mtu yeyote, uliyopata kuiona maishani mwako, fikiria

hata mgonjwa wa UKIMWI aliye taabani sana; bado kamwe hutaweza kumfananisha na miili ya baadhi ya wafungwa tuliokutana nao katika gereza hilo. Walinyauka, walisinyaa na kuifanya miili yao ifikie kiwango hicho cha kutisha. Lakini zaidi ya ngozi ya miili hiyo hali ya kukonda ilitisha zaidi. Baadhi yao, waliokuwa taabani zaidi walionekana kama mifupa iliyounganishwa na aina fulani ya ngozi! Ni pale walipovua mashati ndipo nilipoweza kuona mkia wa binadamu!

Mimi pia nilikuwa mfungwa. Lakini hali ya baadhi ya wafungwa hawa ilinifanya nitokwe na machozi! Nilipouliza nini kinatokea wenyeji walininjibu kwa urahisi tu; Luba.

Luba ndio nini?

Ugonjwa. Unatokana na wadudu ambao hushambulia mpunga. Unajua kilimo cha mpunga kilivyo? Inabidi kuingia katika maji au tope. Kwa mfungwa kulazimishwa kuingia katika maji ya tope linalofika hadi shingoni ni jambo la kawaida. Humo ndimo hukutana na wadudu hawa ambao hushambulia mpunga na hivyo wao pia kushambuliwa.

Msemaji alikuwa mfungwa mzoefu. Ilikuwa vigumu kuamini kweli ni mfungwa kwa jinsi alivyokuwa msafi, kiribatumbo kimejitokeza wazi chini ya kifua chake.

“Ni wajinga,” aliongeza. “Wanaingia kichwakichwa katika miji ya watu. Wangeuliza maradhi hayo yasingewapata.”

“Kwa vipi?” Nilimuuliza.

Alikohoa, kabla hajajibu akisema, “Iko namna. Kuna dawa. Wenzao kabla ya kuzama katika tope lile tunajipaka tumbaku. Wadudu hawatusogelei wala kutudhuru.”

“Kwa nini hamkuwaambia hayo mapema?” nilimsaili.

“Si nimekwambia wanaingia miji ya watu kichwakichwa?” lilikuwa jibu lake.

Kwa mara ya kwanza nilijisikia kumpiga mtu makonde.

Mtu mwenyewe hakuwa mwingine zaidi ya mzee huyu anayezungumzia maisha ya binadamu wenzake kana kwamba anajadili suala la paka. Ili kuepuka kufanya hivyo nilimwacha akiendelea kubwabwaja na kujiunga na wenzangu tuliokuwa nao katika 'skochi'.

Nilishukuru pale siku mbili baadaye tulipochukuliwa na magari kuelekea pwani ya Bagamoyo, ambako majahazi mawili yalitupeleka Unguja yalitia nanga yakitusubiri.

Kutoka pwani hiyo hadi Zanzibar ilikuwa safari ya kilometa zipatazo 25 tu, lakini kwa wenzangu wengi ilikuwa safari ndefu, ngumu iliyojaa mashaka. Mawimbi na upepo vilifanya wengi wapatwe na ule ugonjwa uitwao 'homa ya bahari.' Baadhi walitapika, baadhi wakiwa taabani kana kwamba wanakaribia kukata roho. Askari wawili waliotusindikiza pia walikuwa wakitapika huku wenzao wakiwacheka.

Wakati tunakaribia kutua pwani tulipata burudani tosha toka kwa pomboo, wale viumbe wa baharini ambao mimi huwaita samaki lakini wataalamu uwachukulia kuwa ni wanyama wa majini kwa kuwa wananyonyesha watoto wao kinyume na samaki wengi, kawaida. Viumbe hawa ambao wengi huwaita 'Dolphins' walilizingira jahazi letu, mara kwa mara wakichupa angani na kutuchungulia kwa namna ya kususimua.

Pomboo, ambao nyama yake ni tamu sana ni viumbe wanaofugika na kufundishwa. Nchi kadhaa tayari wamewafundisha michezo mbalimbali kama kushindana, kuruka kwa pamoja kudaka mpira na mambo mengine tele ambayo huvuta watalii. Baadhi ya nchi zilizoendelea tayari wanawafundisha kubaini mabomu ya kutegwa baharini na hivyo kuepusha madhara.

Kwangu walikuwa burudani tosha na walitusindikiza hadi tulipotia nanga ufukwe wa Zanzibar, mji mkuu wa nchi hii ambayo inadaiwa iko chini kidogo ya usawa wa bahari. Baadhi ya wataalamu wanadai kuwa iko siku nchi hiyo itamezwa na maji na kutoweka katika uso wa dunia. Lakini hiyo ni hadithi nyingine. Yetu ni kwamba mara tulipofika magari ya wafungwa yalikuwa yakitusubiri tayari kutupeleka katika gereza la kiinua mguu ambako tungepumzika kidogo kabla ya kusafirishwa tena hadi Pemba yaliko mashamba mengi zaidi ya karafuu.

Tulilundikwa katika makarandinga, ambapo hayakutofautiana sana na yale ya bara. Yakatiwa moto na kuondoka. Kwa kiu yangu ya kuufahamu mji wa Zanzibar nilifanya kila jitihada kuhakikisha nachungulia nje na kujionea chochote ambacho ningeweza kukiona. Kwa mbali, niliweza kuiona hoteli maarufu ya bwawani ambayo ilijengwa na serikali ya Karume. Wakati tukipita mitaani, eneo la Kichenzani nilishangaa kuona mitaa yote ikiwa imemezwa na majumba marefu sana, takribani mita mia tano kila nyumba. Nyumba hizi ambazo zilikwenda juu kwa gorofa tatu au nne tu zilielekezwa kuwa ilikuwa kazi nyingine ya Karume kwa wananchi wake alipotoa amri akisema, 'Wazungu wanashindana kujenga nyumba ndefu kwenda juu kwa ajili ya uhaba wa ardhi yao, sisi tutajenga nyumba ndefu kwa upana.' Matokeo ya kauli hiyo ndiyo nyumba hizo ambazo zilikuwa mkombozi kwa wananchi ambao wengi wao walikuwa masikini sana baada ya kukandamizwa na wageni miaka nenda rudi.

Katika eneo la darajani nilishangazwa na wingi wa waendesha baiskeli. Katika maneno fulani ilibidi waongozwe na askari wa barabarani kama ilivyo kwa magari. Eneo hilo lina soko kuu, wenyewe wakiliita 'markiti' bila shaka jina

hilo lilitokana na neno '*market*' la Kiingereza. Kilichonivutia zaidi hapo ni mavazi, kanzu nyeupe ndala miguuni na baragashia kichwani vilitawala mavazi ya mwanaume. Kwa wanawake mabaibui yaliyofunika sura gubigubi yalitamalaki na kunikumbusha miji ya Tanga. Utamaduni mwingine niliobahatika kuuona hapa katika muda mfupi ni kitendo cha wanaume wengi zaidi kuwa na makapu kununua mahitaji ya nyumbani. Ilikuwa nadra sana kuwaona wanawake wakifanya manunuzi hayo.

Tuliiacha darajani na kuambaa pembeni mwa mji mkongwe. Macho yangu yalivutiwa na nyumba za kale, ambazo baadhi zilijengwa zaidi ya miaka mia mbili iliyopita lakini bado zinatumiwa na binadamu hadi leo. Ajabu ni kwamba nyumba hizo zilijengwa kwa udongo, mawe na miti migumu kama mikoko ambayo mingi ingali imara hadi leo. Kitu kinachovuta macho zaidi ni katika mji huu mkongwe ni mitaa yake. Nyumba hizo zilijengwa katika hali ya kubanana sana kiasi kwamba mitaa yake haiwezi kuruhusu gari kupita na hata baiskeli na pikipiki zililazimika kupita kwa uangalifu sana. Sura hii ya aina yake ya mji huu mkongwe ni moja ya sababu zilizopelekea shirika la elimu la Umoja wa Mataifa liutangaze kama moja ya maeneo ya kihistoria ambayo yanahitaji kuhifadhiwa.

Katika mwambao huo wa bahari nilifurahi sana kuliona jengo maarufu Beit el Ajaib lililojengwa na Sultani Bargash mwaka 1883. Jengo ambalo lina simulizi tele za kila aina. Kwa mfano inaaminika kuwa chini ya kila nguzo ya jengo hilo alizikwa hai mtumwa mmoja. Juu yake likiwa na mnara wenye saa kubwa pia linadaiwa kuwa la kwanza nchini na pengine Afrika nzima kutumia umeme na lifti.

Kando yake nililitembelea pia jengo jingine lililokuwa

likitumiwa kama ngome kuu ya Waarabu. Jengo hilo lenye ukumbi mkubwa na kuta pana lilipanda juu ambako kuna majengo na matunda maalum ya kutumia wakati wa vita. Hata hivyo sisi tulikuta tayari jengo hilo lina maduka, kumbi za wazi za burudani na biashara mbalimbali za sana.

Zanzibar haina wanyama wengi kama bara. Inaaminika kuwa nchi hiyo haina tembo hata mmoja. Jambo ambalo linawashangaza sana wataalamu wa masuala ya wanyama pori kwani mwaka 1295, msafiri mmoja aliyeitwa Marco Polo aliitembelea Zanzibar kutoa taarifa ya kuwepo kwa mamia ya tembo na wanyama wengine.

Kama tusingekuwa wafungwa tungeshiriki katika ngoma ya 'mwaka kongwa' iliyokuwa ikipigwa wakati tukipita eneo la Makunduchi. Tuliishia kuchungulia dirishani tu na kuona wanaume wanavyotoana jasho kwa ndizi na migomba katika ngoma hiyo maarufu ya kila mwaka.

Zanzibar hiyo! Kwa machache niliyobahatika kuyaona, machache niliyopata kuyasikia na kuyasoma sikushangaa pale macho yagu katika tundu nililokuwa nikitumia kuchungulia nje yalipoweza kuona idadi kubwa ya watalii wa Kizungu wakipita hapa na pale katika mitaa, vichochoro na fukwe ya Zanzibar. Nilipata pia kusoma mahala kuwa takribani wageni wapatao 100,000 hutembelea visiwa vya Zanzibar kila mwaka kwa ajili ya shughuli za kitalii.

Gereza la Kiinua Mguu halikuwa tofauti na magereza mengine niliyopata kuyatembelea. Hadithi ilikuwa ileile, chakula kibovu, mlundikano katika selo, chawa na kunguni wakitawala, maradhi ya kila aina na vifo. Tulilala hapo siku tatu kabla ya kupakiwa katika moja ya zile meli zao ziendazo kasi, ambayo ilitufikisha pemba, katika mji wa Wete. Huko

tulielekezwa katika mashamba ya karafuu kuanza kazi.

Nilikuwa nikiifahamu karufuu kwa ladha tu, baada ya kuila sana katika pilau kule Pangani. Aidha, nilifahamu kwa harufu yake tamu puani toka katika marashi ya akina mama wa mjini wanaojiandaa kutoka. Sikupata kufahamu kuwa zao hilo lilikuwa na maajabu zaidi. Kwa mfano, sikujua kama karafuu ilikuwa tiba pia ambayo mafuta yake yalitumiwa kumchua mtu aliyeteguka viungo pamoja na tiba ya meno kwa mwenye maumivu. Nilishangaa zaidi kusikia kuwa karafuu, kwa baadhi ya watu, waliitumia kama sigara wakichanganya na vitu vingine walivyofahamu wao.

Kwa mujibu wa kumbukumbu za kihistoria Sultan Sayyid Said aliyeitawala Zanzibar katika karne ya kumi na nane, alipofika kwa mara ya kwanza nchini humo alishangaa kuona mikarafuu miwili mitatu iliyoota hapa na pale kwa bahari tu ikiwa imestawi vizuri. Wakati huo karafuu likiwa zao hadimu kwa kupatikana katika maeneo machache ya Asia, Sultan huyo alipata wazo. Aliamini kuwa zao hilo lingeweza kuupa nguvu za kiuchumi na umaarufu utawala wake. Hivyo, alilima shamba lake binafsi kama mfano, akapanda miche arobaini na tano. Kisha, akatoa amri kila mtu kulima mikarafuu. Amri ambayo alihakikisha inatekelezwa kwa nguvu zake zote. Hadi anafariki Sultani huyo aliacha tayari biashara ya pembe za ndovu na watumwa ikitishiwa kiuchumi na ile ya karafuu.

Mkarafuu unapendeza kwa macho kama ilivyo harufu yake. Ni mti ambao unakuwa katika rangi yake halisi ya kijani kwa mwaka mzima. Mti huu huenda juu kwa mita kumi hadi ishirini. Maua yake ndiyo karafuu yenyewe. Yako katika sura na maumbile mbalimbali. Maua hayo hupitia rangi mbalimbali kama kahawia, kisha kijani na hatimaye wekundu ambao ndio

huwa dalili ya kukomaa na hivyo huvunwa.

Tulifundishwa yote hayo tukiwa katika uvunaji kazi ambayo ilituweka kisiwani humo kwa miezi mitatu.

Pengine kwa ajili ya ugumu wa usafiri toka kisiwani humo, pamoja na ugeni wetu, hatukushindwa sana kama ilivyokuwa bara na Unguja. Tuliruhusiwa kuchanganyika na wenyeji na, hivyo, kujipatia marafiki wengi wa Kipemba. Hata hivyo, tatizo lilikuwa kuelewana. Ilituchukua muda mrefu kukielewa Kiswahili chao ambacho ama kilichanganyika na kiarabu ama kiliathiriwa na makabila ya asili.

Pemba ilikuwa nyuma kimaendeleo ukiilinganisha na Unguja. Pamoja na kuwa mzalishaji mkuu wa zao hilo la karafuu na mazao mengine, bado wananchi wake wengi zaidi waligubikwa na umasikini. Nyumba zao nyingi zilisikitisha kwa kukosa hata milango, mavazi yao yalikatisha tamaa. Watoto na watu wazima kutembea pekupeku bila viatu ilikuwa jambo la kawaida sana.

Karume amejitahidi. Kila alichokifanya Unguja alikifanya pemba pia. Yale majumba yake marefu yalijengwa pia Wete na mkoani. Wanachi waliishi bila malipo. Hoteli kubwa kama ile ya bwawani pia ilijengwa katika kisiwa hiki kwa kiwango kilekile. Bado wananchi wengi walikuwa taabani na nyuso zao zilionyesha kitu kama kutoridhika au kukata tamaa. *Pemba kunani jamani?* Nilijiuliza. Kwa kweli, pamoja na uhuru tuliokuwa nao miezi mitatu tulioishi huko niliona kama miaka mitatu ya kuishi katika gereza jingine la aina yake.

SURA YA ISHIRINI NA TATU

Mtwara; Tumaini Lilirorejea

Masaibu ya maisha yanaweza kukupangia jambo ambalo hata hukupata kulifikiria. Mfano mzuri ukiwa wangu mwenyewe. Maishani mwangu sikukusudia kuwa mhalifu wala sikupata kutarajia kamwe kujikuta nikiishi gerezani kama mfungwa. Lakini ufungwa nao una yake. Ufungwa wangu ulianza kugeuka kuwa utalii.

Mawazo hayo niliyapata tuliporejea toka Zanzibar na kupumzishwa wiki mbili kabla ya baadhi yetu kupangiwa safari nyingine. Mara hii safari yetu ilikuwa ya kueleka Kusini, mkoani Mtwara, ambako tuliombwa kusaidia kazi ya kuchimba mtaro wa kupitisha gesi katika eneo fulanifulani ambayo waajiriwa wa kawaida waligoma kwenda kutokana na ugumu wa mazingira. Sisi, watumwa wasio na wenyewe tulipewa amri tu, ‘*Skoch*’ ya Mtwara kesho.

Sikupata kufikiria kwenda Mtwara hata mara moja katika ndoto zangu za kimaisha. Mtwara kufanya nini? Wana Mtwara wenyewe walikuwa wanaikimbia. Msamiati wa ‘Wamachinga,’ wale wafanyabiashara vijana, ambao huzunguka na bidhaa zao kila mtaa na kila uchochoro wa jiji la Dar es Salaam, ulizaliwa kutokana na vijana wa Mtwara, pale walipoanza kumiminika mjini baada ya kukata tamaa

vijijini. Walikuja kwa mamia, kutwa wakisaga lami na vumbi la Dar, usiku wakilala kwa dhiki katika vichochoro vya Kariakoo, biashara zao maelfu zikilindwa kama roho zao. Taratibu walianza kuwatishia wamiliki wa maduka, wengi wao wakiwa Wahindi, pale wateja wao walipopunguza kuingia madukani na kuishia kwao. Waliwatishia pia maafisa wa kodi kwani kodi toka kwa wenye maduka zilipungua na kumdai Mmachinga ambaye hujui anaishi wapi, duka lake anatembea nalo, haikuwa kazi rahisi.

Wakati huo ‘Wamachinga’ walichukuliwa kama Wamakua na Wamakonde pekee. Hata jina lao lilitokana na kile kijiji cha Mchinga kilicho Pwani ya Bahari ya Hindi, maili chache toka Lindi. Lakini mafanikio yao tayari yamewavuta Wasambaa na biashara zao za matunda toka Tanga, Wagogo na kahawa zao toka Dodoma, Waha na baiskeli zao toka Kigoma na wengineo. Wote wanafanya kazi za kimachinga na wameafiki jina hilo la Wamachinga pamoja na serikali kuwatafutia majina mbalimbali ya kutia matumaini kama ‘Wajasiriamali,’ au ‘Wafanyabiashara wasio rasmi.’

Moja ya sababu zilizofanya nisiote ndoto ya kwenda Mtwara ni zile sifa za ugumu wa safari za kwenda huko. Usafiri wa meli haukuwa na uhakika. Ilisikika habari ya meli moja tu, tena ya mizigo, ambayo ungeisubiri kwa mwezi au miezi kabla ya safari. Meli ambayo ilidaiwa kufurika kupita kiasi na hivyo kuhatarisha maisha ya wasafiri mara kwa mara. Enzi hizo kufikiria safari ya barabara ilikuwa wazimu zaidi. Njia ilikuwa ndefu kuliko ilivyostahili kutokana na ubovu. Yalikuwepo maeneo yasiyopitika, magari ya madereva vichwa ngumu yakizama au kukwama kwa zaidi ya wiki katika tope kabla ya kufikia kivuko cha mto Rufiji na matawi yake.

Pengine kama si kizingiti cha barabara hiyo Mtwara ya leo ingeweza kuwa mfano wa aina yake wa utajiri wa Tanzania, kwani neema ya uchumi ilikuwa imeishukia Mtwara mwaka 1948 Waingereza walipouteua mkoa huu na kongwa Dodoma, maalumu kwa ajili ya kilimo cha karanga. Ekari milioni 325 au kilomita za mraba 13,200 zilitarajiwa kulimwa katika kipindi cha miaka sita na hivyo kuilisha Tanganyika na Ulaya nzima karanga na mazao yote yatokanayo na karanga.

Mradi huo ulitengewa dola za Marekani milioni 25. Askari wastaafu laki moja na wakazi wengine tele waliojitokeza kufanya kazi hiyo. Hata hivyo, baada ya jitihada za muda mrefu na kupotea kwa dola milioni 49 zaidi ya zilizotarajiwa kazi ilishindikana. Sababu? Ukosefu wa barabara. Reli iliyokuwepo, ambayo ilitarajiwa kutumiwa kwa usafirishaji wa vifaa na mazao ilichukuliwa na mafuriko ya mto Kinyensungwe. Usafirishaji wa vifaa kama matrekta na mbolea kupitia mto Ruvu nao ulikutana na vizingiti tele; tembo, vifarua na viboko walitishia maisha ya wafanyakazi na hivyo wengi kukimbia. Maradhi ya malaria na matumbo kwa ajili ya maji yasioaminika nako kulichangia.

Jambo jingine ambalo lilisababisha mradi huu kushindikana ni mibuyu. Vifaa vidogovidogo vilivyoweza kufika huko havikuwa na uwezo wa kuing'oa mibuyu mikubwa iliyotanda katika baadhi ya maeneo ya shamba. Si hivyo, baadhi ya mibuyu hiyo ilikuwa na maajabu yake. Baadhi ya mibuyu ilishindikana kutokana na wingi wa nyuki waliokuwa wameweka makazi yao humo, ambao waliwatawanya wakulima hao hadi wakashindwa kufanya kazi yao. Mibuyu mingine ilitumiwa na wenyeji kama matambiko, wasingekubali kamwe

ing'olewe. Mbuyu mmoja ulitumiwa kama gereza kwa ajili ya wahalifu. Huu pia usingeng'olewa.

Hayo na mengine tele yalisababisha tani 2000 tu za karanga zipatikane baada ya miaka tele ya majaribio kabla ya bunge la Uingereza halijatamka rasmi kuuachilia mbali mradi huo mwaka 1951. Kupotea kwa tumaini hilo kuliambatana na kusahuliwa kwa Mtwara, na hivyo kuibuka kwa ukimbizi wa vijana wenye nguvu, kwenda mijini kutafuta maisha kwa 'Umachinga'.

Hivyo, kugunduliwa kwa gesi, kulikofanywa na kampuni ya Artumas Co. katika mkoa huo ilikuwa neema ya pekee kwa Mtwara na wakazi wake. Lilikuwa tumaini lilirorejea kwa Wamachinga.

* * *

Kwa mujibu wa taarifa zisizo rasmi, ambazo kama wafungwa tulizipata toka hapa na pale wakati tukifanya kazi yetu ya kuchimba mitaro ni kwamba gesi hiyo iliyogunduliwa ingeweza kutumiwa na mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kupikia, kuendeshea viwanda na mahitaji yote ya umeme kwa zaidi a miaka 800.

Taarifa hizo ziliongeza kuwa uamuzi wa serikali ulikuwa kuhakikisha wakazi wa Mtwara, ambao kwa mwaka 2002 walikuwa 1,128,523 wote wanapatiwa fursa ya kuitumia nishati hiyo kwanza kabla haijaruhusiwa kwenda kuwahudumia watu wengine.

Gesi hiyo iligunduliwa Mnazibay, ambako tulipelekwa kufanya kazi. Zilikuwepo pia fununu za nishati hiyo kugunduliwa katika sehemu mbalimbali za mikoa hiyo ya kusini.

Kazi ya kuchimba mitaro hiyo haikuwa rahisi. Kulikuwa na ule wa kupitisha bomba la kuileta gesi hadi Dar es Salaam ambako tuliambiwa kuwa viwanda kadhaa kikiwemo kile maarufu cha Simenti, Wazo, tayari vilikuwa kutumia nishati hiyo badala ya umeme wa TANESO uliozolekea. Umeme ambao ulitegemea zaidi maji ya mvua hivyo, licha ya gharama kuwa kubwa miaka yenye mvua haba ulikuwa matatizo kibao kiasi cha kuanzisha msamiati wa aibu ‘mgao wa umeme.’

Tulifanya kazi yetu kikamilifu, siku tulizopangiwa tulirejeshwa Ukonga, siku zangu za kukaa kifungoni zikifikia ukingoni.

Siku moja bado tukiwa huko Mtwara, nilitembelewa na wazo la ajabu. *Kuo!* Sijui wazo hilo lilipenyaje katika kichwa changu kilichofura kwa matatizo na migogoro isiyo na kifani. Mfungwa, asiye na mbele wala nyuma, nawezaje kufikiria kuo?

Mimi wazo hilo lilinitembelea. Chanzo chake hakikuwa zaidi ya Lulu, msichana wa Kimakua ambaye alitembelea gereza tulilokuwemo akiwa amefuatana na maafisa wenzake wa ustawi wa jamii. Walituweka kikao kwa maelezo kuwa wamekuja kuzungumza nasi kuhusu ya maisha ya uraiani kwani wengi wetu vifungo vyetu vilikuwa vikifikia ukingoni.

Walizungumza mengi. Lakini naapa kuwa hakuna aliyekuwa akiwasikiliza. Lulu, akimeremeta kwa ngozi yake laini ya maji ya kunde, sauti yake ya upole na tabasamu lililosindikiza kauli zake alivutia zaidi ya nasaha zao. Wafungwa wengi walionekana hivyo na walinong’onezana hivyo. Hali ambayo ilidhihirisha zaidi pale tulipopewa wasaa wa kuuliza maswali. Mfungwa wa kwanza alielekeza swali lake moja kwa moja kwa Lulu “Samahani dada Lulu, umeolewa?”

Kila mtu alicheka, ikiwa pamoja na Lulu mwenyewe.

“Sijaolewa. Unataka kunioa?” alimjibu na kumtupia swali pia.

“Huyu akuoe? Atakulisha nini?” alidakia mfungwa mwingine na kuongeza. “Kwanza ni mzee. Kisha hajui kusoma wala kuandika. Kama kuna mume hapa ni huyu mdogo wetu,” alisema akielekeza kidole chake kwangu. “Ni msomi, anazungumza Kiingereza kama Kiswahili. Hata humu ndani amekuja kama ajali tu,” aliongeza.

Sikutarajia kauli kama hiyo. Nilishikwa na aibu kuona kila mtu akinitazama. Lulu Kalenje, kama alivyojitambulisha, alitabasamu kabla hajatamka taratibu, “Naona nimeshapata mchumba. Kwani kaka unaitwa nani?” aliniuliza.

“Petro Kionambali.” Nilimjibu

“Unatoka upande upi wa nchi hii?” aliongeza swali jingine.

“Natokea Kigoma.”

“Wewe Muha?”

“Haswaa.”

Lulu akacheka tena kabla hajasema. “Sioni kama uchumba wetu utadumu. Watu wa Kigoma hamtuwezi kabisa Wamakua. Tuna tofauti kubwa ya kiutamaduni.”

Nilimwelewa haraka. Nilikuwa nimejifunza mawili matatu juu ya mkoa wa Mtwara na makabila yake kadhaa.

Wageni hao walipoona maswali ya *kijelajela* yakiongezeka badala ya yale waliyoyakusudia waliaga na kuondoka. Wenzangu walitawanyika. Mie nilibakia palepale kwa muda nikitafakari. Wazo la kupenda na kuoa kwa ujumla lilitokea kusikojulika. Lilijikita kwa muda katikati ya ubongo wangu.

Nilitamani kuoa!

Nilitamani kumwoa Lulu!

Nikamfikiria Lulu, mtoto wa Kimakua. Sikupata kuishi Mtwara. Lakini katika maongezi na tafiti zangu vitabuni nilikuwa nafahamu mengi juu ya mila na tamaduni za Wamakuwa na jirani zao Wayao.

Mtwara, ambayo iko kusini mwa Tanganyika, ikiwa imetengana na nchi ya Msumbuji kwa mto Ruvuma inayo makabila mengi. Makubwa kati yake yakiwa Wamakonde na Wamakua ambao waliingia kutokea Msumbiji. Wayao wanaaminika kutokea Malawi. Hizo zikiwa zile enzi za kuhama kabla ya ujio wa watu weupe ambao walifuatiwa na uamuzi wa uroho na uchoyo uliopelekea kuwekeana mipaka baada ya kupora hiki na kile.

Wamakua na Wayao wanapofikia umri wa miaka kumi hadi kumi na mbili lazima wapitie unyago. Jukumu hilo, huendeshwa na wazee wa kike waliobobea katika masuala ya familia.

Wahusika hulazimishwa kutunza siri yoyote watakayo fundishwa au kuonyeshwa katika mafunzo hayo. Miongoni mwa mafunzo hayo ni jinsi ya kujitunza. Wavivu na jeuri hupewa maneno ya kuwatisha ili waachane na tabia hizo na masuala mengine ambayo somo ataona lazima kuyasisitiza.

Mafunzo hayo hufuatiwa na sherehe za mkesha, ngoma aina mbalimbali kama chimakuani, mtotamto, mselemba na nyinginezo hutumbuiza. Sherehe ambazo huambatana na vinywaji hasa pombe ya mtama ambayo huandaliwa maalum kwa shughuli hiyo.

Yote hayo niliyachukulia kama kawaida. Ambacho nilikiona kizito ni ule utamaduni wao wa kumfanya mtoto mali ya mama zaidi ya alivyo kwa baba. Kwa maana nyingine mtoto

anamsikiliza zaidi mjomba. Ujombani ndio kwao zaidi na ndiko anakokulia.

Kwa falsafa yao mama ndiye hasa anayemjua baba wa mtoto na mama ndiye anayekaa na mtoto tumboni kwa miezi tisa na kumnyonyesha kwa miaka miwili. Baada ya hapo ni yeye anayemlisha na kumvisha hadi anapofikia umri wa kuweza kujitegemea. Hali hiyo husababisha Mmakua au Myao anapooa anahama kwao na kwenda ukweni ambako atapewa shamba na kuonyeshwa mahala pa kujenga ‘mdule’ nyumba zao, ambazo hujengwa kwa fito na udongo paa likiwa la nyasi. Huo huwa mwanzo wa maisha mapya ya kijana huyo ambaye hata majina ya watoto wake hutolewa na wajomba.

Kwa jinsi nilivyomfahamu baba yangu, mzee Karimanzira Kionambali, sikuiona namna yoyote ambayo angeweza kukubali niingie katika utamaduni wa aina hiyo.

Jingine lililonitisha ni ule utamaduni wao wa kula ‘dagaa changa’ yaani panya. Makabila mengi ya kusini panya ni mlo halali wanaouthamini sana. Unaweza kutengenezewa kitoweo murua, ambacho kitavutia sana, ukala na kushiba bila kujua kuwa unakula panya. Sikuwa tayari kubahatisha hilo pia!

Kwa kheri Lulu! nilivunja uchumba kimoyomoyo. Uchumba ambao hata ulikuwa haujaanza rasmi, mchumba mwenyewe akiwa hata hazifahamu hisia zangu.

* * *

Sitaweza kuisahau tarehe ya kufunguliwa kwangu. Ni tarehe ambayo nimeishi nayo akilini kwa takribani miaka ishirini nikiisubiri kwa hamu. Lakini pale ilipofika na jina langu kutajwa nikiitwa ofisini nilijikuta nikitetemeka kidogo. Wakati wafungwa wenzangu wakinipongeza kwa kutoka

kwangu salama, mimi nilitokwa na machozi. Waliyachukulia kuwa machozi ya furaha. Laiti wangejua!

Nilikabidhiwa vitu vyangu. Suruali mbili, mashati mawili, viatu na kabrasha langu la vitabu. Nililipokea kabrasha hilo harakaharaka na kulikagua. Kitu nilichokuwa na shauku ya kukiona kilikuwepo! Kitabu changu cha benki. Nikakifunua. Akiba yangu ilikuwa kama nilivyoiacha, shilingi 3,500. Nikakitia mfukoni. Nikakabidhiwa tiketi ya treni, daraja la tatu, ambayo ingenifikisha hadi stesheni ya Kigoma. Toka hapo ningejitegemea kufika Kasulu na hatimaye kijijini kwetu.

Nilikuwa mgeni sana Dar es Salaam. Toka nilivyofika kwa muda ule mfupi na akina Leakey sikupata kurudi tena. Sikuwa na wenyeji wala rafiki ambaye angeweza kunipokea. Hivyo, pale lango la gereza lilipofunguliwa nami nikaruhusiwa kutoka sikujua toka hapo ningelekea upande gani wa dunia.

Kweli Mungu si Athumani. Wakati bado nashangaa hapo nje gari la mkuu wa gereza lilitokea. Aliponiona akaniita. “Hongera,” alisema “Nategemea hutajiingiza tena katika jambo lolote la kinyume cha sheria ambalo linaweza kukurejesha hapa.” Baada ya maneno hayo aliutia mkono wake mfukoni na kuuchomoa ukiwa na noti tatu za elfu kumikumi. Shilingi 30,000! Sikuyaamini macho yangu.

“Mbona nyingi sana mzee?” nilimuuliza

“Nyingi?” alijibu akicheka. “Hazikutoshi, lakini zitakusadia.” Akalitia gari lake moto na kuondoka zake hata kabla sijamshukuru kikamilifu.

Kwa maelekezo ya wapita njia nilifika kituo cha mabasi ya mjini wenyewe waliyaita ‘daladala’. Nikauliza basi la kuelekea stesheni ya treni, nikapanda, kondakta, kijana mdogo mweye lugha ya kihuni alikuwa mtu wa kwanza aliyenipa mshangao

wangu wa kwanza. Ni pale aliponiomba nauli nami kumpa moja ya zile noti nilizopewa na mkuu wa jela. Nilihesabu kwa makini chenji alizonipa. Alikata shilingi mia mbili.

“Nauli mia mbili?” nilifoka.

“Kumbe ngapi?” alinjibu kwa swali vilevile. Alinitazama kwa makini. Nywele zangu zilizoanza kuingia mvi ziliashiriwa ovyoovy. Suruali yangu iliyopauka ilikuwa pana kiunoni, fupi miguuni ikinifanya nionekane kama moja ya vile vikatuni vinavyochorwa magazetini, sura yangu pia, nadhani ilionyesha ugeni na mshangao kwa kila nilichokiona, wingi wa watu wa magari, wingi na ukubwa wa majengo na kadhalika.

“Au umetoka pale mjomba?” Yule kondakta alihoji.

“Pale wapi?” nilimuuliza

Pale mtakuja, ukumbi wa wanaume,” alijibu akielekeza mkono maeneo ya gereza.

“Unauliza jibu?” abiria mmoja alidakia.

Sikuwajibu. Hofu niliyokuwanayo juu ya maisha ya uraiani ilianza kunirejea. Shilingi mia mbili kabla sijaingia gereza ilitosha kumsomesha mtoto wa mwaka mzima. Wakati huohuo kodi ya chumba kwa mpangaji ilikuwa senti ishirini, shati senti kumi. Nauli halali ya basi kama hilo isingezidi senti tano.

Kumetokea nini? Nilijiuliza. Tulipita Tabata, tukaingia barabara ya Mandela na kuifuata hadi Buguruni ambako tulichukua barabara ya Pugu kueleka mjini. Barabara hiyo ikiwa barabara pekee inayoelekea uwanja wa ndege wa Julius Nyerere magari yalikuwa tele barabarani yakishindana kwa kasi. Aidha, barabara hiyo ilikuwa katikati ya viwanda mbalimbali vilivyotapakaa hadi Chang’ombe na Vinginguti, hali iliyozidi kuipa purukushani za aina yake. Mwendo wa kasi

wa magari hayo na majonjo ya dereva wetu utadhani hana roho vilinitia roho mkononi hadi tulipofika kituo cha stesheni ambapo nilishuka.

Mshangao wa pili ulinisubiri nilipofika stesheni. Nilikuta pamefurika watu, wengi wao wakiwa na mizigo tayari kwa safari. Lakini nilipofika dirisha la tiketi kwa nia ya kuithibitisha tiketi yangu niliulizwa swali ambalo sikutarajia.

“Unataka kuondoka lini?”

“Leo.”

“Haiwezekani. Nafasi zimejaa. Labda ufanye *booking* ya siku nyingine.”

“Haya, nipe tiketi ya kesho.”

“Kesho hakuna treni.”

Sikuelewa. “Kwa nini?”

“Treni ni mara tatu kwa wiki,” alinifafanulia. “Na ratiba yangu hapa inaonyesha kuwa daraja la tatu limejaa hadi baada ya wiki tano hivi.”

Sikuamini kama nilikuwa nimemsikia vizuri. Treni inasafiri kwenda bara mara tatu kwa wiki! Treni hiyohiyo ambayo wasafiri ni wengi kiasi cha kuifanya ijae hadi kwa wiki tano zijazo! Treni hiyohiyo ambayo ilikuwa ikisafiri kila siku na abiria wakichagua kiti cha kukaa!

“Kwani kumetokea nini?” nilimuuliza karani huyo.

Alinitazama kwa macho ya mshangao kana kwamba nina pembe ya faru usoni. Nadhani aliishuku hata akili yangu. Kwani badala ya kunijibu alifunga dirisha lake.

Kijana mmoja aliyekuwa pembeni akifuatilia majibizano yetu alinivuta kando na kuniuliza “Unataka tiketi ya kuondoka leo? Toa kitu kidogo tu utasafiri.”

“Tiketi ninayo.” Nilijibu nikimwonyesha.

“Sasa tatizo lako nini? Treni ikifika panda. Hakuna atakayekushusha. Mradi uwe tayari kwenda wima.”

“Wima! Toka Dar es Salaam hadi kigoma!”

Niliamua kuufuata ushauri wa kijana huyo. Bado zilikuwepo saa sita kabla ya treni kufika, masaa mawili kabla ya muda wa kuondoka. Nikaamua kuutumia muda huo kutafuta benki ambayo nilikuwa nimefungua akaunti yangu.

Ilikuwa kazi nyingine ngumu. Mji ukiwa umepanuka sana, majengo mengi yakishindana kwenda angani, huku watu wakiwa tele na pilikapilika kibao ilinichukua muda kabla ya kumpata mtu aliyenielekeza hadi kuifikia benki hiyo.

Afisa niliyeelekezwa kwake alinipokea kwa heshima zote katika chumba chake kidogo chenye hewa safi iliyokuwa ikitoka katika kiyoyozi. Hewa ambayo iliniburudisha sana kutokana na jasho tele lililokuwa likinitoka. Akapokea kitabu changu na kukitazama kwa mshangao kidogo. Nadhani kwa umri wake hakupata kuona aina hiyo ya kitabu, kwani vilishabadilishwa mara nyingi. Hata hivyo, alipoichezea kompyuta yake kwa muda mrefu aliliona jina langu.

“Petro Kionambali sio?” akauliza.

“Ndiyo,” nilimjibu kwa matumaini.

“Mbona huna pesa?” aliniuliza tena

Sikumwelewa, “Kwa vipi? Mara ya mwisho nilikuwa na elfu tatu.”

“Ni kweli kabisa,” alijibu. “Miaka ipatayo ishirini na mbili akiba yako ilikuwa elfu tatu. Halafu ukapotea. Gharama za kutunza akaunti yako na kushuka kwa thamani ya pesa kumefanya uwe huna pesa kabisa. Kwa kweli, benki inakudai.”

Ulikuwa mshangao wangu wa tatu katika siku yangu ya kwanza uraiani. Nilihisi naishiwa nguvu, miguu na mikono

ikitetemeka. Pamoja na kiyoyozi jasho jembamba lilianza kunitoka. Kwa sauti dhaifu niliuliza, “Unasema? Sijakuelewa... Nilitarajia fedha zangu ziwe zimeongezeka sana. Unajua wakati ule fedha zile zingenitosha kununua magari hata mawili na kujenga nyumba?”

“Ni kweli kabisa,” alinijibu. “Tatizo lilikuwa lako wewe. Benki ikaendelea kukata gharama zake, fedha zikaendelea kushuka thamani. Kibenki elfu tatu ni elfu tatu tu. Ungekuwepo ukazitumia zingezalisha faida. Kwa bahati mbaya ulipotea. Kwani ulikuwa wapi mzee?”

Sikumjibu. Nilijikongoja kuinuka. Nikapepesuka. Nikajikongoja tena kutoka nje ya ofisi hiyo, macho yakiwa hayaoni vizuri, miguu ikiwa haina nguvu.

SURA YA ISHIRINI NA NNE

Dar es Salaam, jiji la Raha na Karaha

Dar es Salaam niliiona chungu. Watu, majengo, magari na kila nilichokiona mbele yangu kilinitisha na kuniogofya. Ndiyo, mji ulikuwa mzuri, uking'ara kwa usafi. Barabara zilimeremeta kwa usafi, magari yakipendeza kwa ubora na thamani. Watu pia walipendeza mitaani.

Wengi wao walivaa mavazi ya bei, waliharakisha kwenda hapa na pale huku nyuso zao zikiwa na dalili za matumaini kinyume cha ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Yote hayo niliyaona na yalinivutia, lakini bado Dar es Salaam niliiona chungu. Ilikuwa baada ya lile pigo la mwisho pale benki. Pigo ambalo liliniacha taabani, nusu hai nusu maiti.

Sikujua nilitoka vipi pale benki hadi stesheni ya reli. Sijui ilikuwaje hata nikafika huko bila kugongwa na moja ya magari tele yaliyotapakaa barabarani kama siafu. Mradi nilijikuta mbele ya stesheni, macho yangu yakikodolea macho saa kubwa ya kwenye mnara. Ilionyesha kuwa bado kulikuwa na saa kama tano kabla ya treni kufika! Saa tano, ambazo nilizona kama miaka mitano! Sikuwa na jinsi. Ilibidi niendele

kusubiri. Kila dakika moja ya kuendelea kusubiri ilinitesa kama msumari wa moto moyoni.

Mara kwa mara, nilitoa zile senti zangu nilizopewa na mkuu wa gereza na kuzihesabu. Nilikuwa nimezipunguza kwa nauli ya daladala. Mia moja nyingine nililazimika kuzitumia kwa huduma ya chool! Nilikuwa na kiu lakini kila bomba nililofungua halikutoa maji. Baadhi ya 'wamachinga' walikuwa wakiuza maji ya chupa. Chupa ndogo mia tatu, kubwa mia saba hadi elfu moja. Maji ya kununua? Maji ambayo utoto wangu wote nimeyachezea katika mito, katika maziwa na hata baharini! Niliamua kujikaza kisabuni.

Nilikuwa na njaa vilevile. Lakini sikuthubutu hata kuuliza bei ya chakula. Nilijua ingebomoa zaidi visenti vyangu ambavyo sasa ilikuwa akiba yangu pekee maishani mwangu. Akiba ambayo ilikuwa lazima inifikishe nyumbani kwetu. Nikaamua kuivumilia njaa vilevile, nikifumbia macho watu wanaokula na kuizibia pumzi harufu tamu ya maakuli.

Saa zilikuwa haziendi. Nikaamua kupitisha muda kwa kutembeatembea mitaani. Nilifuata barabara ya Samora. Macho hayana mipaka, yangu yalipenya vioo vya maduka mbalimbali na kushuhudia vitu vilivyofurika madukani. Vifaa vya *elektrtroniki*, kama televisheni, deki, dvd, projekta na vinginevyo vilikuwa tele katika sura na bei mbalimbali. Nguo, viatu, pochi za kinamama na vinginevyo vilikuwa tele. Duka moja lilibandika bei kwenye bidhaa zake, viatu 120,000/= suti 550,000/= pochi 85,000/=! Sikuelewa. Sikuelewa zaidi pale nilipoona maduka hayo yakiwa yamejaa watu wakinunua vitu hivyo kwa fujo kana kwamba wana viwanda vya kuchapa noti.

Macho yangu yalivutwa pia na watu, hasa wasichana. Mavazi yao yalinitisha. Baadhi walivaa nguo fupi sana,

mapaja wazi, sehemu kubwa ya tumbo nje huku wakitembea hadharani bila wasiwasi wowote. Baadhi ilikuwa vigumu kujua kama walikuwa wasichana au wavulana kwa suruali zao za *jeans*. Fulana na kofia kwenye vichwa. Kitu kingine kilichonishangaza ni kuona wasichana wengi walivyofanana. Karibu wote walikuwa weupe! Karibu wote walikuwa na nywele za kizungu! Wengi midomo yao iling'ara kwa rangi nyekundu kama ndege! Wengi walinukia manukato makali ambayo siku za nyuma ungeamini kuwa umepishana na jini! Sikuelewa hali hii hadi nilipofikia duka moja lililokuwa likiua aina mbalimbali za nywele kama nilizoona kwenye vichwa vya akina dada na kila aina ya vipodozi! Kumbel!

Wavulana wengi nao walinikatisha tamaa. Walivaa *jeans* zao ambazo zilichakaa au kuchakazwa makusudi, sweta au fulana zenye picha za wacheza sinema wa Marekani kama Rambo na schwarznegger, huku wakiwa wamefunika vichwa vyao kwa kofia au vitambaa vyenye nembo za bendere ya Marekani. Baadhi yao walisuka nywele zao, baadhi walivaa hereni! Ilikuwa vigumu kujua kuwa vijana hao walikuwa Watanzania au Wamarekani weusi hadi pale utakapowasikia wakizungumza Kiswahili. Lakini Kiswahili hicho nacho kilikuwa na manjonjo yake. Kwa kweli, kilistahili kuitwa Kiswaengilish kwa jinsi kilivyochanganywa maneno ya Kiingereza na hata ya mitaani ambayo watu kama Shaaban Robert wangefufuka, wangeweza kuangua kilio.

Wakati huo nilikuwa tayari nimeloa chapachapa kwa jasho. Joto la hapa, mara nyingi linatisha. Nilitamani kununua lesa kama nilivoona wengine wakifanya lakini sikuthubutu. Shilingi mia tatu za kulipia kitambaa hicho nilizona kama milioni. Nikawa nikitumia kiganja au kiwiko cha mkono walao

kupunguza jasho la usoni ili niweze kuona niendako.

Wingi wa watu lilikuwa tatizo jingine. Mara kwa mara, niligongwa na mtu au kupigwa kikumbo kilichofanya nikaribie kula mweleka. Nilipogeuka kumtazama mtu niliyegongana naye alikwishakwenda zake bila hata kugeuka nyuma. Hiyo ilinifanya nikumbuke kile nilichosoma nikiwa gerezani juu ya kasi ya ongezeko la watu jijini hapa. Kwamba mwaka 1925 mji huu ukiitwa Mzizima ulikuwa na watu 30,000 tu. Leo unatisha.

Nilifika katikati ya mji wa Dar es Salaam. Pale nilipopita miaka mingi iliyopita na kusimama mbele ya sanamu ya yule Mjerumani machachari Bismarck akiwa na bunduki mkononi kaielekeza baharini. Sanamu hiyo haikuwepo tena badala yake ilijengwa sanamu ya askari mweusi kama mkaa, ikiwa na silaha vilevile kuashiria tulivyopigana na kufa kwa vita ambavyo havikuwa vyetu. Nilitazama kwa muda kabla ya kuendelea na safari yangu, taratibu hadi nilipoifikia bustani ya Ikulu. Miti mingi ya asili ilikuwemo kama nilivyoiona mara ya mwisho. Hata hivyo, nilihisi kuwepo kwa aina fulani ya upungufu. Nini kilichopungua? Nilijiuliza. Nikajibiwa na ukimya mkubwa wa eneo hilo. Ni ukimya huo ulionipa jibu. Zile kelele za wanyama na ndege mbalimbali, hasa tausi, hazikuwepo tena. Tausi wale, ambao mara ya mwisho walinivutia sana kwa jinsi walivyoipamba bustani hiyo kwa maringo na ulimbwende, mara kwa mara wakitoa sauti zao nzuri na kuifumua mikia yao iliyoficha kila aina ya rangi hawakuwepo tena. Walienda wapi? Nilijiuliza bila matarajio ya jibu lolote.

Nikashuka kilima cha Ikulu na kufika Pwani ya Magogoni. Kigamboni ilikuwa upande wa pili wa bahari kama nilivyoiacha. Lakini, sasa, badala ya kuvuka kwa mitumbwi ya makasia kulikuwa na chombo maalum ambacho kilipakia

watu, magari, mazao na hata mifugo yao na kuwavusha upande huu au ule. Nilitamani kuvuka katika kupoteza muda. Lakini nilipoambiwa kuwa ningelazimia kulipia, niliachana na mpango huo.

Nikalisogelea soko la mnada wa samaki. Biashara ilikuwa ikiendelea kama kawaida. Kando kidogo, akina mama walioitwa ‘mama ntilie’ walikuwa kazini wakitoa huduma ya chakula kwa haraka na kwa bei nafuu. Wakati huo tayari natetemeka kwa njaa, chango likinguruma kudai chochote, nilishindwa kujizuia zaidi. Nikaingia katika banda la mmoja wao na kuomba wali kwa samaki. Nilikula wali mtamu sana wa nazi ambao sikupata kuula kwa takribani miaka ishirini. Hata kabla sijakitafuna kichwa cha samaki wangu mmoja kunguru tele waliozagaa huko na huko jiji zima alitua ghafla na kukipokonya. Huyoo, akapaa hadi juu ya paa na kuanza kukila huku kunguru wenzake wakimshangilia. Watu wawili watatu walicheka. Mama ntilie wangu akaniongeza mboga, nikaendelea kula nikimlaani kunguru yule.

Nikakumbuka kusoma mahala, ama gazetini ama kitabuni, juu ya tatizo la ndege hao waliozagaa mjini Dar es Salaam, kwamba wameondokea kuwa kero ya kitaifa; wanaiba kila kinachoibika ikiwa pamoja na nyaya za umeme au vifaa vingine vya kiufundi. Kwamba ndege hao waliletwa nchini, kupitia Zanzibar mnamo miaka ya 1900 na wakoloni wa Kiingereza kwa kusudi la kuwafanya wasaidie usafi kutokana na tabia yao ya kula mabaki ya chakula, mizoga na takataka nyinginezo. Lakini hadi kufikia mwaka 1930 walijifanya ndege wa mjini ambao ni nadra sana kuonekana vijijini.

Nikauliza saa. Nilikuwa nimetumia saa moja na robo tu toka nilipoondoka stesheni. Bado nilikuwa na muda wa

kutosha. Nikaamua kutembea tena, safari hii nikielekea Kariakoo. Kinyume na safari yangu ya mwisho mjini hapo sikuona pori wala jani. Kisutu ambayo zama zile nusu yake ilikuwa pori, fisi wakirandaranda kutafuta chochote, sasa ilikuwa sehemu ya mji iliyotapakaa watu na majengo hadi upeo wa macho. Kilabu cha askari wa zamani kilikuwa pale. Lakini sasa kilijengwa jengo bora zaidi la ghorofa likiwa na wapangaji tele wenye shughuli zao. Ukumbi ulikuwa pale lakini haukuwa na pilikapilika zile za zamani. Ama wanachama wengi walikuwa wamekufa kwa umri mkubwa ama wamekata tamaa.

Kariakoo nayo ilikuwa muujiza mwingine. Pengine soko jipya lililojengwa juu ya lililokuwa handaki la kivita enzi za Mjerumani lilikuwa limevuta watu toka kila pembe ya mji na nchi ama Mungu alikuwa amedondoshea neema eneo hilo. Si haki kabisa kusema watu walikuwa wengi, bali walifurika! Mitaa ya Kongo na Msimbazi ilikuwa haipitiki. Kila mmoja akiwa na pilikapilika zake. Nje na ndani ya soko ndiyo ilikuwa kabisa. Kupumua peke yake ilikuwa shida, achilia mbali kutembea.

“Dingi vipi... mbona unashangaashangaa? Ambaa tupite,” kijana mmoja alinifokea baada ya kunipiga kikumbo.

Nikageuka kumtazama.

“Unashangaa nini? Kashangae feri, ambako shilingi inazama meli inaelea. Siyo hapa.”

Aliongeza.

Sikumwelewa kabisa. Nikajikokota kuondoka.

Ilikuwa kazi kubwa kujichoropoa toka katika umati huo na kuifuata barabara ya Uhuru hadi stesheni ambako niliamua kukatisha moja kwa moja na kuisubiri treni.

Nilijiunga na wasafiri wenzangu, wengi wao wakiwa na

mizigo na familia zao. Mmoja kati yao, aliyekuwa na mizigo mingi zaidi alikuwa msichana wa Kizungu. Mwembamba, mwenye pua ndefu na sura ya utulivu. Alikuwa peke yake akilinda mizigo yake kwa makini. Hali hiyo ilinifanya mie pia nizikumbuke pesa zangu. Nikatia mkono wangu mfukoni kwa nia ya kuzipapasa.

Mfuko ulikuwa mtupu! Nilishtuka kama niliyeguswa na waya wa umeme. Nikainuka na kukagua kila mfuko wangu. Hamkuwa na kitu. “Nimeibiwa!” nilisema kwa sauti huku nikitetemeka. Msafiri mmoja aliyekuwa akisubiri usafiri kama mimi aliniuliza taratibu, “Umeibiwa nini mzee?”

“Pesa,” nilimjibu.

“Nyingi?”

“Hapana za kutosha lakini. Zilikuwa pesa zangu pekee.”

“Pole sana. Alisema. Umeibiwa hapa?”

“Hapana. Bila shaka ni Kariakoo.”

Alinishangaa, “Ulienda Kariakoo? Kule hakufai kabisa.”

Nikamkumbuka yule kijana aliyenipiga kumbo na kisha kuniita ‘Dingi’. Nilihisi hatukugongana naye kwa bahati mbaya. Alikusudia. Ni yeye aliyeniibia au kuandaa mazingira ya kuibiwa kwangu. Sasa sina hata shilingi moja. Sina kitu chochote ninachoweza kuuza nipate walao nauli ya kunitoa Kigoma mjini na kunifikisha Kasulu!

Badala ya kulia niliangua kicheko. Kwa jinsi nilivyovaa, nilivyochakaa kwa jasho na vumbi, nadhani watu waliokuwa wakinitazama walishuku iwapo nilikuwa na akili timamu au la. Sikujali. Niliendelea kucheka, peke yangu. Kilikuwa kicheko cha uchungu, ambacho baadaye kiligeuka kuwa kilio. Niliijificha katika uchochoro mmoja na kuruhusu machozi kunitiririka.

Muda wa treni kufika ulikaribia. Kila mmoja alikaa tayari kwa vita ya kuwahi kuingia ndani. Lakini pale mmoja wa makarani wa TRC alipouendea ubao wa matangazo na kuandika kitu kwa chaki kila mtu alipigwa na butwaa. Mimi nilichanganyikiwa zaidi, mara baada ya kuusoma ujumbe ule.

Yule mwanamke wa kizungu, ambaye bila shaka hakujua Kiswahili vizuri alinisogelea na kuniuliza kwa Kiswahili chake kibovu, “Hiyo maana yake gani?”

Nikamfahamisha kwa Kiingereza. “Wanasema leo hakuna treni, hadi kesho.”

Yeye pia alipigwa na butwaa. Akanikazia macho ya mshangao kabla hajauliza tena, “Kwa sababu gani?”

“Sijui. Hawakuandika sababu.”

“Na hiyo kesho, ni saa ngapi?”

“Hilo pia hawakueleza,” nilimjibu.

Mama wa watu alitazama lundo la mizigo aliyokuwa nayo, akatazama kundi la watu waliokuwa pale, ambalo hakuweza kupambanua nani alikuwa msafiri kweli nani kibaka; akazidi kuchanganyikiwa.

Minong’ono mingi ilikua ikiendelea. Habari zilikuwa zimevuja. Treni ya mizigo ilikuwa imeanguka huko Kilosa na kufunga njia. Jitihada za kuinua na kisha kurekebisha uharibifu uliotokea zisingekamilika hadi kesho yake. Hivyo, hakukuwa na namna ya kuondoka hadi jioni ya kesho, kama tutakuwa na bahati.

Nilimfahamisha hayo yule mama wa Kizungu. Kiasi alielewa. Akanishukuru. Nikamwona akihangaika kutafuta namna ya kuondoka na vitu vyake vingi. Masanduku, maboksi na vikorokoro tele ambavyo hata sikuweza kubuni vina nini ndani. Nikajitolea kumsaidia. Tulibeba mizigo hiyo kwa taabu hadi chini ya mnara wa saa ambapo alizungumza na dreva

mmoja wa tekisi, wakakubaliana. Tukapakia vitu hivyo katika gari hilo.

“Wewe je? Utalala wapi?” Aliniuliza wakati akijiandaa kuingia ndani ya gari hilo.

“Nitafanya maarifa.” Nilimjibu

Alinitazama kwa muda kabla hajaifungua pochi yake ndogo na kutoa noti ya shilingi elfu kumi ambayo alinikabidhi. Katika hali ya kawaida nisingeweza kupokea fedha hizo, lakini kwa hali niliyokuwa nayo na shida ingekuwa dhambi kubwa kuzikataa. Nilimshukuru mara mbilimbili, kimoyomoyo nikimshukuru mara elfu na mbili. Ilikuwa kama nimepata milioni kumi!

Nikarudi stesheni. “Maarifa” niliyokusudia kufanya yalikuwa ni kuupitisha usiku hapo stesheni, ikiwezekana nilale juu ya viti vyao vya mbao, kuisubiri kesho. Sikuwa na bahati hiyo. Mara tu nilipopata kiti na kujipumzisha alikuja askari mmoja wa shirika hilo na kututangazia kuondoka hapo mara moja, utadhani tulipenda kuwa hapo. Tulipositasita walianza kutuswaga kama mifugo. Hatukuwa na namna zaidi ya kuinuka na kuondoka.

Niende wapi? Nilijiuliza. Wakati huo usiku ulishaingia, yapata saa mbili hivi. Tukio la mchana kule Kariakoo lilikuwa limenitia hofu kubwa ya kuibiwa tena. Kutembea usiku kucha pia kuliniogopesha. Hatari elfu moja na moja zingeweza kunitokea; ningeweza kupigwa na majambazi kwa kufikiriwa kuwa nina pesa; ningeweza kukamatwa na polisi na kurudishwa jela kwa kosa la uzuluraji. Ningeweza hata kuuawa na walinzi wa mabenki na majumba mengine kwa kisingizio cha kujaribu kuiba; na kadhalika na kadhalika.

Wakati nikijiuliza hayo nilikuwa nikirandaranda mitaani kwa hofu ya kukaa mahala pamoja kwa muda mrefu

na kushukiwa. Nilishangazwa na utulivu wa mji, tofauti kabisa na mchana. Watu wengi walijaa katika vituo vya mabasi wakipigania kurudi makwao, pembeni mwa mji. Katikati ya mji watu wengi niliowaona walikuwa Wahindi. Walipita katika magari yao au kuketi katika sehemu zinazotengenezwa vinywaji na kuku choma wakitumia. Nasikia wao, kwa ajili ya rangi zao na imani ya watu wengi kuwa wana fedha nyingi zaidi ni waoga wa kuishi uswahilini. Wako tayari kuishi mtu na mkewe na mama na na baba na watoto sita katika kijumba chenye chumba na sebule badala ya kwenda kando ya mji ambako wangechanganyika na Waswahili.

Niliacha barabara ya uhuru, nikaifuata ya Bibi Titi. Nikaifikia bustani ya Mnazi mmoja. Nikashangaa kuona kundi la watu, wakubwa kwa wadogo wakiwa humo ndani. Baadhi walikuwa wakipika kwa kuni. Nikawasogelea kwa matumaini ya kupata hifadhi ya kupumzika hadi kesho. Haikuwa. Kumbe hawa walikuwa ombaomba, jamii mpya iliyokuwa imeibuka na kujengeka nchini. Wakati wazazi walikuwa na tatizo moja au jingine, ama katika viungo ama katika mfumo wa kufikiria, watoto walitumiwa zaidi katika kuomba wapita njia, hasa wenye magari. Watoto hawa hawakuwa na mipango wala matumaini ya kwenda shule. Hivyo, walikuwa wakiandaliwa kuwa ombaomba wazoefu au majambazi sugu wenye hasira na maisha. Zaidi ya kuwakamata mara kwa mara na kuwarejesha vijijini, ambako walikaa siku mbili tatu na kurudi zao mijini, hakuna jitihada kubwa ya dhati iliyofanyika kuondoa tatizo hili linalozidi kuchanua.

Jamii hiyo haikuonyesha dalili za kunitaka katika kundi lao. Hata salamu zangu hazikujibiwa. Badala yake walinong'ona wenyewe kwa wenyewe kabla ya kuanza kutafuta silaha zao, fimbo, mawe na hata upanga. Sikusubiri

kufukuzwa. Nikajiondoa harakaharaka na kuendea kituo cha mabasi kilichokuwa na watu tele.

Naweza kupata wapi sehemu ya kulala? Nilimuuliza mtu mmoja aliyekuwa akisubiri basi.

Alinitazama kwa macho ya dharau, bila shaka akinichukulia kama kibaka aliyekuwa akitafuta namna ya kujichanganya ili baadaye apore chochote kinachoporeka.

Mtu wa pili alinijibu kwa kunielekeza kwa mkono. Nikainua uso wangu. Jengo kubwa lililopaa angani kwa takribani gorofa nane lilikuwa likimeremeta mbele yangu kwa nuru ya rangi mbalimbali toka katika vioo. Maandishi yenye maremborembo yalikuwa yakicheza kwa kuwaka na kuzimika, kila herufi kwa wakati wake na kusomeka, *Peacock hotel*.

Nikamtazama jamaa yule na kumcheka kimoyomoyo, jambo ambalo hakunielewa. “Kama haikufai,” alisema. “Ziko nyingine tele. Zipo za shilingi 500,000 kwa siku. Ziko za 100,000/= na hata zile za 20,000/=. Ni mfuko wako tu. Unaweza kulala Sheraton, unaweza kulala Kilimanjaro hotel au ukitaka Holiday Inn. Kama unataka hoteli za ufukweni nenda zAko Kipepeo Kigamboni, nenda Kunduchi au Bahari. Ziko tele...”

Nikabaini kuwa nanidhihaki. Nikasogea na kumnong’oneza karibu kabisa na sikio lake, “Natafuta hoteli za chumba cha shilingi elfu moja au mbili, sio zaidi.”

Akacheka. Kisha akasema, “Hizo pia nyingi tu. Utazipata Manzese kwa mfuga mbwa, Buguruni kwa Bibi Tarabushi au hata Mwananyamala kwa Mama Zakaria. Ukiwa na bahati hata Mapipa utapata.”

“Ni wapi huko?” nilimuuliza.

“Panda basi, nitakuonyesha.”

Nilimfuata ndani ya basi. Tukaketi kiti kimoja. Alishajua

kuwa nilikuwa mgeni wa mji. Hivyo, alinipa hadithi moja baada ya nyingine juu ya mji na vitongoji vyake.

“Unajua kwa nini panaitwa Mapipa?” alitaja. “Zamani palikuwa na vibanda vilivyojengwa kwa mapande ya mapipa juu na chini. Mapipa hayo ni yale yaliyotupwa wakati wa ujenzi wa barabara ya Morogoro. Yalikuwa na soko kubwa pale Mapipa.

“Lakini wakati ule Magomeni haikuwa kama hii ya leo. Mitaa yote ilikuwa na lami. Umeme uliwaka kila mtaa. Mifereji ya maji machafu ilikuwa imejengwa na inahudumiwa vizuri. Leo hii kila kitu kimekufa. Maji machafu yanamwagika hadi barabarani. Taa zimekufa, lami imekufa. Hata mabomba hayatoi maji.”

“Nini kilitokea?” nilimuuliza.

“Sijui,” alijibu

Pamoja na maelezo yake nilikuwa nikishangazwa pia na ukubwa wa mji wa Dar es Salaam. Toka katikati ya mji hadi tunafika Magomeni isipokuwa jangwani ambako wakati wa masika hufurika maji, sikuona pori. Mji ulikuwa umeungana, nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa. Wakazi walikuwa hawalali. Karibu kila mtaa niliona baa mbili au tatu, zikiwa zimechanganyika na makazi ya watu, makelele ya muziki yalishindana kwa sauti.

“Hivi hakuna biashara nyingine Dar es Salaam?” nilimuuliza mwenyeji wangu huyo.

“Kwa nini?”

“Naona baa kila mahala.”

Pombe ndiyo bidhaa inayotoka kuliko nyingine,” alinijibu. “Maduka mengi ya vitabu yamefungwa. Watu hawanunui isipokuwa kile kilicholazimishwa na Wizara ya Elimu. Maduka ya madawa pia yameanza kukosa wateja. Watu hawana uwezo

wa kununua dawa dukani wala hospitalini. Mtu anaweza kufa hata miguuni mwa daktari, kama hana pesa za dawa hakuna matibabu.”

“Kwa nini?” Nilimuuliza kipumbavu.

“Sijui,” alinipa jibu lilelile nililostahili.

Karibu kila kituo cha basi tuliwaona wasichana wadogowadogo waliovalia mavazi yao ya kutisha, wenyewe wakiyaita ya kisasa; wakiwa wamesimama. Hawakupanda basi lolote wala kuonyesha kuwa na haraka yoyote, usiku mwingi kama huo. Niliwatazama kwa mshangao.

Mwenyeji wangu aliusoma mshangao wangu, “Changudoa!” akasema.

“Nini?”

“Wale pale! Wanajiuza. Tunawaita Changudoa,” alifafanua.

“Si nasikia kuna maradhi hatari yanayoitwa UKIMWI?”

“Naam,” alinijibu. Tena omba kusikia usiombe kuuona kwa macho. Lakini kwa wale, UKIMWI ni ajali kazini!”

Sikuelewa. Nikanyamaza.

Tulifika Manzese. Tukashuka kituo cha karibu na daraja pekee la angani, lililoikata barabara ya Morogoro toka kulia hadi kushoto kupunguza ajali za barabarani ambazo niliambiwa ziliua waenda kwa miguu kwa wingi kuliko UKIMWI au malaria.

Nilielekezwa kuelekea kushoto. Kona moja, uchochoro; kona ya pili; uchochoro. Mara tukamezwa na kiza kizito. Bila msaada wa nuru hafifu toka katika vyumba vya wakazi wa eneo hilo nadhani hata mwenyeji wangu angeweza kupotea. Nilimfuata katika vichocho hivo, vilivyobana na kugubikwa na uchafu mwingi. Mara kwa mara tulikanyaga dimbwi la tope.

Mara mbili tatu tulikurupusha wanyama wadogowadogo ambao mimi nilidhani ni paka lakini mwenyeji wangu akaniambia, panya!

“Mbona wanene vile?” nikauliza.

Wanakula na kushiba. Manzese hii mjomba,” alijibu. Tulizidi kuingia ndani. Mwenyeji wangu alitembea haraka akipenya hapa na kutokea pale. Nilianza kuogopa. Kwanza, nilihisi kuwa hajui tunakokwenda. Pili, nilianza kumshuku kuwa huenda alikusudia kunitendea ubaya. Nikatamani kugeuka nirudi nilikotoka. Hata hivyo, hofu ya kupotea na kupatwa na mabaya zaidi ilinizuia. Badala yake nikamuuliza taratibu, “Mbona hatufiki?”

Aligeuka na kunitazama. Aliisoma hofu katika macho yangu. Akacheka. “Hofu ya nini?” aliuliza baadaye. “Hapo ulipo hata laki huna, achilia mbali milioni. Nataka kukusaidia upate mahala pa kulala, kwani unaonekana kuwa unahitaji msaada. Nikikuacha utapigwa na vibaka na kuvuliwa hata nguo ulizovaa.”

Nikamwamini.

Hatimaye tukaifikia nyumba ya wageni aliyoikusudia. Nje ya nyumba hiyo kwenye uchochoro mmoja kulikuwa na watu wanaokunywa pombe, wake kwa waume. Mwenyeji wangu alionekana mwenyeji hapa. Alimwita mmoja wa watumishi wa nyumba hiyo kwa jina, “Rehema! Mpe chumba mjomba wangu. Mchagulie chumba safi. Sawa?”

Rehema, msichana mkubwa mnene, aliyeonekana kalewa aliniashiria kumfuata. Nyumba haikuwa na umeme. Mishumaa miwili, mmoja uliowekwa mlango wa mbele na mwingine mlango wa nyuma ndiyo iliyotuongoza. Niligeuka

ili kumshukuru mwenyeji wangu. Hakuwepo. Alikwishapenya uchochoro mwingine na kuondoka zake. Nikamfuata Rehema.

“Unataka chumba che bei gani?” Aliniuliza. “Vipo vya elfu mbili na elfu na mia tano.”

“Nipe cha elfu na mia tano.”

Kilikuwa chumba cha uwani, kidogo sana. Dirisha lilikuwa moja, dogo vilevile. Kitanda chao kilitosha mtu mmoja tu, si zaidi.

“Kinakufaa?”

“Kinafaa sana.” Nilimjibu.

“Ngoja nilete mshumaa. Umeme umekatwa huu mwezi wa tatu. Na kishoka leo kachelewa kuja.”

“Kishoka ndiyo nani?” nikaomba kuelewa.

“Jamaa yetu ambaye huja usiku kuturudishia umeme. Asubuhi sana huja tena kuukata kabla TANESCO hawajapita mitaa hii,” alifafanua.

“Kwani mnadaiwa pesa nyingi?” nilihoji.

“Nyingi sana. Kama milioni tatu na laki sita hivi. Maji yenyewe mwaka wa nne hayajatoka. Lakini bili yao imefika laki tisa na nusu.”

Nikashangaa. Kwa hesabu za haraka haraka nyumba hiyo, yenye vyumba sita pekee na baa ya uchochoroni haikuwa na uwezekano wa kupata walao laki mbili kwa mwezi. Gharama hiyo ya umeme na maji ilitokea wapi? “Mtalipa?” nilimuuliza.

“Nani alipe? Unalipa deni linalolipika. Lisilolipika unaachana nalo,” alinisomesha.

Rehema alipoondoka nilipanda kitandani kwangu kulala. Ndio kwanza nikabaini kuwa godoro lilikuwa kuukuu, pengine halikupata kubadilishwa toka nyumba hiyo ilipojengwa. Mbavu zangu zilikwenda moja kwa moja kukutana na chaga

za mbao. Si hilo tu, dakika mbili tu za kupumzika juu ya kitanda hicho, nilikaribishwa na mbu na kunguni. Wakati mbu wakiuma baada ya kelele zao za vitisho masikioni, kunguni wao walinitesa kwa kufyonza damu yangu kimyakimya na kunisababishia maumivu mengine. Nilifanikiwa kuwaua kunguni wawili watatu. Lakini harufu yao kali na damu nyingi toka kwa wateja wao ilinitia kichefuchefu

Adha ya tatu ilikua ikinisubiri. Joto. Chumba kilichemka kwa joto kama tanuru. Nikainuka na kufungua lile dirisha pekee. Tendo hilo lilileta karaha badala ya faraja. Harufu nzito, ya kutisha iliyoingia chumbani humo toka dirishani ilinifanya niamke na kumwita Rehema. “Harufu hii ya nini?” nilimuuliza.

“Hilo dirisha huwa alifunguliwi!” alinionya akilifunga mara moja. “Kuna mfereji wa maji machafu hapo. Haujazibuliwa leo mwaka wa sita. Kwa hiyo, maji yametuwama uchafu umeoza na kufanya harufu ya kutisha.”

“Kwa nini hauzibuliwi?”

“Sijui”

Nikazidi kushangaa. Mambo gani haya ninayoyashuhudia, siku moja tu baada ya kutoka jela. Kama maisha ya uraiani ndiyo haya, malazi ndiyo haya, iko wapi tofauti ya kuishi uraiani na gerezani?

Tofauti kati ya maeneo ya Manzese na katika ya mji pia ilinishangaza sana. Wakati kule kulionekana kama Peponi huku hakukutofautiana sana na Jehanamu. Kama ungetokea moto, uteketeze nyumba moja ni dhahiri kuwa mamia ya nyumba yangeungua na maelfu ya watu kupoteza maisha. Nikaelewa kwa nini yanapozuka maradhi kama kipindupindu na hata UKIMWI hayaondoki kabla ya kuteketeza mamia ya watu katika maeneo kama haya. Huu ndio uhuru tulioupigania na kuupata? Nilijiuliza. Huu ndio Ujamaa niliousikia mara

kwa mara toka gerezani? Au ndio Azimio la Arusha lililopigiwa sana kelele?

Wakati nikiwaza hayo jambo la ajabu likatokea. Umeme uliwaka. Kishoka alikuwa amefika nadhani. Feni chafu lililokuwa darini likapata uhai. Ama liliwafukuza mbu ama waliogopa kelele zake, kwani niliona mbu wakipungua ghafla. Kunguni nao walijificha. Nikapanda kitandani na kujilaza. Usingizi ukanichukua.

Niliamka keshoyake saa tatu. Nilikuwa mgeni peke yangu katika nyumba hiyo. Rehema alikuwa akipita chumba hadi chumba kukusanya shuka kwa ajili ya kuzifua. Alinionyesha bafu ambalo lilikuwa na maji ya ndoo, kipande cha sabuni ya mchi kikiwa pembeni. Nilioga na kujisikia nikiburudika kidogo, hali ambayo ilinifanya nisikie njaa ikianza kulitekenya tena tumbo langu. Niliishtakia kwa Rehema ambaye alinielegeza uchochoro wenye ‘mama ntilie’ pekee eneo hilo. Nilimpata. Nikanywa chai ya shilingi hamsini, chapati mbili za mia na maharage ya mia. Chakula na bei vilinifuraisha sana.

Nikaanza kazi ya kutafuta njia ya kurudi barabarani. Nilielekezwa mara nne na kupotea mara mbili kabla ya kumwuliza bwana mmoja mtanashati ambaye aliniambia nimfuate.

“Ni afadhali kupotea *New York*, kuliko katika vichocho vya Manzese. Humu unahitaji akili za ziada kujua njia ya kwenda na kutoka kwako,” alisema kiongozi wangu huyo mpya wa msafara.

“Kwa nini inakuwa hivi?” Nilimuuliza.

“Umeshafika mwanza?” Alinijibu kwa swali jingine.

“Zamani sana.”

“Fika sasa hivi uone,” alisema “Kule watu wanajenga hata juu ya mawe. Ile mandhari nzuri ya asili imepotea kabisa

kwa ajili ya watu kutafuta makazi ya kuishi. Tatizo unaloliona hapa liko katika miji yote mikuu ya nchi yetu. Watu wanajenga hivyo, huyu hapa huyu pale, hakuna barabara, hakuna hewa, hakuna namna ya kuzoa taka.”

“Kwa nini lakini?” niliuliza tena.

Msemaji huyo alisimama na kunitolea macho kama anayenishangaa. “Kama umesoma kidogo ungeelewa kwa nini,” aliniambia. Akaongeza, “Siku zote mipango lazima iandaliwe kabla ya maendeleo. Ukiacha maendeleo yatangulie mipango ije baadaye matatizo ndio haya. Kuongezeka kwa watu wakimbizi wa kiuchumi toka vijijini ndio chanzo cha hali hii. Kutokujiandaa, yaani kupanga namna ya kukabiliana na changamoto hiyo matokeo yake ndio haya.

Bwana huyo alikuwa hajatosheka na maelezo yake. Akaniambia, kwa sauti ya siri kidogo. “Mimi ambaye naishi huku nafanya kazi wizara ya ardhi. Maombi yangu ya kiwanja kilichopimwa yalichukua miaka kumi kabla sijaamua kujihifadhi huku. Nakumbuka miaka ya 1980 na 1985 kulikuwa na maombi ya kupimwa viwanja 151,600 vilipimwa 7,114 tu. Unategemea nini kwa mwenendo huo wa takwimu?

Tukatokea barabarani. Alishika hamsini zake nikashika zangu. Kandokando mwa barabara hiyo niliwaona wauza mitumba wakinadi mali zao, “Shati mia tatu! Suruali mia tano... imefika jana tu toka kwa Reagari.” Nilishawishika kununua walao vazi moja ili nibadili zile nguo zangu za ajabuajabu, ambazo zilianza kunuka kwa jasho na uchafu. Hata hivyo mfuko haukuruhusu.

Nikapata basi lililonipeleka Stesheni.

SURA YA ISHIRINI NA TANO

Tanganyika, Ziwa Lenye neema

Nadhani nilikuwa mtu wa kwanza kufika Stesheni kati ya wasafiri wa siku hiyo. Nilinunua magazeti mawili ya Kiswahili, moja la Kiingereza na kuketi kwenye lile benchi la mbao kujisomea. Kama kawaida zilikuwa habari zilezile za kukatisha tama; Mzee ajinyonga kwa madeni; Msichana akamatwa kwa kutupa kichanga jalalani; Achomwa moto kwa kuiba fuko lenye nepi za mtoto, na nyingine kama hizo. Kurasa za mbele zilipambwa na habari za wakubwa; Rais aenda Uingereza; Waziri Mkuu akutana na Balozi mpya Japan; Hotel mpya kujengwa ufukoni. Upande wa michezo nao ulitawaliwa na habari za vilabu vilevile ambavyo nimekuwa nikivisikia toka mwaka wa 47; Yanga yasajili kinda; Simba kwenda mahakamani; Ligi kuu yahairishwa na kadhalika na kadhalika.

Ziko wapi habari za vijijini? Nilijiuliza. Nilikua na kiu kubwa ya kufahamu chochote juu ya vijiji. Moja ya habari kubwa iliyonigusa sana nilipokuwa gerezani ni ile ya operesheni ya vijiji vya Ujamaa, kwamba serikali ilikuwa imeamua watu wote waende katika vijiji vilivyopimwa kwa ajili ya kupatiwa huduma muhimu za kimaendeleo kama maji, barabara na zahanati. Kwa machache tuliyosikia huko gerezani operesheni

ilileta songobingo kubwa kwa wananchi, kiasi kwamba baadhi waliliwa na wanyama wakali huko porini walikohamishiwa, baadhi walidaiwa kujinyonga wakipinga uamuzi huo.

Mimi nilikuwa mmoja kati ya waathirika wa maamuzi hayo. Kwa jinsi ukoo wangu ulivyojitenga, toka mababu na mababu na kujenga nyumba kandokando ya mashamba yetu, kwa vyovyote vile tungekuwa waathirika wa kwanza katika operesheni hiyo. Safari hii ya kurudi nyumbani ilinitatiza kwa hilo. Sikujua wazazi wangu watakuwa wamehamishiwa wapi. Sikuwa na mawasiliano ya aina yoyote nao. Hivyo, sikujua nitaanzia wapi niishie wapi katika kuwatafuta. Kwa bahati mbaya, vyombo vya habari havikutoa walao fununu juu ya hilo.

Wasafiri walianza kufurika Stesheni hapo. Mmoja wao akiwa yule mama wa Kizungu na lundo lake la mizigo. Aliponiona alitabasamu, akanifuata. Nilimsaidia kuweka mizigo yake vizuri, kabla hajaketi na kuniuliza habari za usiku uliopita.

“Ulipata mahali pa kulala?”

“Naam,” nilimjibu.

“Mjini hapahapa?”

“Hapana. Nje kidogo ya mji.”

Alisita kidogo kabla hajageuka na kuniuliza tena, “Unajua jana hatukuambiana majina? Mie naitwa Jane, Jane Goodhall.”

Jane! Halikuwa jina geni sana masikioni mwangu. Nilipata kulisikia mahala. Wapi vile, sikuweza kukumbuka mara moja. “Nimepata kulisikia jina hilo, lakini sikumbuki wapi,” nilimwambia.

“Bila shaka.” Alijibu. Nimepatwa kuandikwa mara nyingi

katika magazeti na majarida yanayojihusisha na masuala ya maliasili hasa wanyama pori. Niko Kigoma katika hifadhi ya Gombe. Najihusisha na utafiti wa sokwe,” alifafanua.

“Bila shaka!” nilitamka kwa furaha. “Uko Gombe, kilometa zipatazo kumi na tano hivi, mwambao wa ziwa Tanganyika kuelekea kaskazini, sawa?”

“Naam,” alikubali, kiasi akiwa ameshangaa. “Kwa kweli, ni mwendo wa kilomita kumi na sita.” Aliongeza.

“Uko na mtu anayeitwa Hugo Van Lawick. Mpiga picha za wanyama ambaye ametengeneza filamu nyingi za wanyama,” niliongeza.

Mama huyo alizidi kushangaa, “Ni kweli kabisa. Hugo ni mume wangu. Alinikuta kule wakati naendelea na kazi yangu, yeye akifanya yake. Tukapendana, tukaoana. Umejuaje yote hayo?” aliniuliza.

“Nasoma sana. Nasikiliza redio. Habari za wanyama siku zote hunivutia sana. Habari zako za sokwe nimekuwa nikizifuatilia kwa karibu. Umekwishaajua lugha yao?”

Jane alicheka. Kisha akafafanua, “Sokwe, kama wanyama wengine hawana lugha. Wanawasiliana kwa ishara tu ya sauti na miili. Mimi wamenikubali baada ya kunizoea. Tunaelewana nao. Lakini mnyama ni mnyama tu.”

Wakati akimzungumzia sokwe niliona jinsi Jane alivyobadilika. Macho yake yaling’ara, sauti yake ikiwa wazi zaidi. Ilikuwa dhahiri kuwa mapenzi ya mama huyu kwa sokwe hayakuwa na kifani.

Haikuwa uongo. Historia fupi niliyokuwa nayo juu ya msichana huyu ni kwamba alikuwa ameingia katika misitu hiyo ya Gombe mara baada ya uhuru, akiwa mdogomdogo tu, ndio kwanza amemaliza elimu ya sekondari. Jane alifanya

maajabu kwa kuweza kuishi peke yake msituni, akiwafuata sokwe kila wanapokwenda, wakati mwingine akilala nao porini, hadi wakamzowea. Alifungua kituo maalumu ambapo sokwe huja na kupata mahitaji yao hasa ndizi ambazo walizipenda sana. Jane aliweza kumfuatilia sokwe toka anazaliwa, anakua, anabalehe hadi naye anapata mtoto, alinukuu mwenendo na tabia zao, chakula chao, tiba zao na hulka zao mmoja baada ya mwingine. Alimfahamu kila sokwe na kila familia ya sokwe vilivyo, kiasi cha kujua nani kiongozi wao, nani anapinduliwa uongozi na nani kapindua. Utafiti makini wa aina yake duniani ambao tayari umempatia shahada ya udaktari.

“Unajua hujaniambia jina lako?” Alinizindua.

“Naitwa Petro Mtukwao Kionambali,” nilimjibu.

Jane alifahamu Kiswahili kidogo sana. Kati ya machache aliyoyafahamu jina la ‘Mtukwao’ au ‘Kionambali’ lilimpa maana fulani, lakini hakuweza kuifafanua mara moja. Aliyataja majina hayo mara mbili tatu, akikosea, kabla hajakata tamaa na kuniuliza maana yake, “Petro bila shaka ni Peter kwa Kiingereza. Ni jina lenye asili ya Kigiriki likiwa na maana ya mwamba au jabali. Hii Kionambali au Mtukwao ina maana gani?”

Jane alinitazama , “Ni la Kiebrania,” nilimjibu. “Lina maana ya Mungu ni mwenye fadhila sio?” nilimuuliza kabla ya kumjibu.

Jane alionyesha mshangao. Nadhani hakutegemea kuwa pamoja na hali niliyokuwa nayo ningeweza kufahamu mambo mengi kama ilivyokuwa. “Ni kweli kabisa,” alijibu baada ya tabasamu fupi, “Kiona mbali?” alisisitiza.

Wazazi wangu hawakupata kuniambia maana hasa ya majina yangu. Nadhani yalitolewa na babu kwa sababu zake.

Hata hivyo nilimweleza Jane hili na lile juu ya maana ya majina hayo.

Sidhani kama aliridhika. Mara nilimwona akibadilika ghafla kama mtu aliyekumbuka jambo “Kionambali.... Mtu kwao... nadhani nilipata kuyasikia majina hayo kabla ya leo,” alisema.

Nikacheka.

“Unacheka nini?”

“Nina hakika hujawahi kulisikia mahala popote. Ni jina dogo sana katika nchi hii. Sijawahi kuandika kitabu wala kucheza mpira hata nijulikane.”

“Hapana, nimelisikia likitajwa. Si mara moja si mara mbili,” alisisitiza.

Sikuamini. Nikijua kuwa alitokea kwao Uingereza, akakaa Kenya kwa muda kabla ya kuja nchini sikuona vipi angeweza kukutana na jina langu. Hasa ikizingatiwa kuwa muda mwingi nilikuwa gerezani.

“Unakwenda wapi?” alinihoji.

“Kigoma.”

“Nyumbani kwenu?”

“Ndiyo.”

“Kwa hiyo, safari yetu moja.”

“Bila shaka.”

Alisita kwa muda kabla hajauliza swali jingine, “Kwa hiyo, unakwenda likizo?”

“Ndiyo na hapana,” nilimjibu.

“Una maana gani?”

“Nina maana kuwa ndiyo nakwenda nyumbani; hapana siendi likizo.”

Jibu langu lilimshangaza Jane, “Kwani unatokea wapi?”

Sikuona sababu ya kumficha, “Jela.”

Kiasi nilimwona akishtuka. Lakini, akiwa mwanamke mwenye roho ya chuma, anayeweza kuishi na kuvumilia hasira za ghafla za wanyama hatari kama sokwe, alijirekebisha mara moja. Badala yake aliniuliza kwa upole, “Nini kilitokea?”

Alikuwa binadamu wa kwanza uraiani aliyetaka kujua masaibu yangu toka nilivyofungwa hadi kufunguliwa. Akawa binadamu wa kwanza niliyepata kumsimulia, kwa tuo, yote yalinyonitokea hadi nikatupwa gerezani kwa miaka mingi. Sijui kwa nini niliamua kuwa wazi kwake. Nadhani ni kwa kuwa sikuwa na shaka kuwa ni mtu mwenye huruma sana. Kama anaweza kuishi na sokwe...

Nilipofika sehemu ambayo nilimtaja Dakta Leakey kama mwajiri wangu pekee ambaye niliishi naye kwa muda mrefu nilimuona Jane akishtuka. Mara akanikatiza kwa kuuliza, “Leakey yupi?”

“Leakey unaemjua wewe. Na mke wake Mary... wagunduzi wa fuvu la kale zaidi nchini,” nilimjibu.

Jane aliinuka na kunikodolea macho ya mshangao. “Sasa nimefahamu wapi nilisikia jina lako kwa mara ya kwanza,” alisema baadaye.

“Wapi?”

“Kwa akina Leakey. Walikuwa hawaachi kukutaja. Walishangazwa sana na kutoweka kwako ghafla, bila kuaga, mtu ambaye walidai kuwa walimtegemea sana katika shughuli zao.”

Ikawa zamu yangu kushangaa, “Unawafahamu?”

“Vizuri sana,” Jane alinijibu. “Walipata kuniajiri pia. Kutokana na mapenzi yangu kwa wanyama na mazingira

Leakey alinishawishi kwenda kwenu Kigoma kufanya utafiti wa wanyama wale, binamu zetu.”

Sikuwa na la kusema, nikauliza, “Hawajambo?”

“Nani?”

“Akina Leakey.”

Jane akachekeka, “Wazima sana. Kwa nini ulifanya vile?”

“Kufanya nini?”

“Kufungwa. Kukubali kufungwa bila kuwaarifu. Wangeweza kukusaidia.”

Ilikuwa wazi kuwa Jane hajui maana ya kufungwa, hasa katika nchi zetu za dunia ya tatu. Mnyama anayefugwa ana uhuru mara mia zaidi ya mfungwa.

Wakati nikizungumza na Jane nilimwona msichana mmoja, msafiri kama sisi, akinitazama sana. Nilimtupia macho. Nikamwona akiyakwepa macho yangu kwa namna ya haya kiasi. Kitu fulani kilinifanya nipate hisia kuwa namfahamu. Wazo ambalo nililipuuzwa mara moja. Jana tu nimetoka jela, nitamjulia wapi msichana huyu?

Kitu kimoja kilinivutia kumtazama msichana huyu alikuwa ana tofauti kubwa na wasichana wengine wengi niliowaona jijini hapo. Alikuwa Mwafrika halisi. Nywele zake zilikuwa fupi, ambazo hazikupata kuathiriwa na madawa. Ngozi yake laini maji ya kunde, pia haikuwa na dalili zozote za kuathiriwa na madawa hayo. Hata mavazi yake yalikuwa ya heshima. Gauni jekundu lililomkaa vizuri lilimfunika hadi miguuni.

Lakini kuna kitu cha ziada ambacho kilinivutia zaidi kwa msichana huyu. Halikuwa umbile lake wala mavazi yake. Kilikuwa kitu fulani. Kwa bahati mbaya sikuweza kubaini mara moja ni kipi hasa kilichonivutia zaidi kwake. Ningeweza

kukisoma kitu hicho katika macho yake, lakini tayari aliyakwepa macho yangu na kutazama upande mwingine.

Honi ya treni iliyokuwa ikiingia stesheni iliniokoa kujibu swali la Jane pamoja na kuendelea kusumbua fikra zangu juu ya msichana yule. pilikapilka za kuingia katika mabehewa zikaanza. Mimi nikiwa sina mzigo wowote nilifanya kazi ya kumsaidia kupakia vitu vyake katika chumba cha daraja la pili alicholipia. Mimi, nikiwa sina namba ya kiti, nilipata debe moja la msafiri mwenzangu na kulikalia. Roho yangu ilipumua pale dakika ishirini baadaye treni ilipoanza safari ya kuelekea bara.

Jing... jang... jing... jang... tuliua mji na kuingia Buguruni. Jing... jang... jing... jang ... vingunguti. Jing... jang... jing... jang... Karokota. Taratibu tukauacha mkoa wa Dar es Salaam na kuingia Pwani. Tulizipita stesheni za Soga, Ruvu na Magindu kabla hatujaiacha Pwani na kuingia Morogoro katika stesheni za Kidugalilo, Ngerengere, Mikesa na hatimaye Morogoro mjini.

Wakati huo usiku ulikwishaingia. Sikuweza kuziona vizuri stesheni za Mkata, Kimamba na ile ya Kilosa. Toka hapo tuliingia stesheni ya mpaka wa Morogoro na Dodoma, Kidete kabla ya kufika Godegode, Gulwe na Kikombo. Tulifika Dodoma alfajiri ya siku ya pili.

Jane alikuwa akinitafuta. Alinikuta nikiwa nimeegemea mlango nikijaribu kupata chochote ambacho ningeweza kupata juu ya mji wa Dodoma, makao makuu ya serikali baada ya kuhamishwa toka Dar es Salaam. Zaidi ya majengo kadhaa, barabara pana zaidi na watu wa kutosha zaidi bado Dar es Salaam niliyoiacha jana ilifanya Dodoma ionekane kama mzaha kuiita makao makuu.

“Unajisikiaje?” Jane aliniuliza

“Safi kama chuma cha pua,” nilimjibu

Akacheka. “Twende tukapate kifungua kinywa,” aliniambia.

“Wapi?”

“Mgahawa wa humu ndani.”

Nikamfuata. Tulipita mabehewa kadhaa kabla ya kufikia behewa la chakula. Tukaketi. Aliagiza chapati mbili, supu ya kuku na chai kwa kila mmoja wetu. Kwangu ulikuwa mlo ambao sitapata kuusahau kwa muda mrefu. Toka nilipopata chai na maharage ya ‘mama ntilie’ kula Manzese tumbo langu lilikuwa halijaonja chakula zaidi ya karanga za mia moja nilizonunua humo ndani.

Tulikula taratibu. Kila mara Jane akinidodosa juu ya mipango niliyokuwa nayo baada ya kutoka gerezani. Hakunieleva pale nilipomwambia kuwa nilikuwa na mpango mmoja tu katika akili yangu, ambao haukuwa ziadi ya kufika nyumbani, kumwona babu na wazazi wangu, kama wako hai.”

“Bila shaka ulitoka kwenu mikono mitupu... unataka kurudi mikono mitupu?” alinihoji.

“Sina jinsi.”

“Kwa nini?”

Asingeweza kuelewa. Asingeeleva hata kidogo hata kama ningemwelewesha vipi. Kwamba lazima nikaombe radhi kwa kupoteza hirizi! Kwamba nina hakika mikosi na balaa nyingi ninazopata zilitokana na kuipoteza baraka ile, hivyo lazima nioshwe kwa kutemewa mate usoni. Mzungu, mwenye utamaduni tofauti na wangu angeelewaje? Sikujisumbua kumwelewesha.

Jane akaamua kuifichua siri iliyokuwa moyoni mwake. Alinitaka twende wote Gombe nimsaidie kazi. Kwamba alikuwa na mipango ya kufungua kituo kingine cha sokwe kusini mwa ziwa Tanganyika, katika milima ya Mihale, kilometa zipatazo 120 toka mjini Kigoma. Kwa mujibu wa Jane milima hiyo ilikuwa na sokwe waliokadiriwa kuwa 700 katika makundi kama kumi na mitano. “Siwezi kufanikisha peke yangu. Lazima niwe na mtu mwaminifu, mwadilifu na pia tunayeelewana lugha vizuri,” alisema

“Halafu,” aliongeza. “Mume wangu ana mpango wa kutengeneza filamu kubwa, itakayojumuisha vivutio mbalimbali vya Tanzania. Kwa historia yako na uzoefu wako hakuna mtu ambaye atamfaa zaidi yako.”

Hili la pili lilinivutia zaidi. Ningependa sana kuwa sehemu ya historia ya mtu atakayefanikisha kazi hiyo. Lakini nilikwishajiwekea nadhiri ya kutojihusisha na jambo lolote kabla ya kufika kwetu. Ama niwaone wazazi wangu, ama niyaone makaburi yao.

Nilimweleza hivyo Jane. Bado hakunielewa. Lakini hilo lilikuwa tatizo lake, halikuwa langu.

Safari ya mchana ilivutia zaidi. Tulisimama dirishani mimi na Jane tukiangalia nje, kituo baada ya kituo. Nkungu, Nala, Bahi, Kintinku, Saranda, hatimaye tukaingia Manyoni. Watu na mazingira maeneo yote haya havikunifurahisaha sana. Ardhi ilijaa vumbi, mtu mmoja hapa na pale. Hali iliyonifanya hisia za nusu jangwa zinijie akilini. Hali kadhalika hali za wakazi wengi iliashiria umasikini mkubwa. Mavazi ambayo wengi wao walivaa, baadhi wakitembea bila hata kandambili. Ilikuwa dalili tosha ya umasikini. Hata wale waliokuwa na bidhaa, bidhaa zao ziliashiria kuganga njaa tu. Mtu mzima

akiwa na vichane vitatu vya ndizi, mwingine akiwa na chupa moja ya asali, yule sinia la karanga! Kwa gari moshi ambalo hupita hapo mara mbili tatu kwa wiki sikuona kama biashara hizo zilikuwa na namna yoyote ya kuwaondoa katika vibanda vya tembe tulivyokuwa tukiviona toka tunaingia Dodoma hadi tunaiacha.

Stesheni ya Manyoni ilishamiri kwa biashara ya kuku, walio hai kwa waliokaangwa. Takribani kila mtu alikuwa na sinia yenye mapaja ya vidari vya kuku wanaotamanisha kuwala. Bila shibe ya mlo alionipa Jane ningejikongoja kununua paja moja. Ingawa baadhi ya watu hudai kuwa hawa si kuku wa kawaida kwa ajili ya wingi wao. Wanadai baadhi ya tunaowadhamia kuku waliokaangwa ni kunguru na ndege wengine wa porini waliozagaa katika maeneo hayo. Kwa kweli, ulikuwa mzaha wa watani wa Wanyaturu na Wanyiramba.

Toka Manyoni tuliingia Itigi, kaskazini hadi Malingwe. Jua likaanza kuzama. Jane alirudi chumbani kwake kujisomea kitabu mimi nikaendelea kuranda ndani ya mabehewa hayo mengi. Tukafika Nyama, tukaingia Igagula. Saa mbili za usiku tulifika Tabora. Hapo tulichukua muda mrefu kutokana na pilikapilika nyingi za kubadili mabehewa, kukagua vichwa vya treni na pengine kufanya ukarabati.

Nilitamani kuutumia muda huo kuchepuka kidogo nikautupie macho, walao kidogo mji wa Tabora, ambao uko kidogo nje ya stesheni hiyo. Hata hivyo kwa kuchelea kuachwa sikuthubutu. Niliishia kuchungulia tu nje ya stesheni ambako niliiona ile miembe iliyozeeka lakini bado ilikuwa ikipamba na kuzaa embe tamu za dodo na bolibo.

Niliona pia kundi kubwa la mbuzi wasio na mlinzi wakirandaranda kando ya barabara hiyo. *Mbuzi wa Tabora?*

Nilijiuliza nilipokumbuka simulizi ya mji wa Tabora kuwepo na mbuzi wengi wasio na mmiliki ambao hutembea ovyo mitaani bila kubugudhiwa, mbuzi ambao inaaminika kuwa kwa namna moja au nyingine wanahusiana na ama ushirikina ama laana fulani. Mwenyewe alifariki zamani na kufanya wawe hawana mwenyewe, lakini kila mtu ambaye huthubutu kuwala hudhurika na hata kupoteza maisha. Jambo ambalo lilisababisha hata wezi wa mjini hapo wawaogope.

Honi ya kuashiria safari ikapigwa. Nikarudi au kuparamia behewa lolote lililokuwa karibu. Dakika tano baadaye safari ikaanza. Ilikuwa awamu ya mwisho ya safari hiyo ndefu ya kilometa 2600 toka Dar es Salaam hadi Kigoma.

Hamu niliyokuwa nayo ya kufika nyumbani ikaanza kuingia nyongo. Hofu ikaanza kuchukua nafasi. Hofu ya kutojua lipi nitalikuta huko nyumbani. Habari za kufurahisha au kuhuzunisha, heri au shari. Hali kadhalika, aibu ya kurudi mikono mitupu kama nilivyoondoka, baada ya miaka nenda rudi ya kuhangaika pia ilinitesa sana. Sio siri, nilitamani garimoshi hilo lipate ajali, mtu mmoja tu apoteze maisha; Petro Kionambali.

Haikuwa. Treni iliendelea kukata mbuga. Ikiwa safari ya usiku sikuweza kuona mabadiliko ya ardhi toka ile ya nusu ukame. Ya Dodoma hadi Tabora hadi ile yenye rutuba nyingi ya kutokea Tabora hadi Kigoma. Kelele za wasafiri kila tulipofika stesheni ndizo ziliniashiria tuko wapi; Usoke, Kaliua, Suinge, Malagalasi, Uvinza, Simbo, Luiche na hatimaye Kigoma

Ulikuwa mkesha wa aina yake. Pilikapilika za kuingia katika mabehewa kila stesheni zilikuwa kubwa na za fujo kubwa. Mizigo ilirushwa ndani ikifuatiwa na wababe; wake kwa waume. Ilikuwa rahisi kwa mgeni kufikiria kuwa watu

wa Kigoma wana asili ya vurugu. Lakini kamwe mwenyeji asingeweza kufikiria hivyo. Watu hawa hawakuwa na njia nyingine yoyote ile ya usafiri. Maeneo mengi hayakuwa na barabara iliyowaunganisha na upande mwingine wa dunia zaidi ya treni. Hivyo, kuachwa na usafiri huo kulimaanisha kuharibikiwa kwa mipango yako ya safari pengine kwa wiki nzima au zaidi. Hivyo, kutumia nguvu na ubabe lilikuwa jambo la lazima.

Tulifika Kigoma saa moja na nusu za asubuhi, lakini kwa sababu za kijiografia ndio kwanza jua lilikuwa likichomoza. Miale yake ilipenya milima ya Bangwe na kutuangazia pale stesheni, kando kabisa mwa Pwani ya ziwa Tanganyika. Ziwa ambalo liliupokea mwanga huo, likaujumuisha na maji yake yasiyo na rangi na kufanya limeremete kwa mchanganyiko wa nuru ya rangi ya dhahabu toka angani na buluu toka katika lindi la maji na kutoa sura ya kuisisimua sana.

Nilishuka na kusimama kwa muda hapo nje nikitazama huku na kule kana kwamba siamini kuwa nimerejea nyumbani. Macho yangu yalivutwa na jengo imara la stesheni hiyo, lililojengwa na Mjerumani toka enzi zile. Zaidi ya ukarabati wa rangi na pengine bati jengo lile lilikuwa imara kama walivyoliacha. Wala halikuwa na dalili zozote za kupoteza uimara wake katika siku za usoni.

Nikahamisha macho kwenye jengo na kuyatupa ziwani. Kwa mbali, niliweza kuona mitumbwi na mashua za wavuvi wakirejea Pwani baada ya shughuli zao za usiku kucha, lakini kilichovutia zaidi macho yangu ni meli kubwa, yenye rangi nyeupe iliyotia nanga katika bandari hiyo. Jina lake liliweza kusomeka hapo niliposimama, MV LIEMBA.

Hii ni mali yenye historia ya pekee duniani. Kwanza,

inaaminika kuwa ni meli ya kale kuliko zote duniani ambayo bado inafanya kazi. Pili, imezitumikia enzi zote muhimu za historia ya Tanganyika ikiwa imeletwa na kuunganishwa na Wajerumani miaka ya 1914 na kupewa jina la *Graf Von Goetzen*. Mjerumani alipozidiwa katika vita ya pili aliizamisha katika lindi la ziwa Tanganyika wa nia ya kumkomoa Mwingereza aliyechukua madaraka. Lakini wao walifanya kila jitihada kuiibua majini na kuitengeneza. Ikaanza kazi kwa jina jipya la *SS Liemba*. Tanganyika ilipopata uhuru wake *Liemba* ilikarabatiwa tena na mitambo yake badala ya kutumia mvuke ikawa ikitumia dizeli, hivyo ikaitwa *MV Liemba*. Meli hiyo hadi sasa ni tegemeo kuu la usafiri katika mwambao wa ziwa Tanganyika hadi bandari za Mpulungu Zambia, Bunjumbura, Burundi na Kelemie Kongo.

Upande wa pili wa ziwa hilo macho yangu yalivutwa na baadhi ya milima ya nchi hizo. Burundi kwa upande wa kaskazini na Kongo ilionekana mbele yangu, magharibi ya nchi yetu. Hali ya hewa ikiwa safi, anga likiwa angavu niliweza kuiona milima ya nchi hizo kwa uwazi kabisa.

Sijui ningesimama hapo kwa muda gani kama nisingeshikwa bega na nilipogeuka nikakutana na uso mpole wa yule msichana aliyenivutia pale stesheni ya Dar es Salaam. Sura yake ilikuwa iliyojaa haya. Hata hivyo, alijitahidi na kuniuliza kwa sauti yake ya upole, “Samahani kaka. Hivi unaitwa Petro Kionambali?”

“Naam,” nilimjibu.

“Ulipata kuishi katika maeneo ya Bonde la Ufa?” aliongeza swali jingine ambalo pia nililikubali. Nikamwona akibadilika sura. Kwanza alitabasamu. Kisha tabasamu lake likamezwa na uso uliojaa huzuni, machozi yakimlengalenga machoni.

“Vipi kwani?” nilimwuliza kwa mshangao.

“Petro... Hunikumbuki?”

Sikuweza kuelewa anachozungumza. “Nakumbuka kukuona juzi pale stesheni, Dar es Salaam, kwa mara ya pili nakuona leo hapa Kigoma,” nilimjibu

Pamoja na machozi yake nilimwona akitabasamu kisha alisema, “Petro wewe ulipata kuokoa maisha yangu kwa kuhatarisha yako. Ulinichukua hadi Singida ambako ulinipeleka misheni ambako walinilea kiimani na kielimu. Sasa hivi nina kazi nzuri hapa Kigoma.”

Akili zangu zilikimbia na kunirejesha nyuma zaidi ya miaka ishirini iliyopita. Nikamwona yule msichana wa Kimasai aliyekuja katika kambi yangu huku akitetemeka. ‘...*Nisaidie ...Naogopa*’ Nilikumbuka jina lake, “Nashifa sio?”

Nilimwona akichangamka. “Unalikumbuka hata jina langu? Hata hivyo nilibatizwa na kupewa jina jipya la Maria. Lakini sijaliacha jina langu la asili. Nimefurahi sana kukuona Petro. Siku zote nilikufikiria usiku na mchana. Nilikuwa na hakika kuwa ingetokea siku nikakutia machoni. Imetokea...” alisita kuzungumza na kuangua kilio.

Sikujua kilichotokea nilijikuta nimemkumbatia kwa namna ya kumfariji huku yeye pia akinikumbatia na kukilaza kichwa chake juu ya kifua changu akiendelea kulia huku akinong’ona maneno fulani ambayo sikuyasikia vizuri. Nilisikia machache tu, “Uliokoa maisha yangu... kwa gharama ya kuharibu yako... sikupata kujisamehe kwa kitendo kile...”

Nilicheka kidogo kabla ya kumnong’oneza vilevile, “Maisha yangu ni hadithi nyingine. Masaibu yako hayahusiani hata kidogo na yale yaliyotokea. Yangu nayajua mimi na Mungu wangu.”

Tulikuwa bado tumekumbatiana. Kama si macho ya wapita njia kututazama kwa mshangao sijui tungekaa katika hali hiyo kwa muda gani. Macho yao yalifanya nijikumbuke na kujitazama. Nilitoa picha ya kuchekesha sana kwa mavazi yangu ambayo hayakuwa zaidi ya midabwada, kumkumbatia msichana huyu mtanashati ambaye sasa alivaa vitenge vilivyomkaa kana kwamba alizaliwa navyo. Nikajikwanyua toka mikononi mwake na kumtaka radhi.

“Samahani ya nini? Huju nilivyofarijika Petro.” Alisema.

“Lakini tayari njia zetu zimetofautiana sana. Mimi ni ndege wa jela asiyestahili kukukumbatia hadharani. Tazama nilivyo,” nilisema nikijitenga naye zaidi ili anione vizuri zaidi.

Kwa mshangao wangu alicheka kabla ya kusema, “Najua yaliyokusibu. Nilikuwa nikifuatilia kwa karibu maongezi yako na yule mama wa Kiingereza. Anaitwa nani vile, Jane siyo?”

Nilikubali kwa kichwa.

“Hivyo huna haja ya kuniambia chochote zaidi. Najua umerudi kwenu. Najua umerudi mikono mitupu. Usijali. Nitakusaidia kadri ya uwezo wangu. Uliniokoa kwenye mvua mimi pia nitakuokoa kwenye jua.”

Alitia mkono wake kwenye pochi lake la mkononi na kutoa kadi ambayo alinikabidhi. Ilikuwa na majina yake na namba za simu. Kilichonivutia zaidi ni cheo chake. Afisa uhamiaji wa mkoa! Niliduwaa.

“Matunda ya wema wako hayo.” Alinifafanulia.

“Wamisheni wale walinipa elimu bora hadi chuo kikuu. Mara kadhaa nimepelekwa nje kuongeza ujuzi. Huu ni mkoa wangu wa tatu toka nilipopanda cheo.”

Nilizidi kuduwaa. Safari hii aliniondoa mshangao kwa kunishangaza zaidi. Alitia tena mkono wake mfukoni na

kunipa kitita cha fedha. Kwa hesabu za haraka haraka zilipata kuwa shilingi laki moja.

“Za nini?” nilimuuliza.

“Zitakusaidia kidogo. Najua una matatizo mengi. Fika nyumbani, wasalimu wazazi halafu njoo mjini tushauriane.”

Nilitamani kulia. Kwa nini siku zote maisha yangu yamekuwa ya kukutana na binadamu wenye roho mbaya kama shetani na wale wenye roho nzuri mfano wa malaika? Nilijiuliza huku nikiwa nimemkodolea macho. *Unajua wewe ni malaika. Unajua utafika mbinguni?* Nilitamani kumwambia hivyo. Nilishindwa. Badala yake nilijikongoja kumwuliza, “Umешаolewa?”

Alinipa jibu jingine ambalo liliniacha taabani zaidi, “Nilikuwa nikikusubiri wewe.” Nilipomtazama, aliyaepuka macho yangu na kutazama chini. Mara nikaelewa kilichonivutia zaidi juu yake. *Haya!* Pamoja na elimu yake, pamoja na cheo chake, bado alikuwa msichana wa kiafrika halisi, mwenye uso wa soni tofauti kabisa na wasichana wengi wa kileo.

“Sina budi kuondoka,” aliseme. “Tafadhali tuwasiliane. Sawa Petro Kionambali?”

“Bila shaka.” Nilimjibu

Akaifuata gari ambayo muda wote ilisimama nje ya stesheni ikimsubiri. Akaingia upande wa pili wa dereva na kupunga mkono wakati gari ikitiwa moto na kuondoka.

Mara alipotoweka machoni mwangu, nilihisi upweke wa pekee ambao sikupata kuujuu huko nyuma.

Nilizihesabu tena fedha alizonipa. Nilikuwa na laki moja na hamsini. Sikuhitaji kufikiria sana. Niliendea duka la karibu la nguo na kununua shati mbili, suruali mbili na shuka la kujifunika.

Nilikuwa na mfuko wa nguo mpya mkononi ndiyo kwanza nilijiona nilivyochakaa. *Nilikuwa nanuka!*. Niliweza hata kuisikia harufu chafu ya mwili wangu mimi mwenyewe. Jasho la joto la Dar es Salaam na vumbi la Dodoma, purukushani za Tabora na malazi mabaya ndani ya behewa lililotoa mchanganyiko wa kutisha. Nikaamua kuiacha bandari na kuufuata ufukwe nikielekea Mtanga hadi nilipopata sehemu faragha ambayo nilivua nguo zangu na kujitupa ziwani. Sikuwa na sabuni wala mswaki. Nilitumia mchanga na vidole kujisugua. Nikapiga mbizi mara mbili tatu. Kweli, aliyeogelea hafi maji, kwani nilijikuta nikielea juu ya maji kana kwamba maisha yangu yote nilikuwa ziwani humo.

Nilipotoka majini nilijihisi mtu mpya. Hisia fulani ziliniambia kuwa kwa kuoga katika ziwa hili lenye historia ya pekee nilikuwa nikisafisha mikosi na mikasa yote iliyoniandama na kuanza maisha mapya.

Pengine haikuwa uongo. Ziwa Tanganyika lilikuwa mwujiza mwingine wa dunia. Kwanza lilikuwa refu kuliko maziwa yote duniani. Pia, kina chake kwenda chini kilivunja rekodi ya maziwa yote ya ulimwengu. Likiwa limeenda chini kwa takribani meta 2400 toka kilele cha milima ya Mahele iliyopo kilometa 150 toka Kigoma mjini au meta 1500 toka ardhi ya kawaida ya mkoani humo mwisho wa kina hicho uliwiana na usawa wa bahari kwa miji ya Dar es Salaam na Zanzibar. Inaaminika kuwa kuwepo kwa ziwa hilo ni matokeo ya mabadiliko makubwa yaliyopata kuitokea dunia, kama matetemeko ya ardhi au volkano ambayo pia yanaaminika kuibua vitu kama Bonde la Ufa. Walikotokea samaki ainaaina na viumbe wengine hai waliomo tele ziwani humo ni fumbo jingine ambalo mwanadamu hajapata kulipatia ufumbuzi.

Sikuhitaji gari kutoka kigoma hadi Mwanga. Mwendo wa dakika ishirini kwa mguu uliniwezesha kufika katikati ya mji huo. Mwanga ilichangamka. Vijana waliokuwa wakifanya kazi za kushevu walikuwa tele katika ofisi zao zinazovutia kwa vioo na viyoyozi. Niliingia katika kimojawapo cha vibanda hivyo na kukinga kichwa changu.

“Nywele na ndevu,” nilisema.

“Utahitaji tukuwekee *na super black*, kaka?” niliulizwa na kijana huyo

“Kwa nini?”

“Mvi zinakuanza. Unaona hapa?” alielekeza.

Nikajitazama katika kioo. Kweli, kulikuwa na mvi mbili tatu katikati ya kichwa changu. *Nazeeka!* niliwaza kwa mshtuko kidogo. Kuzeeka kabla ya kufanya jambo lolote ambalo familia, jamii na nchi yangu itaweza kujivunia haikuwa dhamira yangu hata kidogo.

“Hapana, shevu tu,” nilimwambia. Sikuona haja ya kuficha shahada ya umri wangu.

“Ndevu unashevu kwa mashine au *magic*?”

“Ndiyo nini hiyo *mejiki*?”

Akanionyesha dawa fulani. “Hii inafanya kidevu kiwe kama cha mtoto mdogo,” Alifafanua.

“Na bei yake?”

“Iko juu kidogo.”

“Kama ni hivyo tumia mashine.”

Muda mfupi baadaye nilikuwa mtu mwingine kabisa, mtu anayependeza kwa usafi hasa kwa kijana huyo kunipaka mafuta ambayo yalilainisha ngozi yangu. Nilijitazama kwenye vioo vyake, mbele na nyuma, kwa muda kabla ya kumlipa na kuondoka.

Niliuliza magari ya kwenda Kasulu. Niliambiwa kuwa nimekwishachelewa, kwamba lilikuwepo basi moja tu la Mwarabu ambalo huondoka saa kumi na mbili za asubuhi kila siku. Pia, nilidokezwa kuwepo kwa malori ya mizigo ambayo huondoka asubuhi hadi saa tatu. Nilipoitazama saa yangu iliitimu saa nne na nusu za asubuhi. Nikaamua kutafuta hoteli ya bei nafuu ili nijipumzishe hadi hiyo kesho.

Kabla ya kuchukua chumba niliamua kuuvinjari kidogo mji wa Mwanga. Kama miji mingine nchini Mwanga ilipanuka sana. Maeneo kama Vumilia na Majengo ambayo zamani yaliogopwa na kudharaulika sasa viwanja vyake vilioneka lulu. Majengo yalikuwa yakiota kama uyoga. Kwa bahati mbaya sana, kama yalivyokuwa maeneo mengi mapya, maeneo haya pia yalikosa huduma muhimu. Hayakuwa na mifereji ya maji machafu, hayakuwa na mfumo wa maji safi, umeme wa barabarani ilikuwa ndoto na hata barabara zilijaa na kujitunza zenyewe. Hali iliyopelekea mafuriko na uchafu kuivuruga dhamira nzima ya wamiliki.

Nilienda Mwanga Katubuka. Nikaingia Sokono. Macho yangu yalikuwa yakiwatafuta samaki niliowazoea na wale ambao nimekuwa nikisikia sifa zao toka utotoni; nonzi, wale samaki wakubwa wanaofanana na ndege, kuhe, samaki mtamu ambaye ana hadhi; singa, samaki mnono aliyejaa mafuta mwili mzima, nika, samaki mwenye nguzu za umeme ambaye kumshika lazima utumie mdomo wake wa chini vinginevyo utarushwa na kumwachia; kuvungwe, anayeitwa nguruwe wa majini kwa umbile na masharubu yake.

Ningependa pia kuwaona kungura, ndubu, kambale na wengineo. Sikuwa na bahati hiyo. Samaki niliowaona sokoni humo siku hiyo ni migebuga ambayo ilikuwa imekufa kwa

wingi. Ndubu? Siku hizi hapatikani sana. Kibonde? Alikuwapo mmoja tu leo, amegombewa kama mpira wa kona. Nikakata tamaa. Nikaenda soko la dagaa ambamo kulikuwa na dagaa wabichi wenyewe wakiwaita “mteke” na samaki wadogo wadogo walioitwa “Masembe.”

Nilipochoshwa na ziara hiyo nilitafuta hoteli na kuagiza chakula. Ngingekula nini zaidi ya ugali wa muhogo kwa migebuga iliyokaangwa kwa mafuta ya mawese? Ulikuwa mlo mtamu uliofanya nijisikie shibe isiyo na kifani.

Baadaye nilipanda basi kwenda Ujiji. Sikujisikia kuondoka Kigoma bila kuuona mji huo wa kihistoria. Mji ambao ulikuwa na uzito mmoja na ile ya Bagamoyo, Zanzibar na Kilwa. Lakini mara niliposhuka kilima cha kutoka Mnarani na Mawemi matumaini yangu ya kuiona Ujiji inayosisimua ilizimika. Macho yangu yalipokelewa na mji wa kale, kama ulivyokuwa enzi za kina Tip Tippu na Livingstone. Mji uliomezwa na nyumba nyingi ambazo zilielezwa kwa nyasi au bati kuukuu. Baadhi ya nyumba zilikuwa kuukuu zikiashiria jambo lilelile ambalo nimekuwa nikiliona huku na huko toka nilipotoka kifungoni; Umasikini.

Hali ya mitaa mingi pia ilitia huzuni. Kwa mtu aliyetoka katika miji inayokua, hata Mwanga tu, Ujiji ingeweza kumtoa machozi. Mitaa mingi ilimezwa na majani. Baadhi ya mitaa majirani walianza kulima mahindi na maharage. *Kuna nini? Nilijiuliza. Yako wapi magari yachangamshe mitaa? Wako wapi watu waitie uhai? Nini kimetokea hapa?*

Nikafikia uamuzi. Bila shaka biashara ya utumwa ilikuwa na laana. Vinginevyo mji huu ambao Dakta Livingstone alitia kambi miaka ya 1871 wakati akifanya utafiti katika nchi za Kongo na Malawi. Mji ambao Novemba 10, mwaka huohuo

Henry Stanley, baada ya kutumwa kumtafuta alikutana naye ufukweni na kusEma “Dr livingstone...! *I presume...*” mwaka mmoja kabla ya kifo chake. Ukiwa njia na kituo kuu cha wafanyabiashara wa Arabuni, Ulaya na Amerika katika kujipatia bidhaa za meno ya tembo na ile biashara haramu ya watumwa. Mji ambao huwezi kuandika historia ya Afrika bila ya kuutaja! *Hadi leo uko hivi! Kama si laana ni nini?*

Nilishuka kwenye basi, nikaifuata barabara ya Livingstone ambayo ilinifikisha Pwani ya Ujiji, pale Livingstone alipokutana na Stanley kwa mara ya kwanza. Palijengwa nguzo ya kumbukumbu yenye maelezo ya hafla yao ile. Nikatupa macho yangu ziwani na kuziona boti za jahazi ya wavuvi waliokuwa katika pilikapilika za safari, ama kuondoka ama ndio kwanza wanafika toka maeneo hayo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

Nikarejea Mwanga na kuanza kutafuta hoteli ya kulala. Ujiji haikuwa na nyumba ya aina hiyo. “Nenda Mwanga... nenda Kigoma mjini. Hapa utalala nje bure,” niliambiwa na msamaria mwema, mtu mzima aliyevaa kanzu na baragashia. Mkewe alivalia baibui lililomfunika gubigubi isipokuwa sehemu ndogo ya macho na miguu. Wazee hao walinikumbusha Bagamoyo na Pangani.

Wakati azana ya kuwakumbusha waumini kuwasili zinaanza kutoka misikiti mbalimbali mimi nilikuwa nikipanda basi kurudi Mwanga.

SURA YA ISHIRINI NA SITA

Hirizi Iliyopotea Na Maajabu Yake

Pengine kwa ajili ya safari ndefu ya wima toka Dar es Salaam, pengine kwa ajili ya chumba murua chenye hewa safi nilicholala nilijikuta nimechelewa kuamka. Hivyo, basi la Mwarabu liliniacha. Nilioga harakaharaka, nikanywa chai kwa dagaa wa mteke, kisha huyoo, nikawahi malori ya mizigo. Nilipata moja lililokuwa likipakia mabati na vifaa vingine vya ujenzi. Kwa namna ya muujiza nilipata kiti cha mbele, tukiwa abiria wawili tu na dereva. Muda mfupi baadaye gari liliondoka.

Nikiwa nimekaa dirishani nilipata fursa nzuri ya kutazama nje, macho yangu yalivutwa na ardhi nyekundu, mimea ya asili, mashamba ya wenyeji na zaidi ya yote watu. Toka Mwanga hadi Gungu na baadaye Mwandiga yalikuwa maeneo ya watu, nyumba ambazo hazikutofautiana sana na zile za Mwanga na Ujiji. Hii hapa ikiwa imejengwa kwa saruji bati na samani nyingine zikiwa zimeipamba; ile ikiwa nyumba ya tope, ilijengwa kwa matete na mianzi na kuezekwa kwa nyasi.

Toka Mwandiga mambo yalibadilika zaidi. Nyumba duni zilianza kutamalaki huku zile za afadhali zikizidi kupungua. Watu pia walibadilika. Wengi walivalia mavazi

duni, baadhi yakiwa yamechanikachanika. Ilikua rahisi sana kumshuku mtu kuwa ni mwendawazimu kutokana na hali hiyo. Lakini pale unapoona idadi kubwa zaidi iko katika hali hiyo, hasa watoto ambao wengi wao walitembea nusu watupu, miguu iliyojaa vumbi jekundu ikiwa pekupeku, unajikuta ukiondokana na wazo lako na kupata jibu mara moja, rahisi; umasikini.

Nyuso za watu wengi zilionyesha dalili ya kukata tamaa. Walicheka ndio, lakini kicheko hicho kilionekana mdomoni tu, moyoni ungeweza kusoma kitu kingine kabisa. Walizungumza pale ulipozungumza nao, lakini sauti zao ziliashiria kuifadhi jambo fulani ambalo hawakuwa na uwezo wa kulifafanua. Sura hizi za msiba, majengo mengi ya maombolezo na ardhi nzuri ambayo haikuwa ikichekelea kwa pamba na kahawa kama nilivyoizowea utotoni ni jambo ambalo lilinitia hofu badala ya shahuku ya kufika nyumbani. Nilihisi huzuni ikinigubika katika fikra zangu katika safari hiyo nzima.

Ndiyo, nchi yetu ni masikini. Lakini umasikini huu unazidiana kati ya mkoa na mkoa. Pengine iko mikoa iliyo taabanizaidi ya Kigoma, hilo halikunisumbua. Kilichonisumbua ni kwa nini Kigoma iwe katika kundi hilo? Kigoma haikuwa na sababu yoyote ya kuwa kama ilivyo. Ni mkoa uliojaaliwa kila ambacho binadamu anahitaji. Ardhi ilikuwa na rutuba tele, mali asili zikiwa zimefurika katika misitu na ardhini. Mito, mabwawa na baba lao; ziwa Tanganyika vikiwa vimejaa samaki tele ambao ladha yake ina uwezo wa kumshangaza mtu yeyote duniani zaidi ya hiyo Kigoma ni lango muhimu kwa nchi za Kongo, Burundi na hata Zambia. Ukweli huo pekee wa kijiografia ni rasilimali tosha. Historia ya Kigoma, hasa Ujiji pia ni rasimali nyingine muhimu ambayo kuitumia vyema

kungeweza kuubadili mkoa kiuchumi.

Kitu gani kimetokea hata mkoa uwe ukirudi nyuma badala ya kwenda mbele? Kitu gani kimesahauliwa? Nani alaumiwe? Nilijiuliza hili na lile. Yako mengi ambayo hayakuhitaji utafiti wa kina kuyaona. Moja la haraka likiwa usafiri. Ilikuwa rahisi zaidi kutoka Kigoma kwenda Burundi au Kongo kuliko kwenda Tabora au Mwanza, achilia mbali Dar es Salaam. Wakati huu wa Kilimanajaro au Arusha anaweza kutoka Dar es Salaam hadi kwao na akarudi jioni au kesho yake ilimchukua mtu wa Kigoma wiki mbili au zaidi kufanya safari hiyo, hali ambayo muuza nyanya au samaki ataishia kuiona bidhaa yake ikioza mbele ya macho yake.

Barabara ilikuwa tatizo la kwanza lisilohitaji mjadala barabara pia lilikuwa tatizo la pili. Kigoma ulikuwa mmoja kati ya mikoa iliyo kimya sana. Pamoja na kukisiwa kuwa na eneo la kilometa za mraba 37,037 mkoa wa Kigoma ulikuwa hauna kiwanda hata kimoja. Hata wale samaki, aina ya migebuga ambao katika misimu fulani huliwa kwa mamilion hiushia kuharibika bure na kutupwa badala ya kusindikwa; achilia mbali dagaa wanono wenye sifa zote.

Hata mafuta ya mawese, yatokanayo na michikichi ambalo ni zao linalostawi sana mkoani humu hayajapata kujengewa kiwanda cha kuyasindika ili yauzwe kimataifa. Nani atafikiria kufanya mradi kama huo mahala ambapo hakuna hata barabara?

Barabara pekee ambayo haikuaminika sana ya kutoka Kigoma kwenda nje ya mkoa na hiyo tuliyokuwa tukiitumia. Sehemu ndogo sana zilikuwa na lami. Sehemu kubwa ikiwa changarawe na tope ambalo lilifanya safari iwe shughuli kubwa badala ya starehe. Lakini hilo halikuwa tatizo kubwa.

Tatizo hasa lilikuwa mzunguko wa njia hiyo ulioifanya kuwa ndefu kupita kiasi. Ili kwenda Dar es Salaam au Tabora miji iliyoko mashariki ya mkoa ulilazimika kwenda kaskazini, upite Kasulu, Kibondo hadi Biharamulo kabla hujageuka kuelekea kusini ili ufike Kahama na Nzega kabla ya kuingia Tabora. Toka Tabora unapanda kaskazini tena na kuridi Nzega kabla ya kwenda Igunga, Iramba, Singida hadi Manyoni. Toka hapo utafika Dodoma na kutelezea Gairo, Morogoro, Chalinze na baadaye Dar es Salaam! Pema hapo?

Ndiyo, Kigoma kuna uwanja mdogo wa ndege. Ndege ndogondogo vilevile huja na kuondoka mara mbili au tatu kwa wiki. Licha ya ukweli kuwa hazitoshi, bado nauli kubwa ya ndege imefanya ziwe na wenyewe badala ya kila mtu. Si kila mtu mwenye laki mbili au tatu kwa safari ya saa nne kwenda na kurudi.

“Vipi unashukia wapi?” dereva alinizindua. “Naona uko mbali sana kimawazo,” aliongeza.

Nikapekecha macho yangu kwa kidole change cha shahada kabla ya kumuuliza, “Kwani hapa ni wapi?”

“Tumeshapita Simbo. Hapa ni Kitawe. Baada ya hapa tunaingia Mayange. Toka hapo ni moja kwa moja hadi Kasulu, mwisho wa safari yetu.”

Sikujua nimjibu nini. Kwa kweli, sikujua hata mahala pa kushuka. Niliondoka nikiwa mdogo sana. Kumbukumbu nilizokuwa nazo zilionyesha kuwa hatukuwa mbali sana na mji wa Kasulu. Lakini udogo, mabadiliko makubwa ya mazingira na hasa kutoweka kwa misitu mingi ambayo ningeweza kuikumbuka kulifanya nisijue wapi pa kuanzia upelelezi wangu wa kutafuta chochote nitakachoweza kupata juu ya wazazi wangu.

Nadhani dereva alizisoma hisia zangu. Kwani alirahisisha kazi yangu pale alipouliza, “Yaelekea wewe ni mgeni sana huku?”

“Nadhani, maana niliondoka nikiwa mdogo sana. Hata sifahamu nianzie wapi kuwatafuta wazee wangu,” niliropoka bila kutegemea.

Kwa wakazi wa mkoa ambao hauna ajira za kutosha, ambao mkoloni aliutumia kama shamba la kuchukulia manamba wakakate mkonge huko Tanga na Kilimanjaro maelezo yangu hayakumshangaza dereva huyo hata kidogo. Alihitaji maelezo mafupi tu; niliondoka lini. Tulikuwa tukiishi wapi, ukoo wangu ni upi na mengineyo. Nilipomweleza juu ya hofu yangu juu ya vijiji vya Ujamaa alinieleva mara moja. Akanishauri nishuke katika kijiji kinachofuata, kinachoitwa Mayange, ambacho ni kikubwa na kilikusanya familia mbalimbali toka maeneo mengi.

“Walisema kingekuwa kijiji cha mfano kwa maendeleo,” alisema akicheka kwa kebehi. “Hebu katazame hayo maendeleo halafu utatuambia.”

Nikaafikiana na ushauri wake. Tulipofika Mayenge nililipa nauli yangu, nikateremka na kuanza kazi ya kutafuta ‘kwetu’.

Kama nilivyotegemea kijiji cha Mayange kilikuwa kinyume kabisa na matarajio ya awali kama ilivyokuwa kwa vijiji vingine vyote tulivyovipita njiani, Mayange ilitoa taswira ileile, umasikini unaonuka. Karibu watoto wote walichakaa miili na mavazi, wakifanya kazi ndogondogo kama kubeba mizigo ya wasafiri kwa mikokoteni yao ya miti au kuomba tu kwa wapita njia. Baadhi walivaa sare za shule. Lakini sare nyingi kati ya hizo hazikufanana kabisa na malengo ya wizara

kwa kuchoka na kuchakaa.

Watu wazima nao walikuwa na yao. Wengi wao walikuwa taabani, suruali zikiwa zimejaa viraka, shati zikiwa zimepasukapasuka, miguu iliyokuwa peku ikiwa imebadilika rangi kutokana na vumbi jekundu lililowapiga pindi wakihangaikia mkono kwenda kinywani.

Waliahidiwa huduma muhimu kama barabara; hazikupata kujengwa au kukarabatiwa. Waliahidiwa maji ya bomba; hawakupata kuyaona. Waliahidiwa umeme; ilikuwa ndoto za mchana. Waliahidiwa huduma ya matibabu; sasa ilibidi kuyalipia kwa fedha ambazo huna. Kwa ujumla, ahadi zote zilizotumiwa ili kuwaondoa katika makazi ya baba na babu zao ziligeuka hewa. Jambo hilo lilifanya nyuso za kila mtu unayekutana naye zitangaze dalili zote za kukata tamaa.

Kazi ya kuitafuta familia moja, kati ya familia zaidi ya mia saba zilizohamishiwa hapo toka maeneo tofauti haikuwa ndogo. Nilitumia zaidi ya saa mbili kabla ya kumpata mzee mmoja ambaye alimfahamu babu, “Familia ya Kionambali, sio? Wala usihangaike. Wako humuhumu. Mtoto wake Karimanzira huwa namwona mara kwa mara.”

Nikapata matumaini. “Ni babu? Kionambali mwenyewe?” niliuliza.

“Huyo sina habari zake. Sijui kama bado yuko hai au tayari ametangulia,” mzee alinijibu. Laiti angejua kauli yake ilivyonishtua.

Nikiwa na matumaini mapya nilianza awamu ya pili ya kuwatafuta wazazi wangu. Zikiwa safari za mguu, katika kijiji kikubwa kisicho walao na jina la mtaa ilinichukua saa moja na nusu kabla ya kuonyeshwa kwa mbali nyumba iliyoaminika kuwa ya baba.

Ilikuwa nyumba iliyofanana na nyingine nyingi kijijini hapo; tofali za tope ambazo zilichakaa kabla ya kupata lipu, achilia mbali rangi. Juu nusu iliezekwa bati kuu kuu nusu nyasi. Sakafu ilikuwa ardhi ileile waliyoikuta palepale.

Nje ya nyumba hiyo alikuwepo bibi mmoja mchovu kama wengine wote kijijini hapo, akisuka ukili. Nilisogelea na kumwamkia. Kisha niliuliza kama hapo palikuwa nyumbani pa mzee Karimanzira. Swali langu lilimfanya bi mkubwa huyo ainuke na kunitazama kwa makini. Mara nikamwona akianza kutetemeka. Machozi yakianza kumtoka.

“Wewe ni Mtukwao!... Mwanangu! Umerudi...” alisema akinijia na kunikumbatia kwa nguzu zake zote.

Alikuwa mama! Mama yangu kipenzi! Fuko nililokuwa nalo mkononi lilidondoka pwaa, mikono yangu pia ikamkumbatia kwa nguvu. Masikioni nilisikia sauti nzito ya kiume ikilia! Kilio cha kwikwi. Ilinichukua muda kubaini kuwa ilikuwa ni mimi niliyekuwa nikilia.

Mara mzee mmoja akatoka nje ya nyumba hiyo. Alikuwa mchovu vilevile. Umbile lake refu lilipinda kwa mbele, ndevu zenye mchanganyiko na mvi zilimeza kidevu na kichwa chake kizima. Akitetemeka miguu na mikono yeye pia alinijia na kunikumbatia, machozi yakimlengalenga.

Baba! Amezeeka kabla hajapata kuwa kijana!

Dakika mbili tatu baadaye nyumbani palifurika. Watu waliotoka huko na huko walijazana kushangilia ujio wangu. Kila mtu alisema lake, ingawa mada ilikuwa ileile; Mwana mpotevu karejea!

Niliingizwa ndani, nikapewa kiti cha kifalme; kigoda cha baba. Fumba fumbua togwa tamu ikaletwa. Nikapewa kata kubwa iliyojaa. Kabla haijaisha nililetewa mihogo mitamu,

huko nje nikiwaona vijana wakikimbizana na jogoo.

Baba na mama hawakubanduka ubavuni mwangu. Walikuwa na mengi ya kuniuliza mengi ya kunisimulia. Kwa bahati mbaya, hali haikuruhusu. Watu walikuwa tele, wakinishangaa kana kwamba nimetoka mwezini. Kelele pia zilishamiri. Watoto ambao hata sikuwafahamu walijipenyeza na kukaa miguuni mwangu, wakijitahidi sana kunikumbatia, walao miguu.

Kwa kweli sikutarajia mapokezi makubwa kama haya. Nikiwa mtu aliyepotea kwa zaidi ya miaka thelathini, mtu aliyerudi akiwa mikono mitupu kama nilivyokuwa, nilitarajia kupokelewa kwa kejeli au dharau. Si vicheko na kushangiliwa kwa takribani kijiji kizima kama ilivyokuwa. Hata hivyo, nilijihisi kama mtu aliyeutua mzigo mzito uliomlelea. Nilijihisi kama ambaye nilifutiwa madhambi yangu yote hata kabla ya kuomba radhi.

Kitu kimoja tu kilikuwa kikinisumbua. Mtu niliyetamani kumwona pengine kabla ya wengine wote hakuwa katika kundi la watu waliojitokeza kunilaki. Mtu huyohuyo nilihitaji sana kumwomba radhi kwa kumwamgusha katika matarajio aliyokuwa nayo juu yangu na kumpotezea hirizi yake muhimu. Nilimtegemea awe katika mjumuiko huo, aniite kando ambako tungeketi peke yetu na kuteta kama mtu na baba yake. Sikumwona. Wala sikuthubutu kuuliza harakaharaka kwa kuchelea kupewa jibu ambalo lingeweza kunitia ugonjwa wa moyo; Babu yake! Mbona alikufa zamani?

Kuku alikwishachinjwa na kupikwa. Ugali mweusi wa nyangwe uliletwa mbele yangu kwa kitoweo cha kuku huyo. Bila kuambiwa wageni walianza kupungua ili kuniachia faragha ya kufaidi chakula changu. Nilishindwa kujizuia. Kabla

ya kumega tonge la kwanza nilimuuliza baba, “Babu yuko wapi?” nilisubiri jibu lake kwa hofu kubwa, moyo ukinidunda. Lakini nilipomwona baba akitabasamu kabla hajanijibu hofu ilitoweka moyoni mwangu.

“Babu yako kwani humjui?” baba alisema. “Aligoma katakata kuhama. Jeshi la polisi, jeshi la mgambo na hata sungusungu walishindwa kabisa kumtoa. Hivi sasa yuko peke yake ndani ya msitu mkubwa wa yaliyokuwa makazi yake. Kila wiki huwa nakwenda kumjulua hali.”

Nikapumua. “Bibi?” niliuliza.

“Yeye hatuko naye tena. Alitutoka miaka mitatu iliyopita. Alipatwa na ugonjwa wa malale uliokataa kila aina ya dawa.”

Ladha ya kuku ikaniishia palepale.

* * *

“Nilijua utarudi salama... nilikuwa nikikusubiri... nisingeweza kufa kabla hujarudi, mjukuu wangu,” ilikuwa kauli ya kwanza ya babu mara aliponitia machoni na kunipapasa kichwani.

Sikuweza kuyastahimili machozi yaliyomiminika toka machoni mwangu. Babu alinikumbatia, huku mkono wake ukiendelea kunipapasa kichwani kwa namna ya kunibembeleza. Kitendo hicho kilizidisha uchungu moyoni mwangu na kunifanya nizidi kulia. Kwa mara ya kwanza, hakunishutumu kwa kitendo hicho. Niliinua uso na kumtazama kwa wizi. Yeye pia alilowa macho kwa machozi.

Babu analia, chuma cha pua!

Kwangu, alikuwa zaidi ya babu. Alikuwa kila kitu; baba, babu, rafiki, mwalimu na zaidi ya hayo. Hayo nilibaini na kuyahakikisha muda huo ambao mzee hataweza kustahimili

kabisa kuficha udhaifu wake kwangu! Nitamsimuliaje *malaika* huyu kuwa jitihada zake zote za kupita mabonde, milima na misitu yenye hatari zote za dunia, hadi kunifikisha nchi ya Wahaya ili nipate elimu zilikuwa kazi bure? Nitaanzaje kumwambia kuwa ile hirizi yake, urithi pekee alioniachia ilipotea kwa uzembe? Niliteseka vibaya sana akilini nilipowaza hayo.

Nilikuwa nimemlazimisha baba alfajiri tu ya siku iliyofuata aniongoze kuja kumwona babu. Yeye akisisitiza kuwa ningepumzika walao siku mbili kabla ya kufanya safari hiyo. Jambo ambalo sikuafikiana nalo.

Kwa kutokuwa na uhakika wa kuwapata wazazi wangu, wakiwa hai nilifika nyumbani mikono mitupu. Hivyo, nilipopata fursa ya faragha ya kumkabidhi baba shilingi 50,000 kati ya zile laki moja nilizobakiwa nazo nilionekana shujaa mkubwa. Baba alianza mipango ya 'kumaliza bati' mama aliongea juu ya kulimisha shamba. Ilikuwa kama nimetoa milioni hamsini.

Tulimkuta babu akifunga mbuzi wake nje ya nyumba. Alivaa nguo zake zile alizozipenda, kaptula na shati nyeupe. Ziling'ara kama nilivyoziacha! Miguuni alitilia buti zake ambazo nazo ziling'ara kwa kiwi, ingawa zilianza kuchoka. Alikuwa peke yake katikati ya pori, isipokuwa kwa mifugo mingi ya mbuzi, kuku na bata. Watu wa pwani wangeweza kuapa kuwa ni jini jeupe linalokaa peke yake msituni. Babu alikuwa ametusikia toka mbali. Hivyo, alimfunga mbuzi yule harakaharaka na kusimama akitukodolea macho. Alipotuona alitukimbilia na kunidaka juujuu. Angeweza kunibeba... angeweza kunitia mweleka.... Babu alikuwa na nguvu zake. Ilikuwa kama ni binadamu pekee aliyebishana na uzee. Binadamu ambaye hakukubali kusalimu amri kwa kifo.

Pamoja na baba tulikuwa na vijana wengine wawili ambao nilielekezwa kuwa ni ndugu zangu. Vijana hao walipewa amri ya kumkamata beberu mkubwa kuliko wote na kumchinja. Akachunwa. Moto ukawashwa. Muda mfupi baadaye, tulikuwa tukimla mbuzi yule, wa kuchoma. Babu, akiwa na meno yake yote alitafuna mguu mzima wakati wengine tukishika shika hapa na pale.

Baadaye babu aliwataka baba na wale wenzetu wengine kuondoka kwa maelezo kuwa alikuwa na mengi ya kuzungumza na mjuu wake faragha. Usiri wangu na babu halikuwa jambo geni kwa baba, toka utoto wangu. Hivyo, hakutia ubishi, walichukua nyama ya kula nyumbani wakaondoka zao kwa ahadi ya kunifuata kesho.

Nikapata wasaa wa kuchomoa zile elfu hamsini nilizobakiza na kumkabidhi babu. “Zawadi pekee niliyoweza kukuletea ni hii,” nilisema kwa masikitiko.

Babu hakuzipokea. Badala yake alicheka kabla ya kusema, “Sidhani kama nazihitaji. Za nini? Kaa nazo, zitakufaa wewe zaidi. Naamini bado unasafari nyingine ndefu, yenye mafanikio makubwa zaidi. Halafu, bado tuna mengi ya kuzungumza, mimi na wewe.”

“Bila shaka. Niliitikia.

“Miaka mingapi vile toka tumetengana?” Babu aliniuliza.

“Mingi sana. Ni aibu kuitaja.” Nilimjibu.

“Aibu ya nini? Mwanaume anayeonea aibu masaibu yake hafai. Kwa nini ufanye jambo ambalo utalijutia maishani mwako?”

Nilijua darasa la babu limeanza. Sikuwa tayari kwa darasa lolote wala somo lolote kabla ya kumtaka radhi. Hivyo nikajikongoja na kumwambia, “Babu ningeomba nianze kwa kukutaka radhi.”

“Radhi ya nini?”

“Hirizi.”

“Ilifanyaje?”

“Ilipotea!”

Nilitarajia babu abadilike, akasirike. Lakini kwa mshangao nilimwona akiachia tabasamu jembamba. “Nisubiri kidogo,” alisema akiinuka na kuingia ndani, aliporejea alikuwa na hirizi mkononi.

“Hirizi hii siyo?”

Niliitazama kwa makini. *Nisingeweza kuisahau. Ilikuwa ileile!*

Sikuyaamini macho yangu. Nikamkodolea babu macho ya mshangao.

“Hii ndiyo inayokusumbua?” babu aliongeza baada ya kicheko kingine. “Usiwe na wasiwasi. Ilipotea ikatafuta njia, ikarudi nyumbani kukusubiri.”

Bado sikuweza kuelewa. Hirizi hiyo ilipotea porini katika purukushani za kuikimbiza isianguke mikononi mwa padri. Yule kimbelembele, Byabato, alinihakikishia kuwa aliokota tena na kumrudishia padri Backhove ambaye aliichoma, ikakataa kuungua. Kwamba baadaye ilitupwa baharini. “Ilifikaje kwako?” nikamuuliza.

“Ni hadithi ndefu. Ili kuifanya fupi pengine nikuambie tu kuwa ililetwa.”

“Na nani?” nilizidi kumbana babu.

“Na mizimu ya babu zetu.”

Bado nilikuwa sijamwelewa. Nikamwambia hivyo.

“Mizimu ina njia nyingi ya kuwalinda wahanga wake,” alifafanua. “Chochote kilichokutokea hadi hirizi hii kutengana nawe wahanga walikuwa wakiona. Ama kwa kujigeuza ndege,

ama kwa kuwatuma ndege, hirizi hii ililetwa hadi katika mikono yangu.”

Babu alipoona kuwa bado sijaridhika na ufafanuzi huo aliamua kuwa wazi zaidi. Alisema kuwa jioni moja alikuwa akiwinda katika mwambao wa mto Malagalasi. Mara akaona kundi kubwa la ndege aina ya hondohondo wakitua hatua chache toka alipokuwa. “Walikuwa wengi. Kama elfu moja hivi. Waliponiona waliruka kunikimbia. Lakini mwenzao mmoja hakuweza kuruka. Alikuwa akipigapiga mabawa kwa nia ya kupaa lakini hakuweza. Nikamsogelea kuona kapatwa na nini. Nikabaini kuwa shingo yake ilikabwa na kamba nyeusi ambayo ilinasa kwenye kichaka cha mti. Nilipomshika ili kumkwamua ile kamba nilishangaa kuona kuwa ilikuwa hirizi ile niliyokupa. Nikaitoa na kumwacha ndege ambaye alipaa kuwaendea wenzake waliokuwa wakihangaika angani kumsubiri.”

Ilikuwa habari ya ajabu kwangu. Hirizi yangu, iliyopotea zaidi ya miaka thelathini iliyopita imerejea mikononi mwangu. Niliipokea, nikaipapasa. Ilikuwa ileile, kwa rangi na uzito. Kwamba imerudi mikononi mwangu halikuwa jambo la ajabu sana, ni namna iliyoifanya irudi ambayo kichwa changu hakikuweza kupokea.

Falsafa nyingi zilipita kichwani mwangu. Kama kweli ilitupwa ziwani bila shaka ingeweza kuoza. Kama hilo halikutokea ni wazi kuwa ilimezwa na samaki ambaye huenda alivuliwa na kuliwa. Kama ilikuwa hivyo hirizi itakuwa ilitupwa kama sehemu ya uchafu wa matumbo ya samaki wanayotayarishwa kwa ajili ya minofu kusafirishwa Ulaya na “mapanki” kuvamiwa na akina baba na mama ntilie. Inawezekana kuwa katika jitihada za kujitafutia chochote ndege yule alijikuta ameivaa hirizi ile na kuisafirisha bila

kujua? Kama ni kweli kwa nini ailete hadi miguuni mwa babu?

Katika pitiapitia yangu vitabuni nilikuwa nimesoma mahala tabia za ndege. Moja ya tabia zao za ajabu ni ile ya kuhama au kusafiri safari za mbali kila ifikapo msimu fulani. Mara nyingi ndege hao wanaweza kusafiri safari za mbali toka Marekani au Ulaya hadi Afrika. Inaaminika kuwa wengi uhama katika vipindi vya hali fulani ya hewa na kurudi hali inapotengemaa. Inaaminika pia huko ambako huenda ndiko ambako ndege huzaliana na kurejea likiwa kundi kubwa zaidi. Inawezekana kabisa kuwa hondohondo aliyebeba hirizi yangu alikuwa katika msafara huo. Anaweza kuwa alikuwa akitoka zake Ulaya au nchi za Kiarabu na kuelekea Afrika Kusini!

Babau alikuwa kama anayeyasoma mawazo yangu. Alikohoa kidogo kabla ya kusema, “Naona na wewe tayari umeambukizwa yale maradhi yenu.”

“Maradhi gani?

“Maradhi ya kisomi. Naona unavyoona shida kuamini kuwa mizimu ya babu wa babu zako imekurejeshea hirizi hii! shauri lako. La msingi ni kwamba hirizi yako imerejea na tangu leo utaivaa tena. safari hii milango yote uliyoshindwa kuifunguwa itafunguka,” alisema akinivisha hirizi hiyo na kisha kunitemea mate kichwani na kifuani.

“Kuna jambo la pili.” Alisema akiinuka tena na kurudi ndani. Aliporejea alikuwa na bahasha tatu mkononi. Alinikadhi. Ilikuwa barua. Juu ziliandikwa jina lake na anuani ya kiji chake. Iielekea barua hizo zilitoka nje ya nchi, kwani stempu zote zilikuwa na picha ya malkia au wafalme wazungu, muhuri ukiosomeka waziwazi “*Stockholm-sweden*”. Tarehe kwenye mihuri hiyo zilionyesha kuwa zilitumwa zaidi ya miaka kumi na mitano iliyopita!

“Barua!” Niliropoka.

“Ndiyo,” babu alijibu “Mbona hazijafunguliwa? Ni za zamani sana,” nilisaili.

Babu naye akaonyesha mshangao wake kwangu, “Mjukuu wangu, zinalekea kuwa ni barua muhimu sana. Unadhani ningeweza kumpelekea mtu yeyote asome siri zangu na kuanza kunitangaza? Nilikuwa nakusubiri, nilijua ungerudi salama.”

“Ni wewe peke yako utakayekuwa wa kwanza kuelewa chochote kilichoandikwa humo.”

“Zilifikaje hapa?” Niliuliza nikianza kufungua moja niliyoiona ya zamani zaidi.

“Zililetwa. DC alileta kwa mkono wake mwenyewe. Alinishawishi kufungua lakini nilikataa katakata.”

Baada ya maelezo hayo babu alikunjua kiti chake cha uvivu, kilichotengenezwa kwa ngozi ya nyati na kujilaza kimya kwa namna ya kunipa wasaa wa kusoma barua hizo kwa tuo.

Barua ya kwanza ilikua ndefu kidogo. Ilianza kwa salamu za siku nyingi, ikaendelea kwa taarifa ya kuipongeza kazi yake alipokuwa nchini humo, “Tumetengeneza filamu mbili za ile michezo uliyoshiriki kuicheza. Filamu hizo zimependwa sana Ulaya nzima zinanunuliwa kama peremende. Taarifa tuliyoichapisha hapa chini ni malipo yako ya mrabaha hadi sasa. Tunaomba ufanye kila uwezalo kuwasiliana nasi ili upokee malipo yako,” ilieleza barua hiyo.

Sehemu ya pili ya barua hiyo ilikuwa na mahesabu ya idadi ya mikanda iliyouzwa na televisheni zilizoununua hakimiliki na hakishiriki. Kwa hesabu za harakaharaka asilimia ya babu ilionyesha kama dola 227,000. Sikuyaamini macho yangu. Nikainua macho kumtazama. Alikuwa amesinzia, tabasamu likiwa mdomoni.

Nikafungua barua ya pili. Hii iliandikwa mwaka mmoja baadaye. Ilisisitiza, umuhimu wa babu kwenda haraka au kumtuma mrithi wake yeyote anayeaminika. Ilongeza kuwa iwapo kuna tatizo lolote la vitambulisho mwakilishi huyo alichotakiwa ni kwenda na ile hirizi ambayo ilikuwa haibanduki shingoni mwake. “Benki yetu tayari imearifiwa juu ya hilo. Usiwe na wasiwasi,” iliongeza barua hiyo.

Barua ya tatu iliambatanishwa na hundi. Hesabu zilizoandikwa juu ya hundi hiyo zilinitatanisha dola 812,000! Barua ilisisitiza fedha hizo kuchukuliwa. Ikiongeza kuwa benki yao tayari imefungua matawi nchini katika miji ya Dar es Salaam na Mwanza, haikuwepo haja ya kusafiri hadi Ulaya tena.

Mara nikaanza kupata njozi za mchana. Nilijiona nikiandika kitabu, ambacho kiliyahusu maisha yangu mwenyewe. Niliyaumba na kuyaumbua matukio, mikasa na visa vyote vilivyonikumba toka katika safari zangu kuu mbili safari ya kimaisha iliyonifikisha kila pembe ya nchi na ile ya kimaumbile ambayo ilinitoa utotoni na kuniingiza ukubwani. Nilihisi hata jina la kitabu likinijia akilini; Kiguu na Njia.

Zikanijia njozi nyingine. Katika njozi hizi nilijiona nikiwalekeza watu wa masuala ya filamu wapi pa kuelekeza kamera zao, katika filamu niliyokua nikiitengeneza. Niliwataka ihusishe maeneo yote muhimu ya nchi yetu, mbuga za wanyama, maziwa na mito yote ambayo haikupata kutangazwa vizuri. Kwa njozi niliona mikanda ya filamu hiyo ikigombewa na kuwafanya watazamaji waone hazina kubwa iliyosahauliwa ambayo walijaliwa na Muumba.

Nikaona jinsi nilivyokuwa nikiishi na mke wangu Nashifa kwa furaha. Watoto wetu wawili wenye afya njema

wakicheka na kufurahi...

Halafu nikamkumbuka mwenye fedha zake, ambazo zingeniwezesha kufanikisha ndoto hiyo. Nikageuka.

“Babu!” niliita tena nikimtazama.

Alikuwa bado amelala vilevile kwenye kiti chake cha uvivu. Tabasamu lake lilikuwa bado limesahauliwa palepale usoni kama mtu aliyekuwa katika dimbwi la starehe. Niliinuka na kumshika bega. Nikamtikisa taratibu, baadaye kwa nguvu kidogo, “Babu... babu... babu...!”

Kimya! Kimya!

Nikashtuka. Alikuwa kama hapumui! Nikamshika kifua kusikiliza mapigo ya moyo. Hayakuwepo. Hata mwili wake tayari ulikuwa umepoa. Ndio kwanza nikabaini kuwa babu hatukuwa naye tena duniani! Tabasamu lake lililobakia palepale kama ishara ya ushindi kwa jambo zito lililokuwa likimsumbua kwa muda mrefu.

Nilitetemeka mwili mzima. Nguvu zikaniishia, furaha, faraja na matumaini makubwa niliyoyapata mara baada ya kuisoma barua yake, ikatumbukia nyongo.

